# HUDUMA YA UTUME MIJINI

Ellen G. White



## HUDUMA YA UTUME MIJINI

**Waandishi, Wahariri, Wahakiki, Wana maombi, Wasaidizi wa teknolojia na washauri n.k**

Grace Masaka Momadi-New Jersey, Marekani
Lyaka Katemani-Mwanza, Tanzania
Petro Johann Tumaini- Iringa, Tanzania
Daniel Nyangaresi Masaka-Kisii, Kenya
Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania
Innocent Wayoga-Dar Es Salaam, Tanzania Gibson
Wilson Mujuni-Masasi, Tanzania
David Masaka-Pennslyvania, Marekani
Paul Masaka-New Jersey, Marekani
Sandra Barron- Carolina, Marekani
Mbusi Mpagalushu-Bariadi,Tanzania
Emmanuel Pelote-Nairobi, Kenya
Cindy Tustch-Washington, Marekani
Judi Mmari-Mugane-Siha, Tanzania
John Mugane-Nakuru, Kenya
Gerard Makori Nyafanga-Rorya, Tanzania

HUDUMA ya VITABU vya Kujisaidia maisha
Uhamishoni, Ughaibuni Mtandaoni Majumbani
Samaritan Laymen Ministries Ltd Of New Jersey

Mwito kwa Mpendwa Msomaji

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ombi letu, usibadilishe chochote, tuite kama kuna kosa! Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini, ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, nasit umekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu vya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine. Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwanini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Wauminin wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zile au wawe na mwenendo kama ule mfano mdogo sana utakuwa, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate nk. Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu. Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tutafutane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa ***Maandishi*** yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia email UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo Bwana

# YALIYOMO


Dibaji ..... vi

SURA YA 1— Masomo Kutoka katika Maandiko Kuhusu Uinjilisti katika miji ..... 10

(AGANO LA KALE) ..... 10

ULIMWENGU WA ANTEDILUVIAN—HENOKO (ulimwengu wa kabla ya Gharika, ulimwengu ulioonywa) ..... 10

SODOMA ..... 11

NINAWI ..... 12

YERUSALEMU-UAMSHO WAKATI WA MFALME YOSIA ..... 13

AGANO JIPYA ..... 15

Miji ya Agano Jipya ..... 17

YERUSALEMU ..... 17

ANTIOKIA YA SYRIA ..... 18

THESALONIKE ..... 20

ATHENS (Athene) ..... 21

KORINTHO ..... 22

EFESO ..... 25

RUMI ..... 26

SURA YA 2- Kazi Muhimu Katika Wakati Huu ..... 28

WATENDAKAZI NA KRISTO KWENYE MIJI ..... 32

WATENDAKAZI WATIWE MOYO ..... 34

URA YA 3 - CHANGAMOTO ZA JIJI ..... 37

UMASIKINI NA KUKOSA AJIRA ..... 39

KUNYONYWA KWA MASIKINI NA WALE WALIO MATAJIRI ..... 41

KUNA WATU WANAOTOA MSAADA ..... 43

VYAMA VYA WAFANYAKAZI (Trade Unions) ..... 43

UCHAFUZI WA MAZINGIRA 47
HUKUMU ZA MUNGU KATIKA MIJI 51
MADAI YENYE KULETA MSISIMKO YANAZUIA KAZI YA UINJILISTI MIJINI 52
Sura ya 4— Jumla ya Ushirikishwaji Unaohitajika 56
MZIGO WA KAZI YA MIJINI 56
CHANGAMKIA MANUFAA YA KILA FURSA 57
CHUKUENI TAHADHARI, MILANGO HUFUNGUKA KWA WAPINZANI PIA 59
WAHUSISHE WAUMINI KWENYE HUDUMA YA JUMUIYA . 59
WAHUDUMU WNAITWA KUFANYA UINJILISTI MJINI 60
WANAFUNZI WANAPASWA KUSHIRIKI 60
VIONGOZI WA KANISA WAHUSISHWE 61
KUTOA SADAKA YA MISHENI AU UTUME, SI MBADALA WA WEWE KUFANYA KAZI YA MUNGU AU HUDUMA 64
Sura ya 5—Mkakati wa Kuifikia Miji 65
MUNGU ANATAKA KAZI MAHSUSI IFANYIKE KWENYE MAJIJI 65
MBINU YA KRISTO KUFIKIA MIJI 69
EPUKA MATENDO YALETAYO MAFARAKANO AU MALUMBANO 71
UONGOZI KATIKA SEHEMU MAHALIA UNAHITAJIKA 74
KRISTO MFANO MKAMILIFU 82
WAKE KWA WAUME WANAHITAJIKA KATIKA HUDUMA MBALIMBALI 87
WAFANYAKAZI WANAOJITEGEMEZA WENYEWE 88
ROHO YA KUJITOA MHANGA INAHITAJIKA 89
KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU 91

KUWATAYARISHA WAMISHONARI WA TIBA 92
VIJANA WAFUNZWE KUFANYA KAZI YA MIJINI 93
SHULE ZA UINJILISTI KWENYE MAJIJI 98
MIKATABA YA ELIMU 100
Sura ya 7—Njia za Kufundisha na Kuvuna 103
Vikundi Lengwa 123
Sura ya 8—Kufanya Kazi Ndani na Nje ya Miji 136
Sura ya 9—Huduma ya Afya Iliyokita kwa Kristo Daraja linaloongoza kuvukia 150
Sura ya 10—Kupanda Makanisa Mijini 171
Sura ya 11—Kazi katika Miji Maalum 185
Miji katika Amerika Kaskazini 185
Miji Nje ya Amerika Kaskazini 209
Sura ya 12—Utafiti maalumu 226

# Dibaji

Zaburi ya 48 ndiyo imekuwa maarufu kwa wakazi wa mijini sawa na Zaburi ya ishirini na tatu ilivyo maarufu kwa wengi wetu leo. Bwana "Bwana Ndiye aliye mkuu, Na Mwenye kusifiwa sana. Katika mji wa Mungu wetu." 48:1. Ni uwepo wa Mungu katika mji ndio hufanya ukuu na uzuri wa mji, kiburi, kujivunia au kujitukuza kwake, "furaha ya dunia yote, ... mji wa Mfalme mkuu" ( mstari wa 2 , NKJV). Uhalisia kwamba Mungu anaweza kujitambulisha sana na miji ya kidunia leo, ni kengele tosha kwetu kuona uzuri wa miji na uwezekano uliopo hapo leo kupitia macho ya Mungu. MTC 9.1

Hata hivyo, mara nyingi majiji yamejipanga kinyume dhidi ya Mungu. Miji hiyo ilishamiri wakati wa Biblia ilipoandikwa. Yesu, Musa, Daudi, Danieli, na manabii wengine wa Biblia walilazimika kushughulika na majiji, ambayo baadhi yake yalikuwa makubwa katika kipindi hicho. Basi Ninawi ulikuwa mji mkubwa mno, ukubwa wake mwendo wa siku tatu." ( Yona 3:3 , NKJV), ukiwa na "zaidi ya watu mia na ishirini elfu" ( Yona 4:11 , NKJV). Babeli ilikuwa na takriban kilomita 16 za kuta zinazozunguka idadi kubwa ya watu na majengo makubwa ambayo yalijumuisha mojawapo ya maajabu saba ya ulimwengu wa kale. Efeso ya Agano Jipya ilikuwa na taa zinazoangaza kwenye mitaa yake mikuu, Arcadiane maarufu. Roma, Aleksandria, Antiokia, Athene, Korintho, Susa, na Thebe yalikuwa miongoni mwa majiji makubwa ya nyakati za Biblia. MTC 9.2

Paulo alikuwa mwinjilisti mkuu wa Ukristo katika miji mikuu ya Dola ya Kirumi. Petro, Filipo, Apolo, na viongozi wengine wa Kikristo walihubiri mijini pia. Wale waliozoea kufikiria majiji kuwa mahali pa uovu wanapaswa kukumbuka

kwamba katika maono Yohana aliona nia kuu ya Mungu hatimaye kwaajili ya wanadamu ni kuwa na jiji na utukufu na furaha isiyoweza kulinganishwa. MTC 9.3

Yesu alipokuwa duniani, “alizunguka katika miji na vijiji vyote,” akifundisha, akihubiri, na kuponya. Umati ulimgusa moyo wake sana: “Alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa … kama kondoo wasio na mchungaji” ( Mathayo 9:35, 36 , NKJV). Leo, idadi kubwa ya watu ulimwenguni inaishi mijini. Je, Yesu anawajali hawa kidogo tu kuliko alivyowajali wale waliokuwa katika miji miaka 2,000 iliyopita? Si ajabu kwamba Ellen G. White alipewa mashauri mengi juu ya miji ili kuliandaa kanisa kwa ajili ya uinjilisti wa mijini na huduma. Walakini maagizo Yake juu ya kazi ya mijini hayajulikani sana kuliko ule wito wake wa kutoka kwenye maeneo ya mijini na kwenda vijijini au nje ya miji, mahali penye mashamba. Mkusanyiko mfupi wa kitabu cha Country Living (1946) umeleta umakini unaostahili kwa wito huu. Kama nyongeza ya mkusanyo huo, chapisho la sasa la Ministry to the Cities (Utume kwa Miji), limekusudiwa kuwasaidia wasomaji kuelewa mpango wa Mungu wa kufanya huduma mjini. Kazi hii imetayarishwa na ofisi za Ellen G. White Estate, nayo haichukui tu kutoka katika nakala, vitabu, na vipeperushi vya Ellen G. White kuhusu mada hii, lakini pia kutoka katika barua na maandishi yake. Huu siyo mkusanyo wa mashauri yake yote kuhusiana na miji, lakini ni mkusanyiko wakilishi unaoelimisha kwa hali ya juu kabisa. Unashughulikia maeneo mengi ya mafundisho ambayo Ellen White alipokea kwa ajili ya kanisa na ufikiaji wa watu katika miji ya ulimwengu. Ili kumsaidia msomaji, miaka imetolewa kutoka matamko yaliyotolewa katika kitabu hiki. Kwa barua na miswada, mwaka uliotolewa unaonyesha wakati wa kuandika (maana kazi inakuwa haijachapwa bado); na kwa

vyanzo vingine, ni wakati wa Toleo la kwanza katika mfumo uliotajwa (1st Edition). Nukuu za Testimonies for the Church, vol 1-5 au Shuhuda kwa Kanisa, zinaonyesha mwaka wa uchapishaji wake wa awali kama vipeperushi vya Shuhuda . MTC 9.4

Miongo mingi imepita tangu Ellen White alipoandika mashauri yake ya mwisho. Kwa njia fulani hali tunazozikabili leo ni tofauti na zile alizozungumza yeye. Msomaji anapaswa kukumbuka kwamba wakati, mahali, na mambo mengine lazima vizingatiwe katika kupanga mipango ya kazi ya leo. Masharti yanaweza kubadilika, mbinu za kushughulika na mambo haya zinaweza kutofautiana, lakini kanuni za mashauri hubaki vile vile. Kanuni hizi zinafaa kufahamisha na kuongoza juhudi zetu katika kukabiliana na changamoto za leo. MTC 10.1

Ujio wa pili wa Kristo unapokaribia, maneno ya Ellen White yana King'ora au tahadhari mpya: "Kazi katika miji ni kazi muhimu kwa wakati huu. Miji inapofanyiwa kazi kama vile Mungu angependa ifanyike, matokeo yake yatakuwa ni kuweka operesheni/vuguvugu kubwa ambalo hatujawahi kulishuhudia" ( Medical Ministry, 304 ).

Ni matumaini yetu na maombi kwamba Huduma ya utume katika Miji inaweza kuwasaidia wasomaji kujitolea zaidi kutekeleza mashauri ambayo tumeyapokea na yenye ufanisi zaidi katika kuifikia miji na ujumbe wa Kristo wa siku za mwisho. MTC 10.2

-Wadhamini wa Ellen G. White Estate Silver
Spring, Maryland

Somo Kutoka kwa Maandiko Kuhusiana na Uinjilisti wa Jiji (Agano la Kale)

## SURA YA 1— Masomo Kutoka katika Maandiko Kuhusu Uinjilisti katika miji

## (AGANO LA KALE)

### ULIMWENGU WA ANTEDILUVIAN—HENOKO (ulimwengu wa kabla ya Gharika, ulimwengu ulioonywa)

**Mfano wa Awali wa Uinjilisti wa** mijini.— Henoko alitembea na Mungu, na bado hakuishi katika ... jiji lolote lililochafuliwa na ... ujeuri, ukatili na uovu.— Ms 94, 1903 ( Ev, 78 ). MTC 11.1

**Enoko Hakuishi Pamoja na Waovu.—** [Enoko] hakufanya makao yake pamoja na waovu. ... Alijiweka mwenyewe na familia yake mahali ambapo angahewa ingekuwa safi kaw kadri iwezekanavyo. Kisha nyakati fulani alienda kwa wakaazi wa ulimwengu na ujumbe aliopewa na Mungu. ... Baada ya kutangaza ujumbe wake, kila mara alirudi pamoja naye baadhi ya watu waliokuwa wamepokea onyo hilo hadi mahali pake pa kupumzikia Ms 42, 1900 ( Maranatha, 184 ). MTC 11.2

**Mbinu za Henoko Zitakuwa Mbinu Zetu.—** Mikakati yenye hekima inapaswa iwekwe, ili ... kazi ifanywe kwa jinsi itakayoleta manufaa zaidi. Jinsi uovu unavyoongezeka zaidi katika miji mikubwa, itatubidi tuifanyie kazi kutoka katika vituo vya nje ya miji (Outpost Centers mifano ni kama vile Kibidula Farm, Riverside Farm Zambia, Wildwood Lifestyle and Retreat Center Georgia nk). Hivyo ndivyo Henoko alivyofanya kazi katika siku za kabla ya gharika, wakati uovu ulipoenea na kushamiri katika kila jumuiya yenye watu wengi, na wakati ambapo ukatili/ujeuri ulikuwa katika nchi.—R&H, Septemba 27, 1906 .
MTC 11.3

## SODOMA

**Upendo wa roho za watu ulihamasisha maombi ya Abrahamu.—** Ingawa Lutu alikuwa ameishi Sodoma, yeye hakushiriki uovu wa wakaaji wake. Ibrahamu alifikiri kwamba katika jiji hilo kubwa lenye watu wengi lazima kuwe na waabudu wengine wa Mungu wa Kweli. Na kwa kuzingatia hili alisihi, "Na iwe mbali nawe kufanya mambo kama haya, kuwaua wenye haki pamoja na waovu; ... hiyo iwe mbali Nawe: Je! Hakimu wa dunia yote hatatenda haki?" Ibrahimu aliuliza si mara moja tu, bali mara nyingi. Akiongeza ujasiri zaidi katika maombi yake alipokuwa anakubaliwa, aliendelea hadi alipopata uhakikisho kwamba ikiwa hata watu kumi waadilifu wangepatikana humo jijini, basi jiji hilo lingeokolewa. {MTC 11.4}

Upendo kwa roho zinazoangamia uliuhisha moyo wa Ibrahimu zinazoangamia. Ingawa alichukia dhambi za mji huu mpotovu, alitamani kwamba wenye dhambi waokolewe. Matamanio yake ya kina kwa Sodoma inaonyesha dukuduku ambayo tunapaswa kuwa nayo kwa wale wasiotubu. Tunapaswa kuthamini chuki ya dhambi, lakini huruma na upendo kwa mwenye dhambi. Kila mahali tumezungukwa na roho zinazoshuka na kwenda kwenye uharibifu usio na tumaini, uharibifu mbaya sana kama ule ulioipata Sodoma. Kila siku mlango wa rehema unafungwa kwa baadhi ya watu. Kila saa inayoenda kwa Mungu, kuna watu wanatumbukia mahali ambapo rehema inashindwa kuwafikia. Ziko wapi basi sauti zenye maonyo na kusihi, zinazomtaka mwenye dhambi aikimbie adhabu hii ya kutisha? Je, ipo wapi mikono iliyonyooshwa ili kumrudisha mtu huyu kutoka katika kifo? Je, wako wapi wale ambao kwa unyenyekevu na imani wanadumu kumsihi Mungu kwa ajili yake?— PP, 139, 140 . (1890) MTC 12.1

**Wakristo Wanaweza Kuathiri Sana Miji.—** Ikiwa Mungu angeokoa Sodoma kwa ajili ya watu kumi waadilifu, Je, ni mvuto gani wa wema ambao ungeenda nje kwa sababu ya uaminifu wa watu wa Mungu ikiwa kila mtu anayelitaja Jina hilo la Kristo alikuwa amevikwa na haki Yake Kristo pia?— ST, Mei 2, 1895 ( In Heavenly Places, 104 ). MTC 12.2

## NINAWI

**Wengi Wataitikia Wito wa Mungu.—** Ninawi, japokuwa ulikuwa mji wenye uovu uliokithiri, haukuwa umejitoa kikamilifu katika uovu. Yeye ambaye "huwatazama wanadamu wote" ( Zaburi 33:13 ) na "huona kila kitu cha thamani" ( Ayubu 28:10 ) na Yeye aliona katika jiji hilo watu wengi waliokuwa wakitafuta kitu kilicho bora na cha juu zaidi, na ambao, kama wangepewa nafasi ya kujifunza juu ya Mungu aliye hai, wangeyaacha matendo yao maovu na kumwabudu. Na hivyo kwa hekima Yake Mungu alijidhihirisha kwao kwa namna iliyo dhahiri kabisa, kiasi kwamba mtu hakuweza kukosea kuona, ili kuwaongoza, ikiwezekana, kwenye toba. {MTC 12.3}

Chombo kilichochaguliwa kwa kazi hii alikuwa ni nabii Yona, mwana wa Amitai. Kwa huyu Neno la Bwana likamjia, kusema, Ondoka, uende Ninawi, mji ule mkubwa, ukapige kelele juu yake; kwa maana uovu wao umepanda juu mbele Zangu" ( Yona 1:1, 2 ). ...... {MTC 13.1}

Yona alipoingia mjini, mara moja alianza "kupaza sauti dhidi ya mji" na ujumbe huu, "Bado siku arobaini Ninawi utaangamizwa" ( Yona 3:4 ). Alikwenda kutoka mtaa hadi mtaa, akipiga sauti ya onyo. {MTC 13.2}

Ujumbe huo haukutoka bure. Kilio kilichovuma katika mitaa ya jiji hilo lisilomcha Mungu kilipitishwa kutoka mdomo hadi mdomo hadi wakaaji wote waliposikia tangazo hilo la kushtua. Roho wa Mungu alisukuma ujumbe huo

nyumbani kwenye kila moyo na kusababisha watu wengi kutetemeka kwa sababu ya dhambi zao na kutubu kwa kujidhili/kujinyenyekesha kwa kina. — {PK, 265-270} (1917) MTC 13.3

## YERUSALEMU-UAMSHO WAKATI WA MFALME YOSIA

**Mguso, Athari na Mvuto wa Viongozi Havipaswi Kudharauliwa.—** Ilikuwa ni lazima kwa mfalme [Yosia] kumwachia Mungu matukio ya wakati ujao; yeye hangeweza kubadilisha amri za milele za Yehova. Lakini katika kutangaza hukumu za kulipiza kisasi cha Mbinguni, Bwana hakuwa ameondoa fursa ya toba na matengenezo; na Yosia, alitambua katika jambo hili na kuwa tayari kuwa upande wa Mungu kuzichanganya hukumu Zake kwa rehema ili zisiwe kali sana, akaazimia mara moja kufanya yote awezayo ili kuleta matengenezo yaliyoazimiwa. Papo hapo alifanya mikakati ya kuitisha kusanyiko kubwa ambalo wazee na waamuzi wa Yerusalemu na Yuda walialikwa, pamoja na watu wa kawaida. Hawa, pamoja na makuhani na Walawi, walikutana na mfalme katika ua wa hekalu. {MTC 13.4}

Kwenye kusanyiko hili kubwa mfalme mwenyewe alisoma “masikioni mwao

Maneno yote ya kitabu cha Agano kilichoonekana katika nyumba ya Bwana” ( 2 Wafalme 23:2 ). Msomaji wa kifalme aliathiriwa kwa kina na Maneno haya, naye alitoa ujumbe wake kwa kwa moyo uliovunjika, na wenye sikitiko. Wasikilizaji wake waliguswa moyo sana. Nguvu ya hisia iliyofunuliwa katika uso wa mfalme, uzito wa ujumbe wenyewe, onyo la hukumu zinazokaribia—yote haya yalikuwa na matokeo yake, na wengi waliazimia kuungana na mfalme katika kutafuta msamaha toka kwa Mungu. {MTC 13.5}

Sasa Yosia alipendekeza kwamba wale walio na mamlaka ya juu zaidi waungane na watu katika kufanya maagano mazito mbele za Mungu ili kushirikiana wao kwa wao katika jitihada ya kuweka maazimio kwaajili ya matengenezo. “Mfalme akasimama karibu na nguzo, akafanya agano mbele za Bwana, kumfuata Bwana, na kuyashika maagizo Yake, na shuhuda Zake, na amri Zake, kwa moyo wake wote, na kwa roho yake yote, na kuyathibitisha Maneno ya agano hilo yaliyoandikwa katika kitabu hicho; nao watu wote wakalikubali Agano lile” Jibu lilikuwa la kutia moyo zaidi kuliko mfalme alivyokuwa amedhamiria: " Watu wote walisimama katika Agano" ( mstari wa 3 ). {MTC 14.1}

Katika matengenezo yaliyofuata, mfalme alielekeza umakini wake kwenye uharibifu wa kila kiashiria cha ibada ya sanamu iliyobakia. ... Kwa muda mrefu sana wenyeji wa nchi walikuwa wamefuata desturi za mataifa jirani katika kusujudia sanamu za miti na mawe, na ilionekana kuwa nje ya uwezo wa mwanadamu kuondoa kila kiashiria cha maovu haya. Lakini Yosia aliendelea na jitihada zake za kuisafisha nchi. Kwa ujasiri alikutana na ibada ya sanamu na kuwaua “makuhani wote wa mahali pa juu”; tena wenye pepo la utambuzi, na wachawi, na vinyago, na machukizo yote yaliyoonekana katika nchi ya Yuda na Yerusalemu, Yosia aliyaondoa yote, ili kuyathibitisha Maneno ya torati. ambayo yaliandikwa katika kitabu ambacho Hilkia kuhani alikiona katika nyumba ya Bwana” ( mistari 20, 24 ).— {PK, 400, 401} . (1917) MTC 14.2

## AGANO JIPYA

**Nenda Kwa Watu.—** Agizo kuu la utume wa injili ni Hati ya Utume mkuu wa ufalme wa Kristo Inayofafanua dhamiri ya timu, wigo wa operesheni au utendaji, malengo, na kujitoa kikamilifu kwa wahusika . Wanafunzi walipaswa kufanya kazi Kwa bidii kwa ajili ya roho za watu, wakitoa mwaliko wa rehema kwa watu wote. Hawakupaswa kungoja watu waje kwao; bali walipaswa kwenda kwa watu wakiwa na ujumbe wao.— {AA,28} . (1911) MTC 14.3

**Huduma ya Kristo duniani Ilionyesha Utume wa Injili.—** Yeye aliye nuru na uzima wa injili alifanyika mwili na kukaa kati yetu. Alikuwa ni Mwenye huruma kwa jamii ya wanadamu (ubinadamu wote), Alilisha wenye njaa, aliponya wagonjwa, na akazunguka katika miji yote nchini akiwatendea watu wema. Kazi zetu zote zinapaswa kutendwa ndani ya Kristo. Kwa kuwa washiriki wa asili Yake ya Uungu, wafuasi Wake wanapaswa kufanya kazi Zake. Huduma ya Kristo kwa wanadamu ilikuwa tafsiri ya agizo Lake kuu kwa wanafunzi, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."— Manuscript 1, 1908 ( Manuscript Releases 5:213, 214 ). MTC 15.1

**Yesu Alifundisha kwa mifano.—** Ilikuwa katika kukutana ana kwa ana na kuwasiliana nao binafsi na kisha kufanya nao ushirika, ndipo ambapo Yesu aliwazoeza na kuwaongoza wanafunzi Wake. Wakati Fulani aliwafundisha, akiwa ameketi kati yao mlimani; wakati fulani kando ya bahari, au katika kutembea pamoja nao njiani, alifunua mafumbo na siri za ufalme wa Mungu. Hakutoa mahubiri tu kama wanadamu wanavyofanya leo. Popote ambapo mioyo ilikuwa wazi kupokea ujumbe wa Mungu, alifunua Kweli za njia ya wokovu. Hakuwaamuru wanafunzi Wake kufanya hili au lile, bali alisema, "Nifuate Mimi." Katika safari Zake katika mashamba na miji, aliwachukua

wanafunzi pamoja Naye, ili wapate kuona jinsi anavyowafundisha watu. Aliungamanisha shauku na makusudi yao na Yake, na nao wakaungana Naye katika kazi hiyo.— {DA, p.152} . (1898) MTC 15.2

**Yesu Alichangamana na Wale Aliowatumikia.—**Wakati wa huduma Yake ya hapa duniani Kristo alianza kubomoa ukutauliokuwa unatenganisha kati ya Wayahudi na wale wasio Wayahudi, (walijulikana kama watu wa mataifa) na kuhubiri wokovu kwa wanadamu wote. Ingawa alikuwa Myahudi, alichangamana kwa uhuru na Wasamaria, akionyesha hakuna sababu ya kuwa na hizo desturi za Mafarisayo za Kiyahudi kuhusu watu hawa waliodharauliwa. Alilala chini ya paa zao, alikula kwenye meza zao, na kufundisha katika mitaa na barabara zao.—
{AA, 19} . (1911) MTC 15.3

**Yesu Alichagua Kapernaumu kwa faida yake ya Kiunjilisti.—** Wakati wa huduma Yake duniani Mwokozi alichukua fursa iliyokuwa kwenye njia kuu za kusafiria. Ilikuwa ni katika Kapernaumu ambapo Yesu aliishi katika vipindi vya safari Zake, akienda na kurudi mjini, nao ukaja kujulikana kuwa "mji Wake Mwenyewe." Mji huu ulichukuliwa kama ndiyo kitovu cha kazi ya Mwokozi. Ulikuwa katika ya njia kuu ya kusafiri, kwani ulikluwae ulikuwa kiungo kilichounganisha barabara kuu kutoka Damaski hadi Yerusalemu na Misri, hadi Bahari ya Mediterania. Watu kutoka nchi mbalimbali walipita katikati ya jiji au walikatisha safari zao na kupumzika wakiwa wakienda huku na huko. Hapa Yesu angeweza kukutana na mataifa yote na nyadhifa zote, matajiri na wakuu, pamoja na maskini na wa hali ya chini; na masomo Yake yangepelekwa katika nchi nyingine na katika kaya nyingi. Uchunguzi wa unabii ungeweza kuleta shauku na

kuwasisimua watu wapitapo hapa; na kisha umakini ungeelekezwa kwa Mwokozi, na misheni Yake ingeletwa mbele ya ulimwengu.— {9T:121} . (1909) MTC 16.1

## Miji ya Agano Jipya

## YERUSALEMU

**Injili Itatangazwa Katika Hali Zote.—** Kristo aliwaambia wanafunzi Wake kwamba wangeanzia kazi yao hapo Yerusalemu. Mji ule ulikuwa ni uwanja wa dhabihu ya ajabu kwa ajili ya wanadamu . Hapo, alikuwa amevaa vazi la ubinadamu, hapo alikuwa ametembea na kuzungumza na wanadamu, na wachache walikuwa wametambua jinsi mbingu ilivyoikaribia dunia (iliigusa!). Hapo alikuwa amehukumiwa na kusulubiwa. Katika Yerusalemu kulikuwa na wengi walioamwamini Yesu wa Nazareti kwa siri, kwamba Ndiye Masihi, na kulikuwa na wengi ambao walikuwa wamedanganywa na makuhani na watawala. Kwa hawa injili lazima itangazwe. Walipaswa kuitwa kwenye toba. Ukweli wa ajabu kwamba ni kupitia Kristo pekee yake, ndiyo kungeweza kupatikana ondoleo la dhambi ulipaswa kuwekwa wazi. Na ilikuwa wakati ambapo Yerusalemu yote imeamshwa na matukio haya yenye kusisimua majuma machache yaliyopita, ndipo mahubiri ya wanafunzi yangevutia sana.— {AA, 31, 32} . (1911) MTC 16.2

**Wanafunzi waliwaheshimu Wengine kwa Ajili ya Nafsi Zilizoongoka.—** Ni hapa katika Yerusalemu, iliyokuwa ngome kuu ya Dini ya Kiyahudi (Judaism), ndio maelfu walikiri waziwazi imani yao kwa Yesu wa Nazareti kuwa Ndiye Masihi.( MTC 17.1)

Wanafunzi walishangazwa na kushangilia kwa wingi wa mavuno ya roho. Hawakuona mkusanyiko huu wa ajabu kuwa tokeo la jitihada zao wenyewe; walitambua kwamba

walikuwa wakiingia yalipo matunda ya kazi za watu wengine.— {AA, 44} (1911) MTC 17.2

## ANTIOKIA YA SYRIA

**Jina "Ukristo" Lilitokana na ushuhudiaji Mjini uliojikita katika Kristo.—** Katika jiji lenye watu wengi la Antiokia, [mtume] Paulo aliliona eneo zuri la kufanya kazi ya utume. Elimu yake, hekima, na bidii yake vilishinkiza mvuto wenye nguvu juu ya wakazi na watu waliokuwa wageni waliokuwa wakitembelea jiji hilo la kitamaduni mara kwa mara; na alithibitisha msaada ambao Barnaba aliuhitaji. Kwa mwaka mmoja wanafunzi hao wawili walifanya kazi kwa umoja katika huduma ya uaminifu, wakiwaletea wengi maarifa ya kuokoa ya Yesu wa Nazareti, Mkombozi wa ulimwengu.
{MTC 17.3}

Ilikuwa huko Antiokia ambapo wanafunzi waliitwa Wakristo kwa mara ya kwanza. Walipewa jina hilo kwa sababu Kristo alikuwa mada na chanzo kikuu cha mahubiri, mafundisho, na mazungumzo yao.— {AA 156, 157} . (1911) MTC 17.4

**Washiriki wa Kanisa la mijini Kujiunga na Wengine katika Huduma.—** Mfano wa wafuasi wa Kristo huko Antiokia unapaswa kuwa msukumo kwa kila muumini anayeishi katika miji mikuu ya ulimwengu leo. Ingawa ni taratibu wa Mungu kwamba watenda kazi waliochaguliwa na kuwekwa wakfu wenye talanta wawekwe katika vituo muhimu vya watu ili kuongoza juhudi za umma, pia ni kusudi lake kwamba washiriki wa kanisa wanaoishi katika miji hii watumie talanta zao walizopewa na Mungu. katika kufanya kazi kwa ajili ya roho. Kuna Baraka tele ambazo zimehifadhiwa kwa wale wanaojitoa kikamilifu kwa wito wa Mungu. Wakati wafanyakazi hao wanapoweka jitihada ili kuleta roho Kwa Yesu, watawapata wengi ambao hawangeweza kufikiwa kwa njia nyingine yoyote, wakiwa

tayari kuitikia jitihada zao binafsi zenye akili katika kuwafikia. (MTC 17.5)

Kazi ya Mungu duniani Leo inahitaji wawakilishi hai wa Ukweli wa Biblia. Wachungaji waliowekwa mikono/wakfu peke Yao hawatoshi kiufanya kazi ya kuonya miji mikubwa. Mungu hawaiti wachungaji tu , bali hata matabibu, wauguzi, wainjilisti wa vitabu , watenda kazi wa Biblia, na walei wengine waliojiweka wakfu, na wenye talanta mbalimbali na walio na maarifa ya Neno la Mungu, na wanaojua nguvu ya neema Yake, kiasi cha kuzingatia mahitaji ya Miji ambayo haijapewa onyo. Muda unapita haraka, na kuna mengi ya kufanya. Kila wakala lazima uwekwe sawa ili kuanza operesheni kazi kusudi fursa zilizopo ziweze kuboreshwa kwa hekima. — {AA158, 159 }. (1911) MTC 18.1

**Kuanzishwa kwa Makanisa Huimarisha Washiriki Wapya.—** Siku iliyofuatia kupigwa mawe kwa Paulo, mitume waliondoka kwenda Derbe, ambako taabu zao zilibarikiwa, na roho nyingi ziliongozwa kumpokea Kristo kama Mwokozi. Lakini "walipokwisha kuihubiri Injili katika mji ule, na kuwafundisha wengi," Paulo wala Barnaba hawakuridhika kuchukua kazi mahali pengine bila kuthibithisha/kuiimarisha imani ya waongofu ambao watalazimika kuwaacha peke yao kwa muda, mahali fulani ambapo walifanya kazi hivi karibuni. Na hivyo, bila kuogopa hatari, "walirudi tena Listra, na Ikonio, na Antiokia, wakizithibitisha roho za wanafunzi, na kuwaonya wadumu katika imani." Wengi walikuwa wamekubali habari njema za injili na hivyo walikuwa wamejianika wazi kwa lawama na upinzani. Mitume hao walitaka kuwaimarisha katika imani, ili kazi njema iliyofanyika ipate kudumu. {MTC 18.2}

Kama mada muhimu katika ukuaji wa kiroho wa waongofu wapya mitume walikuwa waangalifu kuwazungushia ulinzi wa utaratibu wa injili. Makanisa yalipangwa ipasavyo katika sehemu zote za Likaonia na Pisidia ambako kulikuwa na waumini. Maafisa waliteuliwa na kuwekwa katika kila kanisa, na utaratibu ufaao na mfumo, ukaanzishwa kwa ajili ya uendeshaji wa mambo yote yanayohusu hali njema ya kiroho ya waamini.— {AA185
. (1911) MTC 18.3}

## THESALONIKE

**Paulo Alifundisha Kweli Zilizojengwa katika Msingi wa Maandiko.—** kwa ujasiri mtakatifu Paulo alitangaza injili katika sinagogi pale Thesalonike, mafuriko ya nuru yalitupwa kwenye maana halisi ya ibada, desturi na sherehe zinazohusiana na huduma ya Patakatifu. Alibeba mawazo ya wasikilizaji wake juu zaidi ya huduma ya duniani na kwenda kwenye huduma ya Kristo katika Patakatifu pa mbinguni, hadi wakati ambapo, akiwa amemaliza kazi Yake ya upatanishi na Maombezi, Kristo angekuja tena kwa nguvu na utukufu mkuu, na kusimamisha ufalme Wake duniani. Paulo alikuwa anaamini katika ujio wa pili wa Kristo; kwa uwazi sana na kwa nguvu aliwasilisha Ukweli kuhusu tukio hili, hivi kwamba katika akili za wengi waliosikia hubiri hili uliwekwa mguso ambao haukuchakaa kwenye mawazo yao.
{MTC 19.1} Kwa Sabato tatu zilizofuatana Paulo aliwahubiria Wathesalonike, akihojiana nao kutoka katika Maandiko kuhusu uhai, kifo, ufufuo, kazi ya Yesu anayofanya sasa, na utukufu wa wakati ujao wa Kristo, "Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu" ( Ufunuo 13:8 ) Alimwinua Kristo, ambaye kwa ufahamu sahihi wa huduma Yake ambayo ni ufunguo unaofungua Maandiko ya Agano la Kale, anatupa ufikiaji wa hazina zetu nyingi. {MTC 19.2}

Kweli za injili zilipotangazwa hivyo katika Thesalonike kwa nguvu kubwa, usikivu wa makutano makubwa ulikamatwa. “Baadhi yao wakaamini, wakashikamana na Paulo na Sila; na umati mkubwa wa Wayunani waliomcha Mungu, na wanawake wengi si wachache.”— ,{AA228, 229} . (1911) MTC 19.3

## ATHENS (Athene)

**Watu Wasiohudhuria Kanisani, hawapaswi Kupuuzwa—** Alipokuwa akiwangojea Sila na Timotheo, Paulo hakukaa kivivu bila kazi. “Aliohojiana/alibishana na Wayahudi katika sinagogi na watu watauwa, na sokoni kila siku pamoja na wale waliokutana naye.” Lakini kazi yake kuu katika Athene ilikuwa kupeleka habari za wokovu kwa wale ambao hawakuwa na uelewa wenye busara juu ya Mungu na kusudi Lake kwa ajili ya jamii ya wanadamu iliyoanguka. Mtume huyo angekutana na upagani katika umbo lenye hila na kuvutia hivi karibuni.— {AA, p. 234, 235} . (1911) MTC 19.4

**Kuwahubiri wenye Hekima na watu walio na visomo vikubwa.—** Wao [wanafalsafa wakuu wa mahali hapo] ... walimpeleka [Paulo] hadi kwenye Kilima cha Mars. Sehemu hii ilikuwa ni mojawapo ya sehemu takatifu sana katika Athene yote, na kumbukumbu zake na ushirikina wake ulipafanya paonekane kuwa na heshima ya kishirikina ambayo katika akili za wengine ilileta hofu. Ni mahali hapa ndipo ambapo mara nyingi mambo yanayohusiana na dini yalizingatiwa kwa kujadiliwa kwa uangalifu na wanaume ambao walikuwa waamuzi wa mwisho juu ya masuala muhimu zaidi ya kiadili na ya kiraia. {MTC 20.1}

Hapa, mbali na kelele na msongamano wa njiapanda inayoenda mahali pengi, mahali penye msongamano wa

watu, na ghasia za majadiliano * ya uasherati na ukahaba, mtume huyo angeweza kusikilizwa bila kukatizwa. Alizungukwa na watunzi wa mashairi, wasanii, na wanafalsafa—wasomi na wenye hekima wa Athene, ambao walizungumza naye hivi: "Je! kwa maana waleta maajabu masikioni mwetu; basi tungetaka kujua mambo haya ni nini."— { AA, 236 }. (1911) MTC 20.2

**Utamaduni wa Wenyeji Uliathiri Ujumbe wa Paulo.—** Huku akiwa amenyoosha mkono kuelekea hekalu lililojaa sanamu, Paulo aliumimina mzigo wa moyo wake, na kufichua imani yenye makosa na isiyo na busara ya dini ya Waathene. Wasikilizaji wake wenye hekima zaidi walistaajabu waliposikiliza hoja zake. Alionyesha kuwa na ufahamu wa kazi zao za sanaa, fasihi zao, na dini yao. Akielekeza mkono wake kwenye sanamu zao, alitangaza kwamba Mungu hangeweza kufananishwa au kulinganishwa na ubunifu wa mwanadamu. Sanamu hizo za kuchongwa hazingeweza hata kwa udogo, kuwakilisha utukufu wa Yehova. Aliwakumbusha kwamba picha hizi hazikuwa na uhai, bali zilidhibitiwa na kutegemezwa kwa nguvu za mwanananadamu, zilijongea pale tu mikono ya wanadamu ilipozisogeza; na kwa hivyo watu waliokuwa wakiziabudu walikuwa bora zaidi ya kile ya zile sanamu walizokuwa wakiziabudu. {MTC 20.3}

Paulo alivuta akili za wasikilizaji wake waabudu-sanamu kupita mipaka ya dini yao ya uongo kwenye mtazamo wa Kweli wa Uungu, ambaye alikuwa amemwita "Mungu Asiyejulikana."— {AA, p . (1911) MTC 21.1}

## KORINTHO

**Badilisha Mbinu Ikiwa Matokeo Ni Madogo.—** Katika karne ya kwanza ya Enzi ya Ukristo Korintho lilikuwa mojawapo ya majiji makuu yaliyoongoza, si katika Ugiriki tu, bali ulimwenguni kote. Wagiriki, Wayahudi, na Warumi, pamoja na wasafiri kutoka kila nchi, walijaa katika

barabara zake, wakiwa na hamu ya kufanya biashara na kujipatia starehe. Hiki kilikuwa kituo kikuu cha kibiashara, kilicho katika njia rahisi ya kufikiwa na sehemu zote za Himaya ya Rumi, na hivyo palikuwa mahali muhimu pa kuweka kumbukumbu za Mungu na Ukweli Wake. {MTC 21.2}

Miongoni mwa Wayahudi waliokuwa wamekaa Korintho walikuwa Akila na Prisila, ambao baadaye walikuja kujulikana kuwa wafanyakazi wenye bidii kwa ajili ya Kristo. Akiwa amefahamu tabia za watu hao, Paulo 'alikaa pamoja nao. {MTC 21.3}

Mwanzoni kabisa mwa kazi yake katika njia hii ya kusafiri, Paulo aliona kila upande vizuizi vizito kwa maendeleo ya kazi yake. Jiji lilikuwa karibu kabisa kujidondosha katika ibada ya sanamu. Venus (Zuhura) alikuwa mungu wa kike kipenzi, aliyeshabikiwa sana, na pamoja na ibada ya Zuhura ziliunganishwa ibada na sherehe nyingi zenye kufedhehesha. Wakorintho walikuwa wamejulikana, hata miongoni mwa wapagani, kwa upotofu wao wa maadili uliotisha sana. Walionekana kuwa na mawazo kidogo au kujali chochote zaidi ya anasa na kujiachia tu saa yote kwa mambo ambayo hayakupaswa kutiliwa umakini. {MTC 21.4} Katika kuhubiri injili Korintho, mtume alifuata njia tofauti na ile ambayo ilikuwa imetia alama kazi yake katika Athene. Akiwa katika mji huo wa mwisho (Athene), alikuwa ametaka kutoa hubiri lake kwa kuendana na tabia ya wasikilizaji wake; alikuwa amekutana na mantiki na mantiki (logic with logic), sayansi na sayansi, falsafa na falsafa. Alipofikiria juu ya mudauliotumika hivyo, na kugundua kwamba mafundisho yake huko Athene yalikuwa na matunda kidogo tu, ndipo alipoamua kufuata mpango mwingine wa kazi huko Korintho katika juhudi zake za kukamata usikivu wa wazembe na wasiojali. Aliazimia kuepuka mabishano ya

kina na mijadala, na “kutojua lolote” miongoni mwa Wakorintho “ila Yesu Kristo, na Yeye aliyesulubiwa.” Angewahubiria “si kwa maneno yenye kushawishi ya hekima ya mwanadamu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu” ( 1 Wakorintho 2:2, 4 ). {MTC 21.5}

Yesu, ambaye Paulo alikuwa karibu kumwasilisha mbele ya Wagiriki katika Korintho kuwa Ndiye Masihi, alikuwa Myahudi wa asili ya hali ya chini, aliyelelewa katika mji wenye msemo mashuhuri kwaajili ya uovu wake (Nazareti). Alikuwa amekataliwa na taifa Lake Mwenyewe na hatimaye kusulubiwa kama mhalifu. Wagiriki waliamini kwamba kulikuwa na haja ya kuinua jamii ya wanadamu , lakini waliona kubobea katika masomo ya falsafa na sayansi ndiyo njia pekee ya kufikia mwinuko na heshima ya kweli. Je, Paulo angeweza kuwaongoza kuamini kwamba imani katika uwezo wa Myahudi huyu asiyejulikana ingeinua na kuwezesha kila nguvu iliyomo katika kiumbe (mwanadamu)? {MTC 22.1}

Kwa mawazo ya watu wengi wanaoishi wakati huu, msalaba wa Kalwari umezungukwa na kumbukumbu takatifu. Ushirika mtakatifu umeunganishwa na matukio ya kusulubiwa. Lakini katika siku za Paulo msalaba ulichukuliwa kwa hisia za kuchukiza na kutisha. Kumwinua jambo hili lingeleta dhihaka na upinzani kutoka kwa watu. MTC 22.2

Paulo alijua vizuri jinsi ujumbe wake ungechukuliwa na Wayahudi na Wagiriki wa Korintho. “Sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa,” alikiri, “kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi” (1 Wakorintho 1:23 ). Miongoni mwa wasikilizaji wake Wayahudi kulikuwa na wengi ambao wangekasirishwa na ujumbe ambao alikuwa karibu kuutangaza. Kwa makadirio ya Wagiriki maneno yake yangekuwa upumbavu na upuuzi mtupu. Angetazamwa

kuwa mwenye akili dhaifu kwa kujaribu kuonyesha jinsi msalaba ungeweza kuwa na uhusiano wowote na kuinuliwa kwa jamii au wokovu wa wanadamu.— {AA. 243-245 }. (1911) MTC 22.3

**Binadamu Anapaswa Kufichwa Nyuma ya Uungu.— Jitihada** za mtume [Paulo] hazikufungiwa katika kuzungumza hadharani tu; kulikuwa na wengi ambao hawakuweza kufikiwa kwa njia hiyo. Alitumia muda mwingi katika kazi ya nyumba kwa nyumba, na hivyo alichukua muda wake kufurahia ushirika aliokutana nao kwenye mizunguko ya majumbani mwa watu. Aliwatembelea wagonjwa na wenye huzuni, akiwafariji walioteseka, na kuwainua walioonewa. Na katika yote aliyosema na kufanya alililiinua/alililitukuza Jina la Yesu. Hivyo alijitaabisha, "katika udhaifu, na hofu, na kutetemeka sana" ( 1 Wakorintho 2:3 ). Alitetemeka kwa kuhofia kwamba mafundisho yake yasije yakaacha mguso moyoni wa mambo ya kibinadamu badala ya yale ya Bwana.— {A A, 250
.1911)MTC 22.4

**Mdogo Zaidi Anaweza Kuwa Ukumbusho wa Ukuu wa Mungu.—** Jitihada za Paulo huko Korintho hazikutoka bila matunda. Wengi waliacha kuabudu sanamu na kumtumikia Mungu aliye hai, na kanisa kubwa likaanzishwa chini ya bendera ya Kristo. Wengine waliokolewa kutoka miongoni mwa watu wa mataifa waliotawanyika mbali zaidi na wakawa ukumbusho unaoonekana vizuri, wa rehema ya Mungu na ufanisi wa damu ya Kristo itakasayo dhambi.— { A A, 252.1911 MT 23.1

## EFESO

**Upinzani Ukipata Nguvu sana, Badilisha welekeo.—** Kama ilivyokuwa desturi yake, Paulo alikuwa ameanza kazi yake huko Efeso kwa kuhubiri katika sinagogi la Wayahudi.

Aliendelea kufanya kazi huko kwa muda wa miezi mitatu, “akijadiliana na kuwashawishi katika mambo yanayohusu ufalme wa Mungu.” Mara ya kwanza alikutana na mapokezi mazuri; lakini kwa kama ilivyokuwa katika maeneo mengine, haikuchukua muda kwake kupingwa vikali. "Wapingaji wakawa wagumu, wasiamini, bali wakaitukana Njia ile mbele ya mkutano." Walipoendelea kukataa injili, mtume aliacha kuhubiri katika sinagogi. {MTC 23.2}

Roho wa Mungu alikuwa amefanya kazi pamoja kupitia kwa Paulo katika kazi yake kwa ajili ya watu wa nchi yake. Uthibitisho wa kutosha ulikuwa umetolewa ili kuwasadikisha wote waliotamani kwa unyoofu kuujua Ukweli.— {A A, 285.1911) MTC 23.3

## RUMI

**Makanisa Yaliyopo Yapande/Yaanzishe Makanisa Mapya.—** Kuona imani ya Kikristo ikiwa imesimikwa kwa uthabiti kwenye kila kitovu kikuu cha ulimwengu unaojulikana lilikuwa mojawapo ya matumaini yake [Paulo] ambayo moyo wake uliyapenda, na mikakati aliyoithamini sana. Kanisa lilikuwa tayari limepangwa huko Rumi, na mtume alitamani kupata ushirikiano wa watu huko katika kazi ambayo alitarajia kuikamilisha. Ili kuandaa njia kwa ajili ya kazi yake Miongoni mwa ndugu hao, ambao walikuwa bado wageni, alizungumza nao kwa barua, akitangaza kusudi lake la kutembelea Rumi, na pia kwa msaada wao wa kupanda kiwango cha msalaba katika Hispania.— Sketches from the Life of Paul. , 187 . (1883) MTC 23.4

**Paulo Mfungwa Bado Aliendelea Kushuhudia.—** Roma ilikuwa jiji kuu la ulimwengu wa wakati huo. Makaisari wenye majivuno walikuwa wakitoa sheria kwa karibu kila taifa duniani. Mfalme na wasaidizi wake, aidha hawakumjua Mnazareti mnyenyekevu au walimtazama kwa

chuki na dhihaka. Na bado katika wakati wa miaka miwili injili ilipata kuenezwa kutoka katika nyumba ya hali ya ufukara ya mfungwa hadi kwenye kumbi za kifalme. Paulo yuko katika vifungo kama mtenda maovu; lakini “Neno la Mungu halifungwi” ( 2 Timotheo 2:9 ).— { A A, 461, 462 .1911) MTC 24.1

**Viongozi wa Umma Wanaweza kuhamasisha Uwezekano wa Kueneza Injili.—** Kupitia upendeleo wa wale waliokuwa wanamsimamia Paulo kama mabwana magereza, aliruhusiwa kukaa katika nyumba ya hali yenye samani na nafasi ya kutosha kuwa na wageni, mahali ambapo angeweza kukutana kwa uhuru na marafiki zake na pia kuwasilisha Ukweli kila siku kwa wale waliokuja kusikiliza. Hivyo kwa muda wa miaka miwili aliendelea na kazi yake ya injili, “akihubiri ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri wote, asikatazwe na mtu.”— { AA, 453 .1911) MTC 24.2 **Waongofu Katika nafasi za uwajibikaji au utawala, Wanaweza Kushuhudia Mahali Walipo.—** Sio tu kwamba waongofu waliletwa kwenye Ukweli wa injili katika nyumba ya Kaisari, bali baada ya kuongoka kwao walibaki katika nyumba hiyo. Hawakuhisi uhuru wa kutelekeza kituo chao cha kazi kwa sababu mazingira yao hayakuwa ya kupendeza tena. Ukweli ulikuwa imewafikia huko, na huko walibaki, na kwa mtindo wao wa maisha uliobadilika na tabia zao zilizobadilika kushuhudia nguvu ibadilishayo ya imani mpya.— ( A A, 466 . (1911) MTC 24.3

**SURA YA 2- Kazi Muhimu Katika Wakati Huu Mtazamo wa**

**Mungu Unakuwa Mtazamo Wetu. —** Lo, laiti tungeweze kuona mahitaji ya miji hiyo Kama jinsi Mungu anavyoyaona! Kwa wakati Kama huu kila mkono unapaswa kuajiriwa katika kazi hii. Bwana anakuja; mwisho umekaribia, naam, unafanya haraka Sana! Baada ya muda kidogo hatutaweza kufanya kazi kwa uhuru ambao tunaufurahia sasa. Matukio ya kutisha yako mbele yetu, na kile tunachofanya lazima tukifanye kwa haraka— {9T:101. (1909) MTC 25.1

**Wengi Hawabebi Mzigo Kwa Ajili ya Roho za watu wengine. —** Miji mikubwa ilipaswa kufanyiwa kazi mara tu makanisa yalipopokea nuru, lakini makanisa mengi hayajabeba mzigo wowote Kwa ajili ya roho za watu kwenye miji, na Shetani, akiwaona wakiwa katika hatari ya kuteleza kirahisi kwenye majaribu yake, ameuharibu uzoefu wao. Mungu anawaomba watu Wake watubu, wageuzwe, na kuurudia upendo wao wa kwanza, ambao wamepoteza kwa kushindwa kufuata nyayo za Mkombozi aliyejitoa dhabihu Mwenyewe. —
{9T:140. (1909) MTC 25.2

**Umakini Mdogo Sana Umetolewa Kwa Miji. —** Tazama miji, na hitaji lao la injili! Hitaji la watenda kazi wenye bidii miongoni mwa wingi wa miji limewasilishwa mbele yangu kwa zaidi ya miaka ishirini. Ni nani wanaobeba mzigo wa miji mikubwa? Wachache wamehisi mzigo huo, lakini Kwa kulinganisha na hitaji kuu na fursa nyingi kuna umakini mdogo umetolewa kwa kazi hii. — {9T.97, 98. (1909) MTC 25.3

**Kazi katika Miji Bado Iko Mbali na Mpango wa Mungu. —** Umuhimu wa kutoboa njia ili kufikia majiji makubwa bado umekuwa ukiwekwa mbele yangu. Kwa miaka mingi Bwana amekuwa akihimiza juu yetu jukumu hili, na bado ni machache tu yametimizwa katika vituo vyetu vikuu vyenye idadi kubwa ya watu ukilinganisha na maono haya. Ikiwa hatutachukua kazi hii kwa njia ya kuvalia njuga, basi Shetani atazidisha magumu ambayo hayatakuwa rahisi kuyashinda. Tuko nyuma Sana katika kufanya kazi inayopaswa kufanywa katika miji hii iliyopuuzwa Kwa muda mrefu. Kazi sasa itakuwa ngumu zaidi kuliko ilivyokuwa katika miaka michache iliyopita. Lakini tukiichukua kazi hiyo katika Jina la Bwana, vizuizi vitavunjwa, na ushindi ulioamuliwa utakuwa wetu.— {letter 148, 1909 ( MM, 301, 302 ). MTC 25.4

**Maombi ya dhati na Bidii yanahitajika Kwa ajili ya miji. —** Tunabeba mzigo mwepesi Sana Kwa ajili ya nafsi ambazo hazijaokolewa. Hakukuwa na wakati ambapo ulimwengu ulituhitaji zaidi kuliko unavyotuhitaji sasa. Miji ambayo haijaonywa, inatuzunguka kila mahali. Roho zinaangamia, na tunafanya nini? Tunahitaji kuwa na mzigo moyoni kwaajili ya hizi roho, mzingo ambao hatujawahi kuwa na uzoefu nao. ... MTC 26.1

Tunauamini Ukweli huu nusu nusu. Kama tungeuamini Ukweli huu kama ulivyo, tungeonekana katika maombi na kufanya kazi kwa bidii zaidi, katika kujaribu kuzibeba Kweli hizi kwa wakazi wa miji ya nchi yetu. Sasa Mungu anatuita tufungue kazi yenye nguvu katika majiji.— {manuscripts 23, 1910 . MTC 26.2

**Miji Inayopaswa Kufanyiwa Kazi Bila Kuchelewa.—** Ujumbe ambao nimeagizwa kubeba kwa watu wetu wakati huu ni, “Fanyeni kazi mijini bila kukawia, kwa maana wakati ni mfupi. Bwana ameweka kazi hii mbele yetu kwa

miaka ishirini iliyopita au zaidi. Kidogo kimefanywa katika maeneo machache, lakini mengi zaidi yanaweza kufanywa. Ninabeba mzigo mchana na usiku, kwa sababu ni machache sana yametimizwa ili kuwaonya wakazi wa vituo vyetu vikubwa vyenye idadi ya watu kubwa juu ya hukumu ambazo zitawashukia wavunjaji wa sheria ya Mungu.— {Letter 168, 1909 ( MM, 300 ). MTC 26.3

**Ujumbe Utolewe Haraka.—** Bwana amenionyesha kwamba kuna kazi ya kufanywa katika miji ambayo, ni kama haijaingiwa kabisa. Suala hili la kazi ya injili katika miji ni swali lililopo pamoja nasi. Hatupaswi sasa kuweka mikakati ya kazi zetu kufanywa kwa muda mrefu sana, na kwenye eneo kubwa sana. Ujumbe lazima upelekwe haraka. Ucheleweshо katika utekelezaji wa maagizo ya Bwana kuhusu kazi katika miji kumefanya kazi ya kufikia matabaka/madaraja yote kuwa ngumu zaidi. Kazi lazima ifanyike mara moja, na Bwana anawaita watenda kazi waliojiweka wakfu ambao watashugulika kwa dhati na bidii kulingana na nuru aliyotoa.— Letter 42, 1909 ( Ms 17:37 ). MTC 26.4

**Watendakazi Wanahitajika kila mahali.—** Popote ambapo watu wa Mungu wamewekwa, katika miji iliyosongamana/iliyoshonana, katika vijiji, au kati ya njia za mashambani, kuna uwanja wa misheni ya nyumbani, ambao wajibu wao huwekwa juu yao kwa utume wa Bwana wao. Katika kila jiji au makazi ambako Wakristo hukutana Ili kumwabudu Mungu, kuna wanaume na wanawake na watoto wanaopaswa kukusanywa kwenye zizi. Wengi hawajapata kamwe kusikia hotuba kuhusu Neno la Mungu.
— {Manuscript. 87, 1907 ( Ms.6:323 ). MTC 27.1

**Wokovu Lazima Utolewe kwa Wakazi wa mijini. —** Ninahisi wasiwasi mwingi ninapofikiria majiji ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Mchana na usiku mzigo huu uko juu yangu—miji lazima ifanyiwe kazi bila kukawia.

Ujumbe wa Ukweli wa sasa lazima upelekwe kwa wale ambao hawajausikia. ... MTC 27.2

Wokovu huu ni kwa ajili ya wakazi wa miji ambayo haijafanyiwa kazi. Wakati unapita kwa kasi hadi umilele, na miji hii bado miji hii ni kama haijaguswa. Kuna nguvu ambayo Roho wa Mungu anaweza kuwapa Ukweli. Nuru inapomulika akilini, usadikisho utaishika mioyo ambayo itakuwa na nguvu sana kuweza kupinga.— {letter 150, 1909 . MTC 27.}

**Ujumbe Kwa Wasikilizaji Walio Hukumiwa. —** Katika majiji yetu makubwa ujumbe ni kwenda Kama taa iwakayo. Mungu atainua watenda kazi Kwa ajili ya kazi hii, na malaika Wake watatangulia mbele yao. Mtu yeyote asiwazuie watu hawa kuhusu uteuzi wa Mungu. Msiwakataze. Mungu amewapa kazi Yao. Hebu ujumbe utolewe kwa nguvu nyingi sana ili wasikilizaji wasadikishwe.— {R &H, Septemba 30, 1902 ( Ev, 70 ). MTC 27.4

**Shetani Anapendezwa Kuona Maelfu Wangali Gizani.—** Maelfu ya watu katika miji yetu wameachwa gizani, na Shetani anapendezwa sana na kukawia; kwani ucheleweshaji huu unampa fursa ya kufanya kazi katika nyanja hizi na watu wenye ushawishi ili kuendeleza mipango yake. Je, sasa tunaweza kuwategemea wanaume wetu katika nyadhifa mbalimbali za uwajibikaji kutenda kwa unyenyekevu na ubora sehemu yao? Wacha walinzi waamke. Mtu yeyote asiendelee kutojali hali hiyo. Kunapaswa kuwa na uamsho kamili kati ya ndugu na dada katika makanisa yetu yote.— {Manuscript 21, 1910 ( MM, 302 ). MTC 28.1

**Matokeo Makuu ya Uinjilisti wa miji Bado Hayajashuhudiwa.—** Hakuna mabadiliko katika jumbe ambazo Mungu alituma zamani. Kazi katika miji ni kazi muhimu kwa wakati huu. Miji inapofanyiwa kazi jinsi

ambavyo Mungu angependa ifanyike, matokeo yake yatakuwa ni kuanzishwa kwa vuguvugu kubwa ambalo hatujashuhudia bado. … MTC 28.2

Kama watu wa imani, hatuko macho kufahamu vipaumbele na mahitaji yetu katika nyakati tunazoishi. Amkeni walinzi. Kazi yetu ya kwanza inapaswa kuhusu kuichunguza mioyo yetu na kuongoka upya. Hatuna muda wa kupoteza juu ya masuala yasiyo muhimu.- {letter 46, 1910 ( MM, 304 ). MTC 28.3

## WATENDAKAZI NA KRISTO KWENYE MI JI

**Fursa ya Kuwa Watendakazi Pamoja na Kristo.—** Kazi ya kugawa kile ambacho amepokea itamfanya kila mshiriki wa kanisa kuwa mfanyakazi pamoja na Mungu. Wewe mwenyewe huwezi kufanya lolote; lakini Kristo Ndiye mtenda kazi mkuu. Ni fursa ya kila mwanadamu anayempokea Kristo kuwa mtenda kazi pamoja Naye.—
{6T.449 . (1900) MTC 28.4

**Kuitwa Kufanya Kazi Kwa Upatanifu Pamoja na Kristo.—** "Kama vile ulivyonituma Mimi ulimwenguni, vivyo hivyo na Mimi nimewatuma wao ulimwenguni." Si kazi ya yule anayeamini na kumkiri Yesu kuketi chini na kubungaa na kuchukulia maisha kwa urahisi (akistarehe kijiweni), kana kwamba hakuna la kufanywa. Kuna kazi kubwa ya kukamilishwa, na kila mtu anayefikia uzima wa milele anapaswa kushirikiana na Yesu Kristo. "Wala siwaombei hawa peke yao," Mwokozi alisema, "bali na hao watakaoniamini kwa neno lao; ili wote wawe na umoja kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba Ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo umoja; Nimi ndani yao, Nawe ndani yangu, ili wawe kamili katika

umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma, na kuwapenda wao kama ulivyonipenda Mimi.” MTC 28.5

Wachungaji na watu wamejumuishwa katika maneno haya. Wote wawe kitu kimoja, kama Kristo alivyokuwa mmoja na Baba. Hakuwezi kuwa na ukamilifu katika mgawanyiko. Wale wanaomwamini Yesu Kristo watakuwa kitu kimoja katika matamanio yao kwa roho zinazoangamia nje ya Kristo. Uhalisia uliopo ni kwamba tumepoteza mtazamo wa wajibu wetu binafsi, na tunahitaji kuuchukua tena katika Jina la Bwana. Wakati maombi haya ya Kristo yatakapojibiwa kwa ajili ya watu Wake katika zama hii, wakati umoja huu utakapokuwapo kati ya Waadventista Wasabato, kutakuwa na mvuto mkubwa sana unaotoka kwao kwenda ulimwenguni. Matengenezo yatafanyika; kwanza katika jeshi au safu zetu wenyewe, na kisha kwa wale tunaowafanyia kazi, kutaonekana mabadiliko ya tabia ambayo Kristo aliiombea kwa bidii. ... MTC 29.1

Ndugu na dada zangu, hebu tujifunze ili kujua ni kazi gani inayotuhusu sisi binafsi. Una kitu cha kufanya kwa wale walio karibu nawe, na kwa wale walio mbali. Hatuna haki ya kutaoa fedha zetu zote kwa ajili ya kustarehe na kufurahia maisha yetu ya sasa. Hatuna haki ya kutumia senti zetu katika kujitukuza, kujiendekeza na kujifurahisha wenyewe. Hukumu za Mungu zinazokuja juu ya dunia hakika haziko mbali, na tunapaswa kuwa kunyanyuka kufanya sehemu yetu. Tunapofikiria kile ambacho Kristo ameteseka kwa ajili yetu, tunapaswa kutafuta kuingia katika nafasi ya kujikana nafsi na kujidhabihu nafsi, ili tuweze kusaidia katika wokovu wa roho zilizo katika hatari ya uharibifu wa milele. Hatuwezi kuwa na kisingizio cha kumtolea Mungu kwa kupuuza kazi hii. MTC 29.2

Je, tumejitayarisha kwa hukumu? Je, tunajiandaa kukutana na Bwana? Kuna kazi ya kufanywa kwa wale

walio mbali na walio karibu. Tunapaswa kuingia katika majiji na miji na vijiji ambavyo vimeachwa bila ujumbe wa onyo kwa siku hizi za mwisho. Hatutambui jinsi tulivyo karibu na mwisho wa historia ya dunia hii. Hatutambui thamani ya nafsi ambazo Kristo alizitolea maisha Yake ya thamani. Twahitaji kuvaa vazi la haki la Kristo na kufanya kazi kwa kupatana Naye, na kupatana na wahudumu Wake, kupatana na wote wanaoamini kweli kweli, Ukweli wa wakati huu.— Manuscript 91, 1909 . MTC 30.1

**Washirika na Mungu katika Kuokoa Wanadamu.-** Ni neema ya Mungu inayotuongoza kuitii sheria ya Mungu, nakala ya tabia ya Bwana Mwenyewe. Ni maarifa ya Kristo Yesu ambayo tunapaswa kuyakuza kwa uweza wetu wote ili tuwe watendaji wa Neno Lake. ... Je, tutamfurahisha Yesu? Je, tutawafurahisha Malaika wa Mwenyezi Mungu? Tunaweza kufanya hivyo kwa kushirikiana na Mungu katika kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. ... Je, hatutashirikiana na malaika wa mbinguni katika kazi ya kuokoa wanadamu walioanguka?— {R &H, Januari 1896 . MTC 30.2

## WATENDAKAZI WATIWE MOYO

**Wafanyakazi wa Jiji Wanahitaji Kutiwa Moyo.—** Wale wanaoshiriki katika kazi ngumu na yenye kujaribu katika majiji wanapaswa kupokea kila kitia-moyo kinachowezekana. Hebu wasiingizwe kwenye ukosoaji usio na fadhili kutoka kwa ndugu zao. Ni lazima tuwe na uangalifu kwa watenda kazi wa Bwana wanaofungua nuru ya Ukweli kwa wale walio katika giza la makosa na upotovu. Tuna kiwango cha juu kilichowasilishwa mbele yetu.—{ letter 168, 1909 ( MM, 309, 310 ). MTC 30.3

**Wasivunjike Moyo. —** Wajumbe wa Mungu katika miji mikubwa hawapaswi kuvunjika moyo kwa sababu ya uovu,

ukosefu wa haki, upotovu, na ufisadi ambao wanaitwa kukabiliana nao wakati wanapojitahidi kutangaza habari njema ya wokovu. Bwana angemchangamsha kila mfanyakazi Kama huyo kwa ujumbe uleule aliompa mtume Paulo katika Korintho yenye uovu: "Usiogope, bali nena, wala usinyamaze; kwa maana Mimi ni pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia. kwa maana Nina watu wengi katika mji huu" ( Matendo 18:9,10 ).

Hebu wale wanaojishughulisha na huduma ya kuokoa roho wakumbuke kwamba ingawa kuna wengi ambao hawatalitii shauri la Mungu katika Neno Lake, ulimwengu wote hauwezi kugeuka kutoka kwenye nuru na Ukweli, kutoka kwa mialiko ya Mwokozi mvumilivu, na Mwenye subira. Katika kila jiji, ingawa kumesheheni ukatili. jeuri na uhalifu, kuna wengi ambao kwa mafundisho yanayofaa wanaweza kujifunza kuwa wafuasi wa Yesu. Kwa hiyo maelfu wanaweza kufikiwa na Ukweli unaookoa na kuongozwa kumpokea Kristo kama Mwokozi binafsi.— { PK, 277 . (1917) MTC 30.4

**Si Kutangua Kazi ambayo Mungu Huwaita Wengine Waifanye.—** Tunapaswa kujielimisha wenyewe kufuana na agizo la Bwana, ili tusibomoe bali tujenge maslahi ya wanadamu. Wafanyakazi hawapaswi kutengana. Watalazimika kukutana na mambo ya kukatisha tamaa kutoka nje, ila hakuna mtu anayedai kuziba ufa wa sheria ya Mungu, na kujenga mahali palipokuwa ukiwa, na kurejesha misingi ya vizazi vingi, atayakeyepatika akiibomoa kazi ambayo Mungu amewaweka watenda kazi Wake kuitimiza katika matawi mbalimbali ya kazi Yake.—
{Signs of the Times, Julai 3, 1893 . MTC 31.1}

**Jihadhari na Wale Wanaojaribu Kuwakatisha Watu Tamaa na Uinjilisti wa mijini.—** Hali yetu ya dhambi ya

kuwa vuguvugu imekuwa ikija kwa miaka mingi. Tuko nyuma sana katika kufuata maagizo yaliyotolewa kuhusiana na kuingia mijini, na kuweka kumbukumbu kwa ajili ya Ukweli wa sasa. Kwa kuwa ni miaka mingi sasa, maagizo hayo yamekuwa yakirudiwa kwetu kuhusu kazi inayopaswa kufanywa katika miji; bado inaonekana kuna usingizi kama wa mauti juu ya wahudumu na watu wengi. Kuna wachache ambao wamekuwa wakifanya yote katika uwezo wao, lakini mzigo wa kazi hii haujabebwa kwenye mioyo ya watu wetu; hawahimizwi kushirikiana, na kuweka sawa mambo yaliyosalia, yaliyo tayari kufa. ... MTC 31.2

Kuna wengine ambao hawakukubali ujumbe aliotumwa na Mungu, na hawa wamepanda mbegu za kutokuamini hadi magugu yameota na kuongezeka. ....... Wale ambao wamesimama moja kwa moja katika njia ya kazi ya Mungu kwa miaka kumi na mitano iliyopita hawapaswi kutegemezwa/kusaidiwa au kupewa mvuto.— {R& H, Julai 23, 1908 . MTC 31.3

**Kukosa Kutia Moyo wengine na Kuwategemeza Humchukiza Mungu.—** Acheni tumshukuru Bwana kwa kuwa kuna watenda kazi wachache wanaofanya kila liwezekanalo ili kuweka kumbukumbu za Mungu katika miji yetu iliyopuuzwa. Tukumbuke kuwa ni wajibu wetu kuwatia moyo wafanyakazi hawa. Mungu hafurahishwi na ukosefu wa shukrani na kukosa kutoa msaada kunaoonyeshwa wafanyakazi wetu waaminifu katika miji yetu mikubwa.— {Ms 154, 1902 ( Ev, 42 ). MTC 32.1

**Shetani Anajaribu Kuwakatisha Moyo Watendakazi katika miji. —** Unapoitazama miji hiyo, iliyojaa uovu Ssna, Shetani atakuambia kwamba haiwezekani kuifanyia wema wowote. Miji imepuuzwa kwa huzuni. Huwezi kamwe kujua thamani ya lulu hadi utafute kwa bidii kuipata.— {Manuscript 13,1895 ( Ms.10:227 ). MTC 32.2

## SURA YA 3 - CHANGAMOTO ZA JIJI

Kazi ya Shetani Yaonekana kwa Urahisi Katika Miji.— Shetani ana shughuli nyingi katika majiji yetu yenye watu wengi. Kazi yake inaonekana katika mkanganyiko, ugomvi na mafarakano kati ya kazi na mtaji, na unafiki ambao umeingia makanisani. Ili watu wasichukue muda wa kutafakari, Shetani huwaongoza katika mzunguko wa raha, starehe, na kuchukulia mambo kwa wepesi *kwa kutafuta anasa, kwa kula na kunywa. Anawajaza tamaa za kujionyesha ili kujiinua nafsi zao. Hatua kwa hatua, ulimwengu unafikia hali iliyokuwako katika siku za Nuhu. Kila uhalifu unaowezekana kufanyika, unatendwa. Tamaa ya mwili, kiburi cha macho, maonyesho ya ubinafsi na uchoyo, matumizi mabaya ya mamlaka, ukatili, na msukumo unaotumiwakuwafanya wanadamu waungane na mashirikisho na vyama vya wafanyakazi au vyama vinavyohusiana na siasa (Unions)—wakijifunga wenyewe katika matita kwa ajili ya kuchomwa katika ile mioto ya siku za mwisho—yote haya ni kazi ya mawakala wa Kishetani. Duru hii ya uhalifu na watu wajinga huiita ndiyo "maisha yenyewe haswa" ... MTC 33.1

Ulimwengu, ambao hutenda kana kwamba hakuna Mungu, umefyonzwa katika matamanio ya kukimbiza ubinafsi na uchoyo, hivi karibuni utapata uharibifu wa hafula, na hauaweza kutoroka. Wengi huendelea na kujifurahisha, na kujitosheleza kwa njia ya uzembe hadi wanachukizwa na maisha na hata kujiua. Kucheza dansi, kunywa pombe kwenye makundi na kupiga makelele usiku mzima, na kuvuta sigara, wakifurahia tamaa zao za kinyama, wanatembea kama ng'ombe aendaye kuchinjwa.

Shetani anafanya kazi kwa ufundi wake wote na uchawi ili kuwafanya watu wasonge mbele kwa upofu hadi Bwana atakaposimama kutoka mahali Pake ili kuwaadhibu wakaaji wa dunia kwa ajili ya maovu yao, wakati dunia itakapofunua damu yake na haitawafunika tena waliouawa. Ulimwengu wote unaonekana kuwa katika gwaride la kifo.— {Manuscript 139, 1903 ( Eva, 26 ). MTC 33.2

**Mashirika ya Kishetani Hupanga Upinzani kwa Sheria ya Mungu.—** Wanadamu wameungana ili kumpinga Bwana wa majeshi. Mashirika haya yaliyoungana pamoja, yataendelea hadi Kristo atakapoondoka mahali Pake pa maombezi mbele ya kiti cha rehema na kuvaa mavazi ya kisasi. Mawakala wa kishetani wapo katika kila jiji, wakijishughulisha kupanga karamu zinazopinga sheria ya Mungu. Watu wanaodai kuwa ni watakatifu na makafiri waliodhihirishwa kuwa na tabia hiyo, wanachukua msimamo wao na vyama hivi. Huu sio wakati wa watu wa Mungu kuwa wanyonge. Hatuwezi kumudu kuwa nje ya kituo chetu cha ulinzi hata kwa nukta moja.— { 8T.42 .1904} MTC 34.1

**Mgogoro Kati ya Wema na Uovu Utadumu Kadiri Muda Utakavyoendelea. —** Mapambano ya kutisha hufanyika kati ya nguvu za wema na uovu katika vituo muhimu ambapo wajumbe wa Ukweli wanaitwa kufanya kazi. "Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama," atangaza Paulo, "bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili" ( Waefeso 6:12 ). Mpaka mwisho wa wakati kutakuwa na pambano kati ya kanisa la Mungu na wale walio chini ya udhibiti wa malaika waovu.— {AA, p. 219
.1911} MTC 34.2

**Mawakala wa Shetani wanaongeza Ugumu wa Kufanya Kazi katika Majiji.— Hatutambui** ni kwa kadiri gani

mashirika ya kishetani yanafanya kazi katika majiji hayo makubwa. Kazi ya kuleta ujumbe wa Ukweli wa sasa mbele ya watu inazidi kuwa ngumu. Ni muhimu kwamba vipaji vipya na anuwai/tofauti viungane katika kazi inayotumia ubongo kwa watu.—{Letter 168, 1909 ( MM, 300 ). MTC 34.3

## UMASIKINI NA KUKOSA AJIRA

**Watu Walioumbwa kwa Ajili ya Angahewa ya Mbingu.—** Wanadamu hawakuumbwa wawe chini ya umaskini, magonjwa, na mateso, hawakuumbwa kwaajili kutojali au kutoweka umakini kwa mahitaji yao ya kiroho na kimwili, bali kwa ajili ya utu na hadhi ya ubinadamu, usafi, na kuinuliwa kwa tabia katika maisha haya, na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu (1Pet 1:8). Rehema za Mungu zimesambazwa na zinapelekwa kwa aina tofautitofauti duniani kote; na kama mwanadamu angekuwa mtiifu kwa sheria za asili kusingekuwa na 1/10 ya taabu iliyopo sasa. Afya na maisha yanahatarishwa na kuendekeza tamaa kula. Majanga au shida zetu mara nyingi hutokana na kutumia vitu kwa kupitiliza (wingi) na matumizi yasiyo ya kawaida kuliko kutokana na uhaba. Vijana katika miji yetu wamezungukwa na vishawishi vya kujiingiza katika tamaa za mwili kama ngono au chakula isivyofaa . Uovu umerembwa kama matunda ya Sodoma (Sodom Apples), yanaonekana maridadi bila hivyo, lakini ndani ni majivu tupu.—{ Forest Park Reporter, Machi 30, 1879} . MTC 34.4

**Taabu ya Masikini inahitaji msaada wa Haraka.—** Katika majiji hayo makubwa kuna watu wengi ambao hawana matunzo ya kutosha au hata hawatiliwi maanani kuliko wanyama mabubu. Fikiria familia zilizorundikana pamoja katika nyumba zenye hali duni, nyingi zikiwa na vyumba vya chini ya ardhi vyenye giza (basements),

vinavyonuka vibaya kwa unyevunyevu na uchafu. Katika maeneo haya mabovu watoto huzaliwa na kukua na kufa. Hawaoni chochote kuhusu uzuri wa vitu vya asili ambavyo Mungu ameumba ili kufurahisha hisia na kuinua roho zao. Wakiwa na nguo chakavu na zilizopasuka, pamoja na njaa kali mara nyingi, wanaishi katikati ya uovu na upotovu, wakifinyangwa katika tabia na unyonge, shida na dhambi inayowazunguka. Watoto husikia Jina la Mungu likitajwa kwa lugha chafu au viapo vichafu vya makufuru tu. Maneno machafu, matusi, kuapa, laana, makufuru, maneno yasiyofaa, kukosolewa na kugombezwa kwa kupitiliza hujazwa masikioni mwao. Moshi wa vileo na tumbaku, uvundo mbaya unaofanya mtu apate ugonjwa, upotovu wa maadili, hupotosha hisia zao. Hivyo makundi ya watu yanafunzwa kuwa wahalifu, maadui kwa jamii ambayo imewatelekeza kwenye taabu na udhalilishaji. MTC 35.1

Sio masikini wote waliosongamana mijini wamo katika tabaka hili. Wanaume na wanawake wanaomcha Mungu wameletwa kwenye kina kirefu cha umaskini kwa ugonjwa au misiba au mambo yaliyowapata kwa bahati mbaya, hawa mara nyingi wanakuwa wamepitia kwenye mikono ya hila au matendo yasiyo ya haki ya wale wanaoishi kwa kuwinda wenzao. Wengi walio wanyofu na wenye nia njema wanakuwa maskini kwa kukosa mafunzo ya stadi au tasnia za kujikimu kimaisha. Kupitia kutojua au ujinga wao hawawezi kupigana mieleka na ugumu wa maisha. Wamejipeleka mijini, nao mara nyingi hawawezi kupata kazi. Wakiwa wamezungukwa na vituko na sauti za uovu, wanakabiliwa na majaribu ya kutisha sana. Wanasogea wakiwa wengi kama kundi la mifugo, nao mara nyingi huwekwa kwenye kundi la watu wabaya na waliodhalilishwa, ni kwa nguvu tu zisizo za mwanadamu, nguvu zisizo na kikomo, ndipo wanaweza kuhifadhiwa ili wasizame kwenye vilindi vile vile. Wengi hushikilia uadilifu

wao, wakichagua kuteseka badala ya kutenda dhambi. Tabaka hili hasa linahitaji msaada, huruma, na kutiwa moyo.— {MH, 189, 190 . (1905) MTC 35.2

**Maskini Mara Nyingi Hawajui pa Kugeukia ili Wapate Msaada.—** Kuna watu wengi wanaopambana na umaskini, wanaolazimika kufanya kazi ngumu ili kupata ujira mdogo, wanaoshindwa kupata angalau mahitaji machache yaliyo muhimu kwa maisha. Kazi ngumu na maadili mabaya bila matumaini ya mambo yaliyo bora, hufanya mzigo wao kuwa mzito kubebeka. Wakati maumivu na ugonjwa vinapoongezwa, mzigo wao unakaribia kutowezekana kubebeka. Wakiwa wamechoshwa na usumbufu wa maisha na uonevu, hawajui wageukie wapi ili kupata afueni.—
{9T.90 . (1909) MTC 36.1

## KUNYONYWA KWA MASIKINI NA WALE WALIO MATAJIRI

**Matajiri Huwa Matajiri kwa Kuwandamiza Wengine.—** Adui amefaulu kupotosha haki na kujaza mioyo ya watu tamaa ya kujipatia faida. "Haki imesimama mbali; maana kweli imeanguka katika njia kuu, na adili haiwezi kuingia" ( Isaya 59:14 ). Katika miji mikubwa kuna umati wa watu wanaoishi katika umaskini na unyonge, karibu na kukosa chakula, malazi na mavazi; ilhali katika majiji hayohayo kuna wale walio na ugavi wa mahitaji yao zaidi ya moyo wao unavyoweza kutamani, wanaoishi kwa anasa (luxury), wakitumia pesa zao kununua samani za nyumba za gharama kubwa, mapambo ya mwili, au mbaya zaidi zaidi, kwa kujiridhisha na tamaa za kimwili za vileo, tumbaku, na mambo mengine. Tamaa zinazoharibu nguvu za ubongo, zinazofanya akili isiwe timamu (vileo nk), na kuidhalilisha nafsi. Vilio vya wanadamu wenye njaa vinasikika mbele za Mungu, huku katika kila aina ya ukandamizaji na unyang'anyi watu wanajirundikia wenyewe mali nyingi.— { 9T.11, 12 . (1909) MTC 36.2

**Mungu Amekataza Kujitajirisha Kupitia Kuwanyanyasa Maskini.—** Neno la Mungu haliruhusu sera yoyote ambayo itaboresha jamii moja kwa kukandamizwa na kuteseka kwa wengine. Katika shughuli zetu zote za kibiashara Neno linatufundisha kujiweka katika nafasi ya wale tunaoshughulika nao, tusiangalie mambo yetu tu, Bali pia mambo ya wengine (mpende jirani). Yule ambaye angejinufaisha na mabaya ya mwingine ili kujinufaisha mwenyewe, au anayetafuta kujinufaisha kupitia udhaifu au kutoweza kwa mwingine, ni mvunjaji wa Kanuni na Maagizo ya Neno la Mungu.—
{MH, 187 . (1905) MTC 36.3

**Mwaka wa Sabato na Yubile Vilikuza Usawa wa Kijamii**. — Bwana atasitisha na kuratibisha kupenda mali kusiko kwa kawaida, kunakopitiliza na kupenda mamlaka na kuwathibiti wengine. Maovu makubwa yatakuja kama matunda ya kuendelea kulimbikiza mali kwa tabaka moja, na umaskini na udhalilishaji kwa kundi lingine. Bila kizuizi fulani nguvu na mamlaka ya matajiri vingekuwa vinasimama peke yake bila mpinzani (kuhodhi), na maskini, ingawa kwa kila hali wana stahiki kamilifu machoni pa Mungu, wangechukuliwa na kutendewa kama watu duni tu kuliko ndugu zao waliofanikiwa zaidi. MTC 37.1

Hisia ya ukandamizaji au uonevu huu, ingeamsha hasira ya tabaka la wale walio masikini zaidi. Kungekuwa na hisia ya kukata tamaa na kuvunjwa moyo ambayo ingeweza kudhoofisha jamii na kufungua mlango kwa uhalifu wa kila aina. Kanuni ambazo Mungu aliweka zilikusudiwa kukuza usawa wa kijamii. Mpango wa Mungu wa mwaka wa Sabato na Yubile* vingerekebisha kwa kiwango kikubwa yale ambayo wakati wa kipindi hicho yalikuwa yameenda vibaya katika uchumi wa kijamii na kisiasa wa taifa (Mwaka wa Sabato ulikuja kila baaada ya miaka saba (Sabbatical years),

na Mwaka wa Yubile ulikuja baada ya miaka 50 soma katika Walawi 25).— {PP, 534 . (1890) MTC 37.2

## KUNA WATU WANAOTOA MSAADA

**Kwa Huruma Wasaidie Maskini.—** Kuna wanaume na wanawake wenye mioyo mikarimu/mikubwa ambao wanasugua vichwa vyao kuhusu masikini nao wanatafuta jinsi ya kupata pesa ili kuleta afueni kwa watu kama hao. Namna ya watu wasio na ajira na wasio na makazi wanavyoweza kusaidiwa kupata baraka za kawaida za kujikimu kimaisha, baraka za majaliwa ya Mungu za kuishi maisha ambayo Bwana amekusudia mwanadamu aishi ni swali ambalo wengi wanajitahidi sana kupata jibu. Lakini hakuna wengi, hata miongoni mwa waelimishaji na viongozi wa serikali, ambao wanaelewa sababu husika hasa kwa undani, kuhusu hali ya sasa ya jamii. Wale wanaoshikilia hatamu za serikali hawawezi kutatua tatizo la kuongezeka kwa uhalifu, umaskini wa kawaida tunaoujua, na umaskini wa kupitiliza wa kuwa ombaomba mtaan, na kutegemea watu wengine au taifa kumsaidia mtu mahitaji yake ya msingi (poverty and pauperism). Wanajitahidi bila mafanikio kuweka shughuli za kiuchumi kwenye msingi salama zaidi.— {MH, 183. (1905) MTC 37.3

## VYAMA VYA WAFANYAKAZI (Trade Unions)

**Vyama vya Wafanyakazi Huchangia Kuongezeka kwa Shida na Maisha Magumu Mijini.—** Kupitia kufanya kazi kwa amana, na matokeo ya vyama vya wafanyakazi na migomo, hali ya maisha katika jiji inazidi kuwa ngumu zaidi na zaidi. Shida nzito ziko mbele yetu; na kwa familia nyingi kuondolewa kwao katika majiji, kutakuwa ni jambo la lazima.— The Ministry of Healing, 364 .(1905) MTC 38.1

**Wafanyakazi Walio Hatarini Kutoka kwa Vyama vya Wafanyakazi.—** Katika miji yetu yote mikubwa, kutakuwa na kufungwa katika matita na mashirikisho na vyama vya wafanyakazi vilivyoundwa . Mwanadamu atawatawala wanadamu wengine na kudai mengi kutoka kwao. Maisha ya wale wanaokataa kuungana na mashirikisho/miunganiko hii yatakuwa hatarini. Kila kitu kinatayarishwa kwa ajili ya kazi kuu ya mwisho inayofanywa na Yule Mwenye uwezo wa kuokoa na Mwenye uwezo wa kuharibu.— {Manuscript 145, 1902 ( Manuscript Releases 3:42 ). MTC 38.2

**Uanachama wa Vyama vya Ushirika (Unions), Huzuia Kushika Amri Kumi (Dekalojia) —** Miungano au mashirikisho haya hii ni mojawapo ya ishara za siku za mwisho. Wanaume wanafungwa kwenye matita tayari kwa kuchomwa moto. Wanaweza kuwa washiriki wa kanisa, lakini wakati wao ni wanachama wa vyama hivi vya ushirika, hawawezi kuzishika amri za Mungu; kwa kuwa kuwa mwanachama wa vyama hivi inamaanisha kupuuzia Dekalojia (Amri Kumi) nzima.— letter 26, 1903 ( Maranatha, 182 ). MTC 38.3

**Miongoni mwa Jitihada za Mwisho za Shetani Ni Kuunda Vyama vya Ushirika.—** Kufanyizwa kwa miungano hiyo ni mojawapo ya jitihada za mwisho za Shetani. Mungu anawaita watu Wake watoke nje ya miji, wajitenge na ulimwengu. Wakati utakuja ambapo itawabidi kufanya hivi. Mungu atawatunza wale wanaompenda na kuzishika amri Zake.— letter. 26, 1903 ( Manuscript Releases 3:43 ). MTC 38.4

**MAISHA YA MIJINI YAMEPAKWA RANGI NA UTAMADUNI MASHUHURI UNAOPENDWA NA**

**WENGI- (Mitindo ya maisha ni ya kuigiza watu au mkondo mashuhuri)**

**Zisizo na Thamani.—** Maisha ya mijini ni ya madanganyo na bandia. Tamaa kali ya kupata pesa, kimbunga chamsisimko na kujionyesha, anasa na ubadhirifu, yote haya ni misukumo ambayo inaendana pamoja na umati mkubwa wa wanadamu, na kuzigeuza akili kutoka kwenye kusudi la kweli la maisha. Haya yote yanafungua mlango wa maovu elfu moja. Maovu ambayo yana nguvu kwa vijana inayokaribia kutozuilika. MTC 39.1 Mojawapo ya vishawishi vya hila na hatari ambavyo huwavamia watoto na vijana katika miji ni kupenda raha. Siku kuu ni nyingi; michezo na mbio za farasi huwavuta maelfu, na kimbunga cha msisimko na raha huwavuta mbali na majukumu ya maisha ya kiasi (kutotumia ulevi na kuwa na akili timamu ya kuishi maisha mema). Pesa ambazo zilipaswa kuhifadhiwa kwa matumizi bora zaidi hunyanguliwa kwa ajili ya burudani.— {MH, 364 . (1905)

MTC 39.2

**Miji imekuwa Kama Sodoma na Gomora.—** Majiji ya leo yameanza kufanana kwa haraka kama Sodoma na Gomora. Sikukuu na sherehe nyingi huhimiza kukaa bila kufanya chochote au kuwa goigoi. Michezo yenye kusisimua— kwenda kuangalia michezo ya kuigiza au sinema (theatre)*, mbio za farasi, kamari, unywaji pombe, kunywa pombe, kucheza dansi na kupiga makelele kwa kufurahia anasa hizi—huchochea kila tamaa ya mwili ifanye kazi kwa bidii nyingi. Vijana wamesombwa na mkondo maarufu, unaopendwa na watu. Wale wanaojifunza kupenda maburudisho/pumbao kwa ajili yao wenyewe hufungua mlango kwa mafuriko ya vishawishi. Wanajitolea kwa raha na starehe za kijamii na kutumbuizwa/matumbuizo mahali penye makelele, mahali penye ushirika wa wapenda raha ambao kunakuwa na athari ya kuwa kama mtu aliyelewa,

yaani asiyeweza kuchambua mambo kwa akili iliyo timamu. Wanaongozwa kutoka kwa aina moja ya kufurahia ufisadi, ngono chafu, vileo, na maadili mabaya hadi nyingine, hadi wanapoteza uwezo wa kuishi maisha yenye faida, yenye kuwanufaisha wao au kunufaisha watu wengine. Matarajio yao ya kidini yamepoa; maisha yao ya kiroho yametiwa giza. Nguvu zote bora zaidi za nafsi, na vyote vinavyomuunganisha mwanadamu na ulimwengu wa kiroho, vinatelekezwa na mtu anakuwa na maadili mabaya, yaliyoshuka chini.— {COL, 54, 55 . (1900) MTC 39.3

**Uhuru wa Kutenda wa Mtu Binafsi Hauheshimiwi.—** Mazingira ya majiji hayo yamejaa hewa chafu yenye sumu (malaria). Uhuru wa kutenda wa mtu binafsi hauheshimiwi; muda wa mtu hauzingatiwi kuwa ni wake kiuhalisia; yeye anatarajiwa kufanya kama wengine wanavyofanya. ... MTC 40.1

Kujitoa kikamilifu kwa matumbuizo na kuadhimisha sikukuu nyingi sana huipa mahakama biashara kubwa, maafisa na mahakimu pia hujipatia soko la huduma zao (ajira na faini), na kuongeza umaskini, uchafu, hali mbaya na unyonge, mambo ambayo hayahitajiki kuongezeka.— {Special Testimonies On Education, 88 . (1897) MTC 40.2

**Watoto Wasio na Usimamizi Huunda Ushirika Wenye Kuumiza.—** Wazazi humiminika pamoja na familia zao mijini kwa sababu wanaona kwamba ni rahisi kupata riziki huko kuliko vijijini. Watoto, wakiwa hawana la kufanya wakati hawako shuleni, wanajipatia elimu ya mitaani. Wanasomba tabia za uovu, kutoka kwa washirika waovu, ulevi, ubaradhifu, ufisadi, kutokuwa na kiasi, ngono chafu, na maadili mengine mabaya. Wazazi wanaona haya yote; lakini kujitoa mhanga kunahitajika kwao ili wasahihishe kosa lao, ila wazazi hawa wanabakia mahali walipo hadi Shetani anapata umiliki kamili wa watoto wao.—{ 5T.232 .

(1882) MTC 40.3

## UCHAFUZI WA MAZINGIRA

**Mazingira ya miji Huleta Matatizo ya Kiafya kwa Wagonjwa.—** Kelele na msisimko na mkanganyiko wa majiji, maisha yanayobana kila pande na kuthibitiwa na yaliyojaa usanii, yanachakaza, yanaboesha na kuchosha wagonjwa. Hewa, iliyojaa moshi na vumbi, na gesi zenye sumu, na viini vya magonjwa, ni hatari kwa maisha. Wagonjwa, kwa sehemu kubwa ya muda, hufungiwa ndani ya kuta nne, mpaka wanafikia hatua ya kuhisi wao ni kana kwamba wamekuwa wafungwa katika vyumba vyao. Wanatazama nje na kuona majumba, barabara za lami na umati wa watu wanaoharakisha, labda hata hawaoni anga la buluu ama mwanga wa jua, au nyasi au ua au mti. Wakiwa wamefungiwa ndani kwa njia hii, wanatafakari juu ya mateso na huzuni zao, na kuwa mawindo ya mawazo yao ya huzuni. MTC 40.5

Na kwa wale walio dhaifu katika nguvu za maadili, miji ina hatari nyingi. Ndani yake, wagonjwa ambao wana tamaa za kimwili zisizo za asili na ambazo wanapaswa wazishinde, wanakabiliwa na majaribu kila wakati. Wanahitaji kuwekwa katikati ya mazingira mapya ambapo mkondo wa mawazo yao utabadilishwa; wanahitaji kuwekwa chini ya ushawishi tofauti kabisa na ule ambao umeharibu maisha yao. Hebu kwa msimu fulani waondolewe kutoka kwenye mvuto huo unawaoongoza mbali na Mungu, hadi kwenye angahewa safi zaidi.— { MH, 262, 263 . (1905) MTC 41.1

## UHALIFU NA UFISADI

**“Janga la Uhalifu” Hili Limeenea Pote.—** Tunaishi katikati ya “janga kubwa la uhalifu,” mahali ambapo watu

wenye mawazo ya umakini na wanaomcha Mungu kila mahali hushangaa. Ufisadi uliopo, uko nje ya uwezo wa kalamu ya binadamu kuuelezea. Kila siku huleta ufichuzi mpya wa ugomvi wa kisiasa, hongo, na ulaghai. Kila siku huleta rekodi yake yenye kuhuzunisha moyo, ya jeuri, na uasi-sheria, ya kutojali mateso ya wanadamu, ya uharibifu wa kikatili na ukatili wa kutisha wa kishetani ambao unaangamiza maisha ya mwanadamu. Kila siku inashuhudia kuongezeka kwa wazimu, mauaji, na kujiua.

Ni nani anayeweza kutilia shaka kwamba mashirika ya kishetani yanafanya kazi kwa shuguli nyingi zinazoongezeka miongoni mwa wanadamu, ili kuvuruga na kupotosha akili, na kuchafua na kuharibu mwili. MTC 41.2

Na wakati ulimwengu umejaa maovu haya, injili mara nyingi Sana huwasilishwa kwa njia ya kutojali kiasi cha kufanya hisia kidogo tu juu ya dhamiri au maisha ya wanadamu. Kila mahali kuna mioyo inayolilia kitu ambacho hawana.— {MH, 142, 143. (1905) MTC 41.3

**Majiji Yamejaa Uhalifu Ulimwenguni Pote.—** Ulimwenguni pote, majiji yanazidi kuwa mahali pa kuzalisha uovu. Kwenye kila upande kuna vituko na sauti za uovu. Kila mahali kuna vishawishi vya ngono, ulevi, ufisadi, ubaradhifu, starehe, anasa, kujifurahisha nafsi na tamaa zingine mbaya za mwili. Wimbi la ufisadi na uhalifu linaendelea kuongezeka. Kila siku huleta rekodi ya jeuri na ukatili—wizi, mauaji, watu kujiua, na uhalifu usioweza kubadilishwa.— {MH. 363. (1905) MTC 42.1

**Kuongezeka kwa Uhalifu Hutokana na Kumkataa Mungu. —** Hatia ya ulimwengu inakuja kwa upesi na kwa

uhakika kote, juu ya wakaaji wa majiji hayo, kwa sababu ya ongezeko la mara kwa mara la uovu uliodhamiriwa. ... MTC 42.2

Tangu zama hata zama Shetani amejaribu kuwaweka watu katika kutojua ukarimu wa Yehova. Amejitahidi kuondoa machoni pao mambo makuu ya sheria ya Mungu—kanuni za haki, rehema, na upendo zinazoonyeshwa humo. Wanadamu hujivunia maendeleo ya ajabu na kuelimika kwa enzi hii tunayoishi
sasa; lakini Mungu anaona dunia imejaa uovu na jeuri. Watu wanatangaza kwamba sheria ya Mungu imebatilishwa, kwamba Biblia si sahihi, yaani haina ukweli au uhalisia; na kwa sababu hiyo, wimbi la uovu, ambalo halijaonekana tangu siku za Nuhu na Israeli iliyoasi, linaenea ulimwenguni pote. Ubora wa nafsi, upole, uungwana, adabu, uchamungu,vinanadiwa ili kukidhi matamanio ya mambo yaliyokatazwa. Rekodi nyeusi ya uhalifu uliofanywa kwa ajili ya faida unatosha kugandisha damu na kuijaza roho kwa mstuko na hofu. MTC 42.3

Mungu wetu ni Mungu wa rehema. Kwa ustahimilivu na huruma anashughulika na waasi wa sheria Yake. Na bado, katika siku yetu hii, wakati wanaume na wanawake wana fursa nyingi sana za kuielewa sheria ya Mungu kama inavyofunuliwa katika Maandiko Matakatifu, Mtawala mkuu wa Sayari zote, hawezi kuona kuridhika kuyatazama majiji maovu, ambayo yanarindima kwa ukatili na uhalifu. Mwisho wa ustahimilivu wa Mungu kwa wale wanaoendelea kutotii unakaribia upesi.— {PK. (1917) MTC 42.4

**Uhalifu Katika Miji Huzidi Kuongezeka.—** Vijana wa mijini mwetu wanapumua katika hewa yenye ukungu wa uchafuzi wa uhalifu. Ushawishi huo mbaya huendelea kuwasilishwa vijini na kisha jamii nzima inachafuliwa. Watawala hawana stahiki ya maadili mema, bali ni watu ambao wameruzukiwa vizuri na mali za dunia hii, na

hawana hamu wala mwelekeo wa kuangalia ukuaji wa mzizi huu wa uchungu unaoongezeka mwaka baada ya mwaka, na unakuzwa na kupaliliwa kwa machapisho yanayouzwa kila mahali, na kwa visa na maelezo ya matendo ya uhalifu yanayopatikana katika magazeti ya siku hizo.— {Manuscript 13, 1895 ( Manuscript Releases 10:226 ). MTC 42.5

Mungu Huwatazama kwa huruma Watenda Maovu Wachanga (Youth).— Wanawaona * wakiwa wamedhoofika, wamechakaa, na kubondwabondwa, bila nguvu ya kiadili, wamekuwa majeruhi wa kimadili tayari kuwaambukiza mazoea yao maovu kwa wengine. Mioyo ya wazazi imevunjika. Kaka na dada na jamaa wanazungumza juu ya roho hizi maskini kama zisizo na tumaini, lakini Mungu huwaangalia kwa ... huzuni na huruma. Anaelewa hali zote ambazo zimewaingiza katika majaribu, ambayo yamewatenganisha na Mungu. Jinsi gani vijana wa kizazi hiki wanaweza kuepuka fedheha ya kutisha ya kupoteza urithi wao waliopewa na Mungu, wakiuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza kama Esau alivyofanya ..., wakisaliti maslahi matakatifu waliyokabidhiwa kwa ajili ya kubariki wanadamu? Wanajiingiza katika tamaa zisizo na kiasi, ulafi wa chakula na kupitia uroho wa kupata pesa hutumbukia katika mazoea ya kukosa unyoofu/uadilifu. MTC 43.1

Nafsi hizi maskini zinahitaji kuunganishwa na kanuni za juu na safi za Biblia. Lakini kwanza kazi ya kurejeshwa ianze katika kuwapa chakula chenye afya, na kuwaandalia mazingira ya kuwa na miili safi na mavazi safi, na ndipo cheche fulani za shukrani zitaanza kutokeza.— Manuscript 14a, 1897 . MTC 43.2

## HUKUMU ZA MUNGU KATIKA MIJI

**Uvunjaji wa Sheria Huleta Hukumu za Mungu.—** Nikiwa Loma Linda, California, Aprili 16, 1906, kulipita mbele yangu uwakilishi mzuri sana. Wakati wa maono ya usiku, nilisimama juu ya ngome, ambayo niliona nyumba zikitikiswa kama mwanzi kwenye hali ya upepo. Majengo, makubwa na madogo, yalikuwa yakianguka chini. Kumbi za starehe na anasa, kumbi za sinema au maonyesho na michezo (theatre), hoteli, na nyumba za matajiri zilitikiswa na kubomolewa. Uhai wa wengi ulifutwa kabisa, na hewa ikajaa mayowe ya wale waliojeruhiwa na waliojawa na hofu. MTC 43.3

Malaika wa Mungu wanaoangamiza walikuwa wanafanya kazi. Kwa mguso mmoja tu, majengo, yaliyojengwa vizuri sana hivi kwamba watu waliyaona kuwa yapo salama dhidi ya kila hatari, upesi yakawa lundo la takataka. Hakukuwa na uhakika wa usalama mahali popote. Sikujisikia katika hatari yoyote maalum, lakini utisho wamatukio yaliyopita mbele yangu siwezi kupata maneno ya kuelezea. Ilionekana kuwa uvumilivu wa Mungu ulikuwa umechoshwa na kwamba siku ya hukumu ilikuwa imefika. MTC 44.1

Kisha malaika aliyesimama kando yangu akaniagiza kwamba ni wachache wenye uelewa au dhana yoyote ya idadi ya uovu uliomo katika ulimwengu wetu wa leo, na hasa uovu katika miji mikubwa. Alitangaza kwamba Bwana ameweka wakati ambapo Atawatembelea wakosaji kwa ghadhabu kwa ajili ya kuendelea kuipuuzia sheria Yake. MTC 44.2

Japokuwa uwakilishi uliopita mbele yangu ulikuwa ni wa kutisha kama nini, lakini jambo ambalo lilivuta umakini wa akili yangu lilikuwa ni maagizo yaliyotolewa kuhusiana na jambo hilo. Malaika aliyekuwa amesimama kando yangu alitangaza kwamba utawala mkuu zaidi wa Mungu

na utakatifu wa sheria Yake lazima ufunuliwe kwa wale ambao walidumu kukataa kwa ukaidi kutoa utii kwa Mfalme wa wafalme. Wale wanaochagua kubaki bila uadilifu lazima watembelewe kwa rehema kwa hukumu, ili, ikiwezekana, waweze kuamshwa na kutambua jinsi mwenendo wao ulivyo wa dhambi .— {9T.92, 93 . (1909) MTC 44.3

**Uovu Haupo katika Jiji moja Mahsusi. —** Fikiria jiji la San Francisco. Je, ni nini hasa kilicholeta hukumu za Mungu juu ya mji huo? Tunasoma jibu katika mafunuo ambayo yamefanywa kuhusu ufisadi kwa wale waliosimama katika vyeo vya juu. Ufisadi na ulevi, na ujambazi vinagunduliwa kila upande. Na hali hii ya uovu haiko San Francisco pekee. Sisi tulio na Ukweli tunaelewa maana ya hali na matukio haya. MTC 44.4

Tunaishi katika jioni ya mwisho ya historia ya dunia hii. Je, huu siwakati ambaokila nafsi inapaswa kujiweka katika mahusiano yafaayo na Mungu ili kutenda sehemu ya kipekee ambayo mtu binafsi anapaswa kufanya kwa ajili ya kujengwa kwa ufalme wa Kristo?— {manuscript 73, 1909 ( Sermons and talk 2:314, 315 ). MTC 45.1

## MADAI YENYE KULETA MSISIMKO YANAZUIA KAZI YA UIN JILISTI MI JINI

**Madai Yenye Kushtua Hayapaswi Kufanywa.—** "Miaka si mingi iliyopita, ndugu anayefanya kazi kwa bidii katika Jiji la New York alichapisha matangazo yeny kushtua sana kuhusu kuharibiwa kwa jiji hilo. Niliwaandikia mara moja wasimamizi wa kazi huko, nikisema kwamba haikuwa busara kuchapisha matangazo kama hayo; na kuamsha misisimko feki/bandia au ya kinafiki au isiyotumia busara na yenye kupitiliza. kuamshwa ambao ungesababisha vuguvugu la ushupavu, na kuleta matunda yenye kuumiza

kazi ya Mungu. Imetosha kabisa kuwasilisha Ukweli wa Neno la Mungu kwa watu (bila kuwastua au kuwafanya wawe na tahadhari itakayowafanya watende kutokana na mstuko na wala siyo ukweli wa moyoni). Matangazo ya kushtua ni hatari kwa maendeleo ya kazi." ... MTC 45.2

"Sasa limekuja neno ambalo linasema mimi nimetangaza kwamba New York itafagiliwa na wimbi kubwa. Hii sijawahi kusema. Nimesema, nilipotazama majengo makubwa yanayopanda kule, ghorofa baada ghorofa: 'Ni matukio ya kutisha ya namna gani yatatokea wakati Bwana atakapoinuka kuitikisa dunia kwa jinsi kutisha! Kisha maneno ya Ufunuo 18:1-3 yatatimizwa.' Sura yote ya kumi na nane ya Ufunuo ni onyo la kile kinachoujia ulimwengu. Lakini sina mwanga hasa kuhusiana na kile kinachokuja New York, ila tu najua kwamba siku moja majengo makubwa huko yatatupwa chini kwa kupinduliwa-pinduliwa kwa nguvu za Mungu. Kutoka kwa nuru niliyopewa, najua kwamba uangamivu uko ulimwenguni. Neno moja kutoka kwa Bwana, mguso mmoja wa nguvu zake kuu, na miundo- mbinu hii mikubwa itaanguka. Matukio yatatokea kwa wkuleta hofu ambayo hatuwezi hata kuwazia." ...... MTC 45.3

“Kuna wengi ambao Roho wa Mungu anashindana na roho zao. Wakati wa hukumu za uharibifu za Mungu ni wakati wa rehema kwa wale ambao hawana nafasi ya kujifunza Ukweli ni nini. Bwana atawaangalia kwa upole/ulaini. Moyo Wake wa rehema ukiwa umeguswa;
Mkono wake bado umenyooshwa ili kuokoa.” ... MTC 45.4

“Nilipokuwa New York mara ya mwisho, niliitwa katika majira ya usiku kutazama majengo yakipanda ghorofa baada ya ghorofa kuelekea mbinguni. Majengo haya yalikuwa na

uhakikisho wa kutounguzwa moto kabisa na wajenzi wake (fireproof), na yalijengwa ili kuwatukuza wamiliki wake. Juu na bado juu zaidi, majengo haya yalipanda kwenda juu, na ndani yake malighafi za gharama kubwa zilitumiwa. ... MTC 46.1

"Majengo haya marefu yalipokuwa yanapanda juu wakati wa ujenzi, wamiliki wa hizi nyumba walifurahi kwa matamanio ya ukubwa na kiburi kwamba walikuwa na pesa za kutumia kujitukuza. ... Pesa nyingi walizowekeza kwenye majengo haya, zilipatikana kwa kutoza watu pesa kwa nguvu, kwa kusaga nyuso za maskini, yaani kuwatendea masikini uovu, kwa kuwadhulumu na njia nyingine za kuwakosea haki. Katika vitabu vya mbinguni, hesabu ya kila shughuli ya biashara inatunzwa. Hapo kila mpango usio wa haki, kila tendo la ulaghai, hurekodiwa. Wakati unakuja ambapo katika ulaghai wao na jeuri watu utafikia hatua ambayo Bwana hatawaruhusu wapite mstari fulani, nao watajifunza kwamba kuna kikomo kwa uvumilivu wa Yehova. MTC 46.2

"Tukio lililofuata ambalo lilipita mbele yangu lilikuwa ni kengele ya tahadhari ya moto (fire alarm). Wanaume waliyaangalia majengo marefu yaliyodhaniwa kwamba hayawezi kushika moto (fire proof), na kusema, 'Yako salama kabisa.' Lakini majengo haya yaliungua upesi kana kwamba yalitengenezwa kwa lami (ina petroli). Vyombo vya moto havingeweza kufanya chochote kuzuia uharibifu. Wazima moto hawakuweza kusimamia vifaa au injini za magari ya zima moto. MTC 46.3

"Nimeagizwa kwamba wakati wa Bwana utakapofika, na mabadiliko hayakuwa yametokea katika mioyo ya wanadamu wenye kiburi, na wenye matamanio ya ukubwa (ambitious), watu watagundua kwamba mkono ambao umekuwa na nguvu ya kuokoa, sasa utakuwa na nguvu ya kuharibu. Hakuna nguvu ya kidunia inayoweza kuzuia

mkono wa Mungu. Hakuna malighafi inayoweza kutumika katika ujenzi wa majengo, ambayo yatawalinda dhidi ya uharibifu utakapofika, wakati uliowekwa wa Mungu wa kuadhibu wanadamu kwa sababu ya dhuluma yao na kutozingatia kwao sheria Yake.”— Life Sketches of Ellen G. White, 411-414 . (1915; dondoo kutoka 1903, 1904, 1906)
MTC 46.4

## Sura ya 4— Jumla ya Ushirikishwaji Unaohitajika

### MZIGO WA KAZI YA MI JINI

**Kazi ya Kuendelea kwa Nguvu Kuu.—** Miji yetu inapaswa kufanyiwa kazi. Kutoa juhudi zetu kwenye shuguli au pilikapilika zingine zinazostahili, na kuacha miji yetu bila kufanyiwa kazi, miji ambayo idadi kubwa ya mataifa yote huishi humo, sio busara. Mwanzo mpya sasa unapaswa kufanywa, na fedha lazima zitafutwe ili kazi iweze kwenda mbele. Kwa nguvu kuu kilio hicho kinapaswa kutolewa na kusikika tena katika vituo vyetu vikubwa vya watu. ... MTC 47.1

Pesa zinahitajika kwa ajili ya utendaji wa kazi hiyo huko New York, Boston,Portland [Maine], Philadelphia, Buffalo, Chicago, St. Louis, New Orleans, na majiji mengine mengi. Katika baadhi ya sehemu hizi watu walichochewa sana na ujumbe uliotolewa mwaka wa 1842 hadi 1844, lakini miaka ya hivi karibuni ni kidogo sana ambacho kimefanywa ukilinganishwa na kazi kubwa ambayo inapaswa kufanywa. Na inaonekana kuwa vigumu kuwafanya watu wetu wahisi mzigo maalum kwa ajili ya kazi katika miji mikubwa.— {Manuscript 13, 1910 ( A call to the whatchmen pamphlet 020; katika Ev, 34 ). MTC 47.2

**Onyo kwa Ulimwenguni wote Litatolewa.—** Usiku baada ya usiku siwezi kulala, kwa sababu ya mzigo huu ulio juu yangu kwa ajili ya majiji ambayo hayajaonywa. Usiku baada ya usiku ninaomba na kujaribu kubuni mbinu ambazo kwazo tunaweza kuingia katika miji hii na kutoa ujumbe wa onyo. Kwanini hili liwe hivi, na kuna ulimwengu wa kuonywa na kuokolewa, nasi tunapaswa kwenda Mashariki na Magharibi na Kaskazini na Kusini, na kufanya kazi kwa hekima na akili kwa ajili ya watu wote wanaotuzunguka. Tunapofanya kazi hii, tutaona wokovu wa Mungu. Kutiwa

moyo kutuafuata.— {Manuscript 53, 1909 ( Ev, 62 ). MTC 47.3

**Kazi ya sehemu mahalia haipaswi Kupuuzwa.—** Mashamba yaliyo kwenye kivuli cha milango yetu, kama vile miji mikubwa katika nchi yetu, yasiprukwe kirahisi na kupuuzwa. ... Kazi katika uwanja wa nyumbani ndiyo *tatizomuhimu* sasa hivi. Wakati wa sasa ndiyo una fursa nzuri zaidi ambayo tutalazimika kufanya kazi katika mashamba haya. Baadaye kidogo hali itakuwa ngumu zaidi.
— {8T.31, 32 . (1904) MTC 48.1

**Kazi itaendelea Mpaka Kufungwa kwa Rehema.—** Tunawezaje kupata lugha ya kueleza shauku yetu kwa kina, kueleza matamanio yetu kwamba kila nafsi inapaswa kuamka na kwenda kufanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana? Kristo anasema, "Shughulikeni mpaka nitakapokuja." Inaweza kuwa miaka michache tu hadi historia ya maisha yetu ifungwe, lakini lazima tuishi ulimewngu na kutenda kazi hadi wakati huo atakapokuja. Ujumbe wenye mamlaka utatoka, "Mwenye kudhalumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kuwa mchafu. iweni watakatifu," na hapo hakutakuwa tena na nafasi ya kufanya kazi kwa ajili ya roho za watu. Kila kesi itakuwa imeamuliwa.— {R&H, Aprili 21, 1896. MTC 48.2

## CHANGAMKIA MANUFAA YA KILA FURSA

**Tumia Kila Fursa Inayopatikana ili Kufanya Kazi.—** Mungu anahitaji kwamba tutoe ujumbe wa Ukweli wa sasa katika kila jiji, na tusiifungie kazi hiyo katika sehemu chache. Popote ambapo fursa kwa ajili ya ile Kweli inaweza kupatikana, hapo acha wanaume wasimame na kuweka kituo, watu ambao wanaweza kufundisha mafundisho

yake kwa nguvu na ushawishi utakaofikia mioyo. ... MTC 48.3

Mtu yeyote asiifanye njia ya Bwana kuwa njia ya uvumbuzi au ubunifu wa mwanadamu. MTC 48.4

Maneno yalisemwa kwangu kwa nguvu yenye msukumo: Waamshe walinzi kupeleka neno la onyo kwa kila mji Amerika. ... MTC 48.5

Usirukeruke kama vile unarandaranda juu ya makanisa na kurudia tena na tena Kweli zile zile kwa watu, huku miji ikiachwa katika ujinga na dhambi, bila kuonywa na bila kazi. Hivi karibuni njia itawekewa kizuizi kwenye miji hii na kufungwa kwa ujumbe wa injili. Waamshe washiriki wa kanisa, ili waweze kuungana katika kufanya kazi ya uhakika na ya kujikana nafsi (kujinyima).— {Manuscript 61, 1909 ( Manuscript Releases 10:215, 216 ). MTC 48.6

**Ingia Wakati Milango Ipo Wazi.**— Mungu anauliza, Kwa nini minara ya Makumbusho Yangu haijaanzishwa katika miji? Je, tunaweza kurudisha jibu gani? Kazi iliyopuuzwa katika miji yetu inashuhudia ukosefu wa nguvu kama za Kristo miongoni mwa waumini. Hebu sote tuwe macho na hitaji la kuanzisha misheni ya Kikristo katika miji. Waache watenda kazi wa Mungu waingie kwenye milango inayofunguliwa kwao. Waamini wahitaji kuamka na kufanya mengi zaidi kuliko wanavyofanya sasa katika mistari ya jitihada za Kikristo.— The Review and Herald, Februari 4, 1904 . MTC 49.1

**Fursa za Upanuzi Zimekosekana.**— Ikiwa katika muda wa miaka ishirini iliyopita kungekuwako katika majiji yetu makubwa jitihada zenye ari na kali za uanzishaji wa kazi, na kutangaza ujumbe wa ile Kweli, basi ingekubaliwa na maelfu ambao si tu wangelishangilia, bali nao pia wangejitahidi kuusambaza Ukweli kwa wengine. ... MTC 49.2

Katika vituo kama vile Washington na Mountain View na Nashville, hapaswi kuwa na jitihada yenye kuchosha katika kuongeza majukumu mapya na kukusanya pamoja familia zaidi za waumini, lakini badala yake ndugu zetu katika maeneo haya wanapaswa kujifunza jinsi ya kuhama walipo na kuanzisha vituo vyenye mvuto (centers of Influence) katika mahali ambapo kuna hitaji la kazi kufanywa.— Barua ya 41, 1911 . MTC 49.3

## CHUKUENI TAHADHARI, MILANGO HUFUNGUKA KWA WAPINZANI PIA

**Milango Hufunguka kwa Kazi ya Umishenari na kazi ya Wapinzani wa Kweli pia.—** Vita vikali lazima vipiganwe/viingiwe na roho ya kujitolea, ya kujidhabihu ambayo wengi hawajui lolote kuihusu. Kadiri ofa za fursa zinavyotokea, ndivyo milango hufunguka, na Neno la uzima linaletwa kwa watu, na ndipo upinzani dhidi ya Ukweli utaanza kutenda kazi. Mlango ulio wazi kwa mmishenari utakuwa wazi pia kwa mpinzani wa Ukweli. Lakini pale Kweli inapowasilishwa kama ilivyo katika Yesu, wasikilizaji wanawajibika kwa kuikataa Nuru.— {R&H, Julai 2, 1895 . MTC 49.4

## WAHUSISHE WAUMINI KWENYE HUDUMA YA JUMUIYA

**Wito wa Kuamsha Watu Kuhusu Mahitaji ya Majiji.— Wanapoona majiji ambayo hayajafanyiwa** kazi, ndugu zetu wanatambua ukuu wa kazi inayopaswa kufanywa. Wengi ambao hapo awali walipaswa kuwa macho wakiupa umakini ujumbe uliotumwa, wamelala. Watu wetu sasa wameamka. Ikiwa wote watafanya wajibu wao, tutaona kazi ya Bwana ikisonga mbele kwa bidii. Mungu na atusaidie, ndiyo sala yangu.— Letter 102, 1910 . MTC 50.1

**Wafanyakazi Mia Moja Wanahitajiwa Sasa Mahali ambao kuna Mtendakazi Mmoja tu.—** Miji inajaa uovu, na

Shetani adokeza kwamba haiwezekani kufanya wema wowote ndani ya mipaka ya miji hiyo; na hivyo inapuuzwa kwa huzuni. Lakini kuna lulu zilizopotea huko, ambazo thamani yake huwezi kutambua mpaka uzitafute kwa bidii ili uzipate. Huenda kukawa na wafanyakazi mia moja mahali ambapo kuna mmoja tu, ambaye huenda akawa anatafuta kwa bidii, kwa sala, na kwa matamanio makubwa sana ili kupata lulu ambazo zimezikwa kwenye takataka za majiji hayo.— {R&H, Aprili 21, 1896. MTC 50.2

## WAHUDUMU WNAITWA KUFANYA UIN JILISTI M JINI

**Wahudumu wa Kufanya Kazi katika Majiji Makubwa.—** Nimeagizwa nielekeze wahudumu wetu kwenye majiji ambayo hayajafanyiwa kazi na kuwahimiza wafanye kila njia ili wafungue njia ya kuwasilisha ile Kweli. Katika baadhi ya miji ambapo ujumbe wa ujio wa pili wa Bwana ulitolewa kwa mara ya kwanza, tunalazimika kuichukua kazi hiyo kana kwamba ni shamba jipya (utume wa maeneo yasiyofikika). Je, haya mashamba tasa, miji hii isiyofanyiwa kazi, irukwe hadi lini? Bila kukawia, kazi ya kupanda mbegu inapaswa kuanza katika sehemu nyingi sana.— { 9T.123 . (1909) MTC 50.3

## WANAFUNZI WANAPASWA KUSHIRIKI

**Wanafunzi Washiriki Katika Namna Mbalimbali za Uinjilisti.—** Kupitia wanafunzi wa kwanza zawadi ya Bwana ilitolewa kwa Israeli; mwinjilisti mwaminifu leo atafanya kazi kama hiyo katika kila mji ambapo wamishenari wetu wanaingia. Ni kazi ambayo kwa kiasi fulani tumejaribu kuifanya kuhusiana na baadhi ya vituo vya tiba sahili, viitwavyo Sanirarium, lakini uzoefu mpana zaidi katika mistari hii unapaswa kupatikana. MTC 51.1

Je, wenyekiti wetu wa Makoferensi hawawezi kufungua njia kwa wanafunzi katika shule zetu kushiriki katika nyanja/safu hii ya kazi? Tena na tena imewasilishwa

kwangu kwamba "kuwe na makundi yaliyopangwa na kuelimishwa kikamili zaidi kufanya kazi kama wauguzi, kama wainjilisti, wahudumu, kama wainjilisti wa vitabu, kama wanafunzi wa injili, ili kukamilisha tabia inayolingana na mfano wa Mungu."— Ushuhuda na Uzoefu Uliounganishwa na Loma Linda Sanitarium na Chuo cha Wainjilisti wa Kimatibabu (Pamphlet 095), 15 ,{CH541, 542
). (1906) MTC 51.2

## VIONGOZI WA KANISA WAHUSISHWE

**Viongozi wa Kanisa Kusaidia.—** Kwa ndugu zangu katika nafasi za kuwajibika, ningesema, mahitaji ya miji mikubwa yamewekwa mbele yenu. Mmepokea ujumbe baada ya ujumbe kuhusu wajibu wenu. Na sasa mtafanya ili kaulimbiu ya Bwana iweze kutiiwa?— {manuscript 13, 1910 . MTC 51.3

**Kuchelewa kwa Wakati Kunahitaji Hatua itakayohusisha Maombi Sasa.—** Ikiwa viongozi wetu wangetambua wakati wa usiku, wasingeweza kuiacha miji yetu bila kuonywa na kuwa tayari kufanya kidog tu ili kubadili hali ya sasa ya mambo duniani. Mungu anataka kila nafsi imwaminiyo Kristo iende na kuzaa matunda mengi. ... MTC 51.4

Hebu kuwe na mahubiri machache na kunyenyekesha zaidi roho katika maombi kwa ajili ya uwepo wa Mungu kati yetu. Mikutano yetu inapaswa kuwa majira ya unyenyekevu wa kumtafuta Mungu. Loo! Endapo tungeweza kuhisi hitaji letu la Kristo na kwa imani iliyo hai kudai ahadi ya uwepo Wake!— {Letter 172, 1908 ( Spalding and Magan Collection, 436 ). MTC 52.1

**Viongozi wa Kanisa Wanaopuuza Miji Wanawajibika kwa Mungu.—** Nimeagizwa kuwaambia wale ambao kwa muda mrefu wamesimama kama kichwa cha kazi, na ambao kwa miaka mingi wameruhusu miji yetu mingi mikubwa

ubaki bila kufanyiwa kazi: Bwana atawaita watu waliopanga mipango yao wenyewe kufanya kazi kubwa katika maeneo machache huku wakiwa wameacha kazi iliyopaswa kufanywa katika kutoa ujumbe wa onyo wa mwisho kwa miji mingi mikubwa ya ardhi yetu watoe hesabu. Kumekuwa na roho fulani ya kuwakataza wengine, shauku ya kuwazuia ndugu ambao wanatamani kufanya sehemu ya kazi za mijini. Wengine katika upofu wa mioyo yao wamekuwa wakirudisha nyuma kazi, na hii imeleta kutoamini katika mioyo mingi. Sasa nimeshauriwa kuhusiana na hitaji la kuwekeza nguvu zetu zote na mali zetu zote kwa ajili ya kuendeleza kazi. Tunahitaji kutumia ushawishi wetu katika kuwatia moyo wengine kufanya kazi. Acheni roho ya utendaji iliyotakaswa ihamasishwe, badala ya roho ambayo ingejaribu kurudisha nyuma na kukataza, ndipo kutaonekana maendeleo, pale ambapo zamani kumekuwa na kushindwa kufuata mapenzi ya Bwana.— {Ms.61, 1909 (Ms 10:219 ). MTC 52.2

**Viongozi wa Konferensi kuu (General Conference) Walioitwa Kufanya Uinjilisti** wa miji.— Nimeona kwamba Shetani angefurahishwa sana kuona Wazee [WW] Prescott na [AG] Daniells wakifanya kazi ya mchakato wa kusimamia urekebishaji wa uuzaji wa vitabu vyetu kwa jumla, jambo ambalo limefanya kazi nzuri katika shamba la Bwana kwa miaka mingi. Lakini hakuna hata mmoja wenu aliyeitwa na Mungu kufanya kazi hiyo. Ikiwa mngeingia kwenye kazi kama hiyo, muda wenu mwingi ungetumika huko, wakati ambapo ulipaswa kutolewa kwenye kutangaza ujumbe wa onyo la mwisho kwa ulimwengu usio na toba. MTC 52.3

Bwana angalifurahi kama wewe na Mzee Prescott na washirika wako mngechukua jukumu lenu mara tu baada ya General Konferensi iliyopita mzigo wa kuwapa wakazi wa miji mikubwa ujumbe wa onyo wa mwisho. Hii ni kazi

ambayo amekuwa akituita tuifanye kwa miaka hii mingi.—{Letter 70, 1910 ( Ms 10:364, 365 ). MTC 53.1

**Mwenyekiti wa Konferensi Kuu Aliyeitwa Kufanya Uinjilisti** wa mijini.— Bwana Yesu anamwambia Mwenyekiti wa Konferensi Kuu [AG Daniells], "Neema Yangu yakutosha: kwa maana nguvu Zangu hukamilishwa katika udhaifu." Onya miji. Muda ni wa thamani. Tubu, na uongoke. Tubu, na kuukomboa wakati. Acha kila kitu kifanyike ambacho kinaweza kufanywa ili kulipia uzembe wako wa zamani. ... MTC 53.2

Mzee Daniells, achilia moyo na akili zako ziwekwe wakfu kabisa kufanya mapenzi ya Mungu, na ufanye kazi inayofanana na kazi kama hiyo kwenye familia yako. Chukua kazi iliyopuuzwa kwa muda mrefu katika miji. Mwombe Mungu kwa bidii zaidi ili kuweka akili yako kukimbia katika mikondo sahihi. Bwana hajaweka juu yenu wala juu ya mtu mwingine yeyote katika Washington kazi ambayo wengine wametamani ifanywe.— letter.70, 1910 . MTC 53.3

**Mhariri wa Gazeti la Review and Herald Aliyeitwa Kufanya Uinjilisti wa Jiji.—** Wakati wa General Konferensi ya mwaka 1909 nilisikia ujumbe kwa Ndugu [WW] Prescott. Yeye ni mchungaji. Hapaswi kubaki hapa Washington kufanya kazi ambayo mtu mwingine anaweza kuifanya. Yeye anaweza kusimama mbele ya watu na kutoa sababu za imani yetu kwa njia inayokubalika. Najua hili kwa sababu nimehusishwa naye katika kazi ya Mungu. Ana karama ya yenye thamani, na hapa ameajiriwa katika kazi ambayo wanaume wengine wanaweza kufanya, huku kukiwa na uhaba wa vitendakazi wanaoweza kuonya majiji hayo makubwa. Karama yake haitatumika kwa muda mrefu kama ilivyo sasa, kwani akiendelea kufanya kazi hapa, afya yake na nguvu zitakwisha. Lakini ikiwa ataenda katika

huduma ya hadharani, nguvu zitamjia.— Ms 53, 1909 ( Ms 10:360, 361 ). MTC 53.4

## KUTOA SADAKA YA MISHENI AU UTUME, SI MBADALA WA WEWE KUFANYA KAZI YA MUNGU AU HUDUMA

**Wajibu kwa Miji Hautimizwi kwa Kutoa Matoleo ya Sadaka ya Utume/Misheni.—** Isipokuwa mengi zaidi yamefanywa kwa majiji ya Amerika, wachungaji na walei watakuwa na hesabu nzito ya kusuluhisha na Yule ambaye amemwekea kila mtu kazi yake. … MTC 54.1

Mungu atusamehe uzembe wetu wa wa kutisha katika kutofanya kazi ambayo bado hatujaigusa hata kwa ncha ya vidole vyetu. … MTC 54.2

Baada ya kutoa sadaka kwa ajili ya mashamba ya kigeni, usifikiri kwamba wajibu wako umetimizwa.— {8T.35, 36 . (1904) MTC 54.3

## Sura ya 5—Mkakati wa Kuifikia Miji

### MUNGU ANATAKA KAZI MAHSUSI IFANYIKE KWENYE MA JI JI

**Kazi Kubwa Inahitaji Kufanywa Katika Miji.—** Tena na tena nimeagizwa kuwasilisha kwa makanisa yetu kazi ambayo inapaswa kufanyika katika miji yetu mikubwa. Kuna kazi kubwa ya kufanywa, si tu pale ambapo tuna makanisa ambayo tayari yameanzishwa, lakini pia katika sehemu ambazo Ukweli haujapata kuwasilishwa kikamilifu. Hapa hapa kati yetu kuna wapagani kwa hakika kama tu ilivyo katika nchi za mbali.— {Ms 7, 1908 ( Ev, 32 ). MTC 55.1

**Usingoje Jambo Kubwa Litukie Kabla ya Kuanza.—** Kwa nini tuchelewe kuanza kazi katika majiji yetu? Hatupaswi kungoja mpaka jambo fulani la kushangaza lifanyike, au vifaa vya gharama kubwa kutolewa, ili onyesho kubwa lifanyike. Makapi ni nini kwa ngano? Tukitembea na kufanya kazi kwa unyenyekevu mbele za Mungu, Yeye atatuandalia njia. Atawaheshimu wale wanaomheshimu. Na tuna uhakika kuhisi kuwa watenda kazi katika Takoma Park wanatafuta kumheshimu. MTC 55.2

Kwa nini kuchelewesha jitihada za kufanya ulimwengu kuwa bora zaidi? Haijalishi mzunguko wa maisha yetu ya kila siku ni wa unyenyekevu kiasi gani, au hata kama kazi yetu ni ya chini kiasi gani, tukienenda kwa kupatana na Mwokozi wetu, Yeye atajidhihirisha kupitia sisi, na ushawishi wetu utazivuta roho za watu Kwake. Atawaheshimu wale walio wapole na wa hali ya chini wanaotafuta kwa bidii kumtumikia Yeye katika maisha yao ya kila siku. Katika yote tunayofanya,

iwe tunafanya kazi dukani, shambani, au ofisini,hebu tulete jitihada ya kuokoa nafsi za watu.— {letter. 335, 1904 . MTC 55.3

**Vipaji vya Kipekee Vipo ili Kutimiza Kazi.—** Kazi ya misheni inapaswa kufanywa katika majiji yetu yote makubwa. Kuna talanta maalum kati yetu kwa safu hii ya kazi, na talanta za namna hii zinapaswa kuelimishwa na kufunzwa. MTC 56.1

Wahudumu wanaorandaranda juu ya makanisa wanaleta manufaa kidogo kwa washiriki wa kanisa isipokuwa wawatie moyo na kuwafundisha watu hawa kufanya kazi ya umishenari kwa vitendo (practical mission work). Kila mhudumu sasa ajisikie kwamba kuna kazi kubwa zaidi ya kufanya kuliko kurudia tena na tena mahubiri yale yale kwa watu. ... MTC 56.2

Nimeagizwa kuwarejelea watu wetu kwenye sura ya hamsini na nane ya Isaya. Soma sura hii kwa makini, na uelewe aina ya huduma ambayo italeta uhai katika makanisa. Kazi ya injili inapaswa kubebwa kwa njia ya ukarimu wa mali zetu na vile vile kwa kazi zetu za bidii. Unapokutana na roho zinazoteseka ambazo zinahitaji msaada, uwape huo msaada. Ukiwapata wenye njaa, wape chakula. Mkifanya hivi mtakuwa mnafanya kazi katika mistari ya huduma ya Kristo.... MTC 56.3

Si wajibu wa maafisa wa konferensi kuweka mikono inayozuia kazi inayofanywa katika miji yetu. Kwa makatazo ya ajabu ambayo yametekelezwa katika sehemu fulani, Shetani amekuwa akitafuta kuizingira na kuizuia njia ya Ukweli. Watu hawahitaji kitia-moyo cha kutotenda kazi.— Hati ya 7, 1908 . MTC 56.4

**Watendakazi Bora Zaidi Wachaguliwe.—** Ni lazima tufanye kazi sasa kwa ajili ya upanuzi wa ile Kweli, na kwa

sababu hiyo watu wengi watakuja kwenye ujuzi wa Ukweli katika miji yetu ambayo hadi sasa haijafanyiwa kazi. Vyombo vilivyo bora kabisa ambavyo kanisa linavyo vinapaswa kuchaguliwa na kutumwa, na kudumishwa katika kupanua juhudi za kimishenari.— {AUG, Januari 8, 1902 . MTC 56.5}

**Watendakazi Wanaohitajiwa Wanaoweza Kuifikia Mioyo ya Watu.—** Ni lazima tupange kuweka katika majiji haya makubwa watu wenye uwezo, ambao wanaweza kuwasilisha ujumbe wa malaika watatu kwa msukumo wenye nguvu sana hivi kwamba mioyo itaguswa sana. Wanaume wanaoweza kufanya hivyo, hatuwezi kumudu kuwasanya mahali pamoja, kufanya kazi ambayo wengine wanaweza kufanya.— {R&H, Novemba 25, 1909 . MTC 56.6

**Shetani Anajaribu Kuvuruga Mipango Yetu.—** Tunapoanza kazi kwa bidii kwa ajili ya makutano ya watu katika miji, adui atafanya kazi kwa nguvu kuleta mkanganyiko, akitumaini kuvunja msukumo wa kazi. Wengine ambao hawajaongoka kabisa wako katika hatari ya kufikiria mara kwa mara kuwa mapendekezo ya adui ndiyo uongozi wa Roho wa Mungu. Kama vile Bwana alivyotupa nuru, basi na tutembee katika nuru.— {Ms 13, 1910 ( Ev, 100 ). MTC 57.1

**Visingizio vya Kutofanya Uinjilisti mijini Vinaonyesha Ukosefu wa Maono.—** Niliota kwamba ndugu zetu kadhaa walikuwa kwenye mashauriano, wakishugulikia mipango ya kazi ya msimu huu. Waliona ni vyema wasiingie miji mikubwa, bali waanze kazi katika sehemu ndogo, zilizo mbali na miji; hapa wangekutana na upinzani mdogo

kutoka kwa makasisi na wangeepuka gharama kubwa. Waliona ni vyema kwa wachungaji wetu, ambao ni wachache kwa idadi, wasingeweza kuachwa kuwafundisha na kuwatunza wale ambao wangeweza kukubali Ukweli katika majiji, na ambao, kwa sababu ya upinzani mkubwa zaidi ambao wangekutana nao huko, basi, wangehitaji msaada mkubwa zaidi kuliko ule ambao makanisa katika sehemu ndogo za nchi uhitaji. Hivyo matunda ya kutoa kozi za mihadhara mjini yangepotea kwa kiasi kikubwa. Tena, ilisisitizwa kwamba, kwa sababu ya uwezo wetu mdogo, na kwa sababu ya mabadiliko mengi yanayotokea kwa kuhama ambayo yangeweza kutarajiwa kutoka kwa kanisa katika jiji kubwa, ingekuwa vigumu kujenga kanisa ambalo lingekuwana nguvu kwa kazi hiyo..... . Mume wangu alikuwa aliwahimiza ndugu hawa wawe na mipango mipana zaidi bila kukawia na kuitenda katika miji yetu mikubwa, jitihada iliyotanuka na kamilifu ambayo ingelingana vyema na tabia ya ujumbe wetu. Mfanyakazi mmoja alisimulia matukio ya uzoefu wake katika majiji, akionyesha kwamba kazi ilikuwa karibu kufeli/kushindwa, lakini alishuhudia kufaulu vizuri zaidi katika maeneo madogo. MTC 57.2

Mmoja wa heshima na mamlaka—Mmoja ambaye Yuko katika mikutano yetu yote ya baraza—alikuwa akisikiliza kwa shauku kubwa katika kila neno. Alizungumza kwa uangalifu na uhakikisho mkamilifu. “Ulimwengu mzima,” Yeye alisema, “ni shamba kuu la mizabibu la Mungu. Miji na vijiji vinaunda sehemu ya shamba hilo la mizabibu. Hii miji lazima yafanyiwe kazi.” ... MTC 58.1

Mjumbe akamgeukia mmoja aliyekuwepo na kusema: “Maoni yako ya kazi kwa wakati huu ni finyu sana. Nuru yako isifungiwe kwenye dira ndogo, na kuwekwa chini ya pishi, au chini ya kitanda; lazima iwekwe juu ya kinara, ili iwaangazie wote walio katika nyumba ya Mungu—

ulimwengu wote. Lazima uchukue maoni mapana zaidi ya kazi kuliko uliyochukua."— {7T.34-36 Ms1, 1874). MTC 58.2

## MBINU YA KRISTO KUFIKIA MIJI

**Changanyika na Watu, Utimize Mahitaji Yao, Kisha Waalike Wafuate. —** Kristo alipowatuma wanafunzi kumi na wawili katika safari yao ya kwanza ya umishenari, Aliwaambia, "Mnapokwenda, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia. Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepokea bure, toeni bure." ( Mathayo 10:7, 8 ) MTC 58.3

Kwa wale Sabini waliotumwa baadaye Alisema: "Katika mji wowote mtakaoingia, ... wapozeni wagonjwa waliomo, na waambieni, Ufalme wa Mungu umekaribia kwenu" ( Luka 10:8, 9 ). ... MTC 58.4

Baada ya kupaa kwa Kristo kazi hiyo hiyo iliendelea. Matukio ya huduma Yake Mwenyewe yalirudiwa. ... MTC 58.5

Luka, mwandishiwa Injili inayoitwa kwa jina lake, alikuwa mmishenari wa tiba. Katika Maandiko anaitwa "daktari mpendwa" ( Wakolosai 4:14 ). Mtume Paulo alisikia kuhusu taaluma yake ya utabibu na akamtafuta kama mtu ambaye Bwana alikuwa amemkabidhi kazi ya pekee. Alipata ushirikiano wake, na kwa muda fulani Luka aliandamana naye katika safari zake kutoka mahali hadi mahali. ... Hivyo ndivyo njia ilifunguliwa kwa ajili ya ujumbe wa injili. Ufanisi wa Luka kama daktari ulimpatia fursa nyingi za kumhubiri Kristo kati ya wapagani. Ni mpango wa Bwana kwamba tutafanya kazi kama wanafunzi walivyofanya kazi. Uponyaji wa kimwili unafungamana na agizo la injili. Katika kazi ya

injili, mafundisho na uponyaji hayapaswi kutenganishwa kamwe. ... MTC 58.6

Utoaji wa injili kwa ulimwengu ni kazi ambayo Mungu amekabidhi kwa wale wanaobeba jina Lake. Kwa dhambi na taabu ya dunia injili ndiyo dawa pekee. Kuwajulisha wanadamu wote ujumbe wa neema ya Mungu ni kazi ya kwanza ya wale wanaojua nguvu yake ya uponyaji. ... MTC 59.1

Je, hali ikoje duniani leo? Je, imani katika Biblia si kama ilivyoharibiwa na ukosoaji wa ya juu na uvumi? (ukosoaji wa juu au higher criticism ni ukosoaji wa Maandiko kwa namna fulani) ... MTC 59.2

Kazi kubwa ya matengenezo inahitajika, na ni kwa neema ya Kristo tu kwamba kazi ya urejeshwaji wa kimwili, kiakili na kiroho inaweza kukamilika. MTC 59.3

Njia ya Kristo pekee ndiyo itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na wanadamu kama mtu aliyewatakia mema. Alionyesha huruma Yake kwao, alihudumia mahitaji yao, na akapata imani yao. Kisha akawaambia, "Nifuateni." MTC 59.4

Kuna haja ya kuja karibu na watu kwa juhudi binafsi. Ikiwa wakati mdogo ungetolewa kwa mahubiri kibwetani, na wakati mwingi zaidi ukatumiwa katika huduma ya kibinafsi, matokeo makubwa zaidi yangeonekana. Maskini wanapaswa kutulizwa, wagonjwa kutunzwa, walio na huzuni na waliofiwa kufarijiwe, wajinga kuelekezwa, nawasio na uzoefu kushauriwa. Tunapaswa kulia pamoja na wale wanaolia, na kufurahi pamoja na wale wanaofurahi. Ikiandamana na nguvu ya ushawishi, nguvu ya maombi, na nguvu ya upendo wa Mungu, kazi hii haiwezi, haiwezi kutoka bila matunda.— {MH, 139-144 . (1905) MTC 59.5

**Kristo Alikuja Kukidhi Mahitaji ya Wanadamu.**— Mungu alimtuma Mwanawe ulimwenguni ili Apate

kujifunza kwa uzoefu halisi mahitaji ya wanadamu. Kupitia ubinadamu ulioounganishwa pamoja na Uungu, Ilikuwa lazima Yeye amfikie mwanadamu na kumwezesha kushikilia asili ya Uungu.— Manuscript 73, 1909 ( Sermon and talk 2:318 ). MTC 59.6

**Tabia ya Kazi Ipatane na Kweli Tunazofundisha.**— Kazi inapaswa kuwa yenye ulinganifu, na ushahidi hai wa ile Kweli. Mungu anataka tuthamini matamanio bora. Anatamani kwamba tabia ya kazi yetu ipatane na zile Kweli kuu tunazozichochea ili kuuamsha ulimwengu kutoka katika usingizi wake ulio kama mauti.— {letter 4, 1899 . MTC 60.1

**Fundisha kwa Kielelezo.**— Ni lazima tuishi ile Kweli, na kuifundisha kupitia maisha yetu na kwa maneno yetu. Kuna maelfu ya watu ambao tunaweza kuwafikia, na ambao tunaweza kuwafundisha Ukweli, na hili halihitaji kutumia pesa nyingi ili kufikia miji na majiji jirani. Hatuhitaji kwenda kwa watu wanaoishi kwenye mji mgeni kwetu au mji ambao hatuujui kabisa, lakini kwa watu wanaozungumza Kiingereza, na bado mwaka baada ya mwaka umepita, mwito baada ya mwito kutumwa, na bado wanaume, wanawake, na mali zimefanya kidogo kuendeleza kazi. Je, kweli sisi ni nuru ya ulimwengu?— {Ms.60, 1894. MTC 60.2

## EPUKA MATENDO YALETAYO MAFARAKANO AU MALUMBANO

Epuka Kujenga Kuta za Utengano Bila Sababu.— Bwana haisukumi mioyo ya watenda kazi Wake kuchukua njia ambayo italeta wakati wa taabu kabla ya wakati. Hebu wasijenge ukuta wa utengano kati yao na ulimwengu, kwa kuendeleza maoni na fikra zao wenyewe. Sasa kuna mengi

ya mambo kama haya katika mipaka yetu yote. — {S.T.M &W 3:33, 34 ( T.M.G.W, 202 ). (1895) MTC 60.3

## KUPANGA MIKAKATI KWA HEKIMA

**Wakazi wa Jiji Hawatatujia Sisi.—** Je, tunaweza kutarajia wakaaji wa majiji kuja kwetu na kusema: "Ikiwa mtakuja kwetu na kuhubiri, tutawasaidia kufanya hivi na vile"? Hivi wanajua nini kuhusu ujumbe wetu? Tufanye sehemu yetu katika kuwaonya watu hawa ambao wako tayari kuangamia kwa kutoonywa na kutookoka. Bwana anatamani sisi tuache nuru yetu iangaze mbele ya wanadamu hivi kwamba Roho Wake Mtakatifu aweze kuwasilisha Ukweli kwa wanyoofu wa moyo wanaomtafuta.— { 9T.100 . (1909) MTC 60.4

**Fanya Utafiti wa Sehemu za Kufikia.— Maneno** hayo yalinenwa kwangu: "Waambie watu Wangu kwamba wakati ni mfupi. Kila juhudi inapaswa kufanywa sasa ili kuinua Ukweli. Katika miji, mikubwa na midogo, ujumbe unapaswa kutangazwa. Ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kuunganishwa na ujumbe wa malaika wa pili, na unapaswa kutangazwa kwa nguvu nyingi katika miji yetu mikubwa. Hivyo ndivyo ujumbe utakavyotolewa kwa sauti kuu, ujumbe utakaowatayarisha watu kwa ajili ya kuja kwa Mfalme." MTC 61.1

Hali katika miji yote mikubwa lazima ichunguzwe- kufanyiwa utafiti, ili Ukweli uweze kutolewa kwa watu wote. Katika majiji haya makubwa Bwana ana nafsi nyingi adilifu ambazo zinachanganyikiwa na maendeleo mageni katika ulimwengu wa kidini.— {letter. 88, 1910 ( Matoleo ya Hati 5:128 ). MTC 61.2

**Mahitaji ya Maeneo Yanayopuuzwa kufanyiwa utafiti. —** Kuna mstari mwingine wa kazi unaopaswa kuendelezwa, nao ni kazi katika majiji makubwa. Hebu kuwe na makundi

ya watendakazi wenye bidii wanaofanya kazi mijini. Watu wanapaswa kujifunza kile kinachohitajika kufanywa katika maeneo ambayo yamepuuzwa. Bwana amekuwa akielekeza umakini wetu kwenye makundi ambayo yamepuuzwa katika majiji makubwa, lakini jambo hilo limezingatiwa kwa udogo tu.—{R&H, Novemba 11, 1909 ( F.C. E, 537 ). MTC 61.3

**Kupanga Mikakati kwa Uangalifu kwa kutumia Misaada kadhaa Husaidia Kuzuia Makosa.—** Watu wenye uwezo wanahitajiwa, watu ambao watahesabu gharama kwa uangalifu na kutumia busara katika kufanya maamuzi mema katika kukorokotoa kwao- katika hesabu zao. Ukosefu wa watu wenye uzoefu umekuwa ni hasara kubwa.
... Kazi isisimamiwe na akili ya mtu mmoja au maoni ya mtu mmoja tu. ... MTC 61.4

Itakuwa kosa kujenga au kununua majengo makubwa katika miji... Wale wanaoonekana kufikiri kwamba kuna manufaa kubwa kutenda kwa namna au kufanya kwa mtindo huo hakika hawana ufahamu. MTC 62.1

Kuna kazi kubwa inayopaswa kufanywa katika kutangaza ujumbe wa injili wa wakati huu katika majiji haya makubwa, lakini kujumuisha majengo makubwa kwa ajili ya kazi fulani inayoonekana kuwa ya ajabu imekuwa ni makosa.—{Manuscript 30, 1903 ( sermon and talks 2:226 )
) MTC 62.2

**Upangaji wa Mbaya Mikakati, Huleta Matumizi Yasiyo ya Lazima**. — Nimeumia sana kwa fedha zilizowekezwa katika ujenzi wa majengo ya shule ya ziada huko Battle Creek, wakati jambo hili halikuhitajika. Chuo kilikuwa na ukubwa wa kutosha, kiasi cha kuchukua wanafunzi ambao wangeweza kusimamiwa vyema shuleni. Ukweli wa mambo ni kwamba wasimamizi hawakuweza kuwasimamia vyema wanafunzi ambao

tayari walikuwa wanahudhuria shuleni hapo, kama walivyopaswa kusimamiwa, na pesa zilizowekezwa katika ujenzi wa majengo mapya zilihitajiwa zaidi katika kupanda kiwango cha ile Kweli katika majiji ya Amerika , na katika kufungua mashamba mapya kwa mhudumu au Mchungaji aliye na utendaji wa bidii.— {letter 43, 1895 ( Ms 17:308 ). MTC 62.3

## UONGOZI KATIKA SEHEMU MAHALIA UNAHITAJIKA

**Maamuzi Kuhusu Kazi Mahalia ni vyema Yafanywe katika sehemu Mahalia.—** Mara nyingi mimi hufadhaika sana ninapoona viongozi wetu wakichukua nyadhifa zinazopitiliza, na kujitwisha mizigo ihusuyo mambo ambayo hayapaswi kubebwa au kuhangaika nayo, isipokuwa kuyaacha mikononi mwa Mungu ili Yeye Mwenyewe ayarekebishe. Bado sisi tupo ulimwenguni, na hivyo Mungu hutuweka katika mahali ambapo tutahusiana na ulimwengu, Naye anafanya kazi kwa mkono Wake wa kuume ili kutengeneza njia mbele yetu, ili kazi yake iweze kuendelea katika safu Zake mbalimbali. ... MTC 62.4

Hebu Bwana afanye kazi pamoja na watu walio chini, yaani mahali husika, na wale ambao hawako chini, yaani viongozi wa ngazi za juu, watembee kwa unyenyekevu na Mungu, wasije wakatoka mahali pao, na kupoteza dira yao. Bwana hajaweka mzigo wa kukosoa kazi juu ya wale ambao wamechukua mzigo huu, Nao hawajapewa idhini ya Roho Wake Mtakatifu. Wengi hutembea kulingana na maamuzi yao wenyewe ya kibinadamu, na hutafuta kwa bidii kurekebisha mambo ambayo Mungu hajaweka mikononi mwao. Maadamu tuko ulimwenguni, itatubidi tufanye kazi maalum kwa ajili ya ulimwengu; ujumbe wa onyo unapaswa kwenda kwa nchi zote, lugha, na watu.—

{S.T.M&W Series A 3:32, 33 ( T.M&G.W, 201, 202 ). (1895)
MTC 62.5

**Pesa na Talanta, hivi Vyote Vinahitajika Katika Kazi ya Mungu.—** Wale ambao wameongoka kikweli wameitwa kufanya kazi inayohitaji pesa na kujiweka wakfu. Majukumu yanayotufunga kwa kuweka majina yetu kwenye orodha ya kanisa yanatufanya tuwajibike kufanya kazi kwa uwezo wetu wote kwa ajili ya Mungu. Yeye anataka utumishi usiogawanyika, kwa ajili ya kujitoa kwa moyo wote, nafsi, akili, na nguvu. Kristo ametuleta katika fursa ya kanisa, ili aweze kujihusisha na kuingiza uwezo wetu wote katika huduma ya kujitolea kwa ajili ya wokovu wa wengine. Kitu chochote pungufu ya hii ni kupinga kazi.
... MTC 63.1

Bwana anapanga kwamba mali tulizokabidhiwa zitumike katika kujenga ufalme Wake. Mali Zake huwekwa kwa wasimamizi Wake, ili zichuuzwe au kuzungushwa kwa uangalifu kwenye biashara, na kisha Yeye arudishiwe mapato katika kuokoa roho hata uzima wa milele. ... MTC 63.2

Mungu hufanya kazi na kila mwamini wa kweli, na nuru na baraka zinazopokelewa, hizi hutolewa tena katika kazi ambayo mwamini anafanya. Kadiri anavyotoa katika kile alichopokea, uwezo wake wa kupokea unaongezeka. Anapotoa zawadi za mbinguni, yeye hutoa nafasi ya mikondo mipya ya neema na Ukweli kutiririka ndani ya roho kutoka kwenye chemchemi hai. Nuru kuu zaidi, ujuzi ulioongezeka na baraka, ni Zake. Katika kazi hii, ambayo inahusu kila mshiriki wa kanisa, kuna Uhai na ukuaji wa kanisa ulipo. MTC 63.3

Yeye ambaye maisha yake yamo katika kupokea na kutotoa mara moja hupoteza mibaraka. Ikiwa Ukweli hautiririki kutoka kwake hadi kwa wengine, basi anapoteza

uwezo wake wa kupokea.— {Manuscript 139, 1898 ( This Day With God, 303 ). MTC 63.4

**Fedha Zinazohitajiwa Zitakuja.—** Tunapofanya kazi hii, tugundua kuwa malitaingia kwenye hazina zetu, na tutakuwa na njia za kuendeleza kazi pana zaidi na inayofika mbali zaidi. Tunapaswa kusonga mbele kwa imani, kana kwamba tuna maelfu ya dola. Sisi hatuna nusu ya imani tunayopaswa kuwa nayo. Hebu tutende sehemu yetu katika kuionya miji hii.— {Manuscript 53, 1909 ( Ev, 62 ). MTC 64.1

**Washiriki Walio na Rasilimali za Kifedha Kusaidia Juhudi za Ufikiaji Watu.—** Bwana anawaita wale walio katika nafasi za amana, wale ambao **Amewakabidhi karama Zake za thamani, kutumia talanta zao za akili na uwezo katika huduma Yake.** Watendakazi wetu wanapaswa kuwasilisha mbele ya watu hawa taarifa ya wazi ya mpango wetu wa kazi, tukiwaambia kile tunachohitaji ili kuwasaidia maskini na wenye mahitaji na kuanzisha kazi hii kwa msingi thabiti. Baadhi ya hawa watavutiwa na Roho Mtakatifu kuwekeza mali za Bwana kwa njia ambayo itaendeleza kazi Yake. Watatimiza kusudi Lake kwa kusaidia kuunda vituo vya mivuto katika miji mikubwa (centers of Infuence). Wafanyakazi wenye shauku, wataongozwa kujitoa wenyewe kwa ajili ya safu mbalimbali za jitihada za umishenari.— {7T.112 . (1902) MTC 64.2

**Waongofu Mtajiri Watasaidia Kufadhili Uinjilisti katika miji.**— watu walio na mali wataletwa katika Ukweli na watatoa mali zao ili kuendeleza kazi ya Mungu. Nimeagizwa kuwa kuna fedha nyingi mijini ambazo hazifanyiwi kazi. Mungu ana watu wenye shauku huko. Nenda kwao; kisha uwafundishe kama Kristo alivyofundisha; wape Ukweli. Nao Wataukubali. Ni kitu cha uhakika kwamba kadri nafsi zilizo adilifu zinakavyoongoka, ndivyo mali zao zitavyowekwa

wakfu kwa utumishi wa Bwana, nasi tutaona ongezeko la rasilimali.— {9T.100 . (1909) MTC 64.3

**Mikutano ya Kuhifadhi Pesa za Matumizi katika Maeneo Mapya.— Tunapofikiria** kazi ambayo lazima ifanywe katika Jiji la Washington [DC], na kazi mbalimbali zinazopaswa kufanywa katika nyanja ya Kusini na katika miji ya nchi yetu, inazidi kudhihirika kwamba si jambo la hekima kuruhusu mikusanyiko yetu [hivyo] inyang'anywe vifaa hivi kwamba haiwezi kusaidia katika kuanzisha makumbusho katika nyanja ambazo Mungu ametuagiza tufanye kazi ya pekee.—{Letter 190, 1903 ( Spalding na Magan Collection, 316 ). MTC 64.4

**Kipaumbele cha Kifedha Kimetolewa kwa Kufungua Maeneo Mapya.—** Mungu anahitaji kwamba kila dola inayopatikana itolewe kwa kazi ya kufungua mashamba mapya kwa ajili ya kuingia kwa ujumbe wa injili na katika kupunguza milima ya ugumu inayotaka kufunga kazi yetu ya umishonari. Kwa ajili ya Kristo, ninakuomba utekeleze makusudi ya Mungu ya kufungua misheni katika kila jiji, kila mahali.— {Manuscript 61, 1909 ( Ms.10:216, 217 ).
MTC 65.1

**Tenga Pesa Zaidi kwa Maeneo Mapya.—** Peleka ujumbe katika majiji mapya. Ikibidi, ni lazima tutumie fedha kidogo katika maeneo machache ambapo ujumbe umehubiriwa kikamilifu, ili tuweze kwenda mahali pengine ambapo onyo hilo halijatolewa, na ambako wanaume na wanawake hawajui kuhusu maafa makubwa yanayotokea. karibu kuwajia wote wakaao juu ya nchi. Tuna Neno la Ukweli— amri za Mungu na imani ya Yesu—ili kuwapa watu wa kizazi hiki.— {Manuscript 61, 1909 ( Ms. 10:216 ). MTC 65.2

**Ufadhili Wenye Uwiano Unahitajika Kati ya Kazi ya Sasa na kazi Mpya.—** Bwana anaona kazi ambayo lazima ifanywe katika shamba Lake la mizabibu. Anaona mahali ambapo panapaswa kuwa na kumbukumbu Yake, ili Ukweli uweze kuwakilishwa. Anaona mashamba ambayo hayajafanyiwa kazi na kukosa miundo-mbinu na vifaa. Anahitaji kutoka kwa wote wanaomtumikia usawa na hukumu ya haki. Kiasi kikubwa cha mali haipaswi kufyonzwa katika sehemu moja. Kila jengo litakalojengwa linapaswa kujengwa kwa kuzingatia maeneo mengine ambayo yatahitaji majengo sawa na hayo. ... MTC 65.3

Mungu anawaita wale wanaoshiriki katika utumishi Wake wasizuie fedha kwa kusonga mbele kwa ubinafsi kutumia mahali pamoja au katika mstari mmoja wa kazi fedha zote wanazozipata. Katika sehemu zote za ulimwengu kuna kazi ya kufanywa ambayo ilipaswa kufanywa muda mrefu uliopita. Mungu apishi mbali msitoe wito kwa watu ili mpate fedha ya kukamilisha ... [majengo zaidi kwa ajili ya taasisi fulani], wakati tayari ina majengo mengi katika milki yake, na wakati mna maelfu ya dola mbele yenu. Jenga majengo yako kutokana na uwezo wako kifedha. Na kisha toa sehemu nyingine ya fedha pia kwenye shamba la mizabibu la Mungu, nafasi ya kuwa na miundo-mbinu. Acheni vituo vya misheni vijengwe katika majiji mengine.—{S.T, Series B 6:40 . (1908) MTC 65.4

**Kugawanya Wafanyakazi Hudhoofisha Kazi Katika Maeneo Yote Mawili.—** Katika msimu wa usiku nilikuwa katika mkutano wa baraza ambapo Ndugu Smith Sharp alikuwa anazungumza kuhusu kugawanya timu yawatendakazi wa Nashville [Tennessee] na kuchukua sehemu yake hadi Chattanooga [Tennessee]. Mambo mengine kadhaa yaliletwa. Kisha

Mshauri ambaye hajawahi kukosea alizungumza Maneno ambayo yalibadilisha hali ya hewa yote ya mkutano. Aliweka kanuni ambazo zilionyesha kuwa nguvu kazi ya watu haipaswi kugawanywa. Pesa inayohitajika kutengeneza kituo kimoja, isitumike kutengeneza vituo viwili. Weka nguvu zote katika kituo kimoja, na wekeni nguvu kazi kwa kuungana ili kufanikisha kituo hicho kimoja. Nashville inapaswa kufanywa kuwa kitovu au kituo kikuu, na kutoka humo mwanga utasambaa hadi katika mikoa iliyo ng'ambo yake. Iwapo mapendekezo yaliyosisitizwa na Ndugu Smith Sharp yatafuatwa, seti mbili za majengo zitalazimika kujengwa, wakati ambapo kuna uhaba wa fedha wa kuwezesha sehemu moja kufanikiwa. Kujaribu kutenganisha kazi kwa kuisimamisha katika sehemu mbili kungedhoofisha nguvu za sehemu zote mbili. Fanya kazi ya sehemu moja iwe kamili na inayojitegemea kwa kadiri iwezekanavyo.— {letter. 79, 1901 . MTC 66.1

**Matumizi ya Pesa Ili Kuongozwa na Usawa, Haki, na Hukumu.—** Kuwekeza pesa isivyofaa na kuinua kazi katika sehemu moja ya shamba la Bwana ambayo kuna kazi ya jiji inayopaswa kufanywa katika maeneo mengi si jambo la kufaa au busara. Huo ni ubinafsi na kuwa na tamaa. Bwana hushutumu aina ya mambo kama hayo, kwa vile kwa kufanya hivyo, kazi Yake takatifu inawakilishwa vibaya mbele ya ulimwengu. Yeye angetaka kazi Yake idhibitiwe na kuongozwa kwa usawa, haki, na hukumu. Yeye hatoi wito wa kujengwa kwa taasisi kubwa. Kona moja ya shamba la mizabibu sio ulimwengu wote. Katika sehemu nyingi duniani kote, kumbukumbu za Mungu zinapaswa kuanzishwa ili kuwakilisha Ukweli Wake. Na mwenendo wa busara kama huo unapaswa kufuatwa hivi kwamba tutasimama katika miji yetu mikubwa kwa mtazamo wenye busara kiasi kwamba wale wasio wa imani yetu watatupatia msaada kwa mali zao. Kila sentituliyo nayo ni ya Mungu. “Fedha ni mali

Yangu, na dhahabu ni mali Yangu, asema BWANA wa majeshi” ( Hagai 2:8 ). MTC 66.2

Lakini wengine hawatambui mamlaka Yake kama Mmiliki. Ingawa kazi katika sehemu ya shamba ambako wanafanya kazi tayari ina miundo-mbinu mingi, hawa wanaendelea tu kuchota kutoka katika hazina ya Bwana. Hawafikirii sehemu zenye mahitaji shambani mwa Bwana, wale wanaohitaji miundo-mbinu kama ile waliyo nayo tayari, na kwamba ni lazima hawa wasaidiwe. Hawa wanapaswa kufanya kazi kwa usongo na bidii ili kuandaa miundo- mbinu kwenye mahali pengine kuliko kufikiri kwamba inahitajika kuwa kwenye shamba lao? Wote wanapaswa kuzingatia kwamba kuna majiji ambayo hayajawahi kuwa na ujumbe huo.— {Manuscript 53, 1903 ( Ms. 13:406, 407 ). MTC 67.1

**Wivu Juu ya Pesa Huzuia Kazi Kuendelea.—** Kwa miaka mingi, kazi katika miji mewasilishwa mbele yangu, na imesisitizwa kwa watu wetu pia. Maagizo yametolewa ili kufungua uwanja mpya. Wakati mwingine kumekuwa na vihofu vya wivu kwamba mtu ambaye alitaka kuingia katika nyanja mpya anaweza kupokea fedha kutoka kwa watu ambao walidhani anatafutwa kwa kazi nyingine. Wengine walio katika nyadhifa za uwajibikaji wamehisi kwamba hakuna jambo lolote linalopaswa kufanywa bila ujuzi na kibali chao binafsi. Kwa hiyo wakati mwigine watendakazi wafanyao kazi kwa ufanisi wamecheleweshwa na kuzuiwa, na magurudumu ya kubeba maendeleo na kuingia mashamba mapya yamesogea mbele kwa shida/uzito.— {Manuscript. 21, 1910 ( MM, 302 ). MTC 67.2

**Wahudumu Hawapaswi Kulemewa na Taarifa za Kinagaubaga Za Kazi ya Jiji.—** Sijui ni lini wahudumu

wetu watajifunza kuachia mambo ya biashara na fedha. Nimeonyeshwa tena na tena kwamba hii si kazi ya huduma ya kichungaji. Hawapaswi kulemewa sana na maelezo ya kina kuhusu kazi ya jiji. Wanapaswa kuwa na utayari kwenda mahali ambapo matamanio ya injili yameamshwa katika ujumbe, na hasa kuhudhuria mikutano yetu ya kambi. Hawapaswi kurandaranda juu ya majiji wakati ambapo mikutano hii inaendelea.— {Manuscript 104, 1902 ( Ms 17:52 ). MTC 67.3

**Ukuaji wa Kiroho na Ukuaji wa Kanisa Huendana sambamba na Bidii ya Umishenari wa Washiriki.—** Utauwa na ujuzi wa Maarifa ya juu ya hali ya kiroho na ukuaji wa kanisa vinalingana na bidii, utauwa, na akili ya kimisionari ambayo imeletwa ndani yake, na kutekelezwa ndani ili kuwa baraka kwa wale ambao wanahitaji msaada wetu zaidi. Ninawasihi tena kutafamarj Isaya 58 , ambayo inafungua shamba kubwa la mizabibu ambalo litafanyiwa kazi katika mistari ambayo Bwana ametaja. Wakati hili litafanyw,a kutakuwa na ongezeko la chemchemi ya maadili, na kanisa halitabaki katika hali ya kukaribia kusimama tena. —(M 14a, 1897 (SDA BC, EGW. Commemts 4:1148). MTC 69.1)

**Ukuaji wa Kiroho Hutokana na Huduma hai.—** Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kushiriki katika mstari fulani wa huduma kwa ajili ya Bwana. Wengine hawawezi kufanya mengi ukilinganisha n awengine, lakini kila mtu anapaswa kufanya yote awezayo ili kurudisha nyuma wimbi la magonjwa na dhiki ambalo linaloufagia ulimwengu wetu. ...(MTC 69.2)

Hakuna kitu kitakachoamsha usongo wa kujitoa nafsi mhanga, na kupanua na kuimarisha tabia kama kushiriki

katika kazi kwa ajili ya wengine. Wengi wanaojiita kwua ni Wakristo, katika kutafuta mahusiano na kanisa wanajifikiria wenyewe tu. Wanatamani kufurahia ushirika wa kanisa na matunzo ya kichungaji. Wanakuwa washiriki wa makanisa makubwa yenye mafanikio ya kiuchumi, na wanaridhika kufanya kidogo tu kwa ajili ya wengine, na kwa njia hii wanajipora wenyewe baraka zenye thamani zaidi. ...(MTC 69.3)

Miti iliyosongamana kwa karibu haikui kiafya, uimara na kuwa mizito. Mkulima huipandikiza miche yake ili ipate zipate nafasi ya kukua. Kazi kama hiyo ingenufaisha washiriki wengi waliomo katika makanisa makubwa. Hawa wanahitaji kuwekwa mahali ambapo nguvu zao zitatumiwa na kushugulishwa katika jitihada hai ya utendaji ya Kikristo. Wanapoteza maisha yao ya kiroho, kwa kuwa mbilikimo wa kiroho na watu wasio na ufanisi, kwa kukosa kufanya kazi ya kujitolea kwa ajili kwa wengine. Kama watu hawa wangepandikizwa kwenye shamba fulani la umishenairi, basi wangekuwa na nguvu, afya na nishati. (MTC 69.4)

Lakini sisi hatuitaji kungoja mpaka tuitwe kwenye kwenye uwanja fulani wa utume ulio mbali kabla ya kuanza kuwasaidia wengine pale tulipo. Milango ya huduma iko wazi kila pahali. Wote wanaotuzunguka ni wale wanaohitaji msaada wetu. Wajane, yatima, wagonjwa na walio kifoni, watu ambao wana huzuni au maombolezo, watu ambao wamevunjika moyo, watu wajinga kwa vile hawajui, na waliotengwa na jamii, wapo kila upande.— (TMH, 149-152 . (1905) MTC 70.1)

## KRISTO MFANO MKAMILIFU

**Tabia ya Kristo, Si Kuhubiri Tu, Inahitajika.—** Nilihudhuria mkutano wa wachungaji wa asubuhi. Baraka ya Bwana ikaja juu yangu, nami nikanena kwa

udhihirisho wa Roho wa Mungu na kwa nguvu. Kuna wale ambao wanatengeneza duara kubwa. Bwana amemtoa Kristo kwa ulimwengu kwa huduma. Kuhubiri Neno peke yake, hiyo sio huduma. Bwana anatamani watumishi Wake wanaohudumu wakae katika nafasi inayostahili kutiliwa umaanani wa hali ya juu zaidi. Katika mawazo ya Mungu, huduma ya wanaume na wanawake ilikuwepo kabla ya ulimwengu huu kuumbwa. Aliazimia kwamba wahudumu Wake wawe na kielelezo kikamilifu cha Yeye Mwenyewe na makusudi Yake. Hakuna taaluma ya mwanadamu ambayo ingeweza kufanya kazi hii; kwa maana Mungu alimtoa Kristo katika ubinadamu kufanya kazi Yake jinsi inavyofaa na kikamilifu kwa kile ambacho mwanadamu anaweza kuwa kupitia utiifu kamili kwa mapenzi na njia Yake. Tabia ya Mungu ilidhihirishwa katika maisha ya Mwanawe. Kristo hakushikilia tu nadharia ya huduma ya Kweli, bali katika ubinadamu Wake alitoa kielelezo cha huduma ambayo Mungu anaikubali. Ukamilifu umebainisha kila kipengele cha huduma ya Kweli. Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, hakuishi kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa Mungu.— (Ms 23, 1891 ( MR 18:380 ). MTC 70.2)

**Kristo Alijishusha Mwenyewe Ili Kuwainua Wenye Dhambi kwa Uzima wa Utukufu.—** Tunapotazama ukarimu wa Kristo kwa maskini na wanaoteseka,subira Yake kwa wasio na adabu, wajeuri na wajinga, kujikana Kwake nafsi na kujitolea Kwake dhabihu, tunazama katika sifa na heshima/kicho. Ni zawadi iliyoje ambayo Mungu amemkabidhi mwanadamu, aliyetengwa Naye kwa dhambi na kutotii! Naam, Hebu moyo uvunjike na machozi yatiririke kwa kutafakari upendo huu usioweza kuelezeka! Kristo alijishusha Mwenyewe kwenye ubinadamu ili Aweze kumfikia mwanadamu aliyezama ndani ya kina cha majanga/ole na udhalilishaji, na kumwinua katika maisha bora zaidi.— (SP 2:286. (1877) MTC 71.1)

**Ukristo wa Kweli kwa Vitendo.—** Ulimwengu unahitaji uthibitisho wa Ukristo wa dhati. Sumu ya dhambi inatenda kazi katika moyo wa jamii. Miji na majiji imezama katika dhambi na upotovu wa maadili. Ulimwengu umesheheni magonjwa, mateso, na uovu. Karibu na mbali, zipo roho zilizo katika umaskini na dhiki, zimelemewa na hisia ya hatia na kuangamia kwa kukosa mvuto unaookoa. Injili ya Ukweli huwekwa mbele yao daima, lakini bado wanaangamia kwa sababu kielelezo cha wale wanaopaswa kuwa harufu ya uzima kwao ni harufu ya mauti. Nafsi zao hunywa uchungu kwa sababu chemchemi zimetiwa sumu, wakati zinapaswa kuwa kama kisima cha maji yabubujikiayo kwenye uzima wa milele. (MTC 71.2)

Chumvi lazima ichanganywe na dutu ambayo inaongezwa (chumvi na chakula); lazima ipenye, iingie na kuwa kila mahali, ili iweze kuhifadhiwa. Hivyo ni kwa njia ya mawasiliano ya kibinafsi na ushirika ndivyo ambavyo watu wanafikiwa na uwezo wa kuokoa wa injili. Hawaokolewi kama umati, bali kama watu binafsi. Mvuto binafsi ni nguvu. Ni kufanya kazi na mvuto wa Kristo, kuinua pale Kristo anapoinua, kutoa kanuni sahihi, na kuzuia maendeleo ya uharibifu wa ulimwengu. Ni kusambaza neema hiyo ambayo Kristo peke yake anaweza kutoa. Ni kuinua, kufanya maisha na tabia za wengine kuwa na ladha tamu kwa uwezo wa kielelezo safi kilichounganishwa na imani na upendo wa dhati.—(PK, 232 . (1917) MTC 71.3)

**Ubinafsi Wote Utakomeshwa.—** Iwapo Waadventista Wasabato sasa wataamka na kufanya kazi waliyopewa, Ukweli utawasilishwa katika miji yetu iliyopuuzwa katika

mistari iliyo wazi, iliyo tofauti na katika nguvu za Roho. Wakati kazi inafanywa kwa moyo wote, ufanisi wa neema ya Kristo utaonekana. Walinzi juu ya kuta za Sayuni watakuwa macho sana, na kuwaamsha wengine. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wa bidii na waaminifu katika kazi yao kwa ajili Yake hivi kwamba uchoyo/ubinafsi wote utatenganishwa na maisha yao. Watenda kazi wake watatazamana jicho kwa jicho (kwa kukubaliana), na ... nguvu ambayo ilionekana katika maisha ya Kristo, itafunuliwa. Imani itarudishwa, na kutakuwa na umoja katika makanisa katika safu zetu zote.— (TC 9:32, 33 . (1909) MTC 71.4)

**Wahudumu ili Kuwa na Urafiki na Maskini.—** Kila mhudumu wa injili anapaswa kuwa rafiki kwa maskini, wanaoteseka, na waliokandamizwa kati ya watu wanaoamini wa Mungu. Kristo alikuwa daima rafiki wa watu maskini, Naye alilinda masilahi ya watu maskini kwa utakatifu. Mara nyingi sana kumekuwa na upungufu wa ajabu wa huruma ya Kristo na shauku ya upendo kwa maskini na wanaoteseka. Upendo, mtakatifu, upendo uliosafishwa, unapaswa kutekelezwa
kwa ajili ya watu maskini na wale waliokumbwa na majanga kwa bahati mbaya.—(Letter 168, 1909 ( MM, 310 ). MTC 72.1)

## WATENDAKAZI WALIOELIMISHA NI MUHIMU KWA KAZI YA MIJINI

**Akili Zilizokuzwa vyema, na sio Watu wajinga wasiojua, Zinahitajiwa.—** Akili zilizokuzwa vyema zinahitajika sasa katika kila sehemu ya kazi ya Mungu; kwa kuwa wajinga, wasiojua kitu hawawezi kufanya kazi hiyo ipasavyo katika kufunua hazina iliyofichwa ili kuboresha/kutajirisha nafsi. Mungu amebuni kwamba

shule ziwe chombo cha kuendeleza wafanyakazi kwa ajili ya Yesu Kristo ambaye hatawaonea haya, na lengo hili lazima liwe mbele yetu na kuangaliwa daima. Marefu ambayo mwanadamu anaweza kuyafikia kwa utamaduni wa akili unaofaa hayajafikiwa hadi sasa. Miongoni mwetu tuna zaidi ya wastani ya watu wenye uwezo. Ikiwa uwezo wao ungetumika, tunapaswa kuwa na wachungaji ishirini mahali ambapo sasa tunaye mmoja tu. Madaktari, pia, wangeelimishwa kupigana na magonjwa.— (STM &W, Series A 3:22 (TM &G W, 195). (1895) MTC 72.2)

**Kujifunza Asili ya Kibinadamu kwa Makini, na kwa Sala Kwahitajiwa.—** Inahitaji ujuzi wa asili ya kibinadamu, kujifunza kwa ukaribu, kufikiri kwa umakini, na sala ya bidii, ili kujua jinsi ya kuwafikia wanaume na wanawake juu ya mambo makuu yanayohusu ustawi wao wa milele.— (G W, 92 . (1915) MTC 73.1)

**Uelewa wa Ubinadamu Unahitajika.—** Yule anayetafuta kuubadilisha ubinadamu lazima yeye mwenyewe aelewe ubinadamu. Ni kupitia huruma, imani, na upendo tu ndipo wanaume na wanawake wanaweza kufikiwa na kuinuliwa.— (Ev, 78 . (1903) MTC 73.2)

**Utamaduni wa Kiakili Wahitajiwa.—** Utamaduni wa kiakili ni kile sisi kama watu tunachohitaji, na kile tunachopaswa kuwa nacho ili kukidhi mahitaji ya wakati.— (T C 4:414 . (1880) MTC 73.3)

**Ukuaji Unaoendelea Ni Muhimu.—** Wanaume walio katika vyeo vya kuwajibika wanapaswa kujiboresha daima. Hawapaswi kushikilia uzoefu wa zamani na kuhisi kwamba si lazima kuwa wafanyakazi wa kisayansi.— (TC 4:93 . (1876) MTC 73.4)

**Elimu ya Kisayansi ni Muhimu.-** Nimemwandikia [WC White] kuhusiana na wanafunzi, na nimemsisitizia umuhimu wa maboresho katika suala la kupata elimu

katika masuala ya fani zozote za kisayansi. Haya yote yamefunuliwa kwangu kwa muda fulani, na nimezungumza na watu kadhaa kuhusu umuhimu wa kuch angamkia juu ya jambo hili.— (Letter 43, 1895 . MTC 73.5)

## WAKE KWA WAUME WANAHITA JIKA KATIKA HUDUMA MBALIMBALI

**Huduma ya Aina Zote Ndiyo Kazi ya Juu Zaidi.—** Kazi ya juu kuliko zote ni huduma (au huduma ya Uchungaji) katika mistari yake mbalimbali, na inapaswa kuwekwa mbele ya vijana kwamba hakuna kazi iliyobarikiwa zaidi na Mungu kuliko ile ya mhudumu wa injili (au Mchungaji- gospel minister). (MTC 73.6)

Hebu vijana wetu wasizuiwe kuingia kwenye huduma. Kuna hatari kwamba kupitia uwakilishi unaong'aa wengine watavutwa kutoka nje ya njia ambayo Mungu amewaagiza watembee. Wengine wametiwa moyo kuchukua kozi ya masomo ya tiba ambayo wanapaswa kujitayarisha ili kuingia katika huduma. Bwana anaita watu zaidi kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu. Maneno haya yalisemwa, "Imarisheni vituo vya misheni vilivyo nje ya miji (outpost centers): muwe na walinzi waaminifu katika kila sehemu ya dunia." Mungu anawaita ninyi vijana. Anaita majeshi yote ya vijana wenye mioyo mikubwa (mioyo ya ukarimu) na wenye mawazo mapana ambayo yaweza kuchukuliana na mawazo ya wenzao bila ya ubaguzi au kutishwa, na walio na upendo wa kina kwa Kristo na Ukweli.— (GCDB, Mch 2, 1899, p. 129 ( C H, 558 ). MTC 74.1)

**Wanaojitolea Wanahitajika Kufanya Kazi ya Kueneza Injili.—** Bwana anaita watu wanaojitolea ambao watachukua msimamo wao kwa uthabiti upande Wake na watajitolea wenyewe kuungana na Yesu wa Nazareti katika

kufanya kazi inayohitajika kufanywa sasa hivi. Vipawa vya watu wa Mungu vinapaswa kutumika katika kutoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Bwana anawaita wale waliounganishwa na shule zetu na nyumba za tiba mbadala na sahili yaani Sanitarium na nyumba za uchapishaji, kufundisha vijana kufanya kazi ya uinjilisti. Wakati na pesa zetu havipaswi kuwekezwa kwa kiasi kikubwa katika kuanzisha nyumba za tiba sahili yaani Sanitarium, viwanda vya chakula, maduka ya chakula, na migahawa ya chakula cha afya hivi kwamba kazi zingine zipuuziwe. Vijana wa kiume na wa kike wanaopaswa kushiriki katika huduma,

katika kazi ya Biblia, na katika kazi ya uinjilisti wa vitabu, hawapaswi kuhusishwa tu na kazi ya shuguli za kila siku (mechanical work). (CP, T, & S, 494, 495. (1913) MTC 74.2

## WAFANYAKAZI WANAO JITEGEMEZA WENYEWE

**Wafanyakazi wa Wanaojikimu Mahitaji yao Wenyewe Wahitajiwa kwa Maeneo Yasiyofikiwa (Self Supporting Missionaries).—** Katika sehemu nyingi wamishonari wanaojitegemea wanaweza kufanya kazi kwa mafanikio. Paulo aliyekuwa mmishenari wa kujitegemea alifanya kazi kwa bidii katika kusambaza maarifa ya Kristo ulimwenguni pote. Wakati alipokuwa akifundisha injili kila siku katika miji mikubwa ya Asia na Ulaya, alikuwa akitumia stadi yake ya ufundi ili kujikimu yeye na wenzake (kutengeneza mahema)…… … (MTC 74.3)

Ulimwenguni kote, wajumbe wa rehema wanahitajika. Kuna mwito kwa familia za Kikristo kwenda katika jumuiya zilizo katika giza na makosa, kwenda katika mashamba ya kigeni, ili kufahamu mahitaji ya wanadamu wenzao, na kufanya kazi kwa ajili ya kazi ya Bwana. Ikiwa familia kama hizo zingetulia katika mahali

penye giza duniani, mahali ambapo watu wamefunikwa na giza la kiroho, na kuacha nuru ya uhai wa Kristo iangaze kupitia kwao, kazi nzuri na kubwa ingeweza kutimizwa.— (M H, p. -156 . (1905) MTC 75.1)

**Mungu Hukubali Hata Vipaji Hata Vidogo au Vyenye Mipaka Katika Utumishi kwa Wengine.—** Je, hakuna wanaume na wanawake katika kutaniko hili ambao wana kazi ya kumfanyia Bwana? Je, hakuna wale hapa ambao wanapaswa kwenda katika maeneo mapya na kufanya kazi kama wamishenari? Tunahitaji wamishenari nyumbani; na tunahitaji wamishenari ambao wataenda katika nyanja mpya, na kuona kile wanachoweza kufanya. Fanya biashara kwa talanta yako moja au talanta mbili. Ingawa talanta yako inaweza kuwa ndogo au yenye mipaka, Mungu ataikubali. Kwa nini uizike ardhini? Nenda kafanye kazi, na ufanye uwezavyo, na Mungu atakupa matunda kwa kazi yako. Lo! Ni afadhali nije kwa Bwana na miganda iliyokusanywa kuliko kuwa na hazina za dhahabu na fedha. Nipe roho kama matunda ya kazi yangu, na sitaomba maisha yenye urahisi au bwerere katika ulimwengu huu. Je, hakuna wanaume na wanawake hapa ambao Mungu atawaita watoe hesabu kwa uwezo aliowapa? Kuna nafsi ambazo utazifanyia kazi; kuna vijana ambao unapaswa kuwasihi. Kuna kazi ya kufanywa katika mstari wa afya na kiasi; na wewe umeketi hapa tu, nawe umekuwa ukisikiliza Ukweli Sabato hadi Sabato, na, huku roho zikiangamia karibu nawe. Kwa nini usiruhusu nuru ambayo Mungu amekupa iangaze kwenye njia ya wengine? Ninakusihi ufikirie jambo hili kwa uzito.— (R & H, De 18, 1888 . MTC 75.2)

## ROHO YA KU JITOA MHANGA INAHITA JIKA

**Fanya kazi katika Roho ile ile ya Kujidhabihu kama Mwanzo.—** Kazi inapaswa kufanywa katika sehemu zote

za shamba la mizabibu. Katika siku za mwanzo za ujumbe mwanzo mzuri na sahihi ulifanywa, lakini kazi haijaendelea jinsi Mungu alivyotaka iendelezwe. Kazi imejikita zaidi katika miji ya Battle Creek Na Oakland, na katika maeneo mengine machache. Ndugu zetu hawakupaswa kamwe kujenga kwa kiasi kikubwa katika sehemu moja kama walivyojenga huko Battle Creek. Katika maeneo mengi, machache sana yamefanywa ili kuanzisha kumbukumbu za Mungu. Hii ni kosa. Miaka mingi iliyopita wafanyakazi na watu wetu wengi walikuwa na roho ya kujikana nafsi na kujidhabihu. Mafanikio yalionekana katika juhudi zao. Bwana ameashiria kwamba kazi yake inapaswa kuendelezwa katika roho ile ile ambayo ilianzishwa. Ulimwengu unapaswa kuonywa. Maeneo na maeneo bado kufanyiwa kazi. Je, sisi kama watu, kwa matendo yetu, kwa mipango kazi yetu, kwa mtazamo wetu kuhusiana na ulimwengu ambao haujaokolewa, tutoe ushuhuda tofauti kabisa na ushuhuda tuliopewa miaka ishirini au thelathini iliyopita? Je, tutoe uthibitisho wa ugonjwa wa kiroho na ukosefu wa mipango yenye hekima? Juu yetu kumeangaza nuru kuu kuhusiana na siku za mwisho za historia ya dunia hii. Macho yetu yanapoona roho zikiangamia katika dhambi, tunapaswa kuamshwa ili kutoa nuru ya Ukweli wa sasa kwa wale walio gizani sasa. Wajumbe wa Mungu lazima wavikwe nguvu. Ni lazima wawe na kicho kwa ajili ya Ukweli ambao kwa hivi sasa hawaumiliki. Ujumbe mtakatifu wa Bwana wa onyo lazima utangazwe sio tu katika makanisa yetu, bali katika maeneo magumu zaidi na katika miji yenye dhambi nyingi—katika kila mahali ambapo nuru ya ujumbe wa malaika wa tatu bado haijapambazuka. Kila mmoja anapaswa kusikia mwito wa mwisho wa kuja kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo.— (L 128, 1902 ( The Kress Collection, 72,
73 ). MTC 75.3)

## KUJAZWA NA ROHO MTAKATIFU

**Roho Mtakatifu Huwatia Nguvu Watendakazi.—** Wote wanaotamani nafasi kwa ajili ya huduma ya Kweli, na ambao watajitoa wenyewe kwa Mungu bila kujibakiza, watapata nafasi katika uinjilisti wa vitabu fursa kuhubiri juu ya mambo mengi yanayohusu wakati ujao, na maisha ya kutokufa, yale ya milele. Uzoefu utakaopatikana utakuwa wa thamani zaidi kwa wale wanaotaka kupata stahiki kwa ajili ya huduma. Ni kuwepo kwa Roho Mtakatifu wa Mungu ndiko kunakowatayarisha watenda kazi, wanaume na wanawake, kuwa wachungaji wa kundi la Mungu. Wanapolithamini sana wazo kwamba Kristo ni Mwenza wao, kicho kitakatifu, furaha takatifu, vitahisiwa nao katikati ya uzoefu wao wote wa mitihani na majaribu yao yote. Watajifunza jinsi ya kuomba wanapofanya kazi. Wataelimishwa katika subira, fadhili, ukarimu, na usaidizi. Watajizoeza adabu, na uungwana, wa kweli wa Kikristo, wakikumbuka kwamba Kristo, Mwandamani wao, hawezi kukubali maneno makali na yenye ujeuri, yasiyo na fadhili au hisia kama hizo. Maneno yao yatatakaswa-Yatakuwa masafi (hakuna matusi au maneno mabaya). Nguvu ya usemi itachukuliwa kuwa talanta ya thamani, waliyokopeshwa ili kufanya kazi ya juu na takatifu. Wakala wa kibinadamu atajifunza jinsi ya kumwakilisha Rafiki wa Mungu ambaye anahusishwa naye. Kwa Yule aliye Mtakatifu na asiyeonekana, kicho/heshima na staha vitaonyeshwa staha kwa sababu amevaa nira Yake na anajifunza njia Zake safi, na takatifu. Wale walio na imani katika Mtumishi huyo wa mbingu, watasitawisha. Watapewa uwezo wa kuuvisha ujumbe wa Ukweli uzuri mtakatifu.— (T C 6:322 . (1900) MTC 76.1)

## KUWATAYARISHA WAMISHONARI WA TIBA

**Wachungaji na Madaktari Waliojipatia sifa, Wote Wanahitajika.—** Ninafurahi kwamba kuna wale wanaotamani kuwa wamishenari wa tiba. Lakini wote hawawezi kuwa wamishenari wa tiba kwa maana nzima ambayo inabebwa sasa. Kuna wale ambao lazima wahitimu kwa sifa zinazostahili kazi inayofanywa sasa katika kuleta ujumbe wa mwisho wa onyo kwa majiji yote na katika miji yote katika sehemu zote za ulimwengu wetu. Hawawezi kujishughulisha wenyewe kwa idadi fulani ya miaka ili kujifunza kazi ya mmishenari wa tiba. Ingawa wengine wanahisi kwamba hiyo ni kazi yao na kuchagua kujiweka chini ya kufundishwa na kuzoezwa kwa ajili ya kazi hiyo (training), wengine wanahisi kwamba ni lazima wajifundishe na wajizoeze kuwa wahudumu waaminifu, wachungaji stadi wa
kundi la Mungu, ili watoe nyama kutoka ghala kwa majira yake, kwa ajili ya

kondoo na wana-kondoo.— (Lt 86a, 1893 ( The Ellen G. White 1888 Materials, 1148 ). MTC 77.1)

**Wauguzi Wamishenari Wanapaswa Kuelimishwa na Madaktari.—** Katika shule zetu wauguzi wamishenari wanapaswa kupokea masomo kutoka kwa matabibu wenye sifa zinazostahili, na sehemu ya elimu yao inapaswa kujifunzwa jinsi ya kupigana na magonjwa na kuonyesha thamani ya tiba za asili. Kazi hii inahitajika sana. ... Mungu anawaita wanamatengenezo kusimama katika ulinzi wa sheria aliyoiweka ili kutawala mfumo wa kimwili. Wakati huo huo wanapaswa kudumisha kiwango cha juu katika kuzoeza akili na utamaduni wa moyo, ili Tabibu Mkuu ashirikiane na mkono wa kibinadamu katika kufanya kazi ya rehema na ya lazima katika kutuliza mateso.— (T C 6:136 . (1900) MTC 77.2)

## VIJANA WAFUNZWE KUFANYA KAZI YA MIJINI

**Vijana Wanaweza Zaidi Kuhudumia Mahitaji ya Watu.—** Iwapo vijana katika miji yetu wangeunganisha jitihada zao ili kupunguza uasi na uhalifu, ushawishi wao ungeendeleza sana kazi ya matengenezo. Ni fursa na wajibu wa kila kijana, kama malaika wa rehema, kuhudumia mahitaji na shida za wanadamu. Hakuna tabaka linaloweza kupata matokeo makubwa zaidi kwa Mungu na wanadamu kuliko vijana.—{ Signs of the Times, Novemba 3, 1881 . MTC 78.1

**Vijana Wanapaswa Kufundishwa Kuwa Watu Wazima Wenye Manufaa.—** Nia ya kweli ya utumishi inapaswa kuwekwa mbele ya wazee na vijana. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kwa njia ambayo watakua wanaume na wanawake wenye manufaa. Kila njia itakayowainua na

kuwatukuza ni ya kuajiriwa. Wanapaswa kufundishwa kutumia nguvu zao kwa njia bora zaidi.— (R & H, Mei 26, 1904 . MTC 78.2)

**Vijana Kuwa Baraka kwa Jamii.—** Wanafunzi shuleni walipaswa kuamshwa hisia zao za kimaadili kuona na kuhisi kwamba jamii ina madai juu yao, na kwamba wanapaswa kuishi kwa utii wa sheria ya asili, ili waweze, kwa kuwepo kwao na mvuto wao, kwa kanuni na mfano, kuwa faida na baraka kwa jamii. Inapaswa kusisitizwa kwa vijana kwamba wote wana uvutano ambao daima unaizungumzia jamii, kwa kuboresha na kuinua, au kupunguza na kudhalilisha.— (C P, T, & S, 84 . (1913) MTC 78.3)

**Vijana Watapata Usaidizi wa Mungu.—** Mungu atawasaidia vijana wetu kama alivyomsaidia Danieli, ikiwa watajisalimisha bila kujibakiza kama ambavyo Danieli alifanya, na kuthamini fursa za kukua katika ufahamu. Atawapa hekima na maarifa, na ataijaza mioyo yao na kutokuwa na ubinafsi. Ataweka ndani ya akili zao mikakati inayopanuka, na atautia moyo tumaini na ujasiri wanapotafuta kuwaleta wengine chini ya utawala wa Mkuu wa amani.— (M 38, 1904 ( Mrs 4:125 ). MTC 79.1)

**Viongozi Wenye Uwezo na Stadi Waweke Viwango vya juu vya Maadili Mbele ya Vijana Wafanyakazi.—** Umakini mkubwa zaidi unapaswa kutolewa kwa kuzoeza na kuelimisha wamishenari kwa kurejelea kwa njia maalumu kazi katika majiji. Kila kundi la wafanyakazi linapaswa kuwa chini ya uongozi wa kiongozi mwenye uwezo wa kusimamia vyema, na daima inapaswa kuwekwa mbele yao kwamba wanapaswa kuwa wamishenari kwa maana ya juu zaidi ya neno hilo. Kazi

kama hiyo yenye utaratibu, ikifanywa kwa hekima, ingeleta matokeo yenye baraka. (MTC 79.2)

Kitu kimefanywa katika mstari huu, lakini mara nyingi sana kazi imedumaa na kwenda chini, na hakuna kitu cha kudumu ambacho kimekamilika. Sasa kuna haja ya kufanya kazi kwa dhati na bidii. Vijana wanaokwenda katika kuajiriwa katika kazi ya General Konferensi (Konferensi Kuu) wanapaswa kuelewa kwamba wao hawapaswi kuhubiri tu, bali kuhudumu, kutenda kama wanaume waliolemewa na jukumu zito la kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.— (L . 34, 1892 ( MM, 301). MTC 79.3)

**Vijana Hujifunza Kutokana na Kufanya Kazi na Wafanyakazi Wenye Uzoefu.—** Vijana wengi ambao wamekuwa na aina ifaayo ya elimu nyumbani, wanapaswa kufunzwa/kuzoezwa kwa ajili ya utumishi na kutiwa moyo kuinua kiwango cha Ukweli katika maeneo mapya kwa kazi iliyofanyiwa mipango vizuri na ya uaminifu. Kwa kushirikiana na wachungaji wetu na wafanyakazi wenye uzoefu katika kazi ya jiji, watapata mafunzo na mazoezi bora zaidi. Wakitenda chini ya mwongozo wa Bwana na kutegemezwa na sala za watendakazi wenzao wenye uzoefu zaidi, wanaweza kufanya kazi nzuri na yenye baraka. Wanapounganisha kazi zao na zile za watenda kazi wazee, wakitumia nguvu zao za ujana kwa njia bora kabisa, watakuwa na watendakazi wenzi wa malaika wa mbinguni; na kama watendakazi pamoja na Mungu, ni fursa yao kuimba na kuomba na kuamini, na kufanya kazi kwa ujasiri na uhuru. Ujasiri na tumaini ambavyo uwepo wa mawakala ya kimbingu utaleta kwao na kwa wafanyakazi wenzao vitaongoza kwenye sala na sifa na usahili wa imani ya kweli. (MTC 79.4)

Hakupaswi kuwa na uchelewesho katika juhudi hii iliyopangwa vizuri ya kuwaelimisha washiriki wa kanisa.

Watu wanapaswa kuchaguliwa kufanya kazi katika miji mikubwa, ambao wamejiweka wakfu kikamilifu na ambao wanaelewa utakatifu na umuhimu wa kazi hiyo. Usitume wale ambao hawana sifa stahidi katika mambo haya. Watu wanahitajika ambao watasukuma ushindi wa msalaba, ambao watakuwa na ustahimilivu chini ya kukatishwa tamaa, dhiki na ufukara, ambao watakuwa na bidii, kudhamiria na imani ambayo ni ya lazima kwenye uwanja wa umishenari. Na kwa wale ambao hawashiriki kibinafsi katika kazi hii, ningesema: Msiwazuie wale walio tayari kufanya kazi, bali wapeni moyo na kuwategemeza/sapoti— (T C 9:119 . (1909) MTC 80.1)

**Wafanyakazi Wenye Uzoefu Kuandamana na Wamishonari wa Tiba Walio Vijana.—** Kuna kazi kubwa sana inayopaswa kufanywa katika kuwakomboa wanadamu wanaoteseka, na kupitia kazi ngumu ya wanafunzi wanaopokea elimu na mafunzo ya kuwa wamishenari wa tiba wenye ufanisi, hivyo watu wanaoishi katika majiji mengi waweze kufahamiana nao. ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu. Viongozi waliojiweka wakfu na walimu wenye uzoefu wanapaswa kwenda nje na wafanyakazi hawa vijana mwanzoni, wakiwapa maelekezo jinsi ya kufanya kazi. Wakati upendeleo wa chakula hutolewa na wale wanaomcha na kumheshimu Mungu, neema hizi zinaweza kukubaliwa. Hivyo fursa itapatikana kwa mazungumzo, kufafanua Maandiko, kwa kuimba nyimbo za Biblia na kusali pamoja na familia. Kuna wengi ambao kazi kama hii ingethibitisha kuwa baraka kwako. — (T & E C LLS& CME (Pamphlet 095), 15, 16 ( CH, 542 ). (1906) MTC 80.2)

**Watu walio Katika NdoaWanapaswa Kusimamia Vijana Wanaofanya Kazi.—** Misheni inapaswa kuunganishwa na watu waliofunga ndoa ambao watajiendesha kwa uadilifu mkali kabisa. … (MTC 80.3)

Ingawa wanaume na wanawake wanaoongoza misheni zetu wana tabia safi kama dhahabu safi, wanahitaji muunganiko wa kudumu na Mungu ili kujiweka safi na kujua jinsi ya kuwasimamia vijana kwa busara, ili wote wayaweke mawazo yao bila kuchafuliwa, kutiwa doa au uharibifu. Hebu masomo na yawe ya tabia iliyoinuliwa, yenye kuheshimika na bora, ili akili ijazwe na mawazo safi na adhimu/bora. — (M 19a, 1890 (G.C.D.B, February 6, 1893, p. 162). MTC 81.1)

**Elimu ya Vijana Wanaofanya Kazi Inapaswa Kuwa Kamilifu.—** Walimu wenye hekima na uzoefu watahitajika [kufundisha katika chuo kipya huko Washington, DC]— wanaume na wanawake wanaoweza kuwapa vijana masomo ya biashara, na wanaoweza kuwafundisha pia, jinsi ya kufanya kazi ya umishenari ya kweli. Hakuna kinachopaswa kupuuzwa kitakachotoa mafunzo na mazoezi kamili katika kanuni zinazofaa. — (R & H, Mei 26, 1904 . MTC 81.2)

**Vijana Watendakazi Wasio na malengo na wanaofanya mchezo hukosoa na Kudharau Juhudi za Kuwafikia Watu.—** Bwana ana watu wengi ambao ni wa thamani katika miji yetu mikubwa, hawa wanapaswa kufikiwa na Kweli za pekee za wakati huu. Lakini mwenendo unaofuatiliwa na vijana wa kiume na wa kike wanaohusishwa na misheni ni wa mchezo-mchezo tu, usio na umakini, unaoshusha kazi au kupunguza thamani yake, na kuvunja moyo wa misheni. Wahusika hao wenye kasoro humtenga Mungu kutoka kwenye vyumba vya misheni. Hatuhitaji wiki au miezi kusoma tabia za wafanyakazi wengi. Mwenendo wao ni chukizo kwa Mungu. Kuna makosa yaliyopo katika jamii ambayo Wakristo hawayatendi, bali wanayachukia. Wale ambao ni wapuuzi, wanaofanya mambo kimchezo-mchezo na wenye nia ya kimwili wakiachiwa kuwa katika misheni zetu, mvuto wao utaelekea

kwenye kupunguza kila kitu kinachohusiana na misheni.— (G.C.D.B, Febr 6, 1893, uk. 162 . MTC 81.3)

## SHULE ZA UIN JILISTI KWENYE MA JI JI

**Kujikita katika Kuwatayarisha Wafanyakazi wa Jiji.—** Tukiwa kama watu wa imani, hatufanyi hata sehemu moja ya hamsini ya yale tunayoweza kufanya kama wamishonari wenye utendaji wa bidii. Endapo tungehuishwa na Roho Mtakatifu, kungekuwa na wamishenari mia moja mahali ambapo sasa kuna mmoja tu, katika kila mji kunapaswa kuwa na kikosi cha wafanyakazi waliopangwa na wenye nidhamu; sio mmoja au wawili tu, ila kadhaa wanaofanya kazi hapo...... . ... Uangalifu zaidi unapaswa kutolewa kwa kufunza na kuelimisha wamisionari kwa marejeleo maalum ya kazi katika miji.— (G.C.D.B, Jan 30, 1893, uku. 37 . MTC 81.4)

**Mazingira yanayofanana na ya Nyumbani ni mazuri katika Kuwazoeza Wafanyakazi Wamishonari.—** Ndugu na Dada [Stephen na Hetty] Haskell wamekodisha nyumba katika mojawapo ya sehemu bora zaidi za jiji [Nashville], na wamekusanya kuwazunguka familia ya wasaidizi, ambao siku baada ya siku huenda kutoa masomo ya Biblia, kuuza majarida yetu, na kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Wakati wa saa ya ibada, wafanyakazi wanasimulia mambo waliyojionea na uzoefu wao. Mafunzo ya Biblia yanaoongozwa majumbani, na vijana wanaume na wasichana wanahusishwa na misheni hiyo hupata uzoefu kamili na unaofaa wa kutoa masomo ya Biblia na kuuza machapisho yetu. Bwana amebariki kazi zao, watu kadhaa wamekubali Ukweli, na wengine wengi wamekuwa na matamanio nayo. (MTC 82.1)

Wavuvi walioacha nyavu zao kwa mwito wa Kristo walizoezwa na kufunzwa kazi kwa njia hii. Kazi kama hiyo

inapaswa kufanywa katika miji mingi. Vijana wanaotoka kufanya kazi katika miji hii wanapaswa kuwa chini ya uongozi wa viongozi wenye uzoefu na waliojitoa wakfu. Hebu wafanyakazi wapewe familia nzuri (good home), mahali ambapo watapata mafunzo kamili. Bwana ana kazi ya thamani na takatifu ya kuokoa roho, inayopaswa kufanywa ulimwenguni, na inapaswa kufanywa sasa. Kazi hii yapasa kuendelezwa kwa kiwango cha juu zaidi na kuhusisha wajibu binafsi wa mtu, kuliko wakati mwingine wowote.— (R & H, Sept 7, 1905 . MTC 82.2)

**Mafunzo ya Kuhusisha Kazi binafsi na Mikutano ya Watu Wote**.— La umuhimu sawa na jitihada za umma ni kazi ya nyumba kwa nyumba kwenye miji ya watu. Katika miji mikubwa kuna madaraja fulani ambayo hayawezi kufikiwa na mikutano ya hadhara. Hawa lazima watafutwe kama mchungaji atafutavyo kondoo wake waliopotea. Jitihada ya kibinafsi na ya bidii lazima itolewe kwa niaba yao. Wakati kazi ya binafsi inapopuuzwa, fursa nyingi za thamani hupotea, ambazo vinginevyo zingeboreshwa, nazo zingeendeleza kazi hiyo kwa kudhamiria. (MTC 82.3)

Tena, kama tokeo la uwasilishaji wa Ukweli katika makutaniko makubwa, roho ya kuuliza-uliza imeamshwa, na ni muhimu hasa kwamba shauku hiyo iweze kufuatiliwa na kazi ya kibinafsi. Wale wanaotamani kuchunguza Ukweli wanahitaji kufunzwa kwamba wajifunze wenyewe Neno la Mungu kwa bidii. Mtu lazima awasaidie kujenga juu ya msingi thabiti. Katika wakati huu nyeti na wa dharura katika uzoefu wao wa kidini, ni muhimu kiasi gani kwamba watendakazi wa Biblia walioongozwa kwa hekima, waje kuwasaidia, na kuwafungulia uelewa wao wa hazina ya Neno la Mungu! (MTC 83.1)

Kazi iliyosawazishwa vizuri inaweza kufanywa vizuri zaidi mijini wakati shule ya Biblia ya kuzoeza na kufunza

wafanyakazi inapoendelea. Wanaounganishwa na shule hii ya mafunzo au misheni ya jiji wanapaswa kuwa watenda kazi wenye uzoefu na ufahamu wa kina wa kiroho, watu ambao wanaweza kuwapa watendakazi wa Biblia (Bible Workers) mafundisho ya kila siku, na ambao wanaweza pia kuungana kwa moyo wote katika jitihada za umma kwa ujumla . Na wanaume na wanawake wanapoongoka kwa Ukweli, wale wanaosimama kwenye kichwa cha misheni wanapaswa, kwa maombi mengi, kuwaonyesha hawa waongofu wapya jinsi ya kupata uzoefu wa nguvu ya Ukweli mioyoni mwao. Misheni kama hiyo, ikiwa inafanywa na wale wanaojua jinsi ya kusimamia kwa hekima, hakika itakuwa nuru ing'aayo mahali penye giza.— (G W, 364, 365 . (1915) MTC 83.2)

## MIKATABA YA ELIMU

**Mafunzo Yanayoambatana na Mkataba wa Utumishi.—** Kabla ya watu kupokelewa katika shule zetu za mafunzo ya misheni, acha kuwe na makubaliano yaliyoandikwa kwamba baada ya kupokea elimu yao watajitolea kwa muda fulani kwa kazi. Hii ndiyo njia pekee ambayo misheni zetu zinaweza kufanywa jinsi inavyopaswa kuwa. Waache wale wanaojiunganisha na misheni wawe wanyoofu wanaposhugulikia ajenda mbambali, na washikilie kazi kwa namna mashirika yanavyoendeshwa kwa kuweka umakini wa biashara inayoshugulikiwa (fanya huduma hii businesslike! Iwe na faida na kanuni zilizowekwa kufuata). Wale wanaotawaliwa na hisia ya wajibu, ambao kila siku hutafuta hekima na msaada kutoka kwa Mungu, watatenda kwa akili, si kutokana na ajenda au nia zenye binafsi, bali kutokana na upendo wa Kristo na Ukweli. Watu kama hao hawatasita kujitoa bila kujibakiza, nafsi, mwili, na roho, kwa kazi hiyo. Watajifunza kazi au shuguli hiyo, na kuifanya hiyo kazi, na kuomba kwa ajili ya maendeleo yake.— (G.C.D.B, Februari 6, 1893, pg162, 163 . MTC 83.3)

## UZOEFU WA UIN JILSTI WA JI JINI UNATAKIWA

**Uzoefu katika Uinjilisti wa Jiji Huimarisha Imani.—** Wale ambao wamesongamana katika Battle Creek na kuzuiliwa huko huona na kusikia mambo mengi ambayo yanaelekea kudhoofisha imani yao na kuchochea kutoamini au kuwa na hatari ya kutoamini. Watu hawa angepata maarifa ya vitendo zaidi katika jitihada ya kuwapa wengine yale wanayopokea kutoka katika Neno la Mungu. Wanapaswa kutawanyika na kufanya kazi katika miji yetu yote chini ya mafunzo ya watu wazima katika imani (waliokomaa zaidi). Ikiwa wale wanaofundisha wafanyakazi hawa ni wakweli na waaminifu, kazi kubwa itatimizwa. (MTC 84.1)

Kunapaswa kuwa na kazi katika miji yetu ambayo haijawahi kufanyiwa kazi. Yale ambayo yangepaswa kufanywa miaka ishirini iliyopita, naam/ndiyo, zaidi ya miaka ishirini iliyopita, sasa yanapaswa kufanywa haraka. Kazi itakuwa ngumu zaidi kufanya sasa kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita, lakini lazima itafanywa. (MTC 84.2)

Kazi yetu inafanywa kuwa ngumu kupita kiasi kwa sababu ya nadharia nyingi za uongo ambazo wainjilisti hukutana nazo kwenye kazi, na kwa sababu ya upungufu wa walimu wenye ufanisi na wasaidizi walio tayari.— (Lt 277, 1905 ( The Paulson Collection, 109, 110 ). MTC 84.3)

**Kukataa Kutumia Talanta Hatimaye Huzifanya Zisitoe Manufaa au zisizo na faida wala maana (useless).—** Unaweza kukunja mikono yako ukisema, “Mimi ni mshiriki wa kanisa tu; kazi hiyo haina matumaini kwangu kufanya.” Lakini je, wewe umefungwa nira pamoja na Kristo? Je, unafanya kazi katika njia Yake? Loo, hebu wewe usiwe tena chanzo cha huzuni kwa wenye akili za mbinguni na kwa

Yeye ambaye amelipa bei isiyo na kikomo kwa ajili ya nafsi, hata ukakataa kuwa mifereji ya nuru, hata ukakataa kushirikiana na mawakala wa mbinguni kwa ajili ya wokovu wa roho! Lakini na 'tuamke kutoka usingizini,' na tutie uwezo wetu wote tuliopewa na Mungu katika kazi hiyo, ili iandikwe katika vitabu kwamba 'tunaukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. Ikiwa tunazifanya talanta zetu kukaa bila kazi,basi, tunapoteza uwezo wote wa kuzitumia. Akili ni zawadi ya Mungu, iliyokusudiwa kuboreshwa na kukuzwa, ili tuweze kuwaangazia wengine kwa nuru; lakini akili inaweza kupotoshwa vibaya na kutumiwa vibaya katika kufanya kazi ya Shetani.— (R & H, Apr 21, 1896 . MTC 84.4)

## WAZEE WASIPANGIWE KUFANYA KAZI MIJINI

**Huduma ya Jiji Haishauriwi kwa Wazee au Wanyonge.—** Wanaume na wanawake walio na umri mdogo au wazee hawapaswi kutumwa kufanya kazi katika majiji yasiyo na afya, yenye watu wengi. Waache hawa wafanye kazi mahali ambapo maisha yao hayatatolewa dhabihu bila sababu. Ndugu zetu wanaoleta Ukweli kwenye miji hawapaswi kulazimika kuhatarisha afya zao katika kelele, misukosuko na machafuko ya miji, ikiwa maeneo ya yaliyo matulivu yanaweza kupatikana.— (L 168, 1909 ( MM, 309 ). MTC 85.1)

## Sura ya 7—Njia za Kufundisha na Kuvuna Washiriki wa Kanisa Waagizwe Jinsi ya Kufanya Kazi

**kwa ajili ya Wengine.—** Ni wajibu wa wale wanaosimama kama viongozi na walimu wa watu kuwafundisha washiriki wa kanisa jinsi ya kufanya kazi katika safu za umishenari na kisha kuanzisha operesheni ya kazi kuu, ya kutangaza ujumbe kwa upana mwingine, ujumbe huu ambao lazima uamshe kila mji ambao haujafanyiwa kazi kabla ya shida kuja, wakati, kwa njia ya utendaji wa mawakala wa kishetani, milango iliyofunguliwa sasa kwa ujumbe wa malaika wa tatu itafungwa. Mungu anahitaji kwamba tutoe ujumbe wa Ukweli wa sasa kwa kila mji, na tusiifungie kazi hiyo katika sehemu chache. Popote ambapo fursa Kwa ajili ya ile Kweli yaweza kupatikana, watu na wasimame ambao wanaweza kutoa mafundisho ya Ukweli kwa nguvu na usadikisho utakaoifikia mioyo.—(M .61, 1909 (Ms. 10:215, 216). MTC 86.1)

**Washiriki wa Kanisa Wajifunze Kuwagawia Wengine Ukweli.—** Kweli hiyo yenye thamani, na iokoayo, imerudiwa tena na tena kwa washiriki wa kanisa letu, wakati katika miji ambayo makanisa yetu yamepangwa, kuna nafsi zinazoangamia kwa kukosa ujuzi ambao washiriki wa makanisa yetu wangeweza kutoa. Vita vikali havijulikani, labda kwa udogo sana. Ikiwa waamini wangekuwa macho kabisa, wangetafuta fursa za kueneza nuru, wangepata kazi nyingi za kufanya. Umakini, unyofu, kiasi, ufunuo wa hisia ya wajibu mzito ambao uko juu ya wafuasi wa Kristo, ungeegemea na kuleta nguvu katika kuupenda Ukweli. Wale ambao ni Wakristo wenye kujidhabihu watagusa mioyo ya majirani na kuwavutia kuishi maisha ya utauwa yaliyo na utendaji. Watafanya kazi kwa dhati na bidii katika utumishi wa Bwana, wakionyesha sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani

kuingia katika nuru Yake ya ajabu. Watatii agizo la Kristo, "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni." Kila mshiriki wa kanisa anapaswa kujifunza jinsi ya kuwasilisha nuru kwa wengine walioketi gizani. Hebu kila mmoja azilinde roho za watu "kama wale ambao lazima watatoa hesabu."— (R & H, Juni 11, 1895 . MTC 86.2)

## TANGAZA, NA KUHUBIRI UKWELI WA BIBLIA

**Anza kwa Kuwasilisha Injili kwa Uwazi kwa Kadiri Iwezekanavyo, (Watu waweze kuelewa kirahisi).**— Kuna kazi takatifu, iliyowekewa wakfu, na nzito ambayo inapaswa kufanywa katika kuinua kiwango cha juu miongoni mwa wale ambao bado hawajasikia mwito wa kwanza kabisa wa karamu ya injili. Kila aina ya kazi lazima ije kwa mpangilio wake. Tunapaswa kuinua sauti na kutangaza ujumbe kwenye barabara kuu, na kuwakusanya wote watakaokuja kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Jambo hili tunalifanya. Tunaweka mikutano yetu ya kambi katika majiji na miji ambako ujumbe wa Ukweli wa sasa bado haujasikiwa. Hatuwatangazii watu hawa masomo ya mafundisho makuu ya Biblia (doctrines) ambayo hawana uelewa nayo. Jambo la kwanza kabisa na la maana zaidi ni kuyeyusha na kuitiisha roho kwa kumwasilisha Bwana wetu Yesu Kristo kama Ndiye mchukua-dhambi, Mwokozi Mwenye kusamehe dhambi, na kuifanya injili iwe wazi kwa kadri iwezekanavyo.— (Lt. 4, 1899 . MTC 87.1)

**Fichua Kweli za Neno la Mungu kwa Wale Watakaosikiliza.**— Katika miji na majiji yetu kuna nafsi zinazoishi bila kuzijua Kweli za Neno la Mungu; wengi wanaangamia katika dhambi. Wengine huja kwenye

nyumba zetu za ibada kwaajili ya udadisi tu. Hebu basi kila hubiri/hotuba inatolewa iwe ufunuo wa zile Kweli kuu zinazohusika kwa wakati huu. Fumbua mafumbo ya ukombozi mbele ya wanafunzi shuleni na mbele ya makutano wanaokusanyika kusikia Neno la Mungu. Hii ni elimu inayohitajika kwa wenye elimu na wenye visomo vidogo. Elimu ya juu kabisa itapatikana katika kusoma siri na fumbo la utauwa. Kweli kuu za Neno la Mungu, zikiaminiwa na kupokewa na kuchukuliwa katika mazoezi ya maisha, zitaleta matunda ya elimu ya hali ya juu zaidi.— (C.P.T, & S, 398. (1913) MTC 87.2)

**Kweli ya Biblia Inapaswa Kutangazwa kwa Usahili Ili Wote Wapate Kuelewa.—** Bwana anazungumza na watu Wake wakati huu, akisema, Pata mpenyo wa kuingilia katika miji, na utangaze Ukweli kwa usahili na kwa imani. Roho Mtakatifu atafanya kazi kupitia juhudi zako kugusa mioyo. Usilete fundisho la Biblia geni katika ujumbe wako, lakini sema maneno rahisi ya injili ya Kristo (doctrine), ambayo vijana kwa wazee wanaweza kuelewa. Wasio na elimu ya darasani pamoja na walioelimika wanapaswa kufahamu Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, nao lazima wafundishwe kwa usahili/urahisi. Ikiwa ungewaendea watu kwa njia inayokubalika, jinyenyekesheni mioyo yenu mbele za Mungu na mjifunze njia Zake.— ( R & H, Jan 18, 1912 ( MM, 299 ). MTC 88.1)

**Fichua Kweli ya Biblia kwa Kasi inayoendana tu na Uelewa wao.—** Jana usiku katika saa zangu za kulala nilionekana kuwa ninakutana na ndugu zangu, nikamsikiliza Mmoja aliyesema kama mwenye mamlaka. Huyu alisema, “Roho nyingi zitahudhuria mkutano huu ambao kiukweli hawajui kabisa kuhusu Ukweli ambao utawasilishwa mbele yao. Watasikiliza na kuwa na shauku, kwa sababu Kristo anawavuta; dhamiri inawaambia

kwamba yale wanayoyasikia ni kweli, kwa kuwa ina Biblia kwa msingi wake. Umakini mkubwa unahitajika katika kushughulika na roho hizi. ... Usitambulishe mwanzoni kabisa mbele ya watu mambo yatakayowachukiza zaidi au yenye kuleta upinzani katika imani yetu, ili usije ukafunga masikio ya wale ambao mambo haya huwajia kama ufunuo mpya. (MTC 88.2)

"Hebu vipande hivyo vya Ukweli vishugulikiwe kwa kadiri wawezavyo kupata uelewa na kuvithamini; kadri siku zinavyoendelea kwenda, japo mafundisho hayo yataonekana kuwa ya ajabu na ya kushangaza, wengi watatambua kwa furaha kwamba nuru mpya inatolewa juu ya Neno la Mungu; ilhali wakati Ukweli unatolewa kwa kipimo kikubwa, wasingeweza kuupokea, na hivyo wengine wangeondoka, na wasirudi tena. Zaidi ya haya, wangeweza kuupotosha Ukweli; katika maelezo yao ya kile kilichozungumzwa tayari, wangepotosha Maandiko hata kuvuruga akili za wengine. Lazima tunufaike na hali tuliyo nayo sasa. Wasilisha Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. Ni lazima pasiwe na roho ya ugomvi, malumbano au mabishano katika kuitetea Ukweli."— (Ms 44, 1894 ( S.T.M.W, Series A, 3:13, 14 ). MTC 88.3)

### MADA KUU YA KUHUBIRIWA

**Wengi Wanajua Tu Yale Wahubiri Wao Huwaambia.—** Watu hawajui chochote kuhusu Ukweli. Hawajui chochote kuhusu sababu za kuamini kile tunachoamini katika imani yetu. Wanaamini kile ambacho wahudumu/wachungaji wa kanisa wanawaambia. Je, sisi hatupaswi kufanya juhudi yoyote ile ili hawa wajue Ukweli ni upi kwa wakati huu? Je, ni nini kifanyike katika miji hii, bila pesa, ni nini tuanze kufanya basi? Ikiwa unaendelea kuona maeneo ambayo

unadhani unaweza kutumia fedha hapo na kunufaisha kazi, je, nchi hizo ambazo umeshaona manufaa hayo ya injili ziachwe tu na ardhi yake isikatuliwe au
isilimwe wala kupandwa? (Kupandwa Neno la Mungu) Je, Bwana atapendezwa na aina hii ya upuuziaji?— (Lt 9a, 1893 ( Ms.11:7 ). MTC 89.1)

**Hubiri Ishara za Kurudi Kwa Upesi kwa Kristo. —** Tunahisi kwamba wakati umefika wa jitihada zilizoamuliwa kufanywa katika miji yetu. Soma sura ya ishirini na moja ya kitabu cha Luka. Huu ndio ujumbe tunaopaswa kuubeba. Ni ujumbe mzito zaidi kwa wakati huu. — (Lt. 160, 1906 . MTC 89.2)

**Sabato ya Siku ya Saba Inapaswa Kusisitizwa (Jumamosi na siyo Jumapili).—** Kuna mahali pengi ambapo fedha zinapaswa kutengwa ili kufanya vita vikali katika miji na majiji kuhusiana na mahubiri ya hadhara ya kwenye mahema, na kuinua makanisa ambayo yanapaswa kuwa kumbukumbu za Ukwelina haki. Kila pigo la nyundo linapaswa kuzungumza kwa ajili ya Mungu na Sabato Yake takatifu. Jambo hili linapaswa kusimama na kuwa kipaumbele katika kazi yetu yote kwa uwazi na pia kutamkwa, ili liwe ushahidi kwamba siku ya saba ndiyo ishara, muhuri wa Mungu.— (Lt. 45, 1900 (Manuscript Releases 9:88 ). MTC 89.3)

## MAHUBIRI YA HADHARA KWENYE MIJI MIKUBWA

**Kukodisha Kumbi au Sehemu Zingine Zinazofaa kwa ajili ya Mikutano ya Watu Wote.—** Mahali ambapo Ukweli haujulikani, akina ndugu ambao wamejizoeza katika kufanya kazi wanaweza kukodi kumbi, au mahali pengine pa kufaa kukutanikia, na kuwakusanya pamoja wote wanaokuja. Kisha wawafundishe watu Ukweli. Hawahitaji kuhubiri, bali wachukue Biblia, na kumwacha Mungu

aseme moja kwa moja kutoka katika Neno Lake. Ikiwa kuna idadi ndogo tu ya watu waliopo, wanaweza kusoma “Bwana asema hivi,” bila gwaride kubwa au msisimko; wewe soma tu na kuuelezea Ukweli sahili wa injili, na kisha imba na kusali pamoja nao.— (R & H, Sept 29, 1891 . MTC 89.4)

**Jitihada za Kiinjilisti zinahusisha Ufuatiliaji.—** Katika jitihada zetu za kuwafikia watu, kuna hatari ya kutumia mbinu ambazo hazitaleta matokeo bora. Mipango inaweza kufuata, ambayo inaweza kuonekana kama vile inasisimua au kuonyesha shauku za watu kwa wakati huo; lakini athari inathibitisha kuwa kazi haidumu. Matumizi ya gari la injili huenda yakatimiza mema au manufaa fulani; lakini katika hali nyingi matokeo ya baadaye yatakuwa ya kukatisha tamaa. Watu watavutiwa na muziki na watasikiliza mahubiri na miito inayotolewa. Lakini watenda kazi hupita upesi, wakisafiri kutoka mahali hadi mahali, na hakuna wakati wa watu kuimarishwa katika imani baada ya mahubiri. Kuguswa moyo kulikofanywa hivi karibuni kutatokomea. Mbegu ndogo iliyopandwa, itachipua na kuzaa matunda. Msimu utakapokwisha, kutakuwa na miganda michache ya kukusanywa. ... (MTC 90.1)

Katika sehemu nyingi ni kana kwamba imekaribia kutowezekana kupata mpenyo wa kuwa na nyumba yoyote ya ibada. Ubaguzi, husuda, wivu vina nguvu sana hivi kwamba mara nyingi hatuwezi kupata mahali pa kuzungumza na watu Neno la uzima. Ikiwa mikutano ya kambi inaweza kufanywa katika maeneo tofauti, wale wanaotaka kusikia wanaweza kupata fursa. Roho zenye njaa ya mkate wa uzima zitalishwa. (MTC 90.2)

Badala ya kuwa na mikutano ya makambi mikubwa katika maeneo machache mahalia, mazuri zaidi

yangefanywa mara nyingi kwa kuwa na mikutano midogo katika sehemu nyingi. Acheni hili lifanyike katika miji na majiji ambako ujumbe wa Ukweli wa sasa haujawasilishwa.
… (MTC 90.3)

Jambo hili linapaswa kufuatiliwa na mkutano wa hema na kazi ya Biblia. Wafanyakazi wenye uzoefu pamoja na wasaidizi wao wanapaswa kubaki shambani ili kuwatafuta wote wenye matamanio na injili. Wanapaswa kufanya kazi kana kwamba wanatafuta kondoo waliopotea. Wengi waliokuja kwenye mkutano wa kambi ili tu kusikia au kuona jambo fulani jipya watavutiwa na Ukweli, na
wengine watachukua msimamo wao wa kutii.. …(MTC 90.4)

Katika mikutano hii hatupaswi kwanza kuwasilisha masomo ya mafundisho makuu ya imani (Doctrines), ambayo wasikilizaji hawana ufahamu. Shikilia usikivu wa watu kwa kuwasilisha Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. Jambo la kwanza kabisa na la muhimu zaidi ni kuyeyusha moyo na kuitiisha nafsi kwa kumwasilisha Bwana wetu Yesu Kristo kama Mwokozi Mwenye kusamehe dhambi. Weka mbele ya watu msalaba wa Kalvari. Ni nini kilisababisha kifo cha Kristo? Uvunjaji wa sheria. Onyesha kwamba Kristo alikufa ili kuwapa wanadamu nafasi ya kuwa raia waaminifu wa ufalme Wake.(MTC 91.1)

Hebu Ukweli uwasilishwe, si kwa mahubiri/hotuba ndefu zilizo ngumu, bali kwa mazungumzo mafupi, yanayokita moja kwa moja kwenye pointi. Elimisha, elimisha, kuhusiana na huduma kamili, huduma ya nafsi yote. Kujiweka wakfu kabisa, maombi mengi, kuwa dhati na kuwa n abidii kubwa, kutagusa moyo; kwa kuwa malaika wa Mungu watakuwepo ili kuifanya mioyo ya wasikilizaji iguswe. (MTC 91.2)

Hebu kuwe na uimbaji na muziki wa ala. Vyombo vya muziki vilitumiwa katika huduma za kidini nyakati za zamani. Waabudu walimsifu Mungu kwa kinubi na matoazi, na muziki unapaswa kuwa na nafasi yake katika ibada zetu. Huu utaongeza shauku ya watu. — (M 3, 1899 ( General Conference Daily Bulletin, Machi 2, 1899, p. 128 ). MTC 91.3)

Mikutano ya Hadhara Hufaa Katika Maeneo Fulani.— Ni lazima majiji yafanyiwe kazi zaidi. Kuna maeneo ambayo watu wanaweza kufikiwa vyema kwa mikutano ya wazi, yaani nje ya majengo. Kuna wengi wanaoweza kufanya kazi katika nyanja hii hii, lakini lazima wawe wamejivika silaha zote za haki. Sisi kwa ujumla ni dhaifu sana katika kazi yetu; lakini bado uadilifu (maadili mema) na akili timamu yaani busara, vinahitajika.—(M 139, 1898 (An Appeal for Missions [Pamphlet 004], 15 ).MTC 91.4)

## VIPAZA SAUTI KWENYE MIKUTANO YA KAMBI

**Vipaza Sauti vyenye Ubora kwa Kadri inavyowezekana, Vitumike katika Mikutano ya Kambi ya Jiji. —** Sisi sote twahitaji kuwa macho, ili njia inapofunguka, tuweze kusonga mbele katika kuendeleza kazi katika majiji makubwa. Sisi tuko nyuma sana katika kufuata maagizo ya kuingia katika miji hii na kuweka kumbukumbu za Mungu. Hatua kwa hatua tunapaswa kuwaongoza watu katika nuru kamili ya Ukweli. Tunapaswa kuendelea kufanya kazi hii hadi kanisa litakapopangwa na kujengwa nyumba nyenyekevu ya ibada. ..... (MTC 91.5)

Katika kila mji kuna kazi ya kufanywa. Watendakazi wanapaswa kwenda katika miji yetu mikubwa na kufanya mikutano ya kambi. Katika mikutano hii, talanta zilizo bora

kabisa zinapaswa kushugulishwa-kutumiwa, ili Ukweli utangazwe kwa nguvu. Watu wenye karama mbalimbali wataletwa. Mtu mmoja hana karama zote zinazohitajika kwa kazi hiyo. Ili kufanikisha mkutano wa kambi, watendakazi kadhaa wanahitajika. Hakuna mtu yeyote anayepaswa kuhisi kwamba ni haki yake kufanya kazi yote iliyo muhimu.— (R & H, Sept 30, 1902 . MTC 92.1)

**Wahubiri/Wanenaji, Wachunge Maneno Yao.— Endapo wazungumzaji** katika mikutano ya kambi inayofanywa katika miji yetu, watakuwa waangalifu katika yote wanayosema, mioyo ya watu itafikiwa wakati Ukweli unatangazwa katika nguvu za Roho Mtakatifu. Upendo wa Kristo uliopokelewa moyoni utafukuza tabia kupenda makosa au upotovu. Upendo na ukarimu unaodhihirishwa katika maisha ya Kristo unapaswa kudhihirika katika maisha ya wale wanaomfanyia kazi. Matendo ya dhati na bidii, yasiyochoka au kukoma, yaliyoashiria maisha Yake Kristo yanapaswa kuonekana katika maisha yao. Tabia ya Mkristo inapaswa kuwa nakala ya tabia ya Kristo (tabia ya Kristo inapaswa kuzaliwa ndani yao). ... (MTC 92.2)

Mstari huu wa kazi haupaswi kuangaliwa kwamba u kando na tofauti na mistari mingine ya kazi ya mikutano ya kambi. Kila mstari wa kazi ya Mungu unahusiana kwa karibu na kila mstari mwingine. Na wakati mistari hiyo inatofautishwa kwa upekee wake, bado wanapaswa kusonga mbele kwa upatanifu kamili. ...(MTC 92.3)

Hebu wale wote wanaoweza kujitoa kwa kazi iliyopuuzwa kwa muda mrefu katika miji yetu, kazi ambayo imetazamwa na watu na kisha wakatembea upande mwingine ili wasijihusishe nayo, kama msamaria aliyejeruhiwa alivyopitwa bila kujaliwa na kuhani na Mlawi. Anza kazi katika majiji kwa moyo wote, kwa akili,
hekima na bila ubinafsi.— (PUR, Oct 23, 1902 . MTC 92.4)

## EPUKA MAONYESHO MAKUBWA

**Maonyesho Makubwa Hayahitajiki.—** Ningependa kuzungumza kwa kudhamiria. Si mpango wa Mungu kwa kanisa Lake kujipanga katika wakati wowote ule kufanya maonyesho makubwa katika miji yetu. Bwana huchukizwa na kuvunjiwa heshima wakati mali Zake alizowakabith wanadamu kama mawakili, zinatumika katika maonyesho ya namna hiyo (kujionyesha kwa namna hiyo). Niliruhusiwa kuangalia onyesho la hivi majuzi, ambalo liliwasilishwa kwangu, nani nikaagizwa kuwa fedha zilizotumika hivyo zingetumika kuleta afueni kwa kuwaondolea hali mbaya baadhi ya watu waliozikopesha taasisi zetu na sasa wanahitaji pesa zao zirudishwe. Wapo waliotukopesha fedha zao kwa nia njema, ambao japokuwa wamewaita wale walio na pesa zao (kanisa) na kuwasihi, hawakuweza kurudishiwa. Fedha zilizokopwa kutoka kwa watu wetu zinapaswa kurudishwa wanapotuita na kuomba tuwarudishie.— (M 162, 1905 ( Manuscript Releases 10:230 ). MTC 92.5)

**Maombi na Roho Mtakatifu Vitatimiza Zaidi ya Maonyesho ya Nje.—** Wale wanaofanya kazi ya Bwana katika majiji lazima waweke juhudi yenye utulivu, endelevu, thabiti, yenye kujitoa kwa ajili ya elimu ya watu. Wakati wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuvutia wasikilizaji na kuendelea kutunza shauku yao, wakati huo huo lazima wajilinde kwa uangalifu dhidi ya kitu chochote kinachohusiana na na msisimko tu, au mihemko isiyokuwa na matokeo chanya. Katika enzi hii ya ubadhirifu na maonyesho ya nje, watu wanapofikiri kwamba ni muhimu kufanya maonyesho ili kupata mafanikio. Wajumbe wateule wa Mungu wanapaswa kuonyesha udanganyifu huu au imani hii isiyo ya kweli, ya kutumia pesa bila sababu, kwa ajili ya matokeo. Wanapofanya kazi kwa usahili, unyenyekevu, hadhi na ladha, wakiepuka kila kitu chenye

asili ya maonyesho au drama kwenye ukumbi wa michezo ya kuigiza, kazi yao itajenga hisia nzuri ya kudumu kwa mioyo ya watu kuguswa. (Msisimko unaweza kuwa wa visa vya kukata na shoka, na kuwafanya wasikilizaji watekewe kabisa, au madoido mengi yasiyohitajika wakati wa mikutano).(MTC 93.1)

Ni kweli kuwa kuna haja ya kutumia pesa kwa busara katika kutoa matangazo ya kwamba kutakuwa na mikutano na katika kuendeleza kazi kwa uthabiti (advertising). Ila kuna shida zaidi ya hiyo, katika maonyesho haya (mambo bandia na drama) nguvu za kila mtenda kazi zitaonekana kusema uongo, si katika mawakala hawa wa nje, bali katika kumtegemea Mungu kwa uaminifu, katika maombi ya bidii Kwake kwa ajili ya msaada, na katika kutii Neno Lake ndiyo kuna mafanikio. Yanahitajika maombi mengi zaidi, kuwa kama Kristo kwa ukaribu zaidi, kupatana na mapenzi ya Mungu zaidi, vyote hivi vinapaswa kuletwa katika kazi ya Bwana. Maonyesho ya nje na matumizi ya fedha yaliyopitiliza, havitakamilisha kazi inayopaswa kufanywa. (MTC 93.2)

Kazi ya Mungu inapaswa kuendelezwa kwa nguvu. Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tunahitaji kuelewa kwamba Mungu ataongeza kwenye jeshi la watu Wake, watu wenye uwezo na mvuto, ambao watatenda sehemu yao katika kuuonya ulimwengu. Si wote walio ulimwenguni ni waasi na wenye dhambi. Mungu ana maelfu mengi ambao hawajapiga goti kwa Baali. Kuna wanaume na wanawake wanaomcha Mungu katika makanisa yaliyoanguka, kama hii isingekuwa hivyo, tusingepewa kubeba ujumbe huu: “Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu.” “Tokeni kwake, enyi watu Wangu.” Wengi walio dhati mioyoni mwao, wanapambana kwa bidii ili angalau waweze kuvuta pumzi ya uhai itokayo mbinguni. Wataitambua injili inapoletwa

kwao kwa uzuri na usahili ambao kwayo inaonyeshwa katika Neno la Mungu.— (T C 9:109-111 . (1909) MTC 93.3)

**Maonyesho ya Kupindukia ni Kinyume na Mapenzi ya Mungu.—** Mungu ametazama maonyesho makubwa yaliyofanywa na baadhi ya watu ambao wamefanya kazi kwa bidii huko New York; lakini Yeye hapatani na njia hiyo ya kuhubiri injili. Ujumbe mzito unachanganywa na makapi kwa kiasi kikubwa, jambo ambalo huweka moyoni maoni ambayo hayapatani na kazi yetu. Habari njema ya neema inayookoa inapaswa kupelekwa kila mahali; onyo lazima litolewe kwa ulimwengu; lakini utunzaji wa pesa, yaani umakini katika uchumi, lazima ufanyike ikiwa tunasonga mbele katika roho ambayo Kristo ametupa kielelezo katika huduma ya maisha Yake. Yeye hapendi kuwe na chochote kilicho na gharama zinazopilitiza, kiwakilishe matengenezo ya afya mahali popote kama ilivyo sasa. ... (MTC 94.1)

Maonyesho yote makubwa ambayo yamefanywa katika kazi ya umishenari wa tiba, au katika majengo, au katika mavazi, au katika mstari wowote wa mapambo ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Kazi yetu inapaswa kujifunzwa na kuchunguzwa kwa uangalifu, na inapaswa kuendana na mpango wa Mwokozi wetu. Yeye angeweza kuweka majeshi ya malaika ili kuonyesha tabia Yake ya halisi ya kifalme; lakini aliyaweka hayo yote kando na akaja katika ulimwengu wetu katika vazi la ubinadamu, kuteseka pamoja na ubinadamu majaribu yote ambayo mwanadamu hujaribiwa nayo. ... (MTC 94.2)

Mungu anawaita Waadventista Wasabato kuudhihirishia ulimwengu kwamba tunajiandaa kwa ajili ya makao ambayo Kristo amekwenda kuwaandalia wale watakaotakasa roho zao kwa kuutii Ukweli kama Ulivyo ndani ya Yesu. Hebu kila mtu anakayekuja kwa Kristo ni lazima ajikane nafsi yake,

na kuuchukua msalaba wake, na kumfuata YEye. Ndivyo anavyosema Mwalimu mkuu.—( R & H, August 6, 1914 ). MTC 94.3)

## UIN JILISTI BINAFSI

**Ushuhuda Binafsi Una Matokeo Zaidi Kuliko Mahubiri ya Hadharani.—** Kwa wewe kuwa mcheshi na kushirikiana na watu ambao unataka kuwafikia, kwa kuja karibu nao, [ hawa watu tunaotaka kufikia] mkondo wa mawazo yao utabadilishwa upesi zaidi kuliko hotuba au mahubiri yenye uwezo zaidi.Kumwasilisha Kristo katika familia, kando ya majiko ya moto ambayo watu wanaota nyakati za baridi, na katika mikusanyiko midogo kwenye nyumba za watu binafsi, hufaulu zaidi katika kuwaleta roho kwa Yesu kuliko mahubiri yanayotolewa hadharani kwa umati wa watu wanaotembea au wasio na utulivu, au hata katika kumbi au makanisa.— (R&H, Desemba 8, 1885 . MTC 95.1)

**Jitihada za Mahuhubiri Zinapaswa Kuongezwa na Jitihada za kutembea Nyumba kwa Nyumba.—** Majiji yapasa kufanyiwa kazi, si kuhubiriwa tu; bali kunapaswa kuwe na kazi ya nyumba kwa nyumba. Baada ya onyo hilo kutolewa, baada ya Ukweli kuwasilishwa kutoka katika Maandiko, roho nyingi zitasadikishwa. Kisha uangalifu au tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa. Wakala wa kibinadamu hawezi kufanya kazi ya Roho Mtakatifu; sisi ni mikondo tu ambayo Bwana hutenda kazi kwayo. Mara nyingi roho ya kujitosheleza huja mioyoni mwetu wakati mafanikio kidogo yanapokuja katika juhudi za mtendakazi. Lakini kusiwepo na kujiinua nafsi, hakuna kitu kinachopaswa kuhusishwa na ubinafsi (tusiseme ni mimi ndiyo nimefanikisha hili); kazi ni ya Bwana, na Jina Lake la thamani tu, ndilo linapaswa

kupokea utukufu wote. Hebu ubinafsi ufichwe ndani ya Yesu.— (R&H, Oktoba 14, 1902 . MTC 95.2)

## KUFIKIA U JIRANI

**Anza na Ujirani Wako Mwenyewe.—** Bwana amewasilisha mbele yangu kazi ambayo ni lazima ifanywe katika miji yetu. Waumini katika miji hii wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya Mungu katika ujirani wa nyumba zao. Wanapaswa kufanya kazi kwa utulivu na unyenyekevu, wakibeba pamoja nao popote waendako angahewa la mbinguni. Ikiwa watazifanya nafsi zao zisionekane (wasijionyeshe), na daima waelekeze watu kwa Kristo, nguvu ya mvuto wao itahisiwa kwenye upande wa Ukweli.— ( R&H, Agosti 12, 1902 . MTC 95.3)

**Wakristo Wanaoishi Mijini Wanapaswa Kutoa Ushahidi kwa Wengine.—**

Ninazungumza na Wakristo wanaoishi katika majiji yetu makubwa: Mungu amewaweka ninyi kuwa watunza amana wa ile Kweli, sio wapate kuihifadhi tu, bali ili wawagawie wengine. Mnapaswa kutembea nyumba kwa nyumba kama mawakili waaminifu wa neema ya Kristo. Unapoendelea kufanya kazi, kubuni, na kupanga mikakati, mbinu mpya zitaendelea kujionyesha akilini mwako, na kwa kuzitumia nguvu za akili zako, akili zitaongezeka. Utendaji vuguvugu na mlegevu wa wajibu ni jeraha kwa nafsi ambayo Kristo ameifia. Ikiwa tungekuta lulu zimefukiwa kwenye vifusi vya miji, tunapaswa kwenda kwa utayari kufanya kazi inayotakiwa na Mwalimu. Wengine wanaweza kufanya kazi kwa utulivu, wakijaribu kuwafanya watu wawe na shauku, wakati wengine wanazungumza kwenye kumbi. Ni kweli kwamba Shetani atapanga njama kwa kutumia kila njia ili kuzitia ganzi hisia, kupofusha macho, na kuziba masikio ya

watu dhidi ya Ukweli; lakini licha ya hili, nenda kazini. Kazi ya nyumba kwa nyumba, bila kuwapuuzia wale walio maskini, ambao kwa kawaida hupitwa kando. Kristo alisema, “Amenitia mafuta kuhubiri injili kwa maskini,” nasi tunapaswa kwenda na kufanya vivyo hivyo.—(R&H, Juni 11, 1895 . MTC 96.1)

**Shiriki Pamoja na Marafiki.—** Tunapaswa kuhisi kuwa ni jukumu letu la kipekee kuwafanyia kazi wale wanaoishi katika ujirani wetu. Jifunze jinsi unavyoweza kuwasaidia vyema wale wasiopendezwa na mambo ya kiroho/kidini. Unapowatembelea marafiki na majirani zako, waonyeshe kuwa una shauku kuhusiana na hali yao ya kiroho na ya kimwili pia. Zungumza nao juu ya Kristo kama Mwokozi Mwenye kusamehe dhambi. Waalike majirani zako nyumbani mwako, na usome pamoja nao kutoka katika Biblia yenye thamani na kutoka katika vitabu vinavyoeleza Kweli zake. Waalike kuungana nawe katika wimbo na sala. Katika makusanyiko haya madogo, Kristo Mwenyewe atakuwepo, kama alivyoahidi, na mioyo itaguswa na neema Yake. (MTC 96.2)

Washiriki wa kanisa wanapaswa kujielimisha kufanya kazi hii. Jambo hili ni muhimu kama lile la kuokoa roho katika nchi za kigeni. Ijapokuwa wengine wanahisi mzigo wa roho za watu walio mbali, hebu wengi walio nyumbani Marekani wahisi mzigo wa roho za watu zenye thamani zilizo karibu nao, na kufanya kazi kwa bidii vivyo hivyo kwa ajili ya wokovu wao.— ( MH, 152, 153 . (1905) MTC 96.3)

**Wafikie Watu Mahali Walipo.—** Ili kuwafikia watu, popote walipo, na bila kujali cheo au hali yao, na kuwasaidia katika kila njia iwezekanayo—hii ndiyo huduma ya kweli. Kwa juhudi kama hizo unaweza ukaileta

mioyo kwa Kristo na kufungua mlango wa kupata roho zinazoangamia. … (MTC 97.1)

Haisaidii kujaribu kuwarekebisha wengine kwa kushambulia yale ambayo tunaweza kuyaona kuwa ni mazoea mabaya. Jitihada hizo mara nyingi huleta madhara kuliko manufaa. Katika mazungumzo yake na mwanamke Msamaria, badala ya Yeye kudharau kisima cha Yakobo, Kristo aliwasilisha jambo bora zaidi.

… Hiki ni kielelezo cha njia ambayo tunapaswa kufanya kazi. Ni lazima tuwape wanadamu kitu kilicho bora zaidi kuliko kile walicho nacho, yaani, amani ya Kristo, ipitayo ufahamu wote.— (MH, p. 156, 157 . (1905) MTC 97.2)

## WOTE WANAPASWA KUFIKIWA

**Familia Nzima ya Ubinadamu Ni Kutaniko Letu (wote ni washiriki wetu).—** Upendo ulioonyeshwa katika maisha na tabia ya Kristo si shauku finyu, ya ubinafsi. Unapaswa kubidishwa na upendo Wake kuhubiri injili katika sehemu zilizo mbali na wewe, na sio kujivunia mstari wa mtu mwingine wa mambo ambayo ameyafanyia kazi yeye na hivyo tayari yamo mikononi mwako. “Bali yeye ajisifuye na ajisifu katika Bwana. Maana si yeye ajisifuye ambaye amekubaliwa, bali yeye asifiwaye na Bwana.” Kazi ambayo daima ipo mbele ya mhudumu wa Kristo ni kuihubiri injili, kwa wale walio karibu, na “katika maeneo ya mbali.” Inahusisha kujinyima, kujikana nafsi na inalazimu kubeba msalaba. Aina hii ya kazi, ambayo itatuongoza daima kuwa wamishenari waaminifu wa nyumbani na kusonga mbele katika nyanja mpya, lazima iendelezwe zaidi na zaidi tunapokaribia mwisho wa historia ya dunia. Injili haipaswi kuminywa au kuzuiwa kwa wakati wowote au kufungiwa mahali popote.

Ulimwengu ni shamba la mhudumu wa injili, na familia nzima ya ubinadamu ni kusanyiko lake. Anapomaliza kutoa hotuba au kuhubiri, ndiyo kwanza tu kazi yake imeanza; maana Neno la uzima litawasilishwa nyumba kwa nyumba. Kweli lazima ipelekwe kutoka jiji hadi jiji, kutoka mtaa hadi mtaa, kutoka kwa familia hadi familia. Kila mbinu ambayo inaweza inayowezesha kupenya katika majumba ya watu ni lazima ijaribiwe; kwa maana ni lazima mjumbe afahamiane na watu. Ukweli lazima upelekwe kutoka jimbo hadi jimbo, kutoka ufalme hadi ufalme. Barabara kuu na njia za kupita lazima zisachiwe kikamilifu na masazo yote ya mazao yatolewe, na ujumbe lazima uenezwe kutoka bara hadi bara, hadi dunia nzima itakapofungwa mkanda kwa
Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. (MTC 97.3)

Ni lazima wahudumu na wamishenari wakumbuke "maeneo ya ng'ambo." Mwokozi amesema kuhusu watu Wake, "Ninyi ni nuru ya ulimwengu." Ukweli unapaswa kutangazwa; nuru lazima iangaze kwa miale ya wazi, thabiti na endelevu. Kujikana nafsi, kujitolea moyo wote, lazima kuwekwe katika kazi; nuru lazima iangaze mpaka roho za watu zenye thamani ziletwe kuchukua msimamo wao upande wa Bwana. Ndipo mtenda kazi anapaswa kusonga mbele kuingia katika "maeneo yaliyo ng'ambo," ambako roho zitakusanywa na nuru yenye thamani itaangaza katikati ya giza la kiadili linalowafunika watu. Hivyo Ukweli lazima uhubiriwe mpaka akili ya wale walioketi gizani kama chini ya uchungu wa mauti zitiwe nuru, na kuinuliwa, na kupanuliwa. Kila mtendakazi lazima asimame kwenye nafasi yake ya wajibu, si kuhubiri tu, bali kuzikaribia roho za watu, ili kufahamiana nazo nyumbani kwao, kama Yesu alivyofanya, akifanya kazi pasipokuwa na ubinafsi, kwa kujitolea, mpaka kazi itakapofungwa vizuri. Wakati kikundi kimoja kinapoinuliwa ili kubeba nuru kwa jamii, fursa

zitaonekana ambazo zitawaalika vibarua katika “maeneo ya ng’ambo.” Wafanyakazi wa Mungu watasonga mbele daima, wakitegemea mwongozo wa Roho Mtakatifu.— (Bible Echo, Mei 21, 1894 . MTC 98.1)

**Kila Mtu Mwenye Hitaji Ni Jirani Yangu**.— Popote ambapo binadamu ana hitaji au na mateso, kuna shamba kwa ajili ya kazi ya umishonari. Kuna mambo mengi yasiyoleta matumaini kuhusu siku zijazo kwetu sisi ambao tunatoa nguvu za utu wetu tuliopewa na Mungu kwa tabia mbaya zinazoleta kifo (mfano uraibu). Je, tuwadharau watu hawa? Hapana; Bwana Yesu amezinunua nafsi zao kwa bei isiyo na kikomo, hata kwa kumwaga damu ya moyo Wake. Je! ninyi mnaokiri kuwa wana wa Mungu, ni Wakristo kweli kama neno hilo linavyokubalika na kujulikana kikamilifu, au katika maisha yenu ni watu wa kughushi tu au bandia, mnaojifanya (feki)? Je, wewe unauliza kama Kaini, “Je, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” Je! Bwana atamwambia yeyote kati yetu kama alivyomwambia Kaini, “Umefanya nini? sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi”? Je, tutashindwa kufanya kazi tuliyopewa na Mungu, na hatutafuta na kuokoa kile kilichopotea? Kuna wengi wanaouliza, kama yule wakili alivyouliza, “Jirani yangu ni nani?” Jibu linatujia katika mazingira yaliyokuwepo karibu na Yeriko, wakati kuhani na Mlawi walipopita ng’ambo ya pili, na kumwacha maskini mgeni aliyechubuliwa na kuumizwa atunzwe na Msamaria mwema. Kila aliye katika uhitaji ni jirani yetu. Kila mwana na binti wa Adamu aliyemangamanga na kuliacha kundi, ambaye amenaswa na adui wa nafsi na kufungwa katika utumwa wa mazoea mabaya ambayo yanaharibu uanaume au uanawake (utu) aliopewa na Mungu, ni jirani yangu.— (R& H, Nov 12, 1895 . MTC 98.2)

**Ulimwengu Mzima Ufanyiwe Kazi kwa Ajili ya Mungu.— Niliamka k**atika dhiki kubwa. Nikaenda kulala

tena, na nilionekana kuwa kwenye kusanyiko kubwa. Mmoja Mwenye mamlaka alikuwa akihutubia kikundi, mbele yake ilitandazwa ramani ya dunia. Alisema kwamba ramani hiyo ilionyesha shamba la mizabibu la Mungu, ambalo ni lazima lilimwe. Wakati nuru kutoka mbinguni ilipommulikia mtu mmoja, huyo alipaswa kuwaangazia wengine nuru hiyo. Taa zilipaswa kuwashwa katika sehemu nyingi, na kutoka kwenye taa hizo, taa zingine zingewashwa. (MTC 99.1)

Maneno hayo yalirudiwa: "Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Tangu wakati huo haifai kitu, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliowekwa juu ya mlima hauwezi kusitirika. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kinara; nayo yawaangazia wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" ( Mathayo 5:13-16 ). (MTC 99.2)

Nikaona miale ya nuru inayosafiri kwa kasi ikiangaza kutoka katika miji na vijiji, na kutoka mahali pa juu na mahali pa chini pa dunia. Neno la Mungu lilitiiwa, na matokeo yake kukawa na makumbusho Yake katika kila mji na kijiji. Ukweli wake ulitangazwa ulimwenguni pote.— ( 9T.28, 29 . (1909) MTC 99.3)

**Mwangaza wa Jua la Haki Litaenezwa kwa Wahitaji.—** Kuna kazi inayopaswa kufanywa na makanisa yetu ambayo ni wachache tu wanayo wazo lolote nayo. "Nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nikiwa uchi, mkanivika; mlinijia; nalikuwa kifungoni, mkaja Kwangu." Itabidi tutoe mali zetu kusaidia watenda kazi katika shamba la mavuno, nasi tutashangilia kwa miganda iliyokusanywa. Ila

japokuwa jambo hili ni kweli, kuna kazi, ambayo bado haijaguswa, ambayo lazima ifanywe. Utume wa Kristo ulikuwa ni kuponya wagonjwa, kuwatia moyo wasio na tumaini, kuwafunga waliovunjika moyo (kuwaweka karibu na kufunga vidonda vyao). Kazi hii ya urejeshwaji inapaswa kuendelezwa miongoni mwa wahitaji, na watu wanaoteseka kwenye jamii ya ubinadamu. Mungu anakuita si tu kwa ajili ya ukarimu wako, bali pia uso wako wenye ucheshi na tabasamu, na maneno yako yenye kuleta matumaini, na mguso wa mkono wako. Waponye baadhi ya watu wa Mungu waliopata shida. Wengine ni wagonjwa, na tumaini limetoweka kwao kabisa. Warudishie mwanga wa jua. Kuna nafsi ambazo zimepoteza ujasiri wao; zungumza nao, na uwaombee. Kuna wale wanaohitaji mkate wa uzima. Wasomee hawa kutoka katika Neno la Mungu. Kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna tiba/zeri inaweza kuufikia, hakuna dawa inaweza kuponya. Waombee watu hawa, na uwalete kwa Yesu Kristo. Na katika kazi yako yote, Kristo atakuwepo kufanya mguso kwenye mioyo ya wanadamu. (MTC 100.1)

Hii ndiyo aina ya kazi ya umishenari wa tiba unaopaswa kufanywa. Leta mwanga wa jua la Haki kwenye chumba cha wagonjwa na wanaoteseka. Wafundishe wale waliofungiwa katika majumba ya maskini jinsi ya kupika. “Atalilisha kundi Lake kama mchungaji,” kwa chakula cha muda na cha kiroho.—(Manuscript 105, 1898 ( A.C to M.E &H.E, 22, 23 ). MTC 100.2)

**Ustawi wa Wote Kufumwa Pamoja. -** Kusiwe na ukiritimba wa kile kinachostahili kutendwa, kwa kipimo cha wote wa hali ya juu na wa chini, matajiri na maskini, wasomi na wasio na elimu. Hata mwale mmoja wa jua usiachwe kutembea bila kuthaminiwa, au kuzimwa, au kutotambulika, au hata kutambuliwa kwa kusitasita. Hebu wote watende sehemu yao kwa ajili ya Ukweli na uadilifu.

Maslahi ya tabaka tofauti za jamii yana umoja usioweza kutengwa. Sisi sote tumeunganishwa pamoja katika mtandao mkuu wa ubinadamu, na hatuwezi, kuondoa huruma zetu kutoka kwa kila mmoja wetu bila ya kuambulia hasara. Mvuto wenye afya hauwezi kudumishwa katika kanisa wakati maslahi haya ya pamoja na huruma havipo.— (GW, 331 . (1915) MTC 100.3)

## Huduma katika Miji

### Vikundi Lengwa

**Wakazi wengi wa mijini ni wajinga kuhusu Ujio wa Kristo wa Upesi. —** Kuna wale katika miji yetu yote ambao hawakupata Ukweli uliowasilishwa kwao; ambao hawajasikia ujumbe wa onyo la kuja kwa Bwana upesi; ambao hawajasikia kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Isipokuwa wajumbe watakwenda kwa watu hawa katika Roho wa Kristo, watu hawa watasikiaje mwaliko wa injili? Watajuaje kwamba dhambi zao zinaweza kusamehewa kupitia rehema ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka?— ( R&H, Julai 2, 1895 . MTC 101.1)

### MASIKINI

**Maskini Waitikia Injili.—** Watu wa Bwana mara nyingi ndiyo sehemu kubwa ya watu walio maskini wa ulimwengu huu, watu wa kawaida. Si wengi wenye hekima, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye vyeo walioitwa. Mungu “amechagua maskini wa ulimwengu huu.” "Maskini wamehubiriwa Injili." Matajiri wanaitwa, kwa maana moja; wanaalikwa, lakini hawakubali mwaliko huo. Lakini katika majiji haya maovu Bwana ana wengi ambao ni

wanyenyekevu na bado wanamtumaini.— (Manuscript 17, 1898 ( Ev, 565 ). MTC 101.2)

**Wote Wanaitwa Kuwasaidia Wenye Mahitaji.—** Ndugu na dada, ombi hili kwa niaba ya wenye uhitaji linapowajia, ninatumaini kwamba mtaliitikia. Hebu kila mwanachama apewe na shauku kubwa kuhusiana na kazi hii nzuri. Usimruhusu Yesu kukatishwa tamaa kuhusu wewe. Neno la Mungu limejaa mafundisho kuhusu jinsi tunavyopaswa kuwatendea wajane na yatima, na wahitaji wanaoteseka. Ikiwa wote wangefanya kazi ya Bwana, moyo wa mjane ungeimba kwa shangwe, na watoto wadogo wenye njaa wangelishwa, walio fukara wangevikwa nguo, na wale walio tayari kuangamia wangehuishwa.— (Manuscript 26, 1891 ( MM, 1891). Julai 1891 ). MTC 101.3)

**Kila aina/kesi ya Mahitaji inahitaji Kuzingatiwa.—** Ni kusudi la Mungu kwamba matajiri na maskini wafungwe pamoja kwa ukaribu na mahusiano ya huruma na kusaidiana. Anatuagiza tujishughulishe na kila hali ya mateso na hitaji ambalo litakuja kwenye ufahamu wetu. (MTC 102.1)

Usifikirie kuwa unashusha hadhi yako chini kwa kuwahudumia wanadamu wanaoteseka.— (6T.279 . (1900) MTC 102.2)

**Njia Bora Zaidi ya Kufikia Mioyo.—** Kwa kuonyesha shauku kuhusiana na mahitaji ya wanadamu wanaoteseka tunaweza kuifikia mioyo ya wanadamu kwa njia bora zaidi. Utamaduni wa akili na moyo unakamilishwa kwa urahisi zaidi tunapohisi huruma nyororo kwa wengine hivi kwamba tutasambaza manufaa na fursa yetu ili kuwasaidia katika mahitaji yao.— (Lt.116, 1897 ( Welfare Ministry, 192, 193 ). MTC 102.3)

**Kushiriki binafsi Kwahitajika.—** Katika kujaribu kuwasaidia maskini, wanaodharauliwa, wanaochukiwa na waliotelekezwa, usifanye kazi kwao ukiwa umepanda juu na

viatu vyako vya mchuchumio au kwenye nguzo ya hadhi na ukuu wako, kwa kuwa kwa njia hiyo hutaweza kufanikisha lolote. Inabidi uongoke kikweli, na kisha ujifunze Kwake Yeye aliye mpole na mnyenyekevu wa moyo. Tunapaswa tumweke Bwana mbele yetu daima. Kama vile watumishi wa Kristo wanavyoendelea kusema, usije ukasahau kwamba, "Umenunuliwa kwa thamani." (MTC 102.4)

Mungu anatoa wito, si tu kwa ajili ya ukarimu wako, lakini kwa ajili ya uso wako wenye ucheshi na tabasamu, maneno yako ya matumaini, na mguso wa mkono wako. Unapowatembelea walioteswa na Bwana, utapata wengine ambao tumaini limewaondoka; hawa uwarudishie mwanga wa jua. Kuna wanaohitaji mkate wa uzima; wasomee kutoka katika Neno la Mungu. Kwa wengine kuna ugonjwa wa roho ambao hakuna zeri hapa duniani inayoweza kuwafikia au kuponya daktari; waombee hawa, na uwaletee kwa Yesu.— (6T.277 . (1900) MTC 102.5)

**Wasaidie Maskini Wanaoweza Kufaidika. -** Watu maskini wa Bwana wanapaswa kusaidiwa katika kila hali ambayo itakuwa kwa manufaa yao. Wanapaswa kuwekwa mahali ambapo wanaweza kujisaidia wenyewe. Hatuna swali kuhusiana na kesi za tabaka hili la maskini. Njia bora zaidi za kuwasaidia zinapaswa kufikiriwa kwa uangalifu na kwa maombi. (MTC 103.1)

Bwana anaweka wajibu huu juu ya kila kanisa. ... Mungu huwaacha maskini Wake wawemo katika mipaka ya kila kanisa. .... Hawapaswi kumpita kando masikini yeyote wa lakini wanapaswa kujikana nafsi au kujinyima anasa zao (luxury) ... ili kuwafanya wanaoteseka, na wahitaji wapate mahitaji ya muhimu ili wawe na faraja (comfort).(MTC 103.2)

Baada ya kufanya hayo wanaweza kufika mbali zaidi kusaidia wale ambao siyo wa nyumba ya imani, ikiwa wao ndio walengwa wanaofaa kusaidiwa.— (Manuscript 46, 1900 ( Manuscript Relees 4:421, 422) ; & (1T.272-274 ). MTC 103.3)

**Fursa za Ajira Zinapasa Kutolewa.—** Ni nini kinachoweza kufanywa mahali ambapo umaskini umeenea na kupigana mieleka ili kuikabili kila hatua? Hakika kazi ni ngumu. Matengenezo ya lazima hayatafanywa isipokuwa wanaume na wanawake wanasaidiwa na mamlaka nje yao wenyewe. Ni kusudi la Mungu matajiri na maskini wafungwe pamoja kwa ukaribu na mahusiano ya huruma na msaada. Wale ambao wana mali, uwezo, na vipaji, wanapaswa kutumia karama hizi kuwabariki wanadamu wenzao. ... (MTC 103.4)

Umakini uwekwe katika wa uanzishwaji wa stadi/tasnia mbalimbali ili familia maskini zipate ajira. Mafundi seremala, wahunzi, na kwa kweli kila mtu anayeelewa kazi fulani yenye kunufaisha, anapaswa kuhisi wajibu wa kufundisha na kuwasaidia wajinga na wasio na kazi.— (MH, 193, 194 . (1905) MTC 103.5)

**Mungu AnaporwaMaskini Asiposaidiwa.—** Kila ubadhirifu unapaswa kukatiliwa mbali maishani mwetu, kwa maana wakati tunaopaswa kufanya kazi si mrefu sana. Kote karibu nasi tunaona wanadamu wanaoteseka. Familia hazina chakula; wale walio wadogo wanalilia mkate. Nyumba za watu maskini hazina samani na matandiko yanayofaa. Wengi wanaishi kwenye makazi ambayo ni kama mashimo tu, ambayo yanakaribia kukosa kabisa mahitaji ya msingi kwa ufukara. Kilio cha maskini kinafika mbinguni. Mungu anaona; Mungu anasikia. Lakini wengi wanajitukuza wenyewe. Wakati wanadamu wenzao ni maskini na wanaumwa njaa, wakiteseka kwa kukosa chakula, wao hutumia pesa nyingi kwenye meza zao, na

kubugia chakula, zaidi ya wanavyohitaji kula. Ni hesabu iliyoje ambayo wanadamu watalazimika kutoa siku ya mwisho kwa matumizi yao ya ubinafsi ya pesa za Mungu! Wale wanaopuuza uongozi na majaliwa ya Mungu ambayo Yeye amewaandalia maskini, watapata kwamba hawakuwaibia wanadamu wenzao tu, bali kwa kuwapora hawa, wamempora Mungu pia, na wametumia mali Yake Mungu isivyofaa kwa ubaradhifu na wizi.— (Manuscript 60, 1896 (S.T. M&W, Series A 9:68, 69). MTC 104.1)

**Kuwa mkarimu kwa Wengine Hakutasababisha Umaskini Binafsi wa mtu.—** “Maskini,” Yeye [Yesu] asema, “hatakoma katika nchi milele; maskini, na maskini wako, katika nchi yako” ( Kumbukumbu la Torati 15:11 ). … (MTC 104.2)

Hakuna anayepaswa kuwa na hofu kwamba ukarimu wao ungewaletea uhitaji, kupungukiwa au ufukara. Kutii amri za Mungu hakika kutaleta ufanisi. …(MTC 104.3)

Mpango wa maisha ambao Mungu aliwapa Waisraeli ulikusudiwa kuwa somo muhimu kwa wanadamu wote. Ikiwa kanuni hizo zingetekelezwa leo, ulimwengu huu ungekuwa tofauti kwa kiasi gani!— (MH, 186-188 . (1905) MTC 104.4)

**Madaraja ya Juu Zaidi katika Jamii Yanapaswa Kufikiwa.—** Ujumbe wa injili unapaswa kuhubiriwa katika kila jiji; kwa maana hii ni kwa mujibu wa mfano wa Kristo na wanafunzi Wake. Wamishenari wa tiba wanapaswa kutafuta kwa subira na bidii kufikia tabaka za juu. Ikiwa kazi hii itafanywa kwa uaminifu, wanaume wenye taaluma mbalimbali watakuwa wainjilisti waliofunzwa vyema.— (Manuscript 33, 1901 ( MM, 241 ). MTC 104.5)

**Kazi kwa ajili ya Madaraja ya Juu Inahitaji Uwezo Wetu Bora Zaidi.—** Tunapaswa kuwasilisha Ukweli kwa

wale walio katika barabara kuu. Kazi hii imepuuzwa. Tuna kazi ya kufanya kwa watu wa madraja ya juu, na kazi hii inahitaji uwezo wetu wote. Ingawa hatupaswi kuwapuuza maskini na watu fukara,
hatuna watu wala pesa kwa ajili ya kazi hiyo miongoni mwa tabaka la chini kabisa. Tunaelekeza wafanyikazi wetu kwa daraja la juu. Sababu zote za kufanya hili siwezi kuelezea kwa sasa. (MTC 105.1)

Mashamba yaliyoiva kwa mavuno yametandazwa mbele yangu. Tunapaswa kufanya kazi kwa tabaka la juu la watu. Kisha tutakuwa na nguvu na uwezo wa kusonga mbele katika mistari ambayo Mungu ametuelekeza.— (Letter 164, 1901, p. 2 (Manuscript Releases, 4:420, 421). MTC 105.2)

**Mbinu za Kushiriki Injili na Madaraja Yote Inahitajika.—** Mwaliko wa injili unapaswa kutolewa kwa matajiri na maskini, walio juu na walio chini, na lazima tutengeneze njia za kupeleka Ukweli katika maeneo mapya na kwa tabaka za watu wote. Bwana anatuamuru, “Tokeni kwenye njia kuu na viunga, mkawashurutishe kuingia, ili nyumba Yangu ijae.” Anasema, “Anzeni kwenye njia
kuu; fanyeni kazi vizuri kwenye barabara kuu; undeni kikundi ambacho kwa umoja kitaenda pamoja nanyi na kinaweza kufanya kazi ileile ambayo Kristo alifanya katika kutafuta na kuokoa waliopotea.”— (Manuscript 3, 1899 ( MM, 312 ). MTC 105.3)

**Watu Wenye Mvuto/Ushawishi Hawapaswi Kupuuzwa.—** Ulimwengu huu ulioanguka uko mikononi migeni au ya mtu baki. Watu hutawala kwa ajili ya vipato vyao vikubwa au pesa, na kuhubiri kwa ajili ya pesa (watumishi wa mshahara). Katika shughuli zote za biashara kuna kugombania ukuu. Ikiwa Kristo angetembea katika mitaa ya miji yetu leo, wachache wangekuwa na shauku ya

kutosha kumfuata. Wale wanaotenda sehemu katika serikali ya ulimwengu hawana sehemu na Kristo, ambaye ametangaza, "Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya
neno lolote." Je, hawa wanaweza kuwa viongozi wa serikali wenye mafanikio wakati ambapo hawajajifunza njia na mbinu za Mwalimu Mkuu? Watu walio na vyeo vya juu vya uaminifu wanapaswa kuelimishwa katika shule ya Kristo. Msiwakatae au kuwapuuzia watu hawa wenye mvuto.— (R&H, Agosti 21, 1900 . MTC 105.4)

**Matajiri Wanafikiwa kwa Uwasilishaji unaotegemea Biblia.—** Watumishi wa Kristo wanapaswa kufanya kazi kwa uaminifu kwa ajili ya matajiri katika majiji yetu, na pia maskini na watu wa hali ya chini. Kuna watu wengi matajiri ambao wanaweza kuathiriwa na mvuto na hisia za ujumbe wa injili, na ambao,
wakati Biblia, na Biblia pekee inapowasilishwa kwao kama mfafanuzi wa imani na matendo ya Kikristo, wataguswa mioyo na Roho wa Mungu kufungua milango
kwa ajili ya kuendeleza injili. Watafunua imani iliyo hai katika Neno la Mungu na watatumia uwezo wao waliokabidhiwa kuandaa njia ya Bwana, kunyoosha jangwani njia kuu kwa ajili ya Mungu wetu.— (9T.113, 114
. (1909) MTC 106.1)

**Roho Mtakatifu Huwatumia Viongozi wa Serikali Kulinda Kazi ya Mungu.—** Lakini maadamu Yesu anaendelea kuwa mwombezi wa mwanadamu katika Patakatifu pa Patakatifu juu mbinguni, nguvu ya kuzuia ya Roho Mtakatifu huhisiwa na watawala na raia. Bado inadhibiti kwa kiasi fulani sheria za nchi. Kama si sheria hizi, hali ya ulimwengu ingekuwa mbaya zaidi kuliko ilivyo sasa. Ingawa wengi wa watawala wetu ni mawakala hai wa Shetani, Mungu pia ana mawakala Wake miongoni mwa watu wakuu wa taifa. Adui anafanya kazi ya kugusa mioyo ya mbele ya watumishi wake kupendekeza hatua ambazo

zingezuia sana kazi ya Mungu; lakini viongozi wa serikali wanaomcha Bwana wanasukumwa na malaika watakatifu kupinga mapendekezo hayo kwa hoja zisizoweza kujibiwa. Hivyo watu wachache watazuia mkondo wenye nguvu za uovu. Upinzani wa maadui wa Ukweli utazuiliwa ili ujumbe wa malaika wa tatu ufanye kazi yake. Onyo la mwisho litakapotolewa, litavutia umakini wa wanaume hawa wanaoongoza ambao kupitia kwao Bwana anafanya kazi sasa, na baadhi yao watalikubali, na kusimama pamoja na watu wa Mungu wakati wa taabu.— (GC, 610, 611 . (1911) MTC 106.2)

## VYUO VIKUU VYA SERIKALI

**Vijana wa Kutenda Maadili Yaliyofafanuliwa na Mtume Petro.—** Ikiwa vijana wetu wangezingatia na kutenda sheria zilizowekwa katika sura hii ya [2 Petro 1 ], ni mvuto mkubwa kiasi gani ambao wangeushinikiza kwenye upande wa haki na uadilifu, iwe wanaishi katika mji wa Ann Arbor Michigan [yaani, katika chuo kikuu cha serikali cha Michigan State University], au katika taasisi zetu, au mahali popote wanapowajibika.— (Lt 43, 1895 (Peter's Counsel to Parents, 48). MTC 107.1)

## AKILI ZA WATU WA DUNIA (secular)

**Shetani Anajaribu Kuzipindisha Akili Kutoka Kwenye Ukweli.—** Umati ambao bado haujaonywa, unakuwa mchezo wa yule mwovu. Shetani anawaongoza katika aina nyingi za upumbavu na kujifurahisha wenyewe. Wengi wanatafuta yale ambayo ni riwaya za kufikirika na ya kushangaza; akili zao ziko mbali na Mungu na Kweli za Neno Lake. Kwa wakati huu, adui anapofanya kazi kuliko wakati mwingine wowote ili kufyonza umakini wa akili za wanaume

na wanawake na kuwageuza kutoka kwenye Ukweli, tunapaswa kujitahidi katika kuongeza utendaji kwenye barabara kuu na pia katika vinjia vidogo vidogo. Kwa bidii, kwa shauku, tunapaswa kutangaza ujumbe wa mwisho wa rehema katika majiji— katika barabara kuu—na kazi isiishie hapo, bali ipanuliwe hadi katika makazi ya ujirani na katika sehemu za mashambani—kwenye njia za pembezoni na viungani. (MTC 107.2)

Madaraja yote yanapaswa kufikiwa. Tunapofanya kazi, tutakutana na mataifa mbalimbali. Hakuna anayepaswa kupitwa bila kuonywa. Bwana Yesu alikuwa zawadi ya Mungu kwa ulimwengu mzima—sio kwa tabaka za juu pekee, na si kwa taifa lolote lile na kisha kuwatenga wengine. Neema Yake ya kuokoa imezungushiwa kwenye ulimwengu wote. Yeyote anayetaka anaweza kunywa maji ya uzima bure.— (Letter 4, 1911 ( The Upward Look, 60 ). MTC 107.3)

**Akili Zinapaswa Kuvutwa kwa Kristo.**— Madaktari wanapoungana na wachungaji/wahudumu katika kutangaza injili katika majiji makubwa ya nchi, kazi yao iliyounganishwa pamoja italeta ushawishi kwenye akili nyingi kupendelea Ukweli wa wakati huu.(MTC 107.4)

Kutokana na nuru ambayo Mungu amenipa, najua kwamba kazi Yake leo ina hitaji la wawakilishi walio hai wa Kweli ya Biblia. Wahudumu waliowekewa mkono peke yao hawatoshi kufanya kazi hiyo. Mungu hawaiti wachungaji tu, bali pia matabibu, wauguzi, wainjilisti wa vitabu, wafanya kazi wa Biblia, na walei wengine waliojiweka wakfu, na wenye vipaji mbalimbali, walio na ujuzi wa Ukweli wa sasa, wazingatie mahitaji ya majiji ambayo hayajaonywa. Kunapaswa kuwa na waumini mia moja wanaojishughulisha kikamilifu katika kazi ya umishenari binafsi, mahali ambapo sasa kuna mmoja tu. Muda

unayoyoma kwa kasi. Kuna kazi nyingi ya kufanywa kabla upinzani wa kishetani haujafunga njia . Kila wakala lazima ianze operesheni ya kazi hii, ili fursa zilizopo sasa ziweze kuboreshwa kwa hekima.—(R&H, Aprili 7, 1910 ( Medical Ministry, 248, 249 ). MTC 108.1)

## WATALII KWENYE MAONYESHO NA MIKUTANO

**Maonyesho (kama ya kilimo nk) na Mikusanyiko Mingine Mikubwa Hutoa Fursa za Kuhubiri.—** Nilipewa maagizo kwamba tunapokaribia mwisho, kutakuwa na mikusanyiko mikubwa katika majiji yetu, kama ilivyokuwa hivi karibuni huko St. Louis, na kwamba ni lazima matayarisho yafanywe ili kutoa mahubiri ya Ukweli kwenye mikusanyiko hii. Kristo alipokuwa hapa duniani, alitumia fursa kama hizo ili kuleta manufaa. Popote ambapo idadi kubwa ya watu ilikusanyika kwa kusudi lolote, sauti Yake ilisikika, kwa wazi na dhahiri, ikitoa ujumbe Wake. Na matokeo yake, baada ya kusulubishwa na kupaa Kwake, maelfu waliongoka kwa siku moja. Mbegu iliyopandwa na Kristo ilizama ndani kabisa ya mioyo, na kuota, na wanafunzi walipopokea kipawa cha Roho Mtakatifu, mavuno yalikusanywa. (MTC 108.2)

Wanafunzi walikwenda na kuhubiri Neno kila mahali kwa nguvu nyingi hivi kwamba hofu iliwaangukia wapinzani wao, na hawakuthubutu kufanya yale ambayo wangefanya kama ushahidi ungekuwa wazi sana kwamba Mungu alikuwa akifanya kazi. (MTC 108.3)

Katika kila mikusanyiko mikubwa, baadhi ya wachungaji wetu wanapaswa kuhudhuria. Wanapaswa kufanya kazi kwa hekima ili kusikilizwa na kupata nuru ya Ukweli mbele ya watu wengi kwa kadri iwezekanavyo. ... (MTC 108.4)

Tunapaswa kuboresha kila fursa kama ile iliyotolewa kwenye Maonyesho ya St. Louis, Marekani, Katika

mikusanyiko hiyo yote kunapaswa kuweko watu ambao Mungu anaweza kuwatumia. Vipeperushi vyenye nuru ya Ukweli wa sasa vinapaswa kutawanywa kati ya watu kama majani ya msimu wa kupukutisha majani. Kwa wengi wanaohudhuria mikusanyiko hii, vipeperushi hivi vinapaswa kusambazwa kila mahali kama majani ya mti wa uzima, ambayo ni kwa ajili ya uponyaji wa mataifa.(MTC 109.1)

Ninakutumia hii, ndugu zangu [AG Daniells na WW Prescott], ili uwape wengine. Wale wanaokwenda kutangaza Ukweli watabarikiwa na Yeye ambaye amewapa mzigo wa kutangaza Ukweli huu. ... (MTC 109.2)

Wakati umefika kuliko wakati mwingine wowote, ambapo Waadventista Wasabato watainuka na kuangaza, kwa sababu nuru yao imekujia, na utukufu wa Bwana umezuka juu yao.—(Lt.296, 1904 ( Ev, 35, 36 ). MTC 109.3)

## SIYO WOTE WANAOITWA KUFANYA KAZI KWA MADARAJA YA CHINI

**Kazi kwa Maskini na Tajiri Inahitajika.—** [ MAELEZO *NA DK. DANIEL H. KRESS: "Kabla ya kuhitimu kutoka Chuo Kikuu cha Michigan, mwaka jana nilikaa kwa muda wa miezi mitatu katika jiji la Chicago, ambapo tulifungua misheni ya tiba na tulilenga kusaidia wale waliotengwa na waliopuuzwa, waliojulikana kama walio chini na walio nje (chini na nje). -kutoka, katika sehemu mbaya zaidi ya jiji la Chicago. Nilifurahia kazi hii, na katika mfadhaiko wangu nilifikiri labda ningeanza tena kazi hiyo. Nilimwandikia Dada White nikimwambia juu ya kile nilichokuwa nikifikiria, na katika kujibu alisema,* ] (MTC 109.4)

Katika barua yako unazungumzia kazi ya uokoaji katika sehemu maskini zaidi za jiji. Ninafurahi kwamba unahisi

mzigo wa kusaidia wale ambao wanahitaji msaada haswa. Kristo anatamani kazi Yake iwe nuru ya ulimwengu. Yeye Mwenyewe alikuja kujulisha makundi yote injili ya wokovu. Kunaweza kuwa na wale walio na uhusiano nawe, ambao wanapaswa kufanya kazi kati ya watu wasiobahatika, wanaochukiwa au wasioheshimiwa, lakini wewe unafaa hasa kufanya kazi kwa ajili ya madaraja ya juu. Mvuto wako kwao ungepungua iwapo utahusishwa kwa kiasi kikubwa na kazi ya uokoaji kwa wale ambao kwa ujumla hufikiriwa kuwa watu waliotengwa au kukataliwa.—(The Kress Collection, 168,

169. Ellen White's response is from Letter 158, 1909 (Manuscript Releases 7:329,

330). MTC 109.5).

**Vipaumbele Vinavyohitajika Wakati wa Kufanya Kazi kwa Madaraja ya Chini Zaidi.—** Suala kuu la wajibu wetu kwa wanadamu ni zito, na neema kubwa ya Mungu inahitajika katika kuamua jinsi ya kufanya kazi ili kutimiza kiasi kikubwa zaidi cha wema. Sio wote wameitwa kuanza kazi yao kwa kufanya utume kati ya watu wa tabaka la chini kabisa. Mungu hawahitaji watenda kazi Wake kupata elimu na mafunzo yao ili kujitoa kikamilifu kwa madaraja haya.— (Manuscript 3, 1899 ( Ev, 548 ). MTC 110.1)

**Kazi kwa Madaraja ya Chini Zaidi haipaswi kuzidi ile ya Utangazaji wa Injili Ulimwenguni Pote.—** Hatuwashauri watu wetu kufungua kazi katika miji yetu na kufikia kiwango cha kujenga majengo ambayo watawaalika watu walioharibikiwa zaidi kwa uovu na utovu wa maadili kuja kupewa chakula, vitanda vya kulala na matibabu bila pesa, au gharama yoyote. Hakuna hata mmoja anayetakiwa kuanzisha kazi katika mji wowote ambayo inatoa mwaliko

usio na busara kwa tabaka fulani kutegemezwa mkono na mashirika ya misaada ya Waadventista Wasabato, ambao kazi yao maalum ni kutoa ujumbe usiopendwa na ulimwengu. Utume umetolewa ili kupeleka ujumbe huo kwa mataifa yote.— (Letter 90, 1900 (Manuscript Releases 4:420). MTC 110.2)

**Msiwakataze Wale Wanaohisi Kuitwa Kusaidia Sehemu Mbaya Zaidi za Majiji.—** Ikiwa watu wanahisi kwamba Mungu amewaita watoe jitihada zao zote za kimishenari kwenye sehemu mbaya zaidi ya majiji, hakuna mtu anayepaswa kuwakataza kufanya kazi hiyo.—(Lt3, 1900 (Manuscript Releases 4:421). MTC 110.3)

**Pata Usaidizi wa Kifedha Kutoka Duniani ili Kugharimia Kazi kwa Walio**

**Duni Zaidi Katika Jamii. —** Ikiwa kuna watu ambao watachukua kazi ya kufanya kwa watu walio duni zaidi, watu ambao Mungu amewekea juu yao mzigo wa kufanya kazi kwa ajili ya umati wa watu kwa njia mbalimbali. Hebu watu hawa walioongoka waende na kukusanya kutoka ulimwenguni fedha zinazohitajika kufanya kazi hii. Hebu wasitegemee fedha ambazo Mungu anakusudia kuendeleza/kudumisha nazo kazi ya injili.— (Letter 205, 1899 ( Manuscript Releases 20:252 ). MTC 110.4)

## Sura ya 8—Kufanya Kazi Ndani na Nje ya Miji

**Baadhi Ni Lazima Waishi Katika Miji Ili Kuwafanyia Wengine Kazi.**— Ni kusudi la Shetani kuwavutia wanaume na wanawake kwenye miji, na ili kupata kitu hiki anabuni kila aina ya mambo mapya na yasiyo ya kawaida (kufikirika), yenye kila aina ya msisimko. Na miji ya dunia leo inakuwa kama miji ilivyokuwa kabla ya Gharika. (MTC 112.1)

Tunapaswa kubeba mzigo daima tunapoona kutimia kwa Maneno ya Kristo. "Kama vile siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu" ( Mathayo 24:37 ). Katika siku za kabla ya Gharika, kila aina ya matumbuizo au pumbao ilivumbuliwa ili kuwaongoza wanaume na wanawake kwenye usahaulifu na dhambi (wasahau dhambi). Leo, mwaka wa 1908, Shetani anafanya kazi kwa nguvu, kusudi hali zilezile za uovu zitatawale. Na ulimwengu unaharibika. Uhuru wa kidini hautaheshimiwa sana na wale wanaodai kuwa Wakristo, kwa kuwa wengi wao hawana ufahamu wa mambo ya kiroho.(MTC 112.2)

Hatuwezi kukosa kuona kwamba mwisho wa dunia unakuja hivi karibuni. Shetani anafanya kazi juu ya akili za wanaume na wanawake, na wengi wanaonekana kujazwa na tamaa ya kujifurahisha, kutumbuizwa na kusisimka. Kama ilivyokuwa siku za Nuhu, kila aina ya uovu unazidi kuongezeka. Talaka na ndoa umekuwa kama utaratibu wa wakati huo wa Nuhu. Kwa wakati kama huu, watu wanaotafuta kushika amri za Mungu wanapaswa kutafuta mahali patulivu, palipo mbali na miji. Wengine lazima wabaki mijini ili kutoa dokezo la mwisho la onyo, lakini jambo hili litakuwa hatari zaidi na zaidi kulifanya. Hata hivyo Ukweli wa leo lazima uje kwa ulimwengu—Ukweli kama ulivyonenwa kutoka kwenye midomo ya Yeye

aliyeelewa mwisho tangu mwanzo.— (Manuscript 85, 1908 ( Manuscript Releases 10:261, 262 ). MTC 112.3)

**Walei Watahamia Mijini Kuendesha Kazi ya Uinjilisti.—** Karibu nasi kuna majiji na miji ambayo hakuna jitihada zinazofanywa kuokoa roho za watu. Kwa nini familia zinazojua Ukweli wa sasa zisikae katika miji na vijiji hivi, ili kuweka hapo kiwango cha Kristo, wakifanya kazi kwa unyenyekevu, si kwa njia yao wenyewe, bali katika njia ya Mungu, kuleta nuru mbele ya wale wasio na ujuzi wa Injili? ... Kutakuwa na watu wa kawaida ambao watahamia mijini na majijini, na katika sehemu zinazoonekana kuwa nje au kando ya njia, ili waweze kuacha nuru ambayo Mungu amewapa iangaze kwa wengine. Wengine ambao watakutana nao hawataonekana kuwa wale wenye kuwapa matumaini ya kuukubali ujumbe huu, lakini swali pekee lapaswa kuwa, Je, watakuja kuwa na upatanifu na Kristo? Je, watakuwa washirika wa roho Yake, ili kwamba mvuto wao, katika kanuni na mfano, uwasilishe vivutio vya Mwanzilishi wa Ukweli na haki?— (R&H, September 29, 1891 ( Christian Service, 180 ). MTC 113.1)

**Taasisi Ziweke Nje ya Miji; Makanisa Yaanzishwe Ndani.—** Mara kwa mara

Bwana amerudia mara kwa mara kutuagiza kwamba tunapaswa kufanya kazi katika miji kutoka vituo vya nje ya miji (Outpost Centers). Katika miji hii tunapaswa kuwa na nyumba za ibada, kama makumbusho ya Mungu; lakini taasisi za uchapishaji wa maandishi au vitabu vyetu, taasisi za uponyaji wa wagonjwa, na za kuwafundisha na kuwazoeza watendakazi zinapaswa kuanzishwa nje ya miji. La

muhimu haswa ni kwamba vijana wetu walindwe dhidi ya vishawishi vya maisha ya jijini. (MTC 113.2)

Ni kwa kupatana na maagizo haya kwamba nyumba za mikutano zimenunuliwa na kuwekwa wakfu upya huko jijini Washington, DC, na katika Nashville, wakati nyumba za uchapishaji na Sanitarium katika vituo hivi zimeanzishwa mbali na moyo wa jiji wenye msongamano, kama vituo vya nje ya miji. Huu ndio mpango ambao umefuatwa katika kuondoa nyumba zingine za uchapishaji na nyumba za sanitarium toka mijini na kwenda nje ya mijii, na ni mpango ambao sasa unafuatwa huko Uingereza na taasisi ya uchapishaji la London (London Publishing House) na pia shule ya mafunzo huko. Sasa tumepewa fursa ya kusonga mbele katika majaliwa yaliyofunguliwa na Mungu ili kuwasaidia ndugu zetu katika vituo hivi na vituo vingine vingi muhimu kuanzisha kazi hiyo kwenye msingi thabiti, ili iweze kuendelezwa mbele kwa uthabiti.— (Special Testimonies, Series B 8 :7, 8 . (1907) MTC 113.3)

## MAKANISA

**Makanisa Yatakayoanzishwa Katika Miji.—** Katika kila jiji ambako Ukweli unatangazwa, makanisa yanapaswa kuanzishwa. Katika baadhi ya miji mikubwa lazima kuwe na makanisa katika sehemu mbalimbali za jiji. Katika sehemu fulani, nyumba za mikutano zitatouzwa kwa bei nafuu, ambazo zinaweza kununuliwa kwa na kunufaisha utume.— Lt.168, 1909 (MM, 309). (For additional information, see chapter 10, “Planting Churches in the Cities.”) MTC 114.1)(

**Kila Jiji Linapaswa Kuwa na Misheni ya Jiji.—** Ingawa tumeingia kwenye maeneo machache tu, vituo vingi vinapaswa kuanzishwa ambapo mamia ya wafanyakazi wataajiriwa. Katika kila mji kunapaswa kuwa na misheni ya jiji ambayo itakuwa shule ya mafunzo kwa watendakazi.

Wengi miongoni mwa ndugu zetu wanapaswa kusimama mbele za Mungu kama wale waliohukumiwa kwa sababu hawajafanya kazi ile ambayo Mungu angetaka waifanye.— (Lt.56, 1910 (portion in Medical Ministry, 303 ). MTC 114.2) **Kazi ya Wasamaria, Kuwahudumia Wale Ambao Jamii Inawapuuza.—** Hakuna kitu kitakachoweza kutoa tabia ya kazi daima katika uwasilishaji wa Ukweli kwa kuwasaidia watu pale walipo, hii ndiyo kazi ya Msamaria mwema. Kazi iliyofanywa vyema ipasavyo ili kuwaokoa wenye dhambi maskini ambayo watu wameipitia kando na makanisa itakuwa daraja la kuvuka ili kuingia pale ambapo Ukweli utapata nafasi ya kusimama (watu wapo tayari kuukubali na kuuhubiri kwa wengine). Mpangilio tofauti wa mambo unahitaji kuanzishwa kati yetu kama watu wa imani, na katika kufanya aina hii ya kazi, kungekuwa na angahewa tofauti kabisa linalozunguka roho za wafanyakazi, kwa kuwa Roho Mtakatifu huwasiliana na wale wote wanaofanya huduma ya Mungu, na wale wanaofanyiwa kazi na Roho Mtakatifu watakuwa nguvu kwa wema katika kuinua, kuimarisha, na kuokoa roho zilizo tayari kuangamia.— (Manuscript 14a, 1897 ( Ev, 567, 568 ). MTC 114.3)

**Kituo cha Misheni cha Mjini Kitaongeza Miito mingine ya Msaada.—** Tuna eneo kubwa la kuhubiri katika majiji yetu. Wakati misheni inapoanzishwa katika jiji, wito kwa watendakazi wa injili utakuja kutoka vijiji vya jirani. Kulingana na nuru niliyopewa, katika miaka thelathini iliyopita hakuna sehemu moja ya elfu moja (1/1000) ambayo imefanywa ambayo ilipaswa kufanywa. Mipango ya kazi ya mikali, ya kutibua mambo, ingepaswa kufanywa.— (Lt 176, 1901. MTC 115.1)

## TAAISI za ELIMU

**Shule za Kanisa Zitaanzishwa Katika Miji.—** Mengi zaidi yanaweza kufanywa ili kuokoa na kuelimisha watoto wa wale ambao kwa sasa hawawezi kutoka mijini. Hili ni jambo

linalostahili juhudi zetu bora. Shule za kanisa zinapaswa kuanzishwa kwa ajili ya watoto mijini, na kuhusiana na shule hizi mipango inapaswa kufanywa kwa ajili ya kufundisha masomo ya juu pale yanapohitajika. Shule hizi zaweza kusimamiwa kwa njia hiyo, sehemu ikiungana na sehemu, kiasi kwamba zitakuwa kitu kizima na kamili.— (Manuscript 129, 1903 ( Manuscript Releases 10:258 ). MTC
115.2)

**Wazazi Wahimizwa Kuwapeleka Watoto Kwenye Shule za Kanisa.—** Kanisa lina kazi ya pekee ya kufanya katika kuelimisha na kuzoeza watoto wake ili wasiweze kuathiriwa na wale wenye mazoea potovu, wanapohudhuria shule au katika ushirika mwingine wowote. Ulimwengu umejaa uovu na kutozingatia matakwa ya Mungu. Miji yake imekuwa kama Sodoma, na watoto wetu kila siku wanaonyeshwa maovu mengi. Wale wanaohudhuria shule za umma mara nyingi hushirikiana na wengine walioachwa bila kushugulikiwa zaidi kuliko wao, watoto wale ambao, kando na wakati unaotumiwa katika madarasa shuleni, wanaachwa wapate elimu ya mitaani. Mioyo ya vijana inavutwa kwa urahisi; na mazingira yao yasipokuwa ya tabia ifaayo, Shetani atawatumia watoto hawa ambao hakuna mtu anayewajali,ili kuwashawishi watoto wale ambao wamefunzwa na kuzoezwa kwa uangalifu zaidi. Na kabla ya wazazi watunza Sabato kujua kinachoendelea, masomo ya upotovu yanakuwa yamefunzwa tayari, na mioyo ya watoto wao wadogo imepotoshwa.— (C to P, T, &S,
173. (1913) MTC 115.3)

**Kuelimisha Wanafunzi Nje ya Miji ni Muhimu ili Kuokoa Nafsi Zao.—** Hebu wazazi waelewe kwamba kulea watoto wao kwa kuwafundisha ipasavyo ndiyo kazi muhimu katika kuokoa roho. Katika maeneo ya nje ya mji, mazoezi muhimu yapo kwa wingi katika kufanya mambo ambayo yanahitajika kufanywa kwenye shuguli za kila

siku (kuchota maji, kulima, kuni), mambo ambayo yatatoa afya ya kimwili kwa kukuza vyema mishipa ya fahamu na misuli. “Tokeni mijini” ndiyo ujumbe wangu kwa elimu ya watoto wetu. —(Manuscript 85, 1908 (SM 2:355). MTC 116.1)

## SANITARIUM (Tiba sahili)

**Sanitarium Kufikia Madaraja Yote ya Watu.—** Nuru kubwa imekuwa ikiangaza juu yetu, lakini nuru hii tunaiakisi kwa kiasi gani ulimwenguni! Malaika wa mbinguni wanangoja wanadamu tushirikiane nao katika utekelezajiwa vitendo, kanuni za Ukweli. Ni kupitia wakala wa huduma zetu za Sanitarium na taasisi zinazofanana na hii, ndiyo kwamba kazi kubwa inapaswa kufanywa. Taasisi hizi zinapaswa kuwa makumbusho ya Mungu, ambapo nguvu Zake za uponyaji zitafikia matabaka yote, ya watu wa juu na wa chini, matajiri na maskini. Kila senti iliyowekezwa kwenye taasisi hizi kwa ajili ya Kristo italeta baraka kwa mtoaji na kwa wanadamu wanaoteseka.— ( 7T.58, 59 . (1902) MTC 116.2)

**Sanitarium na Shule Havipaswi Kuanzishwa Katikati ya Miji.—** Baadhi ya mambo yamewasilishwa kwangu ambayo ninaona kuwa ya maana sana. Nuru imetolewa kwamba taasisi zetu hazipaswi kujengwa katikati ya miji. Uovu wa miji hii ni mkubwa sana hivi kwamba mengi ya yale ambayo macho yanaona na masikio yanasikia yana ushawishi wa kuvunja moyo. Hasa kwa shule zetu na Sanitarium, hizi zinapaswa kuwa nje ya miji, mahali ambapo ardhi inaweza kupatikana. ... (MTC 117.1)

Itakuwa kosa kwetu kununua au kusimamisha majengo makubwa katika miji ya kusini mwa California kwa ajili ya kazi ya Sanitarium, na wale wanaoona watanufaika katika kufanya hivi wanasogea mbele bila uelewa. Kazi kubwa yapasa kufanywa katika kutayarisha majiji hayo ili kusikia ujumbe wa injili, lakini kazi hii haitafanywa kwa kusimika

ndani yake majengo makubwa kwa ajili ya kuendeleza kazi fulani ya ajabu.— (Manuscript 114, 1902 ( Manuscript Releases 10 :209-211). MTC 117.2)

**Ni Bora kama Sanitarum Zitakuwa Nje ya Miji.—** Taasisi za kuwatunza wagonjwa zitakuwa na mafanikio makubwa zaidi ikiwa zingeanzishwa mbali na miji. Na kwa kadri iwezekanavyo kwa sasa, wote wanaotafuta urejeshwaji wa afya zao wanapaswa kujiweka katikati ya mazingira ya nje ya miji, mahali ambapo wanaweza kunufaika kwa kuishi nje ya nyumba zao (hewa bora). Asili (nature) ni daktari wa Mungu. Hewa safi, mwanga wa jua wenye kuchangamsha, maua na miti, bustani na mashamba ya mizabibu, na mazoezi ya nje ya nyumba katikati ya mazingira kama haya, hutoa afya, na hutoa uhai.— (MH, 263, 264 . (1905) MTC 117.3)

**Uhalifu wa Jiji huongeza Hitaji la Kuanzisha Vituo vya Sanitarium Milimani.—** Kadiri tunavyokaribia mwisho wa wakati majiji yatazidi kuwa fisadi, na yenye kuchukiza zaidi kama mahali pa kuanzisha vituo vya kazi yetu. Hatari za kusafiri zitaongezeka; kuchanganyikiwa na ulevi utakuwa mwingi. Ikiwa kunaweza kupatikana maeneo yaliyo milimani ambayo yametulia, mahali ambapo itakuwa vigumu kwa uovu wa majiji kupenyeza, hebu watu wetu watwae mahali kama hapo kwaajili ya Sanitarium na shule zetu za Sekondari.— (Manuscript 85, 1908 ( Manuscript Releases 10:260 ). MTC 117.4)

**Majengo ya Sanitarium Yakuze Afya na Furaha, ila Kusiwe na Ubadhirifu.—** Kama Enoko alivyofanya, tunapaswa kufanya kazi katika majiji lakini tusiwe wakazi humo. Hakuna kitu ambacho kina ladha ya ubadhirifu kinachopaswa kuonekana katika matumizi ya pesa wakati

wa kununua vifaa vya ujenzi au samani kwa sababu tunatazamia kupokea michango. Tafuta eneo ambalo lina angahewa nzuri na kisha uendelee na kazi yako, lakini ujiepushe na makazi ya viongozi wa miji hiyo iliyo mashambani. Wekeza nguvu zako zote ulizopewa na Mungu kwa watu wanaohitaji kuinuliwa. Usiweke taasisi zako katikati ya nyumba za watu matajiri. Ikiwezekana ni lazima tujipatie kiwanja kwaajili ya sanitarium ambacho hakitakuwa na watu wengi, mahali ambapo kuna ardhi ambayo inaweza kulimwa. Hebu chochote kisifanywe ili kujionyesha. Kwa uchumi Mkali tunapaswa kuonyesha kwamba sisi tunaelewa kuwa tu wageni na wasafiri hapa duniani. ... (MTC 118.1)

Katika kusimamisha majengo yetu, ni lazima tujiepushe na viongozi na watu mashuhuri wa dunia, na kisha tuwaache watafute msaada wanaohitaji kwa kuondoka kutoka kwa wenzao na kwenda kuishi katika maeneo yaliyo na utulivu zaidi. Hebu umakini wao uvutwe kwa watu wanaompenda na kumcha Mungu. Ikiwa Sanitarium haiko karibu na nyumba za watu matajiri, hawatapata fursa ya kutoa maoni yasiyofaa juu yake kwa sababu inaeleweka kuwa ni mahali ambapo wanadamu wanaoteseka wa tabaka zote hupokelewa hapo. ... (MTC 118.2)

Ni nini kinachohitajika kuleta mafanikio ya Sanitarium? Je, ni Jengo kubwa, la gharama kubwa? Ikiwa ndivyo hivyo, basi hatuwezi kuwa na mafanikio. Lakini jambo hili halitoi mafanikio. Angahewa ya neema ndiyo inayoizunguka roho ya mwamini, Roho Mtakatifu akifanya kazi juu ya akili na moyo, humfanya mtu kuwa harufu ya uzima hadi uzima na kumwezesha Mungu kubariki kazi yake. Mungu angeiunganisha familia Yake ya watendakazi pamoja kwa huruma ya kawaida ya mwanadamu na upendo safi. Upendo na heshima kwa kila mmoja kwa mwingine una mvuto unaozungumza na ni kielelezo cha utauwa kwa vitendo.

Kutoamini kuna ubaridi na huchukiza kwa giza na uadui, na kunaweza tu kukana au kuharibu, wakati kazi ya imani chini ya hali zote inaweza kuinua kichwa kwa uelewa wenye hadhi na imani thabiti kwa Mungu. Hata mioyo ya ujana inaweza kudhihirisha uzuri na utukufu mwingi katika barabara ya kujikana -nafsi na kujinyima kwa kufuata pahali ambapo Kristo anaongoza njia, akiinua msalaba Wake na kuubeba, akimfuata Baba Yake nyumbani mbinguni, akitembea katika njia iliyowekwa kwaajili ya wale waliokombolewa na Bwana. ... (MTC 118.3)

Hebu majengo yetu yote yatayarishwe ili kutoa afya na furaha, mipango yake iwekwe kwa jinsi ambayo kila hatua isiyo ya lazima itaokolewa. Hebu sanitariamu iwe pale ambapo wagonjwa watapata faida ya jua. Mahali pa moto panatakiwa pawemo katika kila chumba cha kulala ambamo wagonjwa wanaishi. Mipango hii ya vitu vya ndani ya chumba, lazima ifanywe ingawa jengo haliko katika mstari ulionyoka na barabara au majengo mengine. Vyumba vinapaswa kuwa na viti vinavyosaidia afya mtu akikalia (comfortable) navyo visiwe vya muundo mmoja, yaani vitofautiane-tofautiane. Matokeo yatakuwa ya kuridhisha zaidi ikiwa usahihi wa kupitiliza wa samani hautiliwi mkazo mno. Mungu ametupa mpango wa hili katika aina mbalimbali za maumbo na rangi vinavyoonekana katika uumbaji au mambo ya asili. Fedha lazima zitumike ili kupata fanicha/samani nzuri kwa afya, zinazoleta faraja mtu akikaa na mapumziko mazuri. Wagonjwa watafurahia samani za namna hiyo, kuliko pale fanicha zote zinafanana na kuwa kama jezi.— (Manuscript 85, 1899 ( Manuscript Releases 10:241-247 ). MTC 119.1)

**Viwanja au mali zinazofaa kwaSanitarium Zinapaswa Kuzingatiwa.—** Kutakuwa na sehemu fulani muhimu ambazo kutakuwa na mauzo ya viwanja ambavyo vinafaa

kwaajili ya majengo ambayo yanafaa haswa kwa kazi ya Sanitarium. Manufaa ya mambo haya yanapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu. (MTC 119.2)

Ili baadhi ya maeneo haya yaweze kununuliwa kwa ajili ya kazi yetu, itakuwa muhimu kutunza rasilimali za kanisa kwa uangalifu, kusiwe na ubaradhifu na kufanya maonyesho mahali popote pale. Usahili wa majengo tunayotumia utakuwa somo linalopatana na Ukweli tunaouwasilisha. Kwa kazi yetu ya Sanitarium lazima tupate majengo ambayo mwonekano na mpangilio wake utakuwa kielelezo cha kanuni za afya. —(Lt.168, 1909 (MM, 309). MTC 119.3)

**Kibali Kimezuiwa Kwenye Kujenga Sanitarium Jijini.—** Kutokana na nuru ambayo nimekuwa nayo kuhusu Sanitarium ambapo wagonjwa wanapaswa kutibiwa, siwezi kutoa hata neno moja la ushauri kuhusu kukusanyika mjini na kuwa na msongamano. Siwezi kuifanya mwenyewe, na bado inaweza kuonekana jambo tofauti sana na kwa wengine. Lakini Kwa nuru niliyo nao, sitaweza kushauri kuweka jengo mjini. Wewe ndugu [FB Moran] uko nje ya jiji, nafahamu hilo. Uko nje kwa upande mmoja. Hiyo inabadilisha pendekezo kwa kiasi fulani, lakini zaidi ya hayo, sikuweza kusema. Siwezi kukupa ushauri wowote. Itabidi mpange hilo kati yenu wenyewe kwa sababu siwezi kutoa ushauri wa kujenga sanitarium katika jiji lolote. Mimi siwezi kufanya hivyo, kwa sababu sababu jambo hili limewekwa wazi sana mbele yangu hivi kwamba mahali panapojengwa Sanitarium lazima pawe mahali panapoweza kutimiza mwisho mwema wa mradi huu—Lengo ambalo imeanzishwa kwa ajili yake. — (Manuscript 173, 1902 ( Manuscript Releases 10:250 ). MTC 119.4)

## MIGAHAWA YA VYAKULA VYA MIMEA AU MBOGA MBOGA (VEGETERIAN FOOD)

**Migahawa ya Vyakula visivyokuwa vya nyama Itaanzishwa Mijini.—** Mungu ameagiza migahawa iwekwe mijini. Ikisimamiwa ipasavyo, itakuwa vituo vya wamishenari. Katika migahawa hii machapisho yanapaswa kuwekwa karibu, ili yawe tayari kuwasilisha kwa wale wanaosimamia migahawa. (MTC 120.1)

Swali ambalo mara nyingi huja ni, Je , migahawa hii yapasa ifunguliwe siku ya Sabato? Jibu ni, "Hapana, hapana." Sabato ni alama na ishara yetu, na haipaswi kufutiliwa mbali. Hivi majuzi nimekuwa na nuru maalum juu ya mada hii. Jitihada zitafanywa ili migahawa ifunguliwe siku ya Sabato, lakini hilo halipaswi kufanywa.— (Manuscript 30, 1903 (Sermons and Talks 2:226). MTC
120.2 )

**Migahawa ya vyakula vya Mboga-Mboga Itafunza Kanuni za Kuishi Sahihi (vegeterian restaurants).—** Migahawa yetu lazima iwe mijini; kwa maana vinginevyo wafanyakazi katika migahawa hii wasingeweza kuwafikia watu na kuwafundisha kanuni za maisha zilizo sahihi. Na kwa sasa tutalazimika kumiliki nyumba za mikutano mijini. Lakini hapo awali kutakuwa na ugomvi na machafuko katika miji ambayo wale wanaotaka kuondoka hawataweza. Ni lazima tujitayarishe kwa masuala haya.— ( G.C. B, April 6, 1903, p. 88; {R&H, April 14, 1903 (SM 2:142). MTC 120.3)

**Chakula cha Kiroho Kinapaswa Kushea na Wafanyakazi kwenye Migahawa.—** Wafanyakazi katika migahawa yetu wanapaswa kujitayarisha kwa ajili ya maisha ya baadaye ya kutokufa, maisha ya milele. Hebu wajipatie nguvu na busara ya kuandaa chakula cha kiroho kwa ajili ya roho za wanaume na wanawake katika miji hii mikubwa. Lindeni roho za watu kama wale wanaopaswa kutoa hesabu. Miji inapaswa kuonywa, na vijana hawa na wasichana wanapaswa kukumbuka kwamba wakati ni wa thamani. Ulimwengu unaongezeka katika uovu kama katika siku za Nuhu.— —(Letter 279, 1905 (A Call to Medical Evangelism and Health Education, 22). MTC 121.1)

**Madarasa ya Kupika Yanapaswa Kuendeshwa.—** Kila mgahawa wa afya na usafi unapaswa kuwa shule. Wafanyakazi wanaohusika nayo wanapaswa kusoma, kujifunza na kufanya majaribio kila wakati, ili waweze kuboresha utayarishaji wa vyakula vyenye afya. Katika miji kazi hii ya kufundisha inaweza kuendelezwa kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko katika maeneo madogo. Lakini katika kila mahali palipo na kanisa, mafundisho yatolewe kuhusiana na utayarishaji wa vyakula rahisi, vyenye afya kwa ajili ya matumizi ya wale wanaotaka kuishi kulingana na kanuni za matengenezo ya afya. Na washiriki wa kanisa wanapaswa kuwapa watu wa ujirani wao nuru wanayoipokea kuhusu somo hili.— {7T.112, 113 . (1902) MTC 121.2)

**Migahawa ya daraja la kwanza itafanya watu waulize maswali.—** Nimeagizwa kwamba moja ya sababu kuu kwa nini migahawa ya afya na usafi na vyumba vya tiba (treatment rooms) vinapaswa kuanzishwa katikati ya miji mikubwa ni kwamba kwa njia hii tahadhari ya watu ambao ni viongozi au wakuu wa nchi, waitaitwa kwenye ujumbe wa malaika wa tatu. Wakigundua kuwa migahawa hii inaendeshwa kwa njia tofauti kabisa na jinsi migahawa ya

kawaida inaendeshwa, watu wenye akili wataanza kuuliza sababu za utofauti katika njia za biashara, na watachunguza kanuni zinazotuongoza kusevu au kuleta mezani chakula bora. Hivyo wat wataongozwa kwenye ujuzi wa ujumbe wa wakati huu.—(7T.122, 123 . (1902) MTC 121.3)

**Machapisho ya Kiroho Yatolewe Bila Malipo.—** Wale wanaokuja kwenye migahawa yetu wanapaswa kukabidhiwa vitu vya kusoma. Umakini wao unapaswa kuitwa kwenye machapisho yetu ya kiasi, afya na matengenezo ya lishe, na vipeperushi vinavyoshughulikia masomo ya Kristo vinapaswa kutolewa pia. Gharama ya kusambaza usomaji huu zinapaswa kubebwa na watu wetu wote. Wote wanaokuja wapewe kitu cha kusoma. Huenda wengi wao wakaacha machapisho haya bila ya kuyasoma, lakini baadhi ya wale ambao umeyaweka mikononi mwao, wanaweza kuwa wanatafuta nuru. Watasoma na kujifunza kile unachowapa, na kisha kuwapitishia/kuwapasia wengine.— (7T.116 . (1902) MTC 122.1)

**Migahawa ya wale ambao si Washiriki Inaweza Kufunguliwa Wakti wa Mikutano ya Kambi.—** Kwenye mikutano yetu ya kambi kunapaswa kuwa na mgahawa ambapo maskini wanaweza kupata chakula kizuri na chenye afya, ambacho kimetayarishwa vizuri kwa bei nafuu kwa kadri iwezekanavyo. Kunapaswa pia kuwa na mgahawa mwingine ambamo chakula hutayarishwa kwa misingi ya kutoa elimu kwawatu wa nje, ambapo wanaweza kuona uwakilishi wa lishe yenye kurekebisha afya. — (Pacific Union Recorder, Oktoba 23, 1902 . MTC122.2)

## VYUMBA VYA TIBA (treatment rooms)

**Vyumba vya tiba na Migahawa ya Mazao ya Mimea (Vegeterian diet) Vinapaswa Kuunganishwa Pamoja.—**

Nimepewa nuru kwamba katika majiji mengi ni vyema mgahawa uunganishwe na vyumba vya tiba. Taasisi hizo mbili zinaweza kushirikiana katika kushikilia kanuni zinazofaa. Kuhusiana na haya wakati mwingine inashauriwa kuwa na vyumba vya wageni kulala, na ambavyo vitatumika kama makao ya wagonjwa. Maeneo haya yatatumika kama mahali pa lishe na ugavi kwenye vituo vya Sanitarium vilivyoko nchini.—(7T.60 . (1902) MTC 122.3)

## Sura ya 9—Huduma ya Afya Iliyokita kwa Kristo Daraja linaloongoza kuvukia

**Huduma ya Afya Itakuwa Mahali pa Kuanzia.—** Kazi ya umishenari wa tiba imeonyeshwa kuwa daraja la kuvukia na kuwasilisha Ukweli wa sasa. Ni kwa kazi hii ndipo ambapo mioyo hufikiwa, na wale waliokuwa na chuki au ubaguzi na injili, mara moja wanalainishwa na kujisalimisha. Hii ndiyo kazi inayopaswa kufanywa leo.— (Letter 110, 1902 (Manuscript Releases 4:374). MTC 123.1)

**Uinjilisti wa Afya Hufungua Milango ya Kushiriki Injili.—** Uinjilishaji wa ulimwengu ni kazi ambayo Mungu amewapa wale ambao wanaenda kwa Jina Lake. Hawa wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Kristo, wakiwafunulia wale walio tayari kuangamia upendo Wake mwororo, na wenye huruma. Mungu anawaita maelfu ya watu kufanya kazi kwa ajili Yake, si kwa kuwahubiria wale ambao tayari wanaujua Ukweli, na siyo kupita na kurudi kwenye uwanja huo huo, bali kwa kuwaonya wale ambao hawajapata kamwe kusikia ujumbe wa mwisho wa rehema. Fanya kazi, kwa moyo uliojaa hamu ya dhati kwa roho. Fanya kazi ya umishenari wa tiba. Hivyo utapata ufikiaji kwenye mioyo ya watu. Njia itatayarishwa kwa ajili ya utangazaji wa Ukweli uliodharimiwa zaidi. Utagundua kwamba, hii itawaondolea mateso ya kimwili kutoa fursa ya kuhudumia mahitaji yao ya kiroho.(MTC 123.2)

Bwana atakupa mafanikio katika kazi hii, kwani injili ni uweza wa Mungu uletao wokovu wakati inaposukwa kwenye maisha ya vitendo, na wakati mtu anaishi injili inaishi na kuitekeleza. Muungano wa kazi kama ya Kristo kwa ajili ya mwili wa mwanadamu na kazi kama ya Kristo kwa ajili ya roho ndiyo tafsiri ya kweli ya injili.— (A Call to Medical Evangelism and Health Education, 7. MTC 123.3)

**Wote Wanaohitaji Kusaidiwa na Uinjilisti** wa afya (health evangelism).— Yeye [Bwana] anaona katika miji yetu wengi ambao wamebarikiwa na sehemu kubwa ya uwezo wa kiakili na kimwili wakifagiliwa na kuingia katika kimbunga cha majaribu. Hawa ni lazima wafikiwe. Hapa ndipo matengenezo ya afya yamefanywa kuwa daraja la kuvukia na kuingia. Kwa kazi hii wengi wamefikiwa ambayo vinginevyo wasingefikiwa. Wanaume na wanawake wenye hisia kali, hisia bora, na uungwana, watu wenye huruma nyingi, wameamshwa kufanya jambo fulani, huku kuhani na Mlawi wamekuwa wakipita upande ule mwingine. ... (MTC 124.1)

Kuna kazi ya kufanywa katika miji ya Amerika ambayo ni tofauti sana na kazi ambayo imefanywa tayari. ... Sio tu wale walio katika madaraja ya kuheshimika ya jamii wafanyiwe kazi, [lakini] walioanguka na walioshushwa hadhi wanapaswa kukusanywa. Ni katika barabara kuu na viunga vya miji ndipo roho zinazohitaji kuokolewa zitapatikana. Wengi ni vipofu wa kiakili, wamejeruhiwa kiakili. Kuna wale ambao wamekuwa na upendeleo au fursa ya kielimu, ambao wana vitivo vyenye thamani katika kupokea, na ambao wamejitoa au kujiangusha kwenye majaribu. Hawa ni wa kutafutwa. Wengine wana talanta zaidi, na zisizo za kawaida, lakini ni wafu katika makosa na dhambi, na ni lazima wafanyiwe kazi kwa bidii (Waefeso 2:1-2).— (Manuscript 33, 1899. MTC 124.2)

**Msaada wa Kikristo Unafanya Kazi Ili Kuwabariki Wengine.**— Wewe [Dakt. JH Kellogg] unazungumza kuhusu kazi inayofanywa Chicago. Nina huruma kabisa na kazi inayofanywa huko. Ninaamini katika kusaidia katika kila mstari ambao inawezekana kusaidia, kufuata hatua za Kristo. Wale ambao wameshikilia kazi hii ya msaada kwa Kikristo, ambao watajiweka wakfu kwa Mungu, watapata kwamba Yeye atakuwa msaada tele wakati wa sasa kwao,

katika kila saa ya hitaji. Ninajua kwamba Bwana atawatumia wale ambao watajinyenyekeza Kwake, na kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, watawezeshwa kufanya kazi inayohitaji kufanywa.— (Lt.43, 1895 ( Manuscript Releases 4:131 ) . MTC 124.3)

**Huduma ya Afya Hutayarisha Njia ya Kupokea Ukweli.—** Mkono wa kuume hutumiwa kufungua milango ambayo mwili unaweza kupata mpenyo wa kuingilia . Hii ndio sehemu ambayo kazi ya umishenari wa tiba inapasa kutenda. Kwa kiasi kikubwa, jambo hili linapasa kuandaa njia kwa ajili ya mapokezi ya Ukweli wa wakati huu. Mwili usio na mikono hauna manufaa. Katika kuupa mwili heshima, heshima lazima pia itolewe kwa mikono inayosaidia, ambayo ni wakala muhimu sana, ambao bila hiyo mikono, mwili hauwezi kufanya chochote. Kwa hiyo mwili unaoutendea mkono wa kulia isivyo, bila kujali, na ukikataa msaada wake, hauwezi kutimiza chochote.— (Manuscript 55, 1901 ( MM, 238 ). MTC 125.1)

**Kazi ya Uinjilisti wa Afya Ni Muhimu katika Kuendeleza Kazi ya Mungu.—** Kazi ya umishenari ya tiba ni mkono wa kuume wa injili. Ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Mungu. Kwa vile kupitia kwa hii, wanaume na wanawake wanaongozwa kuona umuhimu wa mazoea sahihi ya mtindo wa maisha, nguvu inayookoa ya Ukweli itajulikana kwao. Kila mji unapaswa kuingiwa na watendakazi waliofunzwa na kuzoezwa katika kufanya kazi ya umishenari wa tiba. Kama mkono wa kuume wa ujumbe wa malaika wa tatu, mbinu za Mungu za kutibu magonjwa zitafungua milango kwa ajili ya kuingia kwa Ukweli wa sasa.— (7T.59 . (1902) MTC 125.2)

**Nafsi zenye Ugonjwa Zitafikiwa Kupitia Uinjilisti wa Afya.—** Nimeona majaliwa ya Bwana katika kazi ya

umishenari wa tiba inapaswa kuwa daraja la kuingilia kuingia kwa watu, ambalo nafsi zenye ugonjwa zinaweza kufikiwa.— (Lt. 36, 1893 ( CH, 535 ) . MTC 125.3)

**Uinjilisti wa Ulimwengu wa Uwazi kwa Afya. —** Kazi ya umishonari ya kimatibabu huleta kwa wanadamu injili ya kuachiliwa kutoka kwa mateso. Ni kazi ya uanzilishi wa injili. Ni injili inayotendwa, huruma ya Kristo iliyofunuliwa. Kwa kazi hii kuna hitaji kubwa, na ulimwengu uko wazi kwa ajili yake. Mungu aruhusu kwamba umuhimu wa kazi ya umishonari wa matibabu ueleweke, na kwamba mashamba mapya yaingizwe mara moja.— (Manuscript 55, 1901 ( MM, 239 ). MTC 125.4)

## MAKANISA YASHIRIKISHWE

**Popote Makanisa Yanapoanzishwa, Kazi ya Huduma ya Afya Inapaswa Kuanzishwa.—** Swali limeulizwa, je, hukumtia moyo Dk. [JH] Kellogg baada ya kuingia katika kazi hii? Najibu, nilifanya hivyo; kwani nilikuwa nimeagizwa kwamba kazi ya tabia hii yapaswa ifanywe na makanisa yetu yote; kwamba shauku ya kina inapaswa kuchukuliwa katika safu hii ya kazi; kwamba kulingana na nuru ambayo Bwana alikuwa amependezwa kunipa, kazi hii ingechukuliwa kwa kuazimia na wahudumu wetu, sio kuunda kituo kikubwa mahali pamoja, lakini kuanzisha kazi katika miji mingi na kuwaamsha watu kutoa fedha za Bwana kwa ajili ya kazi hiyo kwa niaba ya wanadamu wanaoteseka. (MTC 126.1)

Bwana alinipa nuru kwamba katika kila mahali ambapo kanisa lilianzishwa, kazi ya umishenari wa tiba ilipaswa kufanywa. Lakini katika kanisa la Battle Creek kulikuwa na uchoyo/ubinafsi mwingi. Wale waliokuwa kiini cha kazi hiyo

waliendekeza matakwa yao wenyewe, kwa kujifurahisha wenyewe kwa njia ambayo ilimvunjia Mungu heshima. Dk. Kellogg hakutegemezwa katika kazi ya matengenezo ya afya, ambayo umuhimu wake ulikuwa umewekwa mbele ya kanisa kwa miaka thelathini. Kazi hii ilizuiliwa kwa sababu ya hisia na chuki za baadhi ya watu wa Battle Creek ambao hawakuwa na mwelekeo wa kuoanisha mwenendo wao wa utendaji na Neno la Mungu kuhusu kanuni za matengenezo ya afya. (Battle Creek Letters, 11 ). MTC 126.2).

**Kila Kanisa Linapaswa Kuwahudumia Wale Walio na Uhitaji.—** Kazi ya kuwakusanya watu wenye mahitaji, waliokandamizwa, wanaoteseka, na fukara, ndiyo kazi ileile ambayo kila kanisa linaloamini Ukweli wa wakati huu linapaswa kuwa likifanya tangu zamani. Tunapaswa kuonyesha huruma nyororo ya Msamaria mwema ..., tukiwalisha wenye njaa, tukiwaleta maskini waliotupwa nje majumbani mwetu, tukikusanya kutoka kwa Mungu kila siku neema na nguvu ambazo zitatuwezesha kufikia kilindi cha huzuni ya mwanadamu. na kuwasaidia wale ambao hawawezi kujisaidia wenyewe. Katika kufanya kazi hii tuna fursa nzuri ya kumwasilisha kwa wazi Kristo Aliyesulubiwa.— (6T.276 . (1900) MTC 126.3)

**Hekima Inahitajika.—** Wale ambao wataingia katika majiji yetu makubwa kufanya kazi ya uinjilisti wa tiba, ni lazima waanze kazi yao kwa hekima sana. Malaika wa Mungu wataleta hisia, na chini ya ushawishi mtakatifu wa Roho Mtakatifu, mioyo itaguswa. Maneno ya mzungumzaji yataleta umbo la mafundisho yenye uzima katika mawasiliano halisi na msikilizaji, yatasababisha wokovu wa roho.— (Letter 4, 1910 ( Wito kwa Uinjilisti wa Kimatibabu na Elimu ya Afya, 42 ). MTC 127.1)

**Wote Wanaitwa Kushiriki Sehemu ya Kazi Hii.—** Kazi ya umishenari wa tiba ni mkono wa msaada wa Mungu. Kazi

hii lazima ifanyike. Inahitajika katika maeneo mapya, na katika mashamba ambayo kazi ilianzishwa miaka iliyopita. Kwa kuwa kazi hii ni mkono wa msaada wa Mungu na daraja la kuvukia ili kuingia na injili, tunataka ninyi [washiriki wa kanisa] muelewe kwamba mnapaswa kuchukua sehemu yake. Haipaswi kuachwa katika kazi ya injili. Kila mtu aliye mbele yangu asubuhi ya leo anapaswa kujazwa na roho ya kweli ya umishenari wa tiba.—(The General Conference Bulletin, Aprili 7, 1903, p. 105 ( R&H, Aprili 14,1903 ). MTC 127.2)

**Upanuzi wa Kazi ya Uinjilisti wa Kiafya Unahitajika.—** Tunamshukuru Bwana kwa kazi ya umishenari wa tiba ambayo tayari imefanywa, lakini kuna jeshi kubwa la watendakazi ambalo litashiriki katika aina moja la kazi katika maeneo mbalimbali mijini, na vinjia vidogo na nje ya miji. Kuna nuru zaidi ya kutolewa kwa wale wanaoangamia katika dhambi zao. Kutakuwa na kesi za kipekee ambazo hazihitaji tu mahitaji ya kimwili yanayotolewa, ambayo ni muhimu kama kazi ya kufikira roho ambayo ndiyo inapaswa kuwa ya kwanza, lakini wataunganishwa na Sanitarium (vituo vya tiba sahili) na nyumba ambazo zinaweza kuwasilisha kanuni safi, na sahihi za urejeshwaji wa afya ya mwili. Kuna wengi ambao wataushika mkono ulionyooshwa kwao, ili kuwaokoa.— (lt 83, 1897 . MTC 127.3)

**UNGANISHA HUDUMA YA UBINADAMU NA UINJILISHAJI Kazi ya Huduma ya Afya ni Kuwaelekeza Wagonjwa kwa Kristo.—**Tunapaswa kukumbuka daima kwamba lengo la kazi ya umishenari ya matibabu ni kuwaelekeza wanaume na wanawake wagonjwa kwa Mtu wa Kalvari, achukuaye a dhambi ya ulimwengu. Kwa kumtazama Yeye, watabadilishwa kuwa mfano Wake.

Tunapaswa kuwatia moyo wagonjwa na wanaoteseka kumtazama Yesu ili waishi. Hebu watenda kazi na waendelee kumshikilia Kristo daima, Tabibu Mkuu, mbele ya wale ambao ugonjwa wa mwili na roho umewaletea kuvunjika moyo. Waelekeze kwa Yule anayeweza kuponya magonjwa ya kimwili na ya kiroho. … (MTC 127.4)

Mara nyingi Mungu hufikia mioyo kupitia jitihada zetu za kuondoa mateso ya kimwili.(MTC 128.1)

Kazi ya umishenari ya kimatibabu ni kazi ya uanzishaji wa injili. …(MTC128.2)

Karibu katika kila jumuiya kuna idadi kubwa ya watu wasiosikiliza mahubiri ya Neno la Mungu au kuhudhuria ibada yoyote ya kidini. Ikiwa [watafikiwa] na injili, basi, lazima ipelekwe makwao. Mara nyingi msaada wa mahitaji yao ya kimwili ndiyo njia pekee ambayo wanaweza kufikiwa.

… Upendo usio na ubinafsi, unaodhihirishwa katika matendo ya fadhili zisizo na ubinafsi, utafanya iwe rahisi kwa hawa wanaoteseka kuamini katika upendo wa Kristo.

… (MTC 128.3)

Wanapomwona mtu asiye na kichocheo cha kujipatia sifa za dunia au fidia yoyote, akija nyumbani mwao, akiwahudumia wagonjwa, akiwalisha wenye njaa, akiwavisha walio uchi, akiwafariji walio na huzuni, na kuwaelekeza wote kwa upole, kwa Yeye ambaye, yule mtenda kazi wa kibinadamu alikuwa ni mjumbe tu wa upendo na huruma za Mungu—wanapoona hili, mioyo yao inaguswa. Shukrani huchipuka. Imani inawashwa. Wanaona kwamba Mungu anawajali, na wako tayari kusikiliza Neno Lake linapofunguliwa.— (MH, 144, 145 . (1905) MTC 128.4)

## KUONYESHA TABIA YA KRISTO

**Watendakazi wa Uinjilisti wa Afya Kuwakilisha Tabia ya Kristo.—** Kazi ya umishenari wa tiba ina asili ya Bwana Mwenyewe, na ina utume mtukufu zaidi wa kutimiza. Katika fani zake zote inapaswa kupatana na kazi ya Kristo. Wale ambao ni watenda kazi pamoja na Mungu hakika watawakilisha tabia ya Kristo kama vile Kristo alivyowakilisha tabia ya Baba Yake alipokuwa katika ulimwengu huu.— (Manuscript 130, 1902 ( MM, 24 ). MTC 128.5)

**Wito wa Kuwa Wakristo Katika Kukiri kwa mdomo na Vitendo.—** Jifunze maisha na tabia ya Kristo, na utafute kuiga mfano Wake. Mwenendo wa kutojiweka wakfu wa baadhi ya wale wanaodai kuwa waumini wa ujumbe wa malaika wa tatu umesababisha kuwafukuza baadhi ya kondoo maskini jangwani; na ni nani ambaye amedhihirisha utunzaji wa mchungaji kwa waliopotea na wanaomangamanga? Je, huu si wakati wa kuwa Wakristo katika utendaji na kukiri kwetu kwa mdomo? Ni ukarimu ulioje, huruma iliyoje, upendo mwororo ulioje, ambao Yesu ameudhihirisha kwa wanadamu wanaoteseka! Moyo unaodunda kwa pamoja na moyo Wake mkuu wa upendo usio na kikomo ambao utatoa/unatoa huruma kwa kila nafsi yenye uhitaji, na inayodhihirisha kwamba ina nia ya Kristo. "Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima." Kila nafsi inayoteseka ina dai la kupata huruma ya wengine, na wale ambao wamejazwa na upendo wa Kristo, waliojawa na huruma, upole, na huruma Yake, wataitikia kila ombi la huruma yao. Hawatasema, wakati ombi litakapotolewa kwao kwa ajili ya wale wanaoangamia nje ya Kristo, " Jambo hili halinihusu mimi." Hawatatenda sehemu aliyotenda ndugu mkubwa wa Luka 16, bali wataonyesha shauku na huruma ya binafsi.

Watafuata mfano wa Bwana wao, na wataenda kutafuta na kuokoa kile kilichopotea, wakitii Maneno ya Mwokozi aliposema, “Mpendane kama nilivyowapenda ninyi.” Kila nafsi inayojaribu kurejea kutoka kwenye kutanga-tanga kwake na kumrudia Mungu inahitaji msaada wa wale walio na moyo mwororo, moyo wenye sikitiko na upendo kama wa Kristo.— (R&H, Oktoba 16, 1894 . MTC 129.1)

**Matendo yasiyo na Ubinafsi Ndio Hoja Yenye Nguvu Zaidi kwa Ukristo.—** Ukweli ambao unaonyeshwa katika matendo yaliyo hai na yasiyo ya ubinafsi ndiyo hoja yenye nguvu zaidi kwa Ukristo. Kuwapa afueni wagonjwa na kuwasaidia walio na mifadhaiko na huzuni ni kufanya kazi katika mistari ya Kristo, na kuonyesha kweli zenye nguvu zaidi za injili zinazowakilisha misheni na kazi ya Kristo duniani. Maarifa ya sanaa ya kuwaondolea wanadamu wanaoteseka hufungua milango isiyo na idadi ambayo kwayo Ukweli unaweza kupata makao ndani ya moyo, kisha roho zinaokolewa hadi kwenye uzima, uzima wa milele.— (Lt.36, 1893 ( Manuscript Releases 2:240 ). MTC 129.2)

**Kazi ya Matibabu Ili Kuambatana na Huduma ya Injili.—** Katika miji yetu mikubwa kazi ya umishonari ya kitiba lazima iambatane na huduma ya injili. Itafungua milango kwa ajili ya kuingia kwa ukweli.— (Manuscript 117, 1901 ( Ev, 387 ). MTC 130.1)

**KAZI YA TIBA NA KAZI YA HUDUMA INAPASWA KUUNGANA PAMOJA KATIKA UINJILISTI WA MIJINI**

Kazi ya Tiba iambatane na Huduma ya Injili (watu wenye taaluma ya afya kama madaktari nk wafanye kazi na wahudumu/wachungaji).- Katika miji yetu mikubwa, kazi ya umishenari wa tiba lazima iende bega kwa bega na huduma ya injili. Hii itafungua milango ya kupenya Ukweli. **Kazi ya tiba Isitenganishwe na Kazi ya huduma ya Injili.—** Majuzi [1899] shauku kubwa sana imeamshwa

kuhusiana na tabaka la maskini na watu waliotengwa; kazi kubwa imefanywa kwa ajili ya kuwainua walioanguka na kushushwa hadhi. Hii kwa yenyewe ni kazi nzuri. Sisi tunapaswa kuwa na roho ya Kristo kila wakati, na tunapaswa kufanya daraja au aina ileile ya kazi ambayo Yeye aliifanya kwa wanadamu wanaoteseka. Bwana ana kazi ya kufanya kwa watu waliofukuzwa au kutengwa na jamii. Hakuna maswali kuhusu jambo hiil, ila huu unapaswa kuwa wajibu wa baadhi kuufanyia kazi miongoni mwa hawa watu, na kujaribu kuokoa roho zinazoangamia. Hili litakuwa na nafasi ya kuhusiana na kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu na kupokelewa kwa Ukweli wa Biblia.— (Manuscript 3, 1899 ( Ev, 548 ). MTC 130.2)

## Shetani Anajaribu Kugawanya Kazi ya tiba na Kazi ya huduma ili viwe

**Vitu Viwili Tofauti.—** Kazi ya umishonari ya tiba haipaswi kuendelezwa kama kitu tofauti na kazi ya huduma ya injili. Watu wa Bwana wanapaswa kuwa kitu kimoja. Kusiwe na utengano katika kazi Yake. Wakati na mali zinaingizwa katika kazi ambayo inasonga mbele kwa bidii sana, ila iko katika mwelekeo mmoja tu. Bwana hajaweka hili jambo kuwa hivi. Yeye aliwatuma mitume Wake kumi na wawili na baadaye wale sabini kuhubiri Neno kwa watu, na akawapa uwezo wa kuponya wagonjwa na kutoa pepo kwa Jina Lake. Mistari hii miwili ya kazi, kamwe haipaswi kutenganishwa. Shetani atabuni kila njama iwezekanayo ili kuwatenganisha wale ambao Mungu anatafuta kuwafanya wawe kitu kimoja. Hatupaswi kupotoshwa na hila zake. Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kuunganishwa na ujumbe wa malaika wa tatu kama vile mkono unavyounganishwa na mwili; na elimu ya wanafunzi katika mistari ya umishenari wa tiba haijakamilika bado, isipokuwa watu wamefunzwa na

kuzoezwa kufanya kazi kwenye muunganiko wa kanisa na huduma.— (Manuscript 3, 1899 ( CH, 557 ). MTC 130.3)

**Wachungajina Madaktari Wanapaswa Kufanya Kazi Pamoja katika Uinjilisti wa mijini.—** Katika jitihada hii kwa niaba ya majiji, vikundi vyote vya watendakazi vinaweza kushirikiana kwa kujinufaisha (pande zote). Msaada ambao tabibu anaweza kutoa kama mwinjilisti ni wa maana sana. Ikiwa wachungaji na madaktari watapanga kuungana katika jitihada ya kuwafikia wale wenye mioyo minyoofu katika majiji, matabibu, na vilevile wahudumu, watu wote watawekwa kwenye nafasi ya juu sana. Pale wanapojitahidi kwa unyenyekevu kufanya kazi kwa bidii, Mungu atafungua njia mbele yao, na wengi watapata maarifa yenye kuokoa ya Ukweli.— (North Pacific Union Gleaner, Aprili 13, 1910 . MTC 131.1)

## MATABIBU KAMA WAMISHENARI WA TIBA

### Madaktari Wanawakilisha Huduma ya Injili Madaktari ni Nembo ya

**Injili.—** Kazi ambayo [Kristo] aliwapa matabibu wetu ilikuwa ni ishara kwa ulimwengu, huduma ya injili katika kazi ya umishenari wa tiba.—(6T.246 . (1900) MTC 131.2)

**Madaktari Wawasilishe Ujumbe wa Injili kutoka Kwenye Jukwaa lao la tiba.—** Wale ambao ni waganga Wakristo wanaweza kufanya kazi yenye thamani kwa ajili ya Mungu wakiwa wamishenari wa kitiba. Mara nyingi sana mambo mengi yanashugulisha akili za matabibu, kiasi kwamba kwa hizi pilikapilika zinazowakumba, wanazuiliwa kutoka kwenye kazi ambayo Mungu angetaka waifanye kama wainjilisti. Hebu wahudumu wa afya watoe Kweli muhimu za ujumbe wa malaika wa tatu kutoka kwenye mkao maoni ya daktari. Madaktari waliojiweka wakfu na wenye talanta wanaweza kupata nafasi ya kusikilizwa katika miji mikubwa wakati ambapo watu wengine wangeshindwa kabisa kupata masikio ya watu. Madaktari wanapoungana

na wahudumu katika kutangaza injili katika majiji makubwa ya nchi, kazi yao iliyounganishwa na wachungaji italeta matunda ya kushawishi akili nyingi kuunga mkono Ukweli wa wakati huu.—(R& H, Aprili 7, 1910 ( Medical Ministry, 248 ). ) MTC 131.3)

**Kazi ya Matibabu Haipaswi Kuinuliwa Juu ya Kazi ya Kihuduma.—** Wewe [Daktari JH Kellogg] huwezi kujenga na kusimamia ipasavyo kazi ya umishenari wa tiba huku ukiipa umashuhuri na weledi ambao umefikiri kutoa, na unaopaswa kudumishwa. Kwa kuwakilisha kwako huduma ya injili kama ni kazi duni kuliko kazi ya umishenari wa tiba, umeweka maoni/umbo lisilo sahihi juu ya kazi hiyo... (MTC 132.1)

Si mara moja au mbili, lakini mara nyingi, wahudumu wamewasilishwa kwangu wakiwa wameketi mbele yako katika mikutano; nawe umewashtaki wale ambao hawakukuletea wewe sifa yoyote. Wazo lililobakia akilini mwako limekuwa kwamba uliona maamuzi yako kuwa bora ni kuliko ya wengine. Lakini ikiwa njia zako zitafuatwa na ndugu zako katika mambo yote, basi wao wasingekuwa wanatembea katika njia ya Bwana. (MTC 132.2)

Kuwahutubia wachungaji walio mbele ya madarasa yako, na kuinua kazi ya umishenari wa tiba juu ya kazi ya huduma ya kichungaji, ni kuleta hali ya mambo ambayo haipatani na ujumbe wa malaika wa tatu. Nilionyeshwa kwamba malaika walifunika nyuso zao waliposikia maneno yako kuhusu watumishi wa Mungu. Watu hawa wamepewa kazi ya kumfanyia Mungu, na wengi wao wanafanya kazi hii kwa uaminifu sawa na vile unavyofanya kazi yako. Wengine wanafanya kazi chini ya hali ya kukatisha tamaa zaidi, kwa sababu hawana urahisi, nyenzo au miundo mbiu uliyo nayo wewe kwa ajili ya kuendesha kazi zao. (MTC 132.3)

Kuyumba kwa mambo kwa uzito, kwenye mstari mmoja si mpango wa Bwana... (MTC 132.4)

Kazi ya umishenari wa tiba lazima iunganishwe kwa ukaribu na kazi ya huduma ya injili kama vile mkono na kiganja vinavyounganishwa na mwili. Huduma ya injili inahitajika ili kutoa mkazo, umuhimu, jukwaa na uthabiti kwenye kazi ya umishenari wa tiba; na huduma ya kichungaji inahitaji kazi ya umishenari wa tiba ili kuonyesha uhalisia wa injili kwa vitendo. Bwana angeifanya kazi Yake iendelezwe mbele kwa ulinganifu na upatanifu. Ujumbe Wake lazima uenezwe katika sehemu zote za ulimwengu. Kuna shamba kubwa la mizabibu la kufanyiwa kazi. Mkulima mwenye busara analima shamba la mizabibu ili kila sehemu izae matunda. (MTC 132.5)

Soma sura ya sitini na moja ya Isaya. Sura hii itatuambia ni kazi gani iliyo mbele yetu . “Bwana amenitia mafuta kuwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao; kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote wanaoomboleza; kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe uzuri badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe." (MTC 133.1)

Tafadhali zingatia kile Aya hii ... inamaanisha, “Nao watajenga mahali palipoharibiwa zamani, watapainua mahali palipokuwa ukiwa hapo kwanza, nao wataitengeneza miji iliyoharibiwa, mahali palipoachwa kwa vizazi vingi.” ... (MTC 133.2)

Bwana anasonga mbele katika mistari iliyonyooka, na Anataka kila sehemu ya kazi Yake iunganishwe na nyingine.—(Lt.135, 1899 (portion in Manuscript Releases 4:131, 132). MTC 133.3)

**Matengenezo ya Afya Yanayowasilishwa kwa Jinsi Isivyofaa Hujenga Ubaguzi na Chuki.—** Matengenezo ya afya yakifanywa/yakishugulikiwa kwa hekima, yatathibitisha kuwa daraja la kufikia watu na kisha Ukweli unaweza ukufuata kwa mafanikio makubwa. Lakini kuwasilisha matengenezo ya afya bila hekima, na kufanya somo hilo kuwa mzigo wa ujumbe, kumehamasisha kujengwa kwa chuki miongoni mwa wale wasioamini na kuzuia njia ya kuelekea kwenye ile Kweli, na kuacha maoni ya kwamba sisi ni watu wenye msimamo mkali, uliopitiliza. Bwana angependa sasa, tuwe na hekima na ufahamu kuhusu ni nini mapenzi Yake . Hatupaswi kutoa mwanya wa sisi kuchukuliwa [kama] watu wenye msimamo mkali au uliopitiliza. Hili litatuweka sisi na Ukweli Mungu aliotupa kuubeba kwa watu katika hasara kubwa. Kupitia nafsi iliyosukwa na kutojiweka wakfu, kile tunachopaswa kuwasilisha kuwa mbaraka, huwa kikwazo.— (Manuscript 5, 1881 ( Manuscript Relees 2:105 ). MTC 133.4)

## HUDUMA KWA WALE WENYE URAIBU

**Wale Walio na Uraibu (walioathirika) Wanahitaji Kusaidiwa.—** Kila matengenezo ya kweli yana nafasi yake katika kazi ya injili na huelekea katika kuinua nafsi hadi kwenye maisha mapya na ya utukufu. ... (MTC 133.5)

Kila mahali kuna kazi ya kufanywa kwa wale ambao kwa kukosa kiasi wameanguka. ... Kupitia mazoea yasiyo na kiasi wanajiletea magonjwa, na kupitia uroho/tamaa ya kupata pesa kwa ajili ya kuendekeza anasa za dhambi wanaanguka katika mazoea ya kukosa uaminifu/unyofu. Afya na tabia vinaharibiwa. Wanakuwa wageni kwa Mungu, waliotengwa au kutelekezwa na jamii, roho hizi maskini huhisi kwamba hazina tumaini kwa maisha haya au maisha yajayo. Mioyo ya wazazi imevunjika. Wanadamu

huzungumza juu ya watu hawa wakosefu kuwa hawana tumaini; lakini Mungu hawaoni hivyo. Yeye anaelewa hali zote ambazo zimewafanya kama vile walivyo, na Anawatazama kwa huruma. Hili ni kundi linalohitaji msaada. Kamwe wewe usiwape nafasi ya kusema, "Hakuna mtu anayeijali nafsi yangu." ... (MTC 134.1)

Mara nyingi katika kuwasaidia wasio na kiasi ni lazima, kama Kristo alivyofanya mara nyingi, tuzingatie kwanza hali yao ya kimwili. ... Katika kila mji panapaswa kutolewa mahali ambapo watumwa wa tabia mbaya wanaweza kupokea msaada wa kuvunja minyororo inayowafunga. ...(MTC 134.2)

Wale wanaopenda kujifurahisha wenyewe, lazima waongozwe kuona na kuhisi kwamba ukarabati mkubwa wa maadili ni muhimu ikiwa wangekuwa wanaume na wanawake wenye heshima zao. ... (MTC 134.3)

Wale wanaojaribiwa wanahitaji kuelewa msukumo wa kweli wa nia/mapenzi. Hii ndiyo nguvu inayotawala katika asili ya mwanadamu —nguvu ya uamuzi, ya kuchagua. ...(MTC 134.4)

Kupitia kuzoeza kwa usahihi ya mapenzi yako au nia, mabadiliko yote yanaweza kufanywa maishani. Kwa kusalimisha mapenzi kwa Kristo, tunashirikiana na uwezo wa Mungu. Tunapokea nguvu kutoka juu ili kutuweka imara. Maisha safi na adhimu, maisha ya ushindi dhidi ya hamu ya kula na tamaa za mwili, yanawezekana kwa kila mtu ambaye ataunganisha mapenzi yake ya kibinadamu yaliyo dhaifu, na yanayoyumba-yumba kwa mapenzi ya Mungu Mwenye uwezo wote, na mapenzi yasiyotikisika. (MH, p. 171-176 . (1905) MTC 134.5)

**Kazi ya Kiasi inapaswa Kusisitizwa.—** Mungu anataka tusimame mahali ambapo tunaweza kuwapa watu onyo. Anatamani tuichukue hoja ya kiasi. Kwa mazoea mabaya ya

kula na kunywa, watu wanaharibu nguvu waliyo nayo ya kufikiri na akili. Hatuhitaji kuchukua shoka na kuvunja vilabu vyao vya pombe (baa). Tunayo silaha yenye nguvu kuliko hii—Neno la Mungu Aliye hai. Hilo litapasua njia yake katika kivuli cha kuzimu ambacho Shetani anatafuta kuzuia njia yake. Mungu ni mkuu na Mwenye nguvu. Atazungumza na mioyo yao. Sisi tumemwona akifanya hivi.— (The General Conference Bulletin, April 23, 1901, p. 424 ( Eva, 587, 588 ;
Temperance, 235 ). MTC 134.6)

**Kazi ya Matengenezo Kufufuliwa.**— Fikiria jinsi uovu wa kutokuwa na kiasi unavyotenda kazi katika miji yetu. Je, hatujui kwamba pombe inayouzwa kwenye baa au vilabu vya pombe kwenye nchi yetu imetiwa vitu vyenye sumu zaidi? Tunasoma kuhusu mtu mmoja na mwingine ambao wamejiua wakiwa katika ulevi—kileo kimewapora akili zao. Tunahitaji kuwa na ujuzi wa mambo haya, ili tufanye kazi kwa akili katika kuwasaidia wengine. Kazi ya kiasi inahitaji kufufuliwa kwa kuwa bado haijafanyika. Tunahitaji kuhubiri injili, ili wanaume na wanawake waweze kuelewa jinsi ya kulitii Neno la Mungu. Ni Neno la Mungu Aliye hai ndilo litakalowaleta wanaume na wanawake katika uhusiano ufaao Naye; litaleta mguso kwenye moyo, akili na tabia. Hebu kila mmoja wetu aamshwe ili kufanya kazi inayongojea kufanywa—kazi ambayo Kristo aliifanya alipokuwa ulimwenguni. Kwa kutazama kazi za Kristo, ubinadamu utaushika Uungu. Hapo wito wa nafsi unafanywa, na Yeye kamwe hamtupi mtu. Haijalishi nafasi uliyopopo maishani, au vyovyote vile maisha yako yalivyokuwa wakati uliopita, Yeye bado atakupokea.— (R&H, Januari 14, 1909 . MTC 135.1)

**Kiasi Inajumuisha Mambo Yote Yahusuyo Maisha yenye Afya.**— Katika kutetea kazi ya kiasi, jitihada zetu zinapaswa kuzidishwa. Somo la kiasi cha Kikristo linapaswa kupata nafasi katika mahubiri yetu katika kila mji

tunakofanyia kazi. Matengenezo ya afya katika nyanja zake zote yanapaswa kuwasilishwa mbele za watu, na jitihada za kipekee zifanywe katika kuwafundisha vijana, watu wa makamo, na wazee, kanuni za maisha ya Kikristo.— (Manuscript 61, 1909 ( Temperance, 239 ). MTC 135.2)

**Vijana katika kuendeleza Huduma ya Kiasi.—** Hakuna kundi la watu linaloweza kutimiza mengi zaidi katika vita dhidi ya kutokuwa na kiasi kuliko vijana wenye hofu ya Mungu. Katika enzi hii, vijana katika miji yetu wanapaswa kuungana kama jeshi kwa uthabiti na kwa kudhamiria, wakijiweka dhidi ya kila aina ya uchoyo/ubinafsi na uendekezaji wa uharibifu wa afya. Hawa wanaweza kuwa na nguvu kiasi gani! Ni wangapi wangeweza kuokolewa kutokana kwa kuondokewa na ujasiri wa kukaa katika kumbi na bustani zilizo na muziki na vivutio vingine ili kuwavutia vijana! ...(MTC 136.1)

Vijana wa kiume na wa kike wanaodai kuamini Ukweli wa wakati huu wanaweza kumpendeza Yesu tu kwa kuungana katika jitihada za kukabiliana na maovu ambayo, yana ushawishi wa kuvutia ubaya, yamejipenyeza katika jamii. Wanapaswa kufanya yote wawezayo kuzuia wimbi la kutokuwa na kiasi linaloenea sasa kwa nguvu ya kudhoofisha juu ya nchi. Wakitambua kwamba tabia ya 'kutokuwa na kiasi' ina wadau wake waliojitangaza wazi wazi, hivyo wale wanaomheshimu Mungu wachukue msimamo wao kwa uthabiti dhidi ya wimbi hili la uovu ambalo kwalo wanaume na wanawake husombwa kwa upesi hadi kwenye maangamizi.— (YI, July 16, 1903 ( Temperance, 235 ). MTC 136.2)

## HUDUMA KWA AKINA MAMA WANAOLEA WATOTO PEKE YAO, YATIMA NA WAZEE

**Wajane, Yatima, Wazee, Wasiojiweza, na Wagonjwa Wote Huhitaji Msaada.— Wakati y**ote yanapofanywa ili kuwasaidia maskini wajisaidie wenyewe, bado kunabaki wajane na yatima na wale wasio na baba, wazee, na wasiojiweza. Wagonjwa, wanaodai huruma na matunzo. Kamwe hawa hayapaswi kupuuzwa au kuachwa. Hawa ni wa Mungu Mwenyewe na tumekabidhiwa sisi kama wasimamizi, ili tutoe rehema, upendo, na matunzo laini kwao .— (MH, p . (1905) MTC 136.3)

**Yatima na Wazee Wasaidiwe.—** Mungu anatuita kutoa ugavi wa mahitaji ya watoto hawa kwa kadiri tuwezavyo, yanayohusiana na upungufu wa malezi ya baba. Badala ya sisi kusimama pembeni au kutojihusisha, na kulalamika juu ya mapungufu yao, na shida ambazo wanaweza kusababisha, hebu tuwasaidie kwa kila njia iwezekanayo. Tafuta kumsaidia mama aliyechoka kwa masumbufu ya maisha. Mpunguzie mizigo.(MTC 136.4)

Kisha kuna makutano ya watoto ambao wamenyimwa kabisa mwongozo wa wazazi na mvuto wenye kutiisha wa nyumba ya Kikristo. Hebu Wakristo wafungue mioyo na nyumba zao kwa hawa wanyonge. Kazi ambayo Mungu amewakabidhi kama wajibu wa mtu binafsi haipaswi kukabidhiwa kwa taasisi fulani ya wema/ukarimu au kuachwa kwenye nafasi ya hisani ya ulimwengu. Ikiwa watoto hawana jamaa wanaoweza kuwatunza, hebu washiriki wa kanisa wawaandalie makazi. Yeye aliyetuumba na kutuweka katika mshikamano/ugo wa familia, na asili/haiba ya mtoto itakuzwa vizuri zaidi katika hali ya upendo wa nyumba ya Kikristo. ... (MTC 137.1)

Wazee pia wanahitaji ushawishi unaosaidia wa familia. Katika nyumba ya kaka na dada katika Kristo wanaweza kufidia kwa kiasi kikubwa hasara ya kupoteza nyumba yao wenyewe. ... Wafanye hawa wahisi kwamba msaada wao unathaminiwa, kwamba bado kuna jambo la kufanya katika kuwahudumia wengine, na hiyo itachangamsha mioyo yao na kuleta ari kwa maisha yao.(MTC 137.2)

Kwa kadiri inavyowezekana, waache wale ambao vichwa vyao ni vyeupe kwa mvi, ambao hata kutembea kwao kunaanza kuwa na shida na hivyo kuonyesha kwamba wanakaribia kuchungulia kaburi, wabaki miongoni mwa marafiki na watu wanaowafahamu. ... (MTC 137.3)

Wakati wowote washiriki wanapoweza kutunza jamaa zao, jambo hilo linapaswa kuwa fursa ya kila familia kuhudumia jamaa zao wenyewe. Wakati hii haiwezekani, basi, kazi ni ya kanisa, na inapaswa kukubaliwa kama upendeleo na jukumu lao. Wote walio na roho ya Kristo watakuwa na huruma nyororo kwa wale walio dhaifu na waliozeeka.— (MH, p. 203, 204 . (1905) MTC 137.4)

## MBINU ZA JESHI LA WOKOVU ZISIIGWE

**Ingawa Kazi ya Jeshi la Wokovu Si Yetu, Hatupaswi Kuwahukumu.—** Adui ameazimia kuchanganya uongo na Ukweli. Kwa kufanya hivyo anatumia fursa aliyopewa na tabaka potovu ambalo kwa ajili yao kazi nyingi na fedha zinatumika, tabaka ambalo hamu yao ya chakula imepotoshwa kwa kujifurahisha au kujiendekeza, roho zao zimedhalilishwa, tabia zao zimepotoka na kuharibika, mazoea na matamanio yao yamewaangusha, nao hugaragara chini, na daima wanajizoeza kuwaza maovu. Watu kama hao wanaweza kubadilishwa katika tabia; lakini

ni wachache sana ambao kazi hiyo ya kubadilishwa, ni kamili na ya kudumu! (MTC 137.5)

Wengine watatakaswa kupitia ile Kweli; lakini wengi hufanya badiliko la juujuu tu katika mazoea na utendaji wao, na kisha hudhania kwamba wao ni Wakristo. Wanapokelewa katika ushirika wa kanisa, lakini huwa ni tatizo kubwa, nao wanahitaji matunzo mengi (uangalifu mkubwa). Kupitia hawa Shetani anajaribu kupanda katika kanisa mbegu za wivu, ukosefu wa uaminifu, ukosoaji, na mashtaka. Hivyo anajaribu kuwapotosha washiriki wengine kanisani. Tabia ambayo imewatawala tangu utoto, ambayo iliwafanya waachane na makatazo/vizuio vyote na kuwashusha kwenye udhalilishaji, bado inawadhibiti. Wanaripotiwa kuokolewa, lakini mara nyingi sana wakati unaonyesha kwamba kazi iliyofanywa kwa ajili yao haikuwafanya wawe watoto wa Mungu wanaotii. Katika kila jambo dogo, hisia za kinyongo huinuka. Wanathamini uchungu, hasira, na chuki. Kwa maneno na roho zao wanaonyesha kwamba hawajazaliwa upya (mara ya pili). Mielekeo yao ni ya kushuka chini, inayoelekea kwenye tamaa za mwili na ufisadi. Hawaaminiki, hawana shukrani, si watakatifu. Ndivyo ilivyo kwa wote ambao hawajaongoka ipasavyo. Kila mmoja wa wahusika hawa walioharibiwa, wasiogeuzwa kwa kufanywa upya nia zao, anakuwa mtenda kazi mzuri wa Shetani, akizua mafarakano na ugomvi.(MTC 138.1)

Bwana ameweka alama kwenye njia yetu ya kufanya kazi. Kama watu Waadventista hatupaswi kuiga na kuingia katika mbinu za Jeshi la Wokovu. Hii si kazi ambayo Bwana ametupa tuifanye. Wala si kazi yetu kuwashutumu na kusema maneno makali dhidi yao. Kuna roho za thamani, na za zinazojitoa mhanga kwenye Jeshi la Wokovu. Nasi tunapaswa kuwatendea wema. Ndani ya Jeshi hilo kuna roho adilifu, ambazo zinamtumikia Bwana kwa uaminifu na

watu hao wataona nuru kuu zaidi, nao watasonga mbele kwa kukubali Ukweli wote. Wafanyakazi wa Jeshi la Wokovu wanajaribu kuokoa wale waliopuuzwa, waliokandamizwa au kukanyagwa-kanyagwa. Usiwakatishe tamaa. Waache wafanye daraja la kazi hiyo, kwa mbinu zao na kwa njia zao wenyewe. Lakini Bwana ameonyesha wazi kazi ambayo Waadventista Wasabato wanapaswa kuifanya. Mikutano ya kambi na mikutano ya hema inapaswa kufanywa. Ukweli wa wakati huu unapaswa kutangazwa. Ushahidi ulioamuliwa unapaswa kutolewa. Na mahubiri au hotuba zinapaswa kuwa rahisi sana hivi kwamba watoto wanaweza kuzielewa.— (8T.184, 185 . (1904) MTC 138.2)

## Sura ya 10—Kupanda Makanisa Mijini

**Makanisa Yanapawa Kupandwa Jiji Baada ya Jiji.**—Ninapotazama mrundiko wa majengo yaliyo hapa [katika Battle Creek], ninahuzunika moyoni. Iwapo ninyi [viongozi wa kanisa] mngekuwa na roho ya umishenari, kama mngetoka na kwenda kulingana na ukubwa wa ujumbe, kulingana na upana na umuhimu wake, hamngejenga hata nusu ya majengo mliyo nayo hapa leo. Mngejenga maejengo katika jiji baada ya jiji, na Mungu angeikubali kazi yenu. Yeye hapendi uongozi wenu. Yeye Hapendi kukosa kwenu maono. Anataka mfungue mashamba mapya, na kwa miaka mingi amekuwa akiwaita mfanye hivi. Hii inachukua pesa na vibarua; lakini nilisoma katika Danieli ya kwamba hao waongozao wengi kutenda haki watang'aa milele na milele. Sisi tunataka kuwa katika kundi hilo. Tunataka kuwa miongoni mwa wale wanaong'aa katika ufalme wa Mungu. Hapo tungetaka kuwaona wale ambao tumewaombea na kuwafanyia kazi. Mungu atusaidie.—(General Conference Bulletin, Aprili 5, 1901, p. 85 . MTC 140.1)

**Washiriki wa Kanisa Kuwanufaisha Wengine.**— Juu ya wote wanaoamini, Mungu ameweka mzigo wa kuinua makanisa. Kusudi la wazi la kanisa ni kuelimisha wanaume na wanawake kutumia uwezo wao waliokabidhiwa kunufaisha ulimwengu, kutumia mali ambazo Mungu amewakopesha, kwa utukufu Wake. Yeye amewafanya wanadamu kuwa wasimamizi Wake. Wanapaswa kutumia talanta Zake, alizokabidhiwa katika kujenga kazi Yake na kupanua ufalme Wake. Makanisa yetu, makubwa na madogo, hayapaswi kuendeshwa kwa njia ambayo yatategemea kwa kupitiliza msaada wa wahudumu/wachungaji. Washiriki wanapaswa kuwa imara katika imani kwamba watakuwa na ujuzi wa akili

wa kazi ya kweli ya umishenari. Hawa wanapaswa kufuata mfano wa Kristo, kwa kuwahudumia wale walio karibu nao. Wanapaswa kutimiza viapo walivyoviweka wakati wa ubatizo wao kwa uadilifu, nadhiri kwamba watafanya kwa vitendo mafunzo yanayofundishwa katika maisha ya Kristo. Wanapaswa kufanya kazi pamoja ili kuweka katika kanisa kanuni hai za kujikana nafsi na kujitoa, ambazo Kristo, Uungu Wake uliovishwa ubinadamu, ulienda Naye katika kazi Yake kama mmishenari. Ni kutoa ujuzi wa upendo na upole wa Kristo unaofanya kazi zote za umishenari zifae.— (Pacific Union Recorder, Agosti 1, 1901 . MTC 140.2)

**KIPAUMBELE KITOLEWE KATIKA KUPANDA MAKUNDI MAPYA Makanisa Yanayopangwa; Makanisa Makubwa Kusaidia Yale Madogo.—** Mara nyingi nimefikiria jinsi ambavyo tunaweza kubarikiwa kwa wingi zaidi ikiwa katika makanisa makubwa kungekuwa na kikundi cha watendakazi kilichowekewa mikakati vizuri, ambao wangekuwa wamishenari katika miji na majiji, wakiwafundisha wengine masomo ya thamani wanayopata, masomo ya ile Kweli,haki, uadilifu, na juu ya hukumu inayokuja. Wote wanapaswa kuwa wanafunzi, ila wasijifunze siku zote, na kisha wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa ile Kweli (1Timotheo 3:7)...... Muwe wanafunzi wenye bidii, na wakati wote fanyani kile mlichojifunza. Hii itakupa uzoefu ambao utakuwa wa thamani zaidi kwenu , na hakika mtawanufaisha wengine. Mungu ametupa nuru, ambayo ametuamuru tuiache iangaze; na ikiwa watu fulani wanakubali Ukweli katika eneo fulani, wapange kuwa kanisa mara tu jambo hilo linapoweza kufanywa kwa hekima, na waache wafanye kwa kadri wawezavyo, ujenzi wa nyumba ya ibada isiyo ya gharama sana, kama walivyofanya huko Willis [Michigan]; nyumba ambayo

wanaweza kuiweka wakfu kwa Mungu, na hapo wanaweza kukaribisha uwepo Wake Mungu kuwa pamoja nao. Anasema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, Nami nipo katikati yao.” Kisha yale makanisa makubwa zaidi ambayo hayana deni yaje kutafuta msaada kwenye makanisa-dada, na kutoa mali waliyokabidhiwa kuelekea majengo haya madogo ya ibada, ili makanisa madogo yasionewe na kukatishwa tamaa chini ya mzigo wa deni. Tusipite, kama kuhani na Mlawi, tukivuka na kwenda upande mwingine. Baraka kubwa kiasi gani zingetolewa kwa makanisa yanayosaidia kwa njia hii, na upendo mkubwa kiasi gani utaonyeshwa kwa upande wa makanisa maskini zaidi, wanapotambua kwamba walikuwa wakiangaliwa kwa wema! Na kwa msaada huu unaotolewa kwa ukarimu na ucheshi, yatakuja maoni mapana ya msaada/usaidizi wa Kikristo na wajibu. Kifungo cha udugu, na upendo wenye nguvu na laini/mwororo, vingeundwa kati ya washiriki wa makanisa, makubwa kwa madogo; na wivu na husuda zote ndogondogo zingeunguzwa kwa upendo ulioonyeshwa kwa kiasi kikubwa.—(R&H, Julai 21, 1891 . MTC 141.1)

**Kazi Yapaswa Kuendelea Mpaka Kanisa Lisimamishwe Vizuri.—** Wafanyakazi wetu hawagawanyiki katika matawi jinsi wanavyopaswa katika kwa kutumia jitihada zao. Viongozi wetu hawako macho kwa kazi ambayo lazima ikamilike. Ninapofikiria juu ya miji ambayo kazi ndogo sana imefanywa, miji ambambo mle kuna maelfu mengi yanayopaswa kuonywa juu ya ujio wa Mwokozi upesi, moyo wangu unakuwa na shauku kubwa ya kuona wanaume na wanawake wakienda kazini kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, iliyojaa upendo wa Kristo kwa roho zinazoangamia. (MTC 142.1)

Wapagani walio mijini karibu na malango yetu wamepuuzwa kwa njia ya kushangaza. Mikakati

iliyopangwa vizuri ifanywe ili kuwaokoa. Sasa tunapaswa kufanya kazi ya kuleta wongofu kwa wapagani walio katikati yetu—wale ambao wanaishi kwenye kivuli cha milango yetu. Wimbo mpya wapaswa kutiwa vinywani mwao, nao watatoka kwenda kuwapa wengine walio gizani sasa, nuru ya ujumbe wa malaika wa tatu. (MTC 142.2)

Sote tunahitaji kuwa macho, ili, njia inapofunguka, tuweze kuendeleza kazi katika miji mikubwa. Tuko nyuma sana katika kufuata nuru tuliyopewa ya kuingia mijini na kuweka makumbusho ya Mungu. Tunapaswa kuwaongoza watu hatua kwa hatua katika nuru kamili ya Ukweli. Wengi wanatamani chakula cha kiroho. Tunapaswa kuendelea kufanya kazi hadi kanisa litakapopangwa na kujengwa nyumba ya unyenyekevu ya ibada (yenye gharama isiyo kubwa). Ninatiwa moyo sana kuamini kwamba watu wengi wasio wa imani yetu watasaidia sana kwa mali zao. Nuru niliyopewa ni kwamba katika sehemu nyingi, na hasa katika majiji makubwa ya Marekani ya kaskazini, msaada utatolewa na watu kama hao.— (Pacific Union Recorder, Oct 23, 1902 . MTC 142.3)

**Shule za Kanisa Kujengwa kwa Ajili ya Makutaniko Mapya.**— Wakati kundi la waamini linapoinuliwa, maandalizi ya makini yanapaswa kufanywa kwa ajili ya kudumisha kazi na uthabiti. Nyumba ya ibada itahitajika, na shule ambamo mafundisho ya Biblia yanaweza kutolewa kwa watu. Watendakazi hawapaswi kuondoka katika uwanja wao wa kazi bila kujenga kanisa na kujenga angalau chumba kimoja cha shule na kuweka mwalimu. ... Yote haya yamewasilishwa mbele yangu kama mtazamo wa panoramiki (amepata picha kama ya video hivi ya upana wa mambo haya). Niliona watendakazi wakijenga nyumbaza ibada zisizo na gharama. Watu wapya walioingia kwenye imani walikuwa wakisaidia kwa mikono yenye hiari, na wale waliokuwa na mali walikuwa wakisaidia kwa mali zao.

Chumba cha shule kiliandaliwa kwa ajili ya watoto. Walimu walichaguliwa kwenda mahali hapa. Idadi ya wanafunzi shuleni haikuwa kubwa, lakini ulikuwa mwanzo wenye furaha. Nilisikia nyimbo za watoto na za wazazi. Bwana asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure. Isipokuwa Bwana atalilinda jiji, mlinzi anakesha lakini bure.—(Manuscript 3, 1899 ( Australasian Union Conference Record, July 26, 1899 ). MTC 143.1)

**Makanisa Mapya Yanaongeza Idadi ya Wafanyakazi Waliopatikana.—** Tunapaswa kutafuta kila mahali kuinua kundi la waumini ambao wataungana nasi katika kuinua kiwango cha Ukweli, na kufanya kazi kwa matajiri na maskini. Kisha makanisa yanapoanzishwa, kutakuwa na ongezeko la wasaidizi wa kufanya kazi kwa ajili ya maskini na waliotengwa.—(Manuscript 3, 1899 ( GW, 436 ). MTC 143.2)

**Pesa Inatumika kwa Ubora kama Itawafikia Wale Ambao Wanaweza Kusaidia Kuwafikia Wengine.—** Ikiwa jitihada, talanta, kazi, na pesa, ambazo zimetupwa Chicago kwa miaka kadhaa iliyopita zingewekezwa katika kuwafahamisha watu kuijua Kweli ya Mungu kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Kundi fulani la watu lingeweza kufikiwa kwa jitihada zenye hekima, zilizoelekezwa vizuri, na wengi wangepokea Ukweli ambao sasa wangeufanyia kazi ili kuwapa wengine wa daraja lao wenyewe.— (Manuscript 46, 1900 ( Manuscript Relees 4:422 ) . MTC 143.3)

**Kila Jiji la Amerika Linapaswa Kuwa na Makumbusho kwa ajili ya Mungu.—** Kwa nini maeneo mengi sana hupitwa kando? Angalia miji na majiji ambayo bado haijafanyiwa kazi. Kuna miji mingi mikubwa huko Amerika, sio Kusini tu, lakini Kaskazini pia, ambayo bado inapaswa kufanyiwa kazi. Katika kila jiji la Amerika kunapaswa kuwa na makumbusho ya Mungu. Lakini ningeweza kutaja

mahali pengi ambapo nuru ya Ukweli bado haijaangaza. Malaika wa mbinguni wanangojea nyenzo za kibinadamu kuingia mahali ambapo ushuhuda haujatolewa ili kuwasilisha Ukweli. Jina la Bwana limetukanwa. Tafadhali someni Biblia zenu, na muone ikiwa si kweli kwamba kazi yetu ni kama haijaanza kabisa.— ( R&H, Desemba 30, 1902
. MTC 144.1)

**Wachungaji kuhamia Maeneo Mengine Mbalimbali Baada ya Kanisa Jipya Kupangwa na Kujitegemea.—** Wachungaji Vijana hawapaswi kutiwa moyo kuhubiri makanisani. Hii si kazi yao. Wanapaswa kutoka nje ya kambi, wakianza kazi mahali ambapo Ukweli bado haijatangazwa. Hebu waende kwa unyenyekevu na upole wa Kristo, wakipata nguvu kutoka kwenye Chanzo cha nguvu zote.... (MTC 144.2)

Wachungaji hawapaswi kutumia muda wao kufanya kazi kwa ajili ya wale ambao tayari wamekubali Ukweli. Upendo wa Kristo ukiwaka mioyoni mwao, wanapaswa kwenda kuwavuta wenye dhambi kwa Mwokozi. Kando ya maji yote, wajumbe wa Mungu wanapaswa kupanda mbegu za Ukweli. Mahali baada ya mahali panapaswa kutembelewa; kanisa baada ya kanisa linapaswa kuinuliwa/kujengwa. Wale wanaochukua msimamo wao kwa ajili ya Ukweli wanapaswa kupangwa katika makanisa, na kisha mhudumu apitie sehemu nyinginezo zinazofanana, kwa umuhimu uleule.— (R& H, Agosti 19, 1902 . MTC 144.3)

**Makanisa Yamedhoofishwa na Wahudumu Wanaorandaranda tu juu Yake.—** Wakati ambao umetumiwa katika kuhubiri makanisa yetu haujawatia nguvu watu, bali umewafanya kuwa dhaifu na wasio na msaada, wawe wanakunywa maziwa tu na wala si nyama. Mungu amekuwa akiwaita watumishi Wake kuwaacha wale tisini na tisa na kumtafuta yule kondoo mmoja aliyepotea Uzoefu wako [Mzee na Bi. Stephen N. Haskell] unapaswa

kuwa somo kwa wote wanaorandaranda juu ya makanisa— ni walaji tu, na si wazalishaji. Tunakuambia weka imani yako kwa Mungu. Mwache Yeye akuongoze. Bwana Yesu anajibu maombi yako.—(letter 132, 1901 ( Manuscript Relees 10:227, 228 ). MTC 144.4)

## USIFANYE MAKOLONI

**Vituo Vingi Vidogo Vinahitajika.—** Ni matamanio ya Bwana kwamba juhudi mpya zilizofanywa zitawekwa mahali pengi, na mimea midogo ianzishwe (makanisa madogo yaanzishwe). Kazi inapaswa kufanywa ambayo itafungua njia kwa ajili ya kuendeleza Ukweli, na ambayo itaongeza imani kwenye mioyo ya watu.... ...(MTC 145.1)

Kuna maeneo mengi ya kufanyiwa kazi, na mahesabu hayapaswi kufanywa ili kupanda maslahi mengi makubwa katika maeneo machache mahalia yanayopendelewa. Bwana ameniagiza kwamba tusifanye vituo vingi vikubwa; kwa maana katika kila eneo kunapaswa kuwa na miundombinu ya kufanikisha kazi hiyo. Kwa sababu hiyo taasisi chache na kubwa zisiruhusiwe kumalizia mapato yote ya fedha. Katika miji midogo na mikubwa, na katika makazi yaliyo nje ya miji, panapaswa kuwa na vituo vidogo ambavyo walinzi waaminifu wamewekwa ambao watafanya kazi kwa ajili ya roho. Popote mfanyakazi mmishenari aendako, juhudi zake zinapaswa kufuatiliwa na jengo dogo ili kuharakisha kazi kusonga mbele. Watumishi wa Mungu wanapofanya kazi yao kwa uaminifu, Majaliwa ya Mungu yatafungua njia kwa ajili ya miundombinu au majengo ya namna hii katika maeneo mengi.—(Letter 30, 1911 ( Ev, 535 ). MTC 145.2)

**Kazi Inayopaswa Kufanywa Katika Maeneo Mengi Mahalia.—** Wewe [Daktari JH Kellogg] wajua kwamba nimepata nuru kuhusu suala la kuwa na taasisi na

pilikapilika zilizosheheni mjini Battle Creek. Maendeleo yanapaswa kufanywa mahali pengine pia. Kuna miji mingapi huko Amerika ambayo imeachwa bila kuguswa! Kwa nini usiruhusu baadhi ya nguvu zako zitumike kuwaweka watu kazini katika maeneo mahalia mbalimbali? Hebu mvuto wa Ukweli ufike mbali. Hebu ujuzi wa jinsi ya kuhifadhi afya usambazwe sana. Acheni kazi ianze pale ambapo hakuna jambo lolote limetimizwa.—(Letter 43, 1895 (Manuscript Releases 17:309). MTC 145.3)

**Sio Kujificha Katika Makoloni.—** Huu si wakati wa kujenga makoloni na kutawala kurundikana mahali hapo pamoja. Kutoka jiji hadi jiji kazi inapaswa kupelekwa kwa haraka. Nuru ambayo imewekwa chini ya pishi inapaswa kutolewa na kuwekwa juu ya kinara, ili iweze kutoa mwanga kwa wote walio ndani ya nyumba.— (Manuscript 21, 1910 ( MM, 302 ). MTC 146.1)

**Washiriki Wanaokusanyika Mahalp Pamoja Waitwe Kwenye Utumishi Mkubwa Zaidi.—** Muda unapita haraka. Siku ya kutoa hesabu kwa Bwana inakaribia. Waadventista Wasabato hawatakiwi kufanya makoloni na kukaa hapo wakiwa wamerundikana (kama Ngongongare, Usa River Arusha). Tunapaswa kufanya kazi kama vile Yesu alivyotupa mfano. Kuhusu kazi ya Kristo tunasoma: “Akaondoka Nazareti, akaja Kapernaumu, iliyoko kando ya bahari, katika mipaka ya Zabuloni na Naftali; ili litimie Neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, nchi ya Zabuloni, na nchi ya Naftali, kando ya njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya Mataifa; watu waliokaa gizani waliona nuru kuu; nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti nuru imewazukia.” “Naye Yesu alikuwa akizunguka katika Galilaya *yote*, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Injili ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na

udhaifu wa kila namna katika watu." Hii ndiyo kazi ambayo itafungua milango kwa Ukweli. ... (MTC 146.2)

Ndivyo wakati wa Mmishenari Mkuu ulivyotumika. Ninafikiri juu ya kazi ambayo ingeweza kufanyika Battle Creek, na maeneo mengine machache yaliyopendelewa ikiwa wangekuwa wakiendeleza kazi katika vijiji na miji na majiji ambamo hakuna makumbusho ya ile Kweli. ... (MTC 146.3)

Wakati macho ya washiriki wetu waliopo katika makanisa yetu makubwa yanapopakwa dawa ya macho ya mbinguni, watasimama, na kwenda kutimiza agizo hili. Wakati mioyo yao inapojazwa na Roho Mtakatifu, watamwabudu Bwana Mungu wao, na Yeye pekee, Ndiye watamtumikia. Bwana anawaita wale ambao wamekusanyika katika vituo vyenye msongamano wa watu kwenda mahali ambapo Ukweli haujawahi kutangazwa. Wanapaswa kufundisha mambo ambayo Kristo ameamuru, wakiziacha mbali dhana mbalimbali zinazotokana na nadharia zinazotapatapa huku na kule bila mpango. Waalimu wa uwongo wataingia, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu. Shetani ataleta hekaya za uongo ili kuhitimisha kinyume cha kanuni za mafundisho ya Kristo. Mungu anawaita wajumbe Wake waaminifu kulichunguza Neno Lake, na kufundisha yale tu ambayo Kristo ameamuru. ... (MTC 146.4)

Kuna kuzururazurura/kutangatanga kwingi kwenye taasisi zetu, kupenda urahisi wa maisha kupita kiasi . Utume wa Kristo unapaswa kutekelezwa hadi kwenye nukta ndogo. Watu wa Mungu lazima waweke wakfu Kwake mali zao, na uwezo wao. Askari waaminifu wa msalaba wa Kristo wanapaswa kwenda nje ya kambi, wakiwa wamebeba lawama, na dharau na kufuata njia ya kujikana nafsi iliyokanyagwa na Mkombozi. (MTC 147.1)

Wahudumu wanaorandaranda juu ya makanisa, wakiwahubiria wale wanaoujua Ukweli tayari, ni afadhali waende mahali ambapo bado gizani. Isipokuwa watafanya hivi, wao wenyewe na makusanyiko yao yatadumaa na kuwa mbilikimo. Dini yetu imekuwa dhaifu na gonjwa kwa sababu washiriki wa kanisa wameacha upendo wao wa kwanza. Wanaweza kuwa wanaume na wanawake wenye nguvu katika Kristo ikiwa wangetii maagizo ya Bwana. (MTC 147.2)

Nimeamriwa kuinua sauti yangu katika kuonya, na kuwaita watu wetu ambao wamekusanyika pamoja katika mjini Creek kusonga mbele na kuchukua kazi waliyoteuliwa kuifanya na Mungu. Ulimwengu unaangamia katika dhambi. Je, ni mpaka lini mtakubali kushikiliwa kutoka kwa shamba kubwa la mizabibu lenye uhitaji, wakati historia ya ulimwengu huu iko karibu sana kufunzwa?(R &H, Februari 9, 1905 . MTC 147.3)

**Kusimika Taasisi Kubwa Mahali Pamoja Sio jambo Bora.**— Kitu kimefanywa katika misheni ya kigeni, na katika misheni za nyumbani; lakini maeneo mengi sana yameachwa bila kufanyiwa kazi. Kazi imekita zaidi kwenye mahali pamoja tu. Miundo mbiu hapo Battle Creek imekithiri, na hii ina maana kwamba sehemu nyingine za shamba la Bwana zimeibiwa majengo na utume ambao walipaswa kuwa nao. Maandalizi makubwa na bado makubwa zaidi, katika ujenzi na upanuzi wa majengo ambayo yamekusanywa pamoja na kushikilia idadi kubwa sana ya watu katika Battle Creek, si kwa mujibu wa mpango wa Mungu, lakini katika ukiukaji wa moja kwa moja wa mpango Wake. (MTC 147.4)

Imesisitizwa kuwa kulikuwa na faida kubwa kwa kuwa na taasisi nyingi zenye uhusiano wa karibu, kwamba zingekuwa nguvu kwa kila mmoja na kuwa msaada kwa wale wanaotafuta elimu na ajira. Hii ni kwa mujibu wa fikra

za kibinadamu; itakubaliwa kwamba, kwa mtazamo wa kibinadamu, faida nyingi hupatikana kwa kulimbikiza majukumu mengi hapo Battle Creek; lakini maono yanahitaji kupanuliwa. (MTC 147.5)

Taasisi hizi zinapaswa kugawanywa katika sehemu nyingi ili kazi iweze kuanza katika miji ambayo itakuwa muhimu kufanya vituo vya utume. Majengo yapasa kujengwa, na majukumu yajikite zaidi kwenye kwenye maeneo mengi mahalia ambayo sasa yamenyang'anywa umakini muhimu, na msaada wa kiroho ili kujaza wingi ambao upo tayari hapo Battle Creek (Battle Creek ina vingi, na bado wanarundika taasisi na majengo hapo, badala ya kupeleka kwingine).(8T.59, 60)(1904) MTC 148.1)

**Washiriki Walioshonana Pamoja Wanapoteza Umuhimu wa Utume.—** Neno la Bwana limenijia kwamba kuna waumini wengi sana ambao wamerundikana katika sehemu chache na kwamba wengi wanapoteza hisia zao za ufupi wa wakati na mzigo wao wa kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. . Kunapaswa kuwa na wongofu wa kweli moyoni, kwa kila muumini kama huyo anayerundikana hapo. Wale ambao wameunganishwa na ofisi zetu za uchapaji wanahitaji kubeba mzigo wa roho kabisa, na kujifunza njia na mbinu za kufanya kazi ya kibinafsi katika barabara kuu na pembeni ya mji.(MTC 148.2)

Bwana hutukuzwa katika kuongezeka kwa hesabu kunakoonekana katika baadhi ya vituo vyetu vya mafunzo na jitihada zao za umishenari.(Manuscript 53, 1910. MTC 148.3)

**Mioto ya Battle Creek Iliruhusiwa na Mungu ili Kufanya watu wasirundikane karibu na Taasisi za Kanisa (Kulikuwa na chuo, kampuni ya uchapaji, Sanitarium, Hospitali nk).—** Bwana aliruhusu moto uteketeze majengo makuu ya nyumba ya uchapaji iitwayo Review and Herald

na jumba la tiba rahisi, yaani Sanitarium na jambo hilo likaondoa upinzani mkuu uliosisitizwa dhidi ya kuhama kutoka Battle Creek. Ilikuwa ni mpango Wake kwamba badala ya kujenga upya nyumba moja kubwa ya Sanitarium, watu waende miji mingine na kujenga Sanitarium sehemu kadhaa. Hizi nyumba ndogo za tiba rahisi, yaani Sanitarium, zilipaswa kuanzishwa mahali ambapo ardhi ingeweza kununuliwa kwa madhumuni ya kilimo.(8T.227.)

## MKAKATI WA KUPANDA MAKANISA

**Omba Mwongozo wa Mungu Unapopanda Makanisa.—** Ni lazima tutafute hekima ya Mungu, kwa maana kwa imani ninaona kanisa lenye nguvu katika jiji hilo [Palmerston, New Zealand]. Kazi yetu lazima iwe ya kukesha na kuomba, kutafuta shauri la Yeye aliye mshauri mkuu na wa ajabu. Yeye aliye Mwenye nguvu kuliko nguvu za kuzimu anaweza kunyakua mawindo kutoka kwa Shetani, na chini ya uongozi Wake malaika wa mbinguni wataendelea na vita dhidi ya nguvu zote za giza na kupanda kiwango cha Ukweli na uadilifu katika jiji hilo.(Lt.79, 1893 (Ev, 39). MTC 149.1)

**Waongofu wanapaswa Kusimikwa kikamilifu katika Ukweli.—** Popote jitihada inapofanywa ili kusimamisha kanisa, maagizo kamili na ya uaminifu yapasa kutolewa kwa wale wanaokubali Ukweli. Hakuna sehemu ya kazi inayopaswa kupuuzwa, na hatupaswi kuwaacha wongofu wapya wenyewe wakati mtendakazi anaenda kwenye eneo jipya, ila wanapaswa kupokea matunzo na maelekezo. Usiruhusu chochote kibaki bila kufanyiwa kazi kikamilifu, na kuachwa katika hali ya shagalabagala au ovyo. Chochote kile kinachofanyika hebu na kifanywe kwa umakini.

Wachache wanaoletwa kwa njia hiyo katika Ukweli ,baada ya muda watatimiza mengi zaidi kuliko kukiwa na idadi kubwa zaidi ya wasio na elimu, wasio na mafunzo, ambao hawatambui wajibu wao, na ambao sifa zao za kipekee zimefumwa katika uzoefu wao wa kidini. Itakuwa vigumu sana kutengua yale ambayo yamefanywa vibaya, na kuweka msimamo au umbo jingine juu ya kazi, kuliko kuchukua kazi hiyo tangu mwanzo kabisa.(R&H, October 5, 1886. MTC 149.2)

## USIWAJALI WAKOSOAJI

**Washiriki Wasio na Utimamu wa Akili Hudhoofisha Kazi ya Mungu (hawana balansi).—** Katika historia yote ya kanisa, hakuna matengenezo ambayo yamesonga mbele bila kukumbana na vikwazo vizito. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Paulo. Popote ambapo mtume angesimamisha kanisa, kulikuwa na wale waliodai kuipokea imani, lakini walileta mafundisho yenye uzushi, na endapo haya yangepokelewa, hatimaye yangezima kuipenda ile Kweli. Luther alipatwa na mkanganyiko mkubwa na kufadhaika kutokana na mwendo wa watu wenye ushupavu usiotumia busara, ambao walikuwa na misimamo iliyopitiliza, na walidai kwamba Mungu alikuwa amesema moja kwa moja kupitia kwao, na kwa hiyo waliyaweka maoni yao wenyewe juu ya ushuhuda wa Maandiko. Wengi wao walikuwa wamepungukiwa na imani na uzoefu, lakini walikajiamini kuwa wamejitosheleza wenyewe, nao walipenda kusikia na kusema jambo fulani jipya, walidanganywa na walimu wapya waliojifanya (feki au bandia), nao wakajiunga na mawakala wa Shetani katika kazi yao ya kurarua kile ambacho Mungu alikuwa amemsukuma Luther kukijenga. Akina Wesley, na watu wengine waliobariki ulimwengu kwa mvuto na imani yao, walikumbana na hila za Shetani katika kila hatua,

akiwasukuma watu kuwa na usongo uliopitiliza, kutokuwa na utimamu wa akili au balansi, na wale wasiotakaswa kuwa na ushupavu usiotumia busara wa kila aina.(SP.4:245. (1884) MTC 149.3)

## Sura ya 11—Kazi katika Miji Maalum Miji katika Amerika Kaskazini

**Kupanuliwa kwa Kazi Amerika. —** Ningependa kuwaambia, marafiki zangu wapendwa, kwamba kazi hapa Amerika itatanuka sana. Mara nyingi sana kumewasilishwa mbele yangu kazi ambayo ilipaswa kufanywa huko Amerika, lakini ambayo bado haijafanywa, na hivyo roho yangu inalemewa sana. Mji baada ya mji ulipaswa kufanyiwa kazi, na kama hili lingefanywa kwa uaminifu, wangeletwa katika Ukweli wale ambao wangeweza kwenda kuzivuta roho nyingine kwa Kristo. Katika kila mji kuwe na makumbusho ya Mungu. Lakini jinsi kazi ilivyosimamiwa imesababish kupungua kwa hazima. Ukosefu wa juhudi za kupanda kiwango cha Ukweli katika miji ya Amerika umeleta hali ya mambo ambayo matumizi ni makubwa kuliko uzalishaji; na jinsi kazi hii itakavyosonga mbele sasa ni tatizo gumu (tatizo la kupasua kichwa).(Lt.20, 1903 (Ms.7:123 ). MTC 151.1)

### MI JI YA KASKAZINI MASHARIKI

**Miji Iliyoathiriwa na Harakati ya 1844 Ifanyiwe Kazi Tena.** Agizo limetolewa kwangu kwamba ujumbe unapaswa kwenda tena kwa nguvu katika majiji yaliyo kwenye Majimbo ya Mashariki. Katika miji mingi mikubwa ya Mashariki ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili ulitangazwa wakati wa harakati za 1844 ( Majimbo yaliyo karibu na bahari ya Atlantiki, kama vile New York, Maine, Massachuesets, Vermont, New Hampshire, Connecticut, Pennslyvania, Maryland nk). Kwetu sisi, kama watumishi wa Mungu, tumekabidhiwa ujumbe wa malaika wa tatu, ujumbe wa kuwafunga watu pamoja, ambao ni utasaidia kuwandaa watu kwa ajili ya ujio wa Mfalme. Tunapaswa

kufanya kila jitihada il kutoa ujuzi wa Ukweli kwa wote ambao watasikia, na kuna wengi ambao watasikiliza. Katika majiji yote makubwa, Mungu ana watu waadilifu wanaopendezwa na Ukweli.(9T.98 . (1909) MTC 151.2).

**Ujumbe wa Malaika wa Tatu Utangazwe katika Miji ya Kaskazini - Mashariki.** Miji hii yote ya Mashariki ambako ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili ulitangazwa kwa nguvu, na ambapo ujumbe wa malaika wa tatu ulihubiriwa katika siku za mwanzo za historia yetu kama ujumbe kwa watu tofauti, na wa kipekee, na sasa ni lazima ufanyiwe kazi upya. Kuna Portland, Maine; kuna Boston, na miji mingi inayozunguka; kuna New York City, na miji yenye watu wengi karibu na huo; kuna Philadelphia na Baltimore na Washington. Sihitaji kuhesabu maeneo haya yote; unajua yalipo. Bwana anatamani sisi tutangaze ujumbe wa malaika wa tatu kwa nguvu katika miji hii. (MTC 152.1)

Hatuwezi kutumia nguvu hii sisi wenyewe. Tunachoweza kufanya ni kuchagua watuwenye uwezo, na kuwahimiza waende katika njia hizi zenye fursa, na wakifika huko watangaze ujumbe kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.(Manuscript 53,1909 . MTC 152.2)

**Washiriki wa Kanisa wa Magharibi Kutegemeza Uinjilisti Mashariki (Magharibi ni California, Oregon na majimbo yaliyo kwenye Bahari ya Pasifiki ya Marekani).**Tunapofanya kazi kwa uaminifu katika ujirani wetu na katika miji iliyo karibu, na tunapotoa ujumbe uliodhamiriwa katika miji mikubwa ya nchi yetu, tutaona wokovu wa Mungu.(MTC 152.3)

Ukweli ni kwenda nje kama taa iwakayo katika miji ya Mashariki, na ndugu zetu wa Magharibi sasa wana pendeleo la kuendeleza kazi ya Mungu katika sehemu hiyo ya shamba ambako ujumbe wa malaika wa tatu

ulitangazwa kwa mara ya kwanza. **(Manuscript 23, 1910. MTC 152.4)**

**Boston Massachusets**

**Kazi lazima ijumuishe Boston.** Nimeagizwa kuwa Boston lazima ifanyiwe kazi; na ninajua kwamba kumiliki eneo hili na kujenga Sanitarium itakuwa ni mojawapo ya baraka kubwa zaidi ambazo zingeweza kuja kwa kazi yetu katika Majimbo ya Mashariki.( R&H, Septemba 29, 1904 MTC 152.5)

**Maelfu huko Boston Wanangoja Kusikia Ukweli.** Nina tashwishi kubwa kwamba Boston isikie Neno la Bwana na sababu za imani yetu. Mwambie Bwana awainue watenda kazi waingie shambani...... Kuna maelfu katika Boston wanaotamani Ukweli ulio sahili kama ulivyo katika Yesu.(Special Testimonies, Series B 13:8 . (1908) MTC 152.6)

**Ujumbe unapaswa kwenda kwa nguvu.** Ikiwa katika jiji la Boston na katika miji mingine ya Mashariki, wewe [Dk. Daniel H. Kress] na mke wako mtaungana katika kazi ya uinjilisti wa tiba, basi manufaa yako yataongezeka, na kutafunguka mbele yako maoni wazi ya wajibu. Katika miji hii ujumbe wa malaika wa kwanza ulikwenda kwa nguvu nyingi katika 1842 na 1843, na sasa wakati umefika ambapo ujumbe wa malaika wa tatu utatangazwa kwa upana katika majimbo ya Mashariki. Kuna kazi nzuri kwenye Sanitariamu zetu za Mashariki. Ujumbe unapaswa kwenda kwa nguvu wakati kazi itakapofungwa.(Letter 20, 1910 ( CH, 547 ). MTC 153.1)

**Kazi ya tiba Inapaswa Kufanywa katika Miji ya Boston na Miji Mingine ya New England.—** Wakati Sanitarium ya New England ilipoondolewa kutoka Lancaster Kusini [Massachusetts] hadi Melrose [Massachusetts], Bwana

aliniagiza kwamba hii ilikuwa katika utaratibu wa majaliwa Yake yaliyofunguliwa wazi. Majengo na uwanja wa Melrose yana tabia ya kupendekeza kazi yetu ya umishenari wa tiba, ambao iuapaswa kuendelezwa sio tu huko Boston, lakini katika miji mingine mingi ambayo haijafanyiwa kazi huko New England. Jengo la Melrose litatimiza mahitaji ya muhimu kwa watu, jambo ambalo litawavutia wale watu ambao sio wa imani yetu. Watu wa hali ya juu na vile vile watu wa kawaida watatembelea taasisi hiyo ili wapate kujinufaisha kwa yale yanayotolewa kwa ajili ya kurejesha afya. (MTC 153.2)

Boston imeonyeshwa kwangu mara kwa mara kama sehemu ambayo lazima ifanyiwe kazi kwa uaminifu. Nuru ni lazima iangaze pembezoni mwa mji na katika sehemu za ndani kabisa ya mji. Melrose Sanitarium ni mojawapo wa mawakala wakubwa ambao wanaweza kutumiwa kufikia Boston na Ukweli. Jiji na vitongoji vyake lazima lisikie ujumbe wa mwisho wa rehema kutolewa kwa ulimwengu wetu. Mikutano ya hema lazima ifanyike katika sehemu nyingi. Watenda kazi lazima watumie vizuri zaidi uwezo wao ambao Mungu amewapa. Karama za neema zitaongezeka zikitumiwa kwa upana. Ila ni lazima kusiwe na kujiinua. Hakuna mistari sahihi inapaswa kuwekwa chini. Acheni Roho Mtakatifu awaongoze watenda kazi. Wanapaswa kuendelea kumwangalia Yesu, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yao. Kazi ya mji huu mkuu itaonekana kwa alama ya ufunuo wa Roho Mtakatifu, ikiwa wote watatembea kwa unyenyekevu na Mungu.(MTC 153.3)

Tunatumaini kwamba wale wanaosimamia kazi huko New England watashirikiana na wasimamizi wa Melrose Sanitarium katika kuchukua hatua kali ili kufanya kazi ambayo inapaswa kufanywa huko Boston. Wafanyakazi mia moja wangeweza kufanya kazi kwa manufaa katika sehemu mbalimbali za jiji, katika njia anuwai za huduma.(Special

Testimonies, Series B 13:12, 13 ( C. H, 554, 555 ). (1908) MTC 154.1)

## Jiji la New York

**Wafanyabiashara wa New York Wapewe Ujumbe.—** Unapaswa kuhisi wajibu uliodhamiriwa wa kufanya kazi kwa Jiji la New York. Wanaume katika nyumba za biashara za New York na miji mingine mikubwa, kama vile wapagani katika nchi za kigeni, lazima wafikiwe na ujumbe huo. Adui angefurahi kuona Ukweli huu mkuu, unaookoa wa wakati huu, ukifungiwa katika sehemu chache tu. Yeye hajazubaa au kujiziuka. Anaingiza ndani ya akili za watu nadharia zake za udanganyifu ili kupofusha macho yao na kuvuruga ufahamu wao, ili Ukweli unaookoa usiletwe kwenye ujuzi wao (wasipate maarifa hayo). Hivi karibuni sheria za Jumapili zitatiliwa mkazo, na watu walio na vyeo vyenye amana watakuwa na uchungu dhidi ya watu wachache wa Mungu wanaozishika amri Zake.(Lt.168,
1909 ( Ms 4:278, 279 ). MTC 154.2)

**Sanitarium na Shule Zinahitajika Karibu na Jiji la New York na Miji Mengine.**Tunahitaji Sanitarium na shule karibu na Jiji la New York, na kwa kadiri tunavyochelewa kuyanunua haya maeneo, ndivyo itakavyokuwa vigumu zaidi kuyapata. (MTC 154.3)

Ingekuwa vyema kupata mahali kama makazi ya wahudumu wetu wa misheni nje ya jiji. Ni muhimu sana kwamba wana mambo ya kuwanufaisha kama vile maji safi, yaliyo mbali na uchafuzi wa aina yoyote. Kwa sababu hii, mara nyingi ni vizuri kuzingatia faida za maeneo yaliyo milimani. ... tunapaswa kutafuta mahali katika jiji ili pawe na kituo cha kuwapa watu tiba sahili... ..(MTC 154.4)

Hebu nyumba kama hizo zinunuliwe kwenye ujirani wa majiji kadhaa, na jitihada za dhati na zenye kuazimiwa

zifanywe na watu wenye uwezo ili kutoa maonyo katika majiji haya, kwa ujumbe ambao unapaswa kwenda ulimwenguni pote. Ni kana kwamba ndio tumegusa tu miji michache (kazi ni mbichi kabisa).(Lt.168, 1909 ( MM, 308 ). MTC 155.1)

**Ni Muhimu Kuanzisha Kazi ya Umishenari wa Tiba. —** Kuanzisha kazi ya umishenari wa tiba katika jiji la New York, itakuwa jambo bora zaidi ambalo wewe [Mchungaji na Bibi Stephen N. Haskell] mnaweza kufanya. Nimeonyeshwa kwamba ikiwa katika kazi hii kungeweza kuwa na wanaume na wanawake wenye uzoefu, na ambao wangetoa uwakilishi sahihi wa kazi ya kweli au halisi ya umishenari wa tiba, kungekuwa na nguvu nyingi katika kuweka maoni sahihi juu ya watu.(Lt.195, 1901{ Ev, 387 ). MTC 155.2)

**Wafanyakazi Wahitajiwa, Migahawa Ianzishwe.—** Nikiwa New York katika majira ya theluji na baridi, mnamo mwaka1901, nilipata nuru kuhusiana na kazi katika jiji hilo kubwa. Usiku baada ya usiku mwenendo ambao ndugu zetu walipaswa kufuata ulipita mbele yangu. Katika jiji kubwa la New York, ujumbe unapaswa kwenda kama taa iwakayo. Mungu atainua watenda kazi kwa ajili ya kazi hii, na malaika Wake watatangulia mbele yao. Ingawa majiji yetu makubwa yanafikia upesi hali inayofanana na hali ya ulimwengu kabla ya Gharika, japokuwa ni kama Sodoma kwa ajili ya uovu, lakini ndani yake mna watu wengi wanyofu, ambao, wanaposikiliza Kweli zenye kushangaza za ujumbe wa marejeo, watasadikishwa na Roho Mtakatifu. New York iko tayari kufanyiwa kazi. Katika mji huo mkubwa ujumbe wa Ukweli utatolewa kwa uwezo wa Mungu. Bwana anawaita watenda kazi. Anawaita wale ambao wamepata uzoefu katika kazi hiyo kuifanya kazi hii na kuiendeleza katika hofu ya Mungu, kazi itakayofanywa huko New York na katika miji mingine mikubwa ya Amerika. Anatoa wito pia kwa pesa kuletwa, ili zitumike kwa kazi hii. (MTC 155.3)

Iliwasilishwa kwangu kwamba hatupaswi kupumzika kwa sababu tuna mgahawa wa chakula cha mboga-mboga huko Brooklyn (vegeterian restaurant), lakini kwamba migahawa mingine inapaswa kuanzishwa katika sehemu zingine za jiji. Watu wanaoishi katika sehemu moja ya jiji kubwa la New York hawajui kinachoendelea katika sehemu nyingine za jiji hilo kubwa. Wanaume na wanawake wanaokula kwenye migahawa iliyoanzishwa katika sehemu tofauti watatambua jinsi ya kuboresha afya zao. Watakapopata ujasiri, atakuwa tayari kuukubali ujumbe wa pekee wa Ukweli wa Mungu. (7T.54, 55 . (1902) MTC 155.4)

**Watu wenye mioyo minyoofu katika Jiji Wanahitaji Kufikiwa.** New York, ni jiji kuu na lenye maovu. Ainani amebeba mzigo wa eneo hili? Ni nani ameona umuhimu wa kujinyima nafsi yake ili kazi katika mji huo iweze kuendelezwa? Hakika ni mji mwovu, lakini Mungu alikuwa na Lutu katika Sodoma, Naye ana watu huko New York, ambao ni kama ayala aioneaye shauku mito ya maji, ndivyo wayaoneavyo shauku maji safi ya Lebanoni. New York iko tayari kufanyiwa kazi. Nilipokuwa huko mara ya mwisho, kabla tu ya kuondoka nchi hii kuelekea kule Australia, Bwana alinionyesha kwamba kazi Yake inapaswa kuanzishwa huko New York. Alinionyesha kile ambacho kingeweza kufanywa pale ikiwa kila mtu angekuja kwa msaada Wake. Nguvu ya Mungu itabeba Ukweli katika mji huu. (MTC 156.1)

Hakuna uhaba wa mali miongoni mwa watu wetu kama ilivyokuwa huko nyuma. Hakika hakuna uhaba wa fedha miongoni mwa watu wetu huko California. Lakini licha ya hili, eneo kubwa la New York halijashughulikiwa, ilihali juma baada ya juma, kutaniko kubwa hukutana hapa katika kanisa [Battle Creek]. Watu wanapaswa kuhisi

kwamba karipio la Mungu liko juu yao kwa sababu hawamfanyii kazi katika sehemu ambazo hazijui Ukweli. Iwapo wangekuwa na roho ya mababa wasafiri wa imani, basi wangeenda kumfanyia Mungu kazi katika mahali palipokuwa na ukiwa duniani.(General Conference Bulletin, Aprili 10,1901, ukurasa wa 183, 184 . MTC 156.2)

**Kopa Pesa kwa Riba Badala ya Kusimamisha Kazi.**— Badala ya kukatisha kazi hapo New York, ningechukua mkopo [yaani, kukopa] pesa na kulipa ribajuu yake, ili kuendeleza kazi.( Barua ya 141, 1901 {Ms 4:319 ). MTC 156.3)

**Maelfu Wanangoja Kusikia Ujumbe.— Kwenye mji wa** New York kuna wengi ambao wameiva kwa ajili ya mavuno. Katika mji huu mkuu kuna maelfu ambao hawajapiga goti kwa Baali. Malaika akasema, Tazama, nawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote." New York ina sehemu ya "watu wote." (kila kabila, lugha na jamaa) Tunatamani kuona mwaka mpya ukifunguliwa, na walimu wakienda kazini katika sehemu zote za New York. Kuna kazi ya kufanywa katika jiji hili—kazi ambayo ilipaswa kufanywa miaka kumi na miwili iliyopita. NayoHaikufanyika; na ni kwa nini? Kwa sababu wanaume na wanawake hawakuwa macho, kuona umuhimu wa wakati tunaoishi. Hawakuwa wamejiandaa katika kufanya kazi iliyohitajika kufanywa. Wale ambao walikuwa hawajaongoka kuhusiana na matengenezo ya afya hawakuweza kufanya kazi katika utaratibu wa Mungu. Kwa hiyo katika mwaka huu wa 1901 kuna upungufu wa wafanyakazi.(Manuscript 117, 1901 ( Ev, 387 ). MTC 157.1)

**Kazi ya Makabila na Lugha Mbalimbali Inapaswa Kufanywa.**— Katika Jiji la New York, Chicago, na katika maeneo mengine makubwa na yenye watu wengi, kuna watu wengi wanaotoka katika nchi mbalimbali za kigeni—

makundi ya watu wa mataifa mbalimbali, na yote haya hayajaonywa bado. Miongoni mwa Waadventista Wasabato kuna usongo mkubwa—na sisemi kwamba kuna mengi sana—ya kufanya kazi katika nchi za kigeni; lakini hakika ingempendeza Mungu ikiwa bidii ifaayo ingeonyeshwa katika kufanya kazi kwenye miji iliyo karibu. Watu Wake Mungu wanahitaji kusonga mbele kwa busara. Wanahitaji kuanzisha kazi hii kwenye miji kwa bidii kubwa. Watu waliowekwa wakfu na wenye talanta aina mbali mbali ya watu yanapaswa kutumwa katika miji hii na kisha kazi ianze kufanywa. Makundi mengi ya wafanyakazi yanapaswa kuungana katika kufanya jitihada hizi za kuwaonya watu.— (R&H, Oktoba 29, 1914 ( Christian Service, 199 ). MTC 157.2)

**Fanyeni Kazi Jiji la New York Sasa Hivi, Kwa Kutumia Mbinu Mbalimbali.—** Wakati mzuri zaidi wa kufanya kazi Jiji la New York ni sasa, sasa *hivi;* na hebu njia inyooshwe iwezekanavyo ili kazi ifanywe, na wakati huo huo wote wafurahi na kila maslahi yanayoundwa katika maeneo yanayopakana.... (MTC 157.3)

Kazi katika New York Zaidi inapaswa kufanywa kwa njia ambayo itawakilisha ipasavyo utakatifu na utukufu wa Ukweli wa Mungu. Migahawa ya mboga-mboga, vyumba vya tiba, na shule za upishi zitaanzishwa. Watu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuandaa chakula chenye lishe bora, kisichokobolewa au kusindikwa. Wanapaswa kuonyeshwa hitaji la kuacha chai, kahawa, na aina zote za nyama au minofu.(MTC 158.1)

Jiji kubwa la New York lazima lisimame katika uhusiano tofauti na General Konference kuliko maeneo yaliyo jirani na maslahi ambayo ni tofauti, na itabidi lizingatiwe kwa nuru tofauti kuhusiana na kazi ya umishenari. Jiji kubwa

la New York ni kama ulimwengu wenyewe, na linapaswa kuwa na usimamizi tofauti kwa njia fulani na ule wa maeneo yanayouzunguka (kuna watu kutoka kwenye kila nchi).(MTC 158.2)

Mungu ameteua mawakala Wake kwa ajili ya kupanua mzunguko wa ushawishi wetu New York, na kwa ajili ya kuongeza idadi ya wafanyakazi ambao watakuwa wamishenari kwa kweli—watendakazi kwa ajili ya kuokoa roho za wanadamu wenzao. Wale ambao hawataweka mipaka na kuuminya mduara/duru ya kazi zao. Kanisa la Kikristo litakuwa kwenye hatua za mbele mapema, hasa katika kutafakari mipango; daima litakuwa linawaelimisha wafanyakazi kwa ajili ya ushindi mkubwa zaidi kwa ajili ya Kristo. Daima linapaswa kuendelea kusonga mbele, ili Ukweli uenee katika sehemu zote za dunia. …(MTC 158.3)

Bwana angetaka New York pamoja na maeneo yake yote mahalia na miji iliyoizunguka ifanyiwe kazi miaka mingi iliyopita, na sasa kwa kuwa fursa hiyo imefunuliwa kwa uwazi zaidi, katika vitongoji/maeneo yote, katika kila kanisa, mioyo inapaswa kuvutwa na kwenda kuunganishwa na maendeleo ya ujumbe wa injili. Katika sehemu zote zilizopuuzwa za shamba la mizabibu, mioyo inapaswa kusisimka kwa uzoefu wa yale yaliyo ya dhati, yaani yasiyo bandia, yaliyo hai; na sasa kwa kuwa kuna kazi kubwa ambayo imeanza, hakuna mtu anayepaswa kukunja mikono yake, lakini wote wanapaswa kuzingatia kwa shauku kila harakati ya kanisa. (MTC 158.4)

Katika sehemu mbalimbali za Jiji la New York kubwa (metropolitan) makanisa yanapaswa kuhisi majukumu yao matakatifu, waliyopewa na Mungu. Neno la Bwana linataka kazi ya uaminifu ifanyike katika uwanja huu mpana wa umishenari, na kila chembe ya ukosoaji na kutafuta makosa ya wengine, na kutenganisha ndugu kukome.

Ubaguzi, chui, mawazo yao na kusema maovu, vyote hivi vinapaswa kuondolewa. Mungu hatavumilia tena roho ambayo imekuwa ikitawala mambo katika makanisa yetu ya New York. Mashamba hapa yako tayari kwa mavuno. Haijalishi upande tunaouangalia, ndugu zetu lazima wafanye kazi yao iliyowekwa hapo, ambayo inaenea kwa mzunguko mkubwa, usio na kipimo. Wale ambao wanapenda na kukuza ubaguzi hawapaswi kusikilizwa. Kazi inapaswa kwenda mbele chini ya uongozi wa Mungu, na wale wanaotaka kuendeleza roho ya mafarakano wanapaswa kujiondoa wenyewe nje ya njia, na kuacha kazi ya Mungu isonge mbele.— (ST (038), 6-9 . (1903) MTC 158.5)

**Majiji ya Karibu, Trenton na Brooklyn, Yatafanyiwa Kazi.—** Moyo wangu umeguswa sana kwamba Trenton [New Jersey] iwe kitovu cha mvuto wa injili,pamoja na Brooklyn [New York], na bado pia kuna maeneo mengine nje ya jiji la New York. Hakika tunaona maeneno katika kila upande ndani na nje ya New York yanayopaswa kufanyiwa kazi. Lazima mumiliki ukumbi hapo ili muweze kuwaita watu pamoja katika Jiji la New York, na kutoka maeneo ya jirani nje ya Jiji la New York. ... (MTC 159.1)

Mungu sasa anataka miji yetu ifanyiwe kazi sasa kwa njia ya majaliwa Yake, na mvuto uliotakaswa kuletwa kwenye akili ya mwanadamu. Kugeuzwa kwa fikra na nia ya mwanadamu mmoja kunamaanisha, ikiwa mapenzi ya Mungu yatafanyika , mabadiliko ya akili nyingi za wanadamu yatakuwepo. "Hakuna hata mmoja wetu anayeishi kwa ajili yake mwenyewe." Hakuna hata mmoja wetu anayepanga kujipatia utukufu. Bwana alimtoa Kristo kwa ulimwengu wetu, na pamoja na Kristo hakuzuia chochote ambacho kingeweza kumsaidia mwanadamu katika ubinadamu wake. Wakati kanisa lililopangwa halijazuia chochote kuhusu talanta na ushawishi [wake]

uliokabidhiwa—Bwana alipomtoa Kristo, na kisha kumwita mwanadamu kuweka nguvu na ushawishi huo chini ya nguvu na kipawa cha Roho Mtakatifu ili kuweka taji ya kazi yake kwa mafanikio; kufanya kazi yao [ya pamoja] kuwa ishara ya mafanikio—je, mwanadamu ashindwe kweli kwa upande wake? ... (MTC 159.2)

Je, kanisa linapendekeza kufanya nini kama nyenzo ya Kikristo kwa ajili ya uongofu wa ulimwengu? Bwana anatoa wito wa makumbusho Yake kusimikwa na kuimarishwa katika kila mji. Lazima kuwe na kazi katika kila jiji ambayo lazima itendwe ili kusambaza mvuto wa ile Kweli, ambayo ina nguvu ya kutakasa wale watakaosikia na kuitikia.— (Lt.183, 1901 . MTC 159.3)

**MIJI YA KATIKATI YA ATLANTIKI Philadelphia, Pennsylvania Kazi ya uinjilisti itafanyika vyema Mahali Masuala ya Kidini Huwatibua Raia.—** Filadelfia na maeneo mengine muhimu yapasa kufanyiwa kazi. Wainjilisti wanapaswa kutafuta njia ya kuingia katika maeneo yote ambayo akili za watu zimeingia wasisiwasi kuhusiana na suala la sheria ya Jumapili na mafundisho ya dini katika shule za umma. Kutoboresha fursa hizi za majaliwa ya Mungu katika kuwasilisha Ukweli unaolemea moyo wangu na kunifanya niwe macho usiku baada ya usiku, ni upuuziaji kwa upande Waadventista Wasabato. ( R&H, Aprili 20, 1905 ( Ev, 394, 395 ). MTC 160.1).

**Kufanya Kazi Chini ya Mwongozo wa Roho Mtakatifu Huleta Matokeo.—** Tunapaswa kufurahishwa kuona kazi maalum ikifanywa Philadelphia na Boston. Nafsi nyingi zitaongoka ikiwa wanaume na wanawake watafanya kazi binafsi inayohitaji kufanywa. Kupitia wafanyakazi wanaofanya kazi chini ya mvuto wa Roho Mtakatifu, nafsi nyingi zitaletwa kwenye ujuzi wa Ukweli.— (Manuscript 162, 1905 ( Manuscript Releases 10:228 ). MTC 160.2)

## Washington, DC

**Wachache Katika Mji Mkuu wa Marekani Wameonywa.—** Nimekuwa nikiandika mengi kuhusiana na hitaji la kufanya jitihada zilizodhamiriwa zaidi huko Washington, DC. Nimepewa nuru kwamba jambo fulani linapaswa kufanywa katika jiji hili mara moja. Ni ajabu jinsi gani kwamba katika moyo wa taifa (makao makuu), ni machache sana ambayo yamefanywa ili kuwakilisha uadilifu wa watu wa Mungu. Ukweli mkuu uliowahi kutolewa kwa wale walio na mwili wa kufa (wanadamu), umetolewa kwetu sisi. Washington D.C, mji mkuu wa Marekani, ni mahali pale ambapo Ukweli huu unapaswa kuangazia watu. Lakini ni nini kimefanywa huko ili kutangaza Ukweli? Tunaweza kumpa Mungu kisingizio gani kwa uwakili wetu usio na uaminifu?—(Lt. 132, 1903 . MTC 160.3)

**Wafanyakazi Hawapaswi Kuhamishwa Wakati wa Mikutano ya Kiinjilisti.—** Juhudi kubwa ya uinjilisti lazima ifanyike katika mji mkuu wa taifa.... (MTC 161.1)

Ninafurahi kwamba wewe [Mzee WW Prescott] umechukua kazi hii ya uinjilisti huko Washington, na kwamba shauku kubwa tayari imeamshwa. Ripoti ambazo zimezotolewa kuhusu kazi huko zinashabihiana kwa karibu, kwa kadri iwezekanavyo na wasilisho nililopewa kwa kile ambacho kingekuwa. Nina uhakika na jambo hili kwani suala hilo limewasilishwa kwangu, na kazi hii haipaswi kudhoofishwa na watendakazi muhimu kuitwa na kwenda mahali pengine.
... (MTC 161.2)

Kazi ya uinjilisti lazima ifanywe huko Washington, na haipaswi kuvunjwa kwa simu kutoka sehemu zingine. Mungu angefanya kazi Yake katika barabara kuu isogezwe mbele kwa mistari iliyonyooka. (MTC 161.3)

Upo mahali ambapo Bwana anataka uwe. Mzee [AG] Daniells na wewe mwenyewe hatupaswi kubebeshwa mizigo mingi sana. Washington imepuuzwa kwa muda wa kutosha. Kazi iliyoamuliwa lazima sasa ifanyike hapo. Bwana atakupa nguvu na neema. Wafanyikazi wanapaswa kutoruhusu kabisa kukengeushwa kutoka kwenye kazi na mambo mengi ambayo yatalazimika kuminya umakini wao. Hii ndiyo sababu ambayo nimekuwa na wasiwasi kwamba kila talanta ya wafanyakazi huko Washington itatumiwa kwa njia ambayo itaendeleza kazi Yake vyema zaidi.— (Letter 53, 1904 ( Ev, 395 ). MTC 161.4)

**Kazi ya Binafsi Inahitajika Mijini.—** Ninatoa wito kwa waumini wa mji wa Washington kuja kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana dhidi ya nguvu kuu za giza (Waamuzi 5:23). Kazi binafsi itahitajika pia, katika jiji hili na vitongoji vyake. Safisha barabara kuu ya Mfalme. Inua kiwango cha juu na bado juu zaidi. Kuna kazi ya uinjilisti inayopaswa kufanywa huko Washington na Baltimore na katika miji mingine mingi mikubwa ya Kusini na Mashariki. Hebu kazi ya kufundisha, tiba na uponyaji viende pamoja. Hebu wahudumu na wamisionari wa tiba wavae silaha zote za Mungu na wasonge mbele kutangaza ujumbe wa injili. Ujumbe ulioamuliwa utatangazwa huko Washington D.C. Baragumu inapaswa kutolewa kwa sauti fulani.— (Lt. 304, 1908 ( Ev, 397 ). MTC 161.5)

## Takoma Park, Washington, DC

**Michango Kusaidia Wafanyakazi Karibu na Jiji la Washington, DC—** Tunawasihi wale wanaoishi katika mji wa Takoma Park (Karibu na mji wa Washington D.C), wawe watenda kazi pamoja na Mungu katika kupanda kiwango cha Ukweli katika maeneo ambayo hayajahubiriwa. Acheni sehemu kubwa ya michango ambayo imetolewa baada ya

wito, itumike kukimu/kutegemeza maisha ya watendakazi katika miji yetu iliyo karibu na Washington. Acheni kazi ya uadilifu ya nyumba kwa nyumba ifanywe. Nafsi zinaangamia nje ya safina ya usalama. Hebu kiwango cha Ukweli kiinuliwe na washiriki wa kanisa katika
ujirani wao. Hebu wahudumu wapige hema zao, na kuhubiri Ukweli kwa watu kwa nguvu, na kisha kuhamia eneo jingine na kuhubiri Ukweli huko.— (Lt.94a, 1909 ( Ev, 397 ). MTC 162.1)

**Eneo Karibu na Washington, DC, Litanyiwe Kazi.—** Jumapili iliyopita tulisafiri kwa gari kwa muda mrefu katika wilaya inayopakana na ardhi yetu [Takoma Park]. Dada Daniells alikuwa nasi, na alituonyesha makazi ya watu karibu na eneo letu. Tulifurahishwa sana na mwonekano wa makazi haya. Nyumba hizo zilikuwa safi na zinazoletea watu faraja, na zimezungukwa ardhi yao imezungukwa na mambo mazuri-(maua, majani yaliyokatwa na usafi). (MTC 162.2)

Maeneo ambayo tuliyaona yalinikumbusha yale tuliyoona tulipotembelea Oakland na San Francisco kwa mara ya kwanza. Wakati huo Oakland haikuwa kubwa kama ilivyo sasa. Iliitwa chumba cha kulala cha San Francisco, kwa sababu wafanyabiashara wengi wanaofanya kazi huko San Francisco walikuwa na nyumba huko Oakland*. Mji wa Takoma Park (ilipo misheni) inaweza kuitwa kwa usahihi moja ya vyumba vya kulala vya Washington D.C. Wafanyabiashara wengi sana wanaishi hapa, wakienda kazini kwao jijini kila asubuhi na kurudi usiku kwenye sehemu tulivu na ya mapumziko ya nje ya mji. ... (*Wakati huu Takoma Park yalikuwa makao makuu ya General Conference, Hospitali na Chuo cha Columbia Union College, sasa kinaitwa Washington Adventist University. General Conference ilihamia mji wa Silverspring karibu na hapo ila hizo taasisi zingine zilibakia hapo) (MTC 162.3)

Ninashukuru sana kwamba kazi yetu itaanzishwa mahali hapa. Kristo angekuwa hapa duniani, angetuambia, “Inueni macho yenu, mkatazame mashamba; kwa maana ni meupe tayari kuvunwa.” Tuna kazi ya kufanya katika kuziongoza nafsi za thamani mbele hatua kwa hatua. ... (MTC 162.4)

Matumaini yangu kwa mahali hapa ni makubwa, kama yalivyokuwa huko nyuma nilipoingia katika maeneo mapya. Huko nje ya mji wa Washington D.C, maili na maili kuzunguka zinapaswa kufanyiwa kazi. Hatutazungumza juu ya kile ambacho kingefanyika ikiwa pesa zilizotumiwa katika sehemu chache zingetumika katika kuanzisha makumbusho Mungu pale ambapo makumbusho kama hayo yanahitajika sana; tutageukia mambo yanayoendelea sasa. Tunataka kuwasilisha Ukweli kwa upendo na imani na matumaini na ujasiri. ... (MTC 163.1)

Tunaamini kabisa kwamba Bwana ametangulia mbele yetu katika ununuzi wa ardhi hii, na tutafanya yote tuwezayo kutekeleza mapenzi Yake katika kusimamisha kazi Yake mahali hapa. Tutahitaji vijana wenye talanta bora zaidi katika kazi yetu huko Washington. ... Ujumbe lazima utangazwe huko Washington, na lazima utoke mahali hapo hadi miji mingine ya Kusini. ...(MTC 163.2)

Sabato iliyopita nilizungumza katika Ukumbi wa Takoma, ambao ulikuwa umejaa sana. Nilizungumza kutoka sura ya kumi na tano ya Yohana, na nafsi yangu iliburudishwa nilipokaa juu ya somo hili muhimu. Idadi kubwa ya wananchi walikuwepo, na mwenye ukumbi alikuwapo pia. (MTC 163.3)

Siku ya Jumapili nilizungumza katika Kanisa la M Street Memorial Church kwa kundi la wafanyakazi ambao wamekusanyika Washington kufanya mikutano ya hema na kufanya kazi ya Biblia. Moyo wangu umejawa na matamanio yenye shauku kubwa kwamba wote wanaoungana na kazi hii muhimu wawe na uzoefu wa kila siku katika mambo ya

Mungu, ili wapate kujaza nafasi waliyopewa kwa njia ambayo watapata kibali cha Bwana. Wanapaswa kuwa wakamilifu katika yote wanayofanya. Juu ya kipengele hiki hatuwezi kuwa wa haraka sana. ... (MTC 163.4)

Matamanio makubwa yanapaswa kuonyeshwa na watu wetu nchini Amerika katika upanuzi wa kazi ya Bwana. Wapaswa kuhisi huzuni nyingi na kujidhili wanapofikiri kwamba majiji ambayo yamewekwa mbele ya macho yao kwa miaka ishirini na mitano iliyopita bado hayajasikia ujumbe wa Ukweli wa sasa. Kuna wapagani, kama ilivyo, katika mipaka yetu, katika miji yetu mikubwa. Lakini ni nani aliye na mzigo kwa hawa watu ambao hawajapewa onyo bado? Ni nani aliye tayari kuwekeza mali [yake] katika kazi ya kuwaelimisha watu hawa?— (Hati 38,1904 . MTC 163.5)

## MI JI YA MAREKANI

### Chicago Illinois

**Chicago inapaswa Kufanyiwa Kazi Kuanzia Maeneo ya Vijijini.—** Kwa sasa, wengine watalazimika kufanya kazi katika Chicago; lakini hawa wanapaswa kutayarisha vituo vya kazi kwenye maeneo/mitaa iliyo nje ya mji, ili wafanye kazi ya majiji kutoka nje ya mji (wanaishi nje ya majiji na wanafanya kazi ndani ya majiji). Bwana angetaka watu Wake wayatazame maeneo walipo na kupata maeneo manyenyekevu, yasiyo na maonyesho, ya gharama nafuu kuwa kama vitovu vya kazi yao. Na mara kwa mara maeneo makubwa yatakuja kwenye umakini wao, ambayo wataweza kuyapata kwa bei ya chini, jambo ambalo linashangaza.— (Manuscript 33, 1906 ( MM, 305, 306 ). MTC 164.1)

**Kazi ya Lugha, jamaa na kabila Mbalimbali Inapaswa Kufanywa Katika Majiji Yote Makubwa.—** Tulitoka nje ili kuona Misheni mpya ya Uswidi (Sweden) iliyoanzishwa kwenye Oak Street [huko Chicago]. Huko tulionyeshwa jengo ambalo ndugu zetu wa Uswidi, chini ya uongozi wa

Mzee S. Mortenson, wamelinunua hivi karibuni kwa ajili ya makao makuu ya kazi yao huko Chicago. Jengo linatoa muonekano wa kupendeza. Katika sehemu ya nyumba iliyo chini ya ardhi (basement) wana mgahawa wa mboga-mboga (basement) ulio na vifaa vizuri vilivyojitosheleza kabisa. Kwenye orofa ya kwanza kuna ukumbi wa kupendeza wa mikutano, ambao kutaniko la watu mia moja hamsini hivi wanaweza kuketi kwa starehe, na orofa mbili za juu hukodishwa kwa wakazi. Hakika nilifurahi kuona uthibitisho huu wa maendeleo katika kazi ya Uswidi huko Chicago. (MTC 164.2)

Kuna kazi kubwa ya kufanywa kwa ajili ya watu wa mataifa yote katika miji mikubwa ya Amerika, na maeneo kama haya ya mikutano yanaweza kuwa msaada mkubwa katika suala la kupata usikivu wa watu, na katika mafunzo ya watendakazi. Katika kila jiji kubwa la Amerika kuna watu wa mataifa tofauti, ambao lazima wasikie ujumbe wa wakati huu. Ninatamani kuona ushahidi kwamba mistari ya kazi ambayo Bwana ameiweka wazi kwetu, inatendwa na watu bila kujali. Kazi inayofanana na ile inayofanywa huko Chicago kwa watu wa Uswidi inapaswa kufanywa katika maeneo mengi.— (R&H, Februari 9, 1905 ( Ev, 572 ). MTC 164.3)

**Tahadhari Kuhusu Kununua Ardhi au Mali Katika Majiji.—** Matukio ambayo yangetendeka hivi karibuni huko Chicago na majiji mengine makubwa yalipita mbele yangu. Kadri uovu ulipoongezeka na nguvu ya kulinda ya Mungu ilipoondolewa kulikuwa na pepo za uharibifu na tufani. Majengo yaliharibiwa kwa moto na kutikiswa na matetemeko ya ardhi. ...(MTC 164.4)

Muda fulani baada ya hapa nilionyeshwa maono ya majengo huko Chicago na ubaradhifu wa mali za watu uliofanywa ili kuyasimamisha haya, na uharibifu wake baada ya hapo, hili lilikuwa somo la mfano kwa watu wetu,

likiwaonya wasiwekeze kiasi kikubwa mali zao katika majengo na ardhi katika mji wa Chicago, au jiji lingine lolote, isipokuwa pale ambapo majaliwa ya Mungu yanafungua njia kwa uhakika na kuonyesha waziwazi wajibu wa kujenga au kununua ardhi pale inapobidi ili kutoa matamko ya maonyo. Tahadhari kama hiyo ilitolewa kuhusu ujenzi huko Los Angeles. Mara kwa mara nimeagizwa kwamba hatupaswi kuweka mali katika ujenzi wa majengo ya gharama kubwa katika miji.- (Manuscript 33, 1906 ( LDE, 113, 114 ). MTC 165.1)

**Injili Itawasilishwa kwa Uwazi Katika Maeneo Nje ya Chicago.—** Nimepewa uwakilishi wa kuhubiriwa kwa Neno la Ukweli kwa uwazi na nguvu katika maeneo mengi ambako Neno hili halijapata kusikiwa. Bwana angetaka watu waonywe; kwa maana kazi kubwa itafanywa kwa muda mfupi. Nimesikia Neno la Mungu likitangazwa katika maeneo mengi nje ya jiji la Chicago. Kulikuwa na sauti nyingi zinazotangaza Ukweli kwa nguvu kubwa. Yale waliyoyatangaza hayakuwa nadharia za kufikirika au kufurahisha moyo, bali ujumbe wa onyo. Ingawa Ukweli thabiti wa Biblia ulitoka katika midomo ya wanadamu ambao hawakuwa na nadharia za uwongo na zenye kupendeza na kufikirika au sayansi yenye kupotosha, kulikuwa na wengine waliojitahidi kwa nguvu zao zote kuleta nadharia za uwongo kuhusu Mungu na Kristo. Na miujiza ilifanyika, ili kudanganya, ikiwa inawezekana, hata wale walio wateule.— (Manuscript 33, 1906 ( MM, 305). MTC 165.2)

**Licha ya Matatizo, Kazi Inapaswa Kufanywa huko Denver.—** Jambo hilo linapowekwa wazi mbele yangu, ninaona kwamba kuna hitaji kubwa la kazi inayopaswa kufanywa huko Denver. Katika siku za nyuma mambo mengi yamefanya kazi dhidi ya ustawi wa kazi huko, na

ushawishi huu usiofaa bado haujaondolewa kabisa.—(Lt.84, 1901 ( Ev, 402 ). MTC 165.3)

**MIJINI YA KUSINI Nashville, Tennessee**

**Ujumbe Uonyeshwe kwa Usahili.**— Kwa kazi ya Nashville na karibu na mji huo, tunapaswa kufanya yote tuwezayo ili kuiweka kwenye msingi thabiti. Kazi inapaswa kufanywa kwa usahili, na kwa njia ambayo itapendekeza Ukweli. Kuna maeneo mengi Kusini yaliyo wazi kwa kazi yetu; lakini kwa njia zozote zile, hebu tuanze katika miji muhimu, na kubeba ujumbe sasa. “Kwa maana Bwana wa majeshi asema hivi; Bado mara moja, bado kitambo kidogo, Nami nitazitikisa mbingu, na nchi, na bahari, na nchi kavu; Nami nitatikisa mataifa yote, na matamanio ya mataifa yote yatakuja, Nami nitaijaza nyumba hii utukufu, asema Bwana wa majeshi.”— (Special Testimonies, Series B 11:4 . (1908) MTC 166.1)

**Wafanyakazi Wawe na Maslahi Bora Zaidi ya Kazi Moyoni.**— New Orleans itafanyiwa kazi. Kwa wakati ufaao wa mwaka juhudi za umma zinapaswa kufanywa huko. Mikutano ya kambi inapaswa kufanywa katika sehemu nyingi, na kazi ya uinjilisti inapaswa kufanywa baada ya mkutano wa kambi kwisha. Hivyo miganda ya mavuno itakusanywa. (MTC 166.2)

Sasa kwa kuwa kazi katika New Orleans inapaswa kushugulikiwa kikamilifu zaidi, nimeagizwa kusema, Hebu wanaume na wanawake walio na ujuzi wa Ukweli, na kuelewa njia ya Bwana, waingie katika jiji hili kufanya kazi kwa hekima na hofu ya Bwana. Watenda kazi waliochaguliwa kwa ajili ya kazi huko New Orleans wanapaswa kuwa wale walio na kusudi lililo jema moyoni mwao, watu ambao watauweka utukufu wa Mungu mbele yao daima, na ambao watafanya nguvu za Mungu wa Israeli

kuwa ulinzi wao mbele na nyuma yao. Bwana hakika atasikia na kujibu maombi ya watendakazi Wake ikiwa watamtafuta kwa ajili ya ushauri na maelekezo.— (Manuscript 49, 1907 ( Ev, 399 ). MTC 166.3)

**Nendeni Mkafanye Kazi Mijini Badala ya Kuwakosoa Wale ambao tayari Wanafanya Kazi Huko.—** Bwana Mungu amekuwa akifanya kazi. Ndugu zanguni, badala ya kukosoa yale yaliyofanywa tayari, hebu mtunze hotuba zenu kwaajili ya miji mikubwa ambayo bado haijafanyiwa kazi, kama vile New Orleans, na Memphis. Nendeni kwenye maeneo haya na mfanye kazi kwa ajili ya watu, lakini msiseme neno la kukemea kuhusu wale ambao wamejaribu sana kufanya kila kitu katika uwezo wao kwa ajili ya kuiendeleza kazi. Nyakati zingine wafanyakazi hao walikaribia kuvunjika moyo kabisa, lakini sisi tuliendelea kuwaombea. Popote nilipokuwa, niliwaomba watu wa Mungu kufanya maombezi kwa niaba yao.—(R&H, May 25, 1905 ( Ev, 401 ). MTC 167.1)

**MIJI ya MAGHARIBI mwa MAREKANI California Zingatia Nishati kwenye Ujenzi wa Kusudi la Mungu.—**

Katika onyo langu la mwisho nilionyeshwa kwamba tunapaswa kuwa na sehemu ya kutenda huko California katika kupanua na kuthibitisha kazi ambayo tayari ilikuwa imeanza. Nilionyeshwa kwamba kazi ya umishenari lazima ifanyike California, Australia, Oregon, na maeneo mengine kwa upana zaidi kuliko watu wetu walivyowazia, au kuwahi kutafakari na kupanga. Nilionyeshwa kwamba kwa wakati huu hatusogei haraka kama vile majaliwa ya Mungu yanavyotuongoza. Nilionyeshwa kwamba Ukweli wa leo unaweza kuwa na nguvu katika California ikiwa waamini katika ujumbe hawangetoa nafasi kwa adui katika kutoamini na ubinafsi, bali wangeelekeza juhudi zao kwenye

kitu kimoja—kujenga sababu ya Ukweli wa sasa.—(life sketch Ellen G. White, 209, 210 . (1874, 1915) MTC 167.2)

## Wachungaji/Wahudumu Wanahitaji Kutambua Wito wa Mungu wa

**Kueneza Injili katika Miji ya California.—** Je! hatutafanya yote tuwezayo Ili kuanzisha kazi katika miji mikuu ya San Francisco na Oakland, na katika miji mingine yote ya California? Maelfu kwa maelfu wanaoishi katika miji iliyo karibu nasi wanahitaji msaada kwa njia mbalimbali. Hebu wahudumu wa injili watambue kwamba Bwana Yesu Kristo aliwaambia wanafunzi Wake, "Ninyi ni nuru ya ulimwengu."— (Manuscript 79, 1900 ( Ev, 403 ). MTC 167.3)

**Redlands na Miji Mingine ya Kusini mwa California Yatakayofanyiwa Kazi.—** Miaka mingi iliyopita maeneo mengi kusini mwa California yaliwaslishwa kwangu kama maeneo muhimu sana, yanayohitaji kazi ya dhati na bidii. Nikiwa Redlands, niliutambua mji huu kama mojawapo ya maeneo haya.Nilipewa Nuru kwamba hali ya kutofanyiwa kazi ya miji ya kusini mwa California ni aibu kwa wale wanaojua Ukweli. Hivi majuzi Mchungaji [William Ward] Simpson alifanya mikutano ya hema huko Redlands, kama matokeo, washiriki wengi wapya waliongezwa kwenye kanisa. Kwa hili tunamsifu Bwana. Lakini bado kuna mengi ya kufanywa huko Redlands. Tunahitaji sasa kufanya jitihada za dhati na bidii katika majiji ya kusini mwa California.—( R&H, Aprili 6, 1905 . MTC 168.1)

**Migahawa na Vyumba vya Tiba Vitaanzishwa katika Miji ya Mapumziko ya Watalii.—** Nilipokuwa Los Angeles niliagizwa kwamba si tu katika sehemu mbalimbali za jiji hilo, bali pia San Diego na katika maeneo mengine ya mapumziko ya watalii, yaliyo Kusini mwa California, migahawa ya afya na vyumba vya tiba vinapaswa kuwepo.

Juhudi zetu katika mistari hii zinapaswa kujumuisha hoteli kuu za pwani. Kama vile sauti ya Yohana Mbatizaji ilivyosikika nyikani, “Itengenezeni njia ya Bwana,” vivyo hivyo sauti ya wajumbe wa Bwana inapaswa kusikika katika vivutio vikubwa vya kitalii na kando ya bahari.—(7T.55; 56
. (1902) MTC 168.2)

**Sehemu Zote za San Francisco na Oakland Zinahitaji Kuhubiriwa.—** Kuna kazi ya kufanywa huko California, kazi ambayo imepuuzwa kwa njia ya ajabu. Kazi hii isicheleweshwe tena. Milango inapofunguliwa kwa ajili ya uwasilishaji wa Ukweli, hebu na tuwe tayari kuingia. Kazi fulani imefanywa katika jiji kubwa la San Francisco, lakini tunapojifunza kuhusu shamba hilo tunaona wazi kwamba ni mwanzo tu ndio ambao umefanywa. Juhudi zilizopangwa vyema zinapaswa kuwekwa katika sehemu mbalimbali za jiji hili na pia katika Oakland haraka mno. Uovu wa San Francisco watu hawajauelewa vizuri. Kazi yetu katika jiji hili lazima ipanuke na iwe ya kina. Mungu huona ndani yake nafsi nyingi zitakazookolewa.— (7T.110 . (1902) MTC 168.3)

**Kazi ya Mungu katika San Francisco Ili Kupanuka na Kuzama zaidi.—** Ingekuwa vigumu kueleza hisia zangu niliposimama mbele ya Kanisa la San Francisco, Sabato, Novemba 10 [1900], na kutazama kutaniko kubwa. Akili yangu ilirudi nyuma kwenye wakati, miaka ishirini na minne iliyopita, wakati ambapo mimi na mume wangu tulipokuwa tukipanga mambo kwaajili ya ujenzi wa nyumba ya ibada huko San Francisco. Wengine, walipouona mpango huo, walisema, “Ni mpango mkubwa sana. Nyumba hiyo haitajazwa kamwe." Wakati huo huo tulikuwa tukisimamisha jengo la kwanza la nyumba ya uchapaji ya Pacific Press na jumba la mikutano huko Oakland. Mahangaiko yalikuwa makubwa kama nini, na sala

zilizotolewa kwa Mungu kwa dhati na bidii kwa kiasi kikubwa, ili kwamba Yeye afungue njia kwa ajili ya kuendeleza shuguli na biashara hizo! (MTC 169.1)

Wakati huo niliota kwamba ninaona mizinga miwili ya nyuki, mmoja huko San Francisco na mwingine huko Oakland. Katika mzinga huko Oakland nyuki walikuwa wakifanya kazi kwa juhudi kubwa. Kisha nikatazama mzinga huko San Francisco, na nikaona kidogo sana kilichokuwa kinafanywa. Mzinga huko Oakland ulionekana kuwa na matumaini zaidi. Baada ya muda usikivu wangu uliitwa tena kwenye mzinga wa huko San Francisco, na nikaona kwamba mabadiliko kamili yalikuwa yamefanyika. Shughuli kubwa ilionekana kati ya nyuki. Walitenda kazi ya dhati na bidii. (MTC 169.2)

Niliposimulia ndoto hii, ilifasiriwa kumaanisha kwamba huko San Francisco kulikuwa na kazi kubwa ya kufanywa. ... (MTC 169.3)

Tuliomba sana kuhusiana na mahitaji ya injili na maana ya ndoto hii, na tukaazimia kujitosa kwa mujibu wa nuru iliyotolewa. Mume wangu, nami tuliamua kuuza mali yetu huko Battle Creek, ili tuweze kutumia mapato katika kazi hii. ... Hili lilifanyika, na tukasaidia kujenga makanisa huko Oakland na San Francisco.Na Bwana alitufunulia kwamba ingawa mwanzoni kazi huko San Francisco ingesonga polepole, ila maendeleo yake yangekuwa thabiti, na San Francisco ingekuwa kituo kikuu. Bwana angevuvia moyo wanadamu kwa Roho Wake Mtakatifu, ili kuendeleza kazi kwa imani na ujasiri na ustahimilivu. ... (MTC 169.4)

Tulipoingia katika Sabato kwenye Kanisa la San Francisco asubuhi tulilikuta limeshonana watu kwa uwezo wake wote. Niliposimama mbele ya watu, nilifikiri juu ya ndoto na mafundisho ambayo nilikuwa nimepewa miaka mingi iliyopita, na nilitiwa moyo sana. Nikiwatazama watu waliokusanyika, nilihisi hakika naweza kusema kwamba

Bwana ametimiza Neno Lake. Baada ya kumaliza kuzungumza, wote waliotaka kujitoa kwa Bwana katika kujiweka wakfu kwa dhati walialikwa kujitokeza. Kwa mwaliko huo watu mia mbili waliitikia. ... (MTC 170.1)

Tunatumai kwa dhati kwamba hatua zilizochukuliwa katika siku zijazo katika kazi huko San Francisco bado zitakuwa hatua za maendeleo. Kazi iliyofanyika huko ni mwanzo tu wa safari. Mji wa San Francisco ni ulimwengu kama ilivyo yenyewe, na kazi ya Bwana huko inapaswa kutanuka na kwenda kwa kina zaidi....(MTC 170.2)

Kuna kazi kubwa ya kufanywa huko San Francisco na Oakland. Bwana atatumia watu wanyenyekevu katika miji hii mikubwa. ... (MTC 170.3)

Kuna wanaume na wanawake ambao Bwana, kupitia hali zao za pekee, atawaleta mbele katika kazi Yake.— (Australasian Union Conference Record, Machi 1, 1901 . MTC 170.4)

## KANADA

**Toronto Itafanyiwa Kazi.—** Moyo wangu unaumia ninapoona kazi inayohitaji kufanywa na hakuna mtu wa kuifanya. Tunapaswa kufunga na kuomba ili Bwana ainue watenda kazi waende kwenye shamba la mavuno. Tufanye nini kwa watendakazi? Mchungaji [Daniel T.] Bourdeau anasema Toronto ni uwanja bora wa[ambamo] kufanya kazi. Kuna baadhi ya watu bora ambazo roho zao zimekatwa na Ukweli. Hebu mtu fulani atumwe kwenye eneo hili.— (letter 26, 1883 . MTC 170.5)

## Miji Nje ya Amerika Kaskazini

**Ujumbe Unapaswa Kutafsiriwa Ili Mataifa Yote Yapate Ukweli.—** Kazi kubwa imetunukiwa kwa wale wanawasilisha Ukweli katika Ulaya. ... Kuna Ufaransa na Ujerumani, pamoja na miji yake mikubwa na idadi ya watu wengi. Kuna Italia, Uhispania, na Ureno, baada ya karne

nyingi za giza, … sasa imefunguliwa kwa Neno la Mungu—kufunguliwa kupokea ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu. Kuna Uholanzi, Austria, Romania, Uturuki, Ugiriki, na Urusi, makao ya mamilioni kwa mamilioni, ambao nafsi zao ni zenye thamani machoni pa Mungu kama zetu, watu wasiojua lolote kuhusu Kweli za pekee za wakati huu. … (MTC 171.1)

Kazi nzuri tayari imefanywa katika nchi hizi. Kuna wale ambao wamepokea

Kweli, na kutawanyika kama wabeba nuru karibu kila nchi. …

(MTC 171.2) Lakini ni machache sana ambayo yamefanywa ukilinganisha na kazi kubwa

iliyo mbele yetu! Malaika wa Mungu wanayasukuma mawazo ya watu, na kuwatayarisha kupokea onyo. Wamishonari wanahitajika katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa kwa urahisi. Sehemu mpya zinafunguliwa kila wakati. Ukweli ni lazima utafsiriwe katika lugha mbalimbali, ili mataifa yote yapate kufurahia mvuto wake safi, wenye kutoa uhai. … (MTC 171.3)

Wainjilisti wa vitabu wanakutana kwa mafanikio yenye kutia moyo katika uuzaji wa vitabu vyetu. Kwa hiyo nuru inaletwa kwa watu, wakati mwinjilisti wa vitabu—ambaye katika visa vingi amefukuzwa kazi kwa kuukubali Ukweli (sasa inabidi afanye uinjilisti)—anawezeshwa kujitegemeza kimaisha, na mauzo hayo ni msaada wa kifedha kwa ofisi. Katika siku za Matengenezo ya Kanisa, watawa waliokuwa wameacha nyumba zao za kitawa, na ambao hawakuwa na njia nyingine ya kujikimu kimaisha, walizunguka nchi nzima, wakiuza kazi za Luther, ambazo zilisambazwa kwa kasi katika Ulaya yote. Kazi uinjilisti wa vitabu ilikuwa mojawapo ya njia zenye ufanisi zaidi za kueneza nuru ya wakati huo, na ndivyo itakavyothibitisha sasa.— (R&H,

Desemba 6, 1887 ( Life Sketches of Ellen G. White, 304, 305 ). MTC 171.4)

**Baadhi ya Nchi Ni Rahisi Kufanya Kazi Humo Kuliko Nyingine.**— Nchi fulani zina manufaa yanayozozitia alama kuwa vitovu vya elimu na mvuto. Katika mataifa yanayozungumza Kiingereza na mataifa ya Kiprotestanti ya Ulaya ni rahisi ukilinganisha na nchi zingine, kufikia watu, na kuna faida nyingi za kuanzisha taasisi na kuendeleza kazi yetu. Katika nchi nyinginezo, kama vile India na China, watendakazi lazima wapitie kozi ndefu ya elimu ili watu waweze kuwaelewa. Na katika kila hatua kuna matatizo makubwa ya kukutana nayo katika kazi. Huko Amerika, Australia, Uingereza, na nchi zingine za Ulaya, vikwazo vingi hivi havipo. Amerika ina taasisi nyingi za kutoa tabia kwa kazi hiyo. Miundo mbiu au majengo kama hayo yanapaswa kutayarishwa kwa ajili ya Uingereza, Australia, Ujerumani, na Skandinavia, na nchi nyingine za Bara, jinsi kazi inavyoendelea. Katika nchi hizi Bwana anao watenda kazi hodari, watenda kazi wenye uzoefu. Nchi hizi zinaweza kuongoza katika uanzishwaji wa taasisi, mafunzo ya watendakazi, na uendelezaji wa kazi katika safu zake tofauti. Mwenyezi Mungu amepanga wapewe fedha na miundombinu. Taasisi zilizoanzishwa zingetoa sifa ya kazi katika nchi hizi, na zingetoa fursa kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi kwenye mataifa ya kipagani. Kwa njia hii ufanisi wa wafanyakazi wetu wenye uzoefu ungeongezeka mara mia.— (6T.25 . (1900) MTC 171.5)

**Majiji ya Australasia Yafanyiwe Kazi.**— Mara kwa mara katika miaka mitano iliyopita, imewasilishwa kwangu kwamba kazi kubwa inapaswa kufanywa katika majiji ya Australasia, kwamba sasa ni wakati mzuri wa kufanya kazi, na kwamba hakuna wakati muafaka hili linapaswa kufanywa kama sasa, na msipoteze muda; na hivi majuzi

nuru imenijia, ikitutia moyo kuweka juhudi kubwa zaidi katika Sydney, Melbourne, na Brisbane, na kuonyesha kwamba wakati umefika wa sisi kuingia Newcastle na miji inayoizunguka. Makundi kadhaa madogo yaliwasilishwa kwangu, na pamoja yalikuwepo makundi makubwa mawili yaliyokuwa yakinyoosha mikono yao kwa kusihi, yakisema, " 'Njoo huku ..., na utusaidie.' Tuna njaa ya Mkate wa uzima."— (R& H, Aprili 11, 1899 . MTC 172.1)

**Uinjilisti wa afya Utaongoza katika Kazi Nchini Australia.—** Kazi ya umishenari wa tiba yaahidi kufanya mengi zaidi nchini Australia kuliko ilivyo katika Amerika, kwenye kufungua njia kwa ajili Ukweli kupennya kwa watu. Watu wa Bwana sasa na wazingatie mialiko ufunguzi ya majaliwa ya Mungu, na kutambua kwamba ni wakati mwafaka wa kufanya kazi.— (Letter 41, 1899 ( Ev, 425, 426 ). MTC 173.1)

**Taasisi za Afya Hutoa Tabia ya Kufanya Kazi Katika Nyanja Mpya.—** Kwenye mikutano yetu huko Australia, hotuba kuhusu masuala ya afya zilitolewa kila siku, na watu wakaamka na kuwa na shauku kubwa. Hema kwa matumizi ya matabibu na wauguzi lilikuwa chini; ushauri wa tiba ulitolewa bure, na ulitafutwa na wengi. Maelfu ya watu walihudhuria mihadhara hiyo, na mwisho wa mkutano wa kambi watu hawakuridhia kuyaacha mambo hayo ambayo tayari walikuwa wamejifunza yadondoke chini. Katika majiji kadhaa ambako mikutano ya kambi ilifanywa, baadhi ya wananchi na viongozi mashuhuri walihimiza kwamba taasisi ya tawi la Sanitarium ianzishwe, nao wakaahidi ushirikiano wao. Katika miji kadhaa kazi imeanza na mafanikio mazuri. Taasisi ya afya, iliyosimamiwa kwa usahihi, inatoa tabia kwa kazi yetu katika maeneno mapya. Na si tu kuwa ni faida kwa watu,

bali watenda kazi waliounganishwa nayo wanaweza kuwa msaada kwa watenda kazi wenzao katika nyanja za uinjilisti pia. (MTC 173.2)

Katika kila mji ambao tuna kanisa, kuna haja ya mahali ambapo tiba inaweza kutolewa. Miongoni mwa nyumba za washiriki wa kanisa letu kuna wachache ambao wanaweza kumudu kodi ya chumba na majengo ya huduma ifaayo ya wagonjwa. Mahali panapaswa kutolewa ambapo tiba inaweza kutolewa kwa magonjwa ya kawaida. Jengo linaweza kuwa lisilo la kifahari na hata rafu au lililochoka, lakini linapaswa kuwekewa vifaa na samani ili kutoa tiba rahisi. Haya majengo yakitumika kwa ustadi, yangethibitisha baraka si kwa watu wetu tu, bali kwa jirani zao, na yangeweza kuwa njia ya kuelekeza usikivu wa wengi kwenye kanuni za afya.— (6T.112, 113 . (1900) MTC 173.3)

**Kazi Kuenea Katika Nchi Nyingi Kutoka Australia.—** Katika jitihada zao za kuendeleza kazi katika mistari thabiti na kuingia katika eneo jipya, ndugu na dada zetu katika Australasia wametoa zawadi na mikopo kwa kadiri ya uwezo wao. Katika nyakati za mfadhaiko mkubwa, Bwana amegusa mioyo ya wanaume na wanawake katika Australasia na Amerika kutenda uwakili wao vyema kwa kuendeleza mali za kusaidia katika kuanzisha taasisi zinazojengwa huko. Wale ambao wamekuja kwa msaada wa Bwana kwa njia hii wamekuwa wakiweka hazina kando ya kiti cha enzi cha Mungu. (MTC 173.4)

Licha ya uhaba wa nyenzo, mengi yametimizwa na watendakazi nchini Australasia. Vita vikali vimepiganwa. Hakuna chochote isipokuwa nguvu ya Mungu ya kutenda miujiza ndiyo ambayo imekamilisha kazi ambayo imefanywa. Tuliona nguvu Zake tulipokuwa tukisonga mbele kutoka hatua moja hadi nyingine; na tunamsifu kwa moyo na nafsi na sauti. Lo, Jinsi tulivyothamini kwa kiasi

kikubwa fadhili zenye upendo za Mungu wetu alipokuwa akituongoza hatua kwa hatua! ... (MTC 174.1)

Australasia ni kitovu kilichowekwa na Mungu, ambamo nuru ya Ukweli wa sasa itaangazia nchi nyingi. Sauti inatujia kutoka nchi za mbali, “Njooni huku mtusaidie.” Baadhi ya mashamba haya ambayo hayajaingiwa bado, na ambayo hayajaangaziwa, hayafikiwi kwa urahisi sana, na pengine hayako tayari kupokea nuru, kama mashamba yaliyo karibu na macho yetu; lakini hazipaswi kupuuzwa. Tunapaswa kusukuma ushindi wa msalaba. Kauli mbele yetu ni , Mbele daima. Mzigo wetu kwa “maeneo yaliyo ng’ambo” hauwezi kamwe kuwekwa mpaka dunia nzima itakapoangazwa kwa utukufu wa Bwana.— (Atlantic Union Gleaner, Juni 17, 1903 . MTC 174.2)

**Watu Wanaoishi Katika Miji ya Australia Wanapaswa Kutahadharishwa.—** Mkutano wetu wa tatu wa kambi ya Australia ulifanyika Armadale, kitongoji chenye watu wengi cha Melbourne, karibu maili tatu kusini- mashariki kutoka katikati ya jiji. Katika sehemu ya mwanzo ya mwaka ndugu zetu walikuwa wamepanga kwa ajili ya mkutano kufanyika katika Ballarat, jiji la watu elfu thelathini, kama maili tisini kaskazini kutoka Melbourne. Kuna kanisa dogo adilifu huko ambalo lilihitaji kuimarishwa, na kwa vile Konferensi ya Australia ina deni, ilionekana vyema ufanywe mkutano mahali ambapo pangekuwa na gharama ndogo kuliko huko Melbourne. (MTC 174.3)

Lakini Bwana amekuwa akinipa mwanga kuhusu kazi inayopaswa kufanywa katika miji yetu mikubwa. Watu wa mijini wanapaswa kuonywa, na ujumbe unapaswa kuwafikia sasa. Wakati utakuja ambapo hatuwezi kufanya kazi kwa uhuru katika miji mikubwa; lakini sasa, watu watasikiliza ujumbe, na huu ni wakati wetu wa kufanya kazi kwa dhati na bidii zaidi kwa ajili ya watu walio katika vitovu

vyenye idadi kubwa ya watu. Wengi watasikia na kutii, na kubeba ujumbe kwa wengine. (MTC 175.1)

Shauku ambayo ilianza kuamshwa na mkutano wa kambi uliofanywa miaka miwili iliyopita huko Brighton inapaswa kuendelezwa na mkutano wa kambi katika sehemu fulani ya Melbourne kila mwaka. Ndugu zetu walipotilia maanani mambo hayo, waliamua kwamba mkutano ufanyike Melbourne, na katika kutafuta kwao uwanja waliongozwa kujipatia mahali huko Armadale. Mpango wa kwanza ulikuwa kufanya mkutano huko Northcote, ambako pangekuwa rahisi kwa ndugu na dada zetu. Lakini Bwana alifunga njia huko Northcote, na kuwaongoza hadi eneo linalofaa kwenye vitongoji vilivyo na watu wengi, mahali ambapo ujumbe haujawahi kutolewa. (MTC 175.2)

Wakati wa mkutano tumekuwa na uthibitisho mwingi kwamba Bwana amekuwa akiongoza mahali na kazi inayohusu mkutano huo. Sehemu mpya imefunguliwa, na inaonekana kuwa ni eneo la kutia moyo. Watu hawasheheni kutokana na udadisi tu katika mkutano wetu wa kwanza huko Brighton, na kama huko Ashfield mwaka jana. Wengi walikuja moja kwa moja kwenye hema kubwa la kukutania, ambapo walisikiliza kwa makini Neno hilo; na mkutano [ulipoisha], walirudi nyumbani kwao kimya-kimya, au walikusanyika katika vikundi ili kuuliza maswali au kujadili/kuzungumzia yale waliyosikia.— (R&H, Januari 7, 1896 . MTC 175.3)

**Sanitariums Inahitajika Karibu na Kila Jiji Kubwa.-** Kwa muda mrefu Sanitarium ya Battle Creek ilikuwa ndiyo taasisi pekee ya tiba iliyoendeshwa na watu wetu. Lakini kwa miaka mingi nuru imetolewa kwamba Sanitariamu zingine zinapaswa kuanzishwa karibu na kila jiji kubwa. Sanitarium zinapaswa kuanzishwa karibu na miji kama vile Melbourne na Adelaide. Na fursa zinapokuja za kuanzisha kazi katika maeneo mengine bado, hatupaswi kamwe

kunyoosha mkono na kusema: La, hampaswi kuanzisha kusitawisha kituo mahali pengine, kwa kuhofu kwamba sapoti, fursa na fedha vitapungua.— (Lt.233, 1905 ( MH, 326). MTC 175.4)

**Kazi ya Mijini Itatoa Matunda ya Nafsi Nyingi Zitakazookolewa.—** Kuna kazi ya kufanya ulimwenguni pote, na tunapokaribia wakati wa mwisho, Bwana atawavutia watu wengi washiriki katika kazi hii. Ikiwa wewe [Dr. Daniel H. Kress] unaweza kutumia ushawishi wako katika kuwekesha kwenye kazi ambayo inahitaji kufanywa huko Sydney, roho nyingi zitaokolewa ambazo hazijawahi kusikia Ukweli. Miji inapaswa kufanyiwa kazi. Nguvu ya kuokoa ya Mungu inapaswa kwenda mbele kupitia kwao kama taa iwakayo.— (Letter 79, 1905 ( Ev, 425 ). MTC 176.1)

**Wasimamizi Wenye Uzoefu Wanahitajika Kuongoza na Kuunganisha Pamoja Juhudi za Kiinjilisti.—** Sasa kuna kazi ya kufanywa, iliyodhamiriwa zaidi katika Sydney na maeneo ya jirani. Vitongoji vyote viko katika hali nzuri zaidi ya kufanyiwa kazi kuliko kipindi chochote cha awali, na manufaa yanayotolewa sasa katika kufanya kazi ya umishenari wa tiba yanahitaji ukorokotoaji na na uzoefu uletwe katika usimamizi wa kazi. ... (MTC 176.2)

Kuna matawi mengi ambayo yatakua kutoka kituo kilichotengenezwa sasa huko Sydney, na kila safu ya kazi inahitaji wasimamizi wenye uzoefu, sehemu hiyo inaweza kuungana na sehemu nyingine, na kufanya sehemu moja kamili (1/2 + 1/2= 1).— (Letter .63a, 1898 ( Ev, 425 ). MTC 176.3)

**Kwa Nini Matukio ya Michezo Huleta Msisimuko Zaidi Kuliko Ahadi za Mungu?—** Ulimwengu umejaa msisimko. Wanaume hutenda kana kwamba wamechukizwa na mambo ya chini, ya ovyo na yasiyoridhisha. Nimewaona

wakifurahi sana katika mechi ya mchezo wa kriketi! Nimeona barabara za Sydney zikishonana na watu wengi mitaa, hadi mitaa na, nilipouliza kuna tukio gani la msisimko hapa, niliambiwa kwamba mchezaji fulani aliyebobea kriketi alikuwa ameshinda mchezo huo. Nilihisi kuchukizwa. (MTC 176.4)

Kwa nini wateule wa Mungu hawana shauku zaidi? Wao wanashindania kupata taji isiyoweza kufa, wakifanya bidii kuipata nyumba ambayo haitakuwa na haja ya mwanga wa jua au mwezi, au mshumaa unaowaka; kwani Bwana Mungu atakuwa nuru, nao watatawala milele na milele. Watakuwa na maisha yanayolingana na maisha ya Mungu, yaani wataishi milele; lakini mshumaa wa waovu utazimwa katika giza la aibu, na ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao.—(Special Testimonies for Ministers and Workers, Series A 5:12 ( Counsels to Parents, Teachers. , and students, 343, 344 ). (1896) MTC
176.5)

## Uingereza

**kufanya Kazi nchini Uingereza kusipuuzwe kwa Kazi Nyingine Kwingineko.—** Inaonekana kwangu kwamba ulazima wa kazi nchini Uingereza ni swali muhimu sana kwetu katika nchi hii. Tunazungumzia juu ya Uchina na nchi zingine. Hebu tusisahau nchi zinazozungumza Kiingereza, ambako, ikiwa Kweli ingetolewa, wengi wangeipokea na kuitenda.— (The General Conference Bulletin, Aprili 22, 1901, uku. 396 ( Uinjilisti, 415 ). MTC
177.1)

**Uingereza Imepuuzwa Sana.—** Kuna kazi kubwa ya kufanywa nchini Uingereza. Mwangaza unaotoka London unapaswa kuangaza miale angavu, iliyo wazi hadi kwenye maeneo ya nje. Mungu ametenda mambo huko Uingereza, lakini ulimwengu huu unaozungumza Kiingereza umepuuzwa sana. Uingereza imehitaji watendakazi wengi

zaidi na fedha nyingi zaidi. London haijaanza hata kuguswa. Moyo wangu unaguswa sana wakati hali katika jiji hilo kubwa ilikuwa inaonyeshwa mbele yangu. … Katika jiji la London pekee si chini ya wanaume mia moja wanapaswa kushiriki kazi. Bwana anarekodi kupuuzwa kwa kazi Yake, na kutakuwa na kutoa hesabu nzito siku ya mwisho. (MTC 177.2)

Ikiwa wafanyakazi katika nchi ya Amerika watawapa wengine rehema zao kuu, wataona ufanisi katika Uingereza. Watawahurumia watenda kazi wanaohangaika na matatizo huko, na watakuwa na moyo wa kusema, si kwa maneno tu bali kwa vitendo: "Ninyi nyote ni ndugu" ( Mathayo 23:8 ). Basi wataona kazi kubwa ikifanywa London, na kotekote katika majiji ya Uingereza, na kotekote katika nchi mbalimbali za Ulaya.—( 6T.25, 26 . (1900) MTC 177.3)

**Kazi Kubwa Inayopaswa Kufanywa London.—** London imeonyeshwa kwangu tena na tena kama mahali ambapo kazi kubwa itafanywa, nami nimejaribu kuwasilisha hili mbele ya watu wetu. Niliishi miaka miwili Ulaya, nikizunguka kwenye hili shamba mara tatu. Na kila nilipoenda, niliona maendeleo na uboreshaji katika kazi, na mara ya mwisho uboreshaji ulioamuliwa ulionekana. Na loo, ni shauku kubwa kiasi gani, iliyojaa moyoni mwangu kuona uwanja huu mkubwa, haswa London, ikifanyiwa kazi inavyopaswa kuwa. Kwa nini watendakazi hawajatumwa huko, wanaume na wanawake ambao wangeweza kuweka mipango kazi kwa ajili ya kuendeleza kazi? Nimejiuliza kwa nini watu wetu, wale ambao si hawajawekewa mikono ya huduma rasmi, lakini ambao wana uhusiano na Mungu, nao wanaelewa Maandiko, ila hawafungui Neno kwa wengine. Ikiwa hawa wangeshiriki katika kazi hii, mibaraka mikubwa ingekuja kwa nafsi zao wenyewe. Mungu anataka watu Wake wafanye kazi. Kwa kila mwanaume—na hiyo

inamaanisha kila mwanamke, pia—Yeye ametoa kazi Yake, na kazi hii kila mmoja anapaswa kuifanya kulingana na uwezo wake kadhaa/anuwai aliopewa.— (The General Conference Bulletin, Aprili 22, 1901, uk. 396 ( Sons of God, 134, 135 ). MTC 178.1)

**Jeshi la Wafanyakazi Lahitajiwa kuhubiri London.—** Mtu yeyote asiseme kwamba kazi katika London inaweza kusogezwa mbele na mtu mmoja au wawili. Huu sio mpango sahihi. Ingawa ni lazima kuwe na wale wanaoweza kusimamia kazi hiyo, kunapaswa pia kuwa na jeshi la watendakazi wanaojitahidi kufikia tabaka mbalimbali za watu. (MTC 178.2)

Kazi ya nyumba kwa nyumba lazima ifanywe. Kazi hii tumeifanya katika nchi ya Australia, na tumeona wokovu wa Mungu wakati kazi hii ilivyosonga mbele.— (General Conference Bulletin, Aprili 22, 1901, ukurasa wa 396, 397 . MTC 178.3)

**Hakuna Woga; Shuguli ya Bwana Inahitaji Kuharakisha.—** Kuna uhitaji wa bidii katika kanisa, na hekima ya kuisimamia bidii hiyo. Wewe [E J Waggoner] umefanya kazi ngumu sana ya kuokoa roho. Ikiwa [ungependa] kuona kazi inafanywa katika London na miji inayozunguka, lazima uwe na nguvu iliyoungana, isiyozuilika; ya kusukuma vita mpaka langoni, na uweke kiwango kwa uthabiti, kana kwamba unamaanisha kwamba Ukweli unapaswa kushinda. Woga, harakati za tahadhari, zimekuwa zimeonyesha kutokuwa na imani; na hivyo kumekuwa na matarajio madogo ya matokeo. ...(MTC 178.4)

Ukweli kwamba mambo yanasonga polepole huko Uingereza sio sababu kwa nini kazi kuu ya umishenari isonge polepole ili kuchukuliana na tabia na desturi za watu kwa kuogopa kuwashangaza watu. Watu wanahitaji kushangazwa zaidi kuliko hapo awali. Biashara ya Bwana inahitaji uharaka; nafsi zinaangamia bila ujuzi wa

Ukweli.— (Letter 31, 1892 ( Manuscript Relees 3:13, 14 ; Evangelism,414, 415 ). MTC 179.1)

## U JERUMANI

**Migahawa ya afya na Vituo vya Sanitarium Vinahitajika.—** Katika nchi za kigeni biashara nyingi zinazohitaji pesa lazima zianzishwe na kuendelezwa. Ufunguzi wa migahawa ya usafi na afya, uanzishwaji wa Sanitariums kwa ajili ya huduma ya wagonjwa na mateso, ni muhimu nchini Ujerumani kama vile ilivyo Amerika. Hebu wote wafanye yote wawezayo, wakijisifu katika Bwana, na kuwabariki wengine kwa matendo yao mema.— (Letter 121, 1902 ( Evangelism, 413 ). MTC 179.2)

**Wahamiaji toka Ujerumani Wahimizwa Kusaidia Shule nchini Ujerumani.—** Ndugu na dada zangu Wajerumani katika Amerika, ujumbe huu umetolewa kwangu kwa ajili yenu: Mungu anao waaminifu Wake nchini Ujerumani na katika nchi nyingine zote ambako Wajerumani wametawanyika. Fikiria mema yanayoweza kufanya, ni watu wangapi wanaoweza kusaidiwa, kwa kuuza nakala ya Kijerumani ya *Christ's Object Lessons/Mifano ya Yesu,* ukifanya yote uwezayo kwa bidii yako na kwa uwezo wako kushiriki katika gharama ya kuanzisha na kuendeleza kazi ya shule. Ujerumani.— (letter 121, 1902 ( The Publishing Ministry, 367 ). MTC 179.3)

## SKANDINAVIA

**Msaada toka Nje Unahitajiwa, Lakini Washiriki Wa Kanisa Mahalia Wafanye Yote Wawezayo.—** Ninatoa wito hasa kwandugu zetu katika Skandinavia. Je, humtaishika kazi ambayo Mungu amewapa? Je, hamtafanya kazi kwa uwezo wenu wote ili kunusuru taasisi zinazoaibika katika uwanja wenu? Msiangalie kwa kukata tamaa, ukisema: "Hatuwezi kufanya lolote." Acheni kuongea maneno ya

kukata tamaa. Shikilieni mkono wenye Nguvu Isiyo na Kikomo. Kumbuka kwamba ndugu zako katika nchi nyingine wanaungana ili kukupa wewe msaada. Usifeli au kukata tamaa. Bwana atawategemeza watenda kazi Wake katika Skandinavia ikiwa watatenda sehemu yao kwaimani, katika maombi, kwa matumaini, wakifanya yote wawezayo kuiendeleza kazi Yake na kuharakisha Ujio Wake.(MTC 179.4)

Acheni jitihada za dhati zifanywe na watu wetu katika Uingereza ili kuwatia moyo ndugu zao huko Skandinavia kwa imani na ujasiri. Ndugu zangu, ni lazima tuje kwa msaada wa Bwana, kwa msaada wa Bwana dhidi ya mashujaa. (MTC180.1)

Kumbukeni kwamba kadiri tunavyokaribia zaidi wakati wa kuja kwa Kristo, ndivyo tunavyopaswa kufanya kazi kwa bidii na kwa uthabiti zaidi; kwa maana tunapingwa na sinagogi lote la Shetani. Hatuhitaji msisimko wa joto, bali ujasiri unaotokana na imani ya kweli.— (Testimonies For The Church 6:474, 475 . (1900) MTC 180.2)

**Wakati Kupanua Kazi Katika Skandinavia Umefika.—** Kuna kazi ya kufanywa katika Skandinavia. Mungu Yuko tayari kufanya kazi kupitia waumini wa Skandinavia kama anavyofanya kupitia waumini wa Marekani. (MTC 180.3)

Ndugu zangu, jifungeni pamoja na Bwana, Mungu wa majeshi. Mwachieni awe hofu yenu, na awe woga wako. Wakati umefika wa kazi Yake kukuzwa. Nyakati za taabu ziko mbele yetu, lakini tukisimama pamoja katika ushirika wa Kikristo, bila ya kugombania kupata ukuu, Mungu atatufanyia kazi kwa uweza mkuu.— (Testimonies For The Church 8:38 . (1904) MTC 180.4)

**Kuna fursa nyingi Kuliko Idadi ya Wafanyakazi wa Kukidhi Mahitaji.—** Uswidi bado imekuwa na kazi kidogo tu, na sauti ya Ukweli imefikia masikio machache tu; bado

huu ni uwanja mzuri, na juhudi za dhati, za kudumu zinapaswa kufanywa ili kupanua maarifa ya Ukweli. Miito inaingia kutoka Norway, Denmark, na Sweden kwa ajili ya mikutano itakayofanywa katika majiji makubwa, ambako watu wachache tayari wamepatikana. Tunaitazama miji ambayo hatuna wamisionari zaidi wa kuwatuma kwao kwa uchungu. Wale wachache ambao wamepokea Ukweli katika sehemu mbalimbali huachwa karibu bila msaada, wakati ambapo wanapaswa kutembelewa mara nyingi, na kuelimishwa ili wawe watendakazi. Nafasi ni nyingi; lakini watendakazi wako wapi? (MTC 180.5)

Nchini Sweden ndugu zetu wengi ni maskini, na wanapoangalia mwonekano, wanaona kuwa haiwezekani kwao kufanya mengi kuendeleza na kupanua kazi. Lakini katika siku za mapema za skazi katika Amerika matatizo kama hayo watu walipaswa wakutane nayo.—(The Review and Herald, Oktoba 5, 1886 . MTC 181.1)

**Nchi za Skandinavia Ni Maeneo Yenye Mafanikio ya Kazi.—** Hali ya baadhi ya makanisa hayo ilikuwa imeonyeshwa kwangu katika miaka ya nyuma, na mambo mengi yalionyesha kwamba Denmark, Norway, na Sweden kwamba yalikuwa mashamba yenye matumaini kwa ajili ya kazi ya Mungu. Tulijua kwamba kazi kubwa ilikuwa mbele ya wamishenari katika uwanja huu.—(Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 174
. (1886) MTC 181.2)

**Tabia ya Kazi Huamuliwa Kulingana na Jinsi Inavyowasilishwa kwa Umma.—** Huko Örebro [Sweden], na pia huko Copenhagen [Denmark], ninasadiki kwamba tungeweza kusikilizwa vizuri huko ikiwa ndugu zetu wangepata ukumbi unaofaa, na wenye kutosheleza watu. Lakini hawakutarajia mengi, na kwa hivyo hawakupokea mengi. Hatuwezi kutarajia watu wajitokeze ili kusikia

Ukweli usiopendwa au usio maarufu na watu wengi mikutano inapotangazwa kufanywa katika chumba cha chini cha ardhi/basement, au katika jumba dogo ambalo litakaa watu mia moja tu hawatajitokeza inavyopaswa. Tabia na umuhimu wa kazi yetu hupimwa kutokana na juhudi zinazofanywa kuifikisha mbele ya umma. Jitihada hizi zinapokuwa chache sana, maoni yanatolewa kwamba ujumbe tunaowasilisha haustahili kutiliwa umakini. Hivyo kwa ukosefu wao wa imani watendakazi wetu wakati mwingine hufanya kazi kuwa ngumu sana kwao wenyewe.— (Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh- day Adventists, 200 ( Evangelism, 422 ). (1886) MTC 181.3) **Dini Rahisi Inayopendwa na Watu Wengi.—** Tunaambiwa kwamba watu katika nchi hizo watapendezwa na hotuba zetu ikiwa tutakazia sana upendo wa Yesu. Ujumbe wa namna hii kamwe hawauchoki, lakini tuko katika hatari ya kupoteza mikusanyiko yetu ikiwa tutazingatia maswali makali ya wajibu na sheria ya Mungu. Kuna uzoefu wa uwongo unaoenea kila mahali. Wengi huendelea kusema, "Tunachopaswa kufanya ni kumwamini Kristo peke yake." Wanadai kwamba imani ndiyo yote tunayohitaji. Kwa maana yake kamili, hii ni kweli; lakini hawaichukui kwa maana kamili. Kumwamini Yesu ni kumchukua kama mkombozi wetu na kielelezo chetu. Tukikaa ndani Yake na Yeye anakaa ndani yetu, sisi ni washirika wa asili Yake ya uungu, na ni watendaji wa Neno Lake. Upendo wa Yesu moyoni utaongoza kwenye utii kwa amriZake zote. Lakini upendo wa mdomoni tu, ni udanganyifu; hautaokoa nafsi yoyote. Wengi hukataa Kweli za Biblia, huku wakidai upendo mkuu kwa Yesu; lakini mtume Yohana anatangaza, "Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Ingawa Yesu amefanya yote ili kutustahilisha, sisi wenyewe tuna kitu cha kufanya katika njia ya kutii

masharti. “Ikiwa mnanipenda,” Mwokozi wetu alisema, “zishike amri Zangu.”— (Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, 188, 189 . (1886) MTC 182.1)

**Mioyo minyoofu ipo ingawa watu wengi waliozunguka wamejaa Udunia mioyoni.—** Copenhagen inaonekana kama Athene katika siku za Paulo. Kutafuta mali na anasa kunavuta fikira za watu. Ukana-Mungu au ukafiri ni maarufu. Kula na kunywa, kucheza dansi na kufanya sherehe, ni mada ya mawazo na mazungumzo. Kuna makanisa mengi makubwa na mazuri; lakini watu hawa, kama baadhi ya Waathene, wanaabudu Mungu asiyejulikana. Hakuna ukosefu wa madaktari wa elimu ya theolojia, wahubiri wasomi, ambao hakika hawajui dini ya Biblia ni nini. ... (MTC 182.2)

Inaonekana ni jambo gumu kuamsha shauku ya mambo ya kidini katika miji hii mikubwa; na bado kuna nafsi nyingi adilifu ndani ya miji hiyo, ambazo bado zitakubali nuru na kuakisi miale yake kwa wengine. Copenhagen inatuma wamishenari kuwaongoa wapagani katika nchi za mbali, wakati kuna umati wa watu wake ambao kwa kweli hawamjui Mungu na Neno Lake. Wanaume wenye roho ya Paulo wanahitajika ili kumhubiri Kristo na Yeye aliyesulubiwa.— (Historical Sketches of the Foreign Missions of the Seventh-day Adventists, p . (1886) MTC 182.3)

**KAZI ZAIDI NGAMBO KWENYE MABARA MENGINE**

**Mamilioni ya Watu Wanaoishi Afrika na Asia Bado Wanahitaji Kuisikia Injili.—** Katika Afrika, China, India, kuna maelfu, ndiyo, mamilioni, ambao hawajasikia ujumbe wa Ukweli wa wakati huu. Haw ni lazima waonywe. Visiwa vya bahari vinangojea maarifa ya Mungu. Katika visiwa hivi shule zapaswa kuanzishwa ili kuwatayarisha wanafunzi kwenda shule za sekondari zinazoweza kufikiwa, ili huko

waelimishwe na kuzoezwa, na kurudishwa kwenye makao yao ya visiwa ili kuwapa wengine nuru ambayo wamepokea.— (Testimonies For The Church 9 51 . (1909) MTC 183.1)

**Ulimwengu Mzima Una Dai Sawa Nasi, la Huruma ya Mungu.—** Ulimwengu wote unafunguka kwa injili. Ethiopia inanyoosha mikono yake kwa Mungu. Kutoka Japani na Uchina na India, kutoka nchi ambazo bado ziko gizani za bara letu, kutoka kila sehemu ya dunia yetu hii, kinakuja kilio cha mioyo iliyopigwa na dhambi kwa ajili ya kumjua Mungu wa upendo. Mamilioni kwa mamilioni hawajawahi kusikia hata kidogo kuhusu Mungu au upendo Wake uliofunuliwa katika Kristo. Ni haki yao kupata elimu hii. Hawa wana madai sawa nasi katika rehema ya Mwokozi. Nasisi ambao tumepokea ujuzi huo tunategemewa kwa hili, pamoja na watoto wetu ambao tunaweza kuwapa nuru, ili wajibu kilio chao.— (Education, 262, 263 . (1903) MTC 183.2)

**Licha ya Matatizo na ugumu, Ulimwengu Bado Lazima Uonywe.—** Katika kila jiji na kila kitongoji kuna kazi ya kufanywa katika kuwasilisha ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu ulioanguka dhambini. Na tunapojaribu kufanya kazi katika mashamba haya duni, kilio kinatoka katika nchi za mbali, "Njooni huku mtusaidie." Haya hayafikiwi kwa urahisi sana, na pengine hayako tayari kwa mavuno, kama mashamba yaliyo mbele yetu, lakini hayapaswi kupuuzwa. Tunataka kusukuma ushindi wa msalaba. Neno letu la kaulimbiu linapaswa kuwa, "Nenda, daima mbele!" Mzigo wetu kwa "mikoa ya ng'ambo" hauwezi kamwe kuwekwa mpaka dunia nzima itakapoangalizwa na utukufu wa Bwana.— (Australasian Union Conference Record, Januari 1, 1900 ( Life Sketches of Ellen G. White, 375 ). MTC 183.3)

## Sura ya 12—Utafiti maalumu

### KUINJILISHA SAN FRANCISCO OAKLAND

*Mnamo 1872 James na Ellen White walitembelea California kwa mara ya kwanza. Wasiwasi wa Ellen White kwa watu wanaoishi San Francisco na Oakland ulidhihirika katika miaka iliyofuata. Mnamo mwaka 1900 alirudi Amerika kutoka Australia. Mara tu baada ya kuwasili alinunua nyumba kaskazini mwa California, ambayo aliiita "Elmshaven." Kuanzia wakati huo hadi kifo chake katika 1915, Ellen White aliandika mashauri mengi juu ya mada mbalimbali, lakini alikuwa na mzigo fulani wa kuinjilisha miji. Miongoni mwa miji aliyoandika habari zake ni miwili katika eneo la ghuba la kaskazini mwa California: San Francisco na Oakland. Kinachofuata ni mifano ya mashauri yake juu ya kueneza injili kwenye majiji hayo mawili.* MTC 185.1

*San Francisco na Oakland hazijateuliwa kama ndizo muhimu zaidi kuliko miji mingine mikubwa kote ulimwenguni. Badala yake, utafiti mfupi unaowasilishwa hapa umeandikwa ili kuonyesha wasiwasi wa Ellen White katika uinjilishaji wa miji, na pia kuona mfano wa mashauri yake kuhusu miji, kwa kuangalia ushauri wake kwa hiyo miji*

*miwili . Sio kila kitu alichoandika kuhusu miji hii miwili kimejumuishwa katika sura hii, lakini maingizo haya yanatosha kudhihirisha wigo mpana wa kazi na uhusikaji kamili wa kanisa ambalo alitoa wito wa kuhamasisha uinjilisha kwenye jiji kubwa. Kanuni zinazopatikana kwenye kesi hizi, zinaweza kusaidia kuwaongoza wote wanaohusika katika uinjilisti wa majiji, mahali popote pale ulimwenguni kupanga kazi yao kwa uangalifu, kwa maombi, na kwa mapana.* MTC 185.2

## UAMSHO WA KIROHO WA WASHIRIKI BINAFSI UNAHITAJIKA

**Uongofu wa Kweli na Mzigo kwa Roho za Watu Unaohitaka Kutoka kwa Washiriki wa Kanisa.—** ... nilikutana na makanisa ya Oakland na San Francisco chini ya hema kubwa huko San Francisco. ... Nilihisi mzigo wa ushuhuda na hitaji kuu la kuwa na uvumilivu kwa juhudi binafsi kwa upande wa makanisa haya ili kuwaleta wengine watu kwenye ujuzi wa Ukweli. Nilikuwa nimeonyeshwa kwamba San Francisco na Oakland ni maeneo yana umishenari, na daima yatakuwa mahali pa umishenari. Ongezeko lao la idadi yao lingekuwa la polepole; lakini ikiwa wote katika makanisa haya wangekuwa washiriki hai na wangefanya kile ambacho wangeweza kufanya katika kutoa nuru mbele ya wengine, wengi zaidi wangeletwa katika jeshi la Bwana na kutii Ukweli. Waumini wa sasa wa ile Kweli hawakujali au kufurahia wokovu wa wengine jinsi wanavyopaswa. Kutofanya kazi na uvivu katika kusudi la Mwenyezi Mungu kungesababisha kurudi nyuma kutoka kwa Mungu kwao wenyewe, na kwa mfano wao wangewazuia wengine wasiendelee mbele. Juhudi zisizo na ubinafsi, zenye kustahimili, na zenye bidii zingeweza kuleta matokeo bora zaidi. Nilijaribu kukazia juu yao yale ambayo Bwana alikuwa amewasilisha mbele yangu, kwamba Yeye

angewezesha Ukweli uwasilishwe kwa wengine na watenda kazi wenye bidii, na si wale wanaodai tu kuiamini Kweli. Hawapaswi kuwasilisha Ukweli kwa maneno tu, bali kwa maisha ya uangalifu na tahadhari, kwa kuwa wawakilishi hai wa Ukweli. MTC 186.1

Nilionyeshwa kwamba wale wanaounda makanisa hayo wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia, wanaojifunza mapenzi ya Mungu kwa dhati bidii zaidi ili wajifunze kuwa watenda kazi katika kusudi la Mungu. Wanapaswa kupanda mbegu za Ukweli popote walipo, nyumbani, kwenye warsha, sokoni, na pia katika jumba la mikutano. Ili kuifahamu Biblia, wanapaswa kuisoma kwa uangalifu na kwa sala. ... MTC 186.2

Akitumaini baraka za Mungu, Mkristo yuko salama popote pale. Mjini hataharibikiwa-hatakuwa fisadi. Katika chumba cha kuhesabu pesa nyingi, atatiliwa alama/umakini kwa tabia zake za uadilifu mkali. Katika duka la mekanika kila sehemu ya kazi yake itafanywa kwa uadilifu, jicho lake likiwa limekazwa kwa utukufu wa Mungu. Mwenendo huu unapofuatiliwa na mshiriki binafsi, kanisa litafanikiwa. Ufanisi hauwezi kuwepo kamwe kwenye makanisa haya hadi washiriki wake mmoja mmoja wawe wameunganishwa kwa ukaribu na Mungu, wakiwa na nia isiyo na ubinafsi katika wokovu wa wanadamu wenzao. Wahudumu wanaweza kuhubiri hotuba au mahubiri ya kupendeza na ya kuleta mvuto mkubwa wa kushangaza, na kazi nyingi inaweza kuwekwa ili kulijenga na kulifanya kanisa kustawi; lakini bila washiriki wake binafsi kufanya sehemu yao kama watumishi wa Yesu Kristo, daima kanisa litakuwa gizani na bila nguvu... ... MTC 186.3

Baadhi ya makanisa haya yamo katika hatari ya mara kwa mara kwa sababu mahangaiko ya maisha haya na mawazo ya kidunia yanakaa sana akilini mwao, hivi kwamba

hawafikiri juu ya Mungu au mbingu na mahitaji ya nafsi zao wenyewe. Wanaamka kutoka kwenye usingizi wao mara kwa mara, lakini wanarudi tena katika usingizi mzito zaidi. Washiriki hawa wasipoinuka kikamilifu kutoka kwenye usingizi wao, Mungu ataondoa nuru na baraka ambazo Amewapa.— {4T.284-286 . (1879) MTC 187.1

**Kila Dhambi Inayozuia Ushirikiano Pamoja na Mungu Inapaswa Kuwekwa Mbali.—** Jitihada ya pekee inapofanywa ili kupata roho watenda kazi wenye uzoefu katika jumuiya ambamo watu wetu wenyewe wanaishi, kila mwamini katika eneo hilo ana wajibu mzito sana wa kufanya yote yaliyo katika uwezo wake ili kusafisha njia kuu ya Mfalme kwa kuweka mbali kila dhambi ambayo ingemzuia kushirikiana pamoja na Mungu na ndugu zake. MTC 187.2

Kwa kawaida jambo hili halijaeleweka kikamilifu. Shetani mara nyingi ameleta roho ambayo imewafanya washiriki wa kanisa kutoweza kutambua fursa za huduma. Waumini wamemruhusu adui mara kwa mara kufanya kazi kupitia wao wakati ule ambapo walipaswa kujiweka wakfu kabisa kwa Mungu na kuendeleza kazi Yake. Bila kujua wametangatanga mbali na njia ya haki. Wakipalilia roho ya kukosoa wengine na kutafuta makosa, roho ya utauwa wa kifarisayo na kiburi, hawa wanamhuzunisha Roho wa Mungu, na kuchelewesha sana kazi ya wajumbe wa Mungu.— {R&H, Desemba 6, 1906 . MTC 187.3

**Kufanywa Upya kwa moyo Kunahitajika Kabla ya Kushiriki Kweli ya Biblia Pamoja na Wengine.—** Usiku baada ya usiku siwezi kulala zaidi ya saa chache; na mara nyingi nyakati za usiku najikuta nimeketi kitandani, nikimwomba Mungu kwa niaba ya wale ambao hawatambui hali yao ya kiroho; na kisha ninainuka na kutembea chumbani, na kusema, Ee Bwana, waweke watu Wako kwenye utaratibu, kabla hawajachelewa milele! MTC 187.4

Wakati fulani katika majira haya ya maombezi, mzigo unaponilemea kwa uzito sana, moyo wangu huonekana kuwa na matamanio makubwa kwa muda mrefu, na machozi huanza kutoka machoni mwangu, na ninakunja- kunja mikono yangu mbele za Mungu kwa wasiwasi, kwa sababu najua kuna roho hatarini katika makanisa. huko Oakland na maeneo ya karibu—nafsi ambazo, kama hali yao ya kiakili ilivyo, hazijui kabisa jinsi zinavyosimama mbele za Mungu kama wale ambao hawajawahi kudai kuwa watu wa dini katika maisha yao. ... MTC 188.1

Inatupasa kutamani kwa moyo wote wongofu kamili, ili Ukweli upate kutawazwa moyoni na akilini, na kwamba, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, tuwe tayari kuwasilisha ujumbe wa malaika wa tatu mbele ya wengine wanaouhitaji. sana.— {R& H, Desemba 13, 1906 . MTC 188.2

## TAFUTA UONGOZI WA MUNGU HUKU UNAPANGA

**Kwa Unyenyekevu, kwa Sala, Mshirikishe Mungu, Tangu Mwanzo Mpaka Mwisho.—** Iwapo, katika wakati huu unaofaa, washiriki wa makanisa watakuja kwa unyenyekevu mbele za Mungu, wakiondoa kutoka mioyoni mwao uovu wote, na kushauriana Naye katika kila hatua, Yeye atajidhihirisha Mwenyewe kwao, na atawapa ujasiri katika Yeye. Ni lazima tuwe tayari kutumia uwezo wetu tuliopewa na Mungu katika kazi ya Bwana. Ni lazima tuwe tayari kuzungumza maneno wakati ufaao na wakati usiofaa—maneno ambayo yatasaidia na kubariki. MTC 188.3

Washiriki wa kanisa wanapofanya sehemu yao kwa uaminifu, Bwana atawasimamia na kuwaongoza wahudumu Wake waliochaguliwa, na kuwaimarisha kwa ajili ya kazi yao muhimu. Katika maombi mengi tuungane sote katika kuinua mikono yao, na katika kuichota miale angavu kutoka Patakatifu pa mbinguni. Tunayo njaa ya roho, tunataka kuona kazi ikiendelea inavyopaswa. Kristo Ndiye alfa na

omega yetu. Ni kwa nguvu Zake tu ndipo tunaweza kupata mafanikio.— { R&H,Desemba 20, 1906 . MTC 188.4

## KU JIFUNZA BIBLIA KIKAMILIFU WASHIRIKI WA KANISA

**Mafunzo ya Biblia Yanashinda Nafasi ya Usomaji Usio na Maana (tamthiliya, magazeti, hadithi au hata mengine ya mtandaoni).—** Tunahitaji kupata vitu vipya kila siku kutoka kwenye ghala kuu la Neno la Mungu. Hii haitatoa muda wa usomaji wa riwaya, au kwa kitu kingine chochote ambacho hakijengi na kuimarisha kila kazi njema.— {R&H,Oktoba 4, 1906 ( Sons and Daughters of God, 325 ). MTC 189.1

## KUSHIRIKISHWA KWA WOTE

**Vijana na Wazee wa Kushiriki.—** Jitihada za dhati zaidi zinapaswa kufanywa ili kuwaongoza washiriki wakubwa na wachanga zaidi wa makanisa yetu kushikilia kazi mahali pale walipo.— Manuscript 3, 1901 ( Manuscript Relees 17:47 ). MTC 189.2

**Wahudumu Wanakumbushwa Wito Wao .—** Je! hatutafanya yote tuwezayo kuendeleza kazi katika San Francisco na Oakland, na katika miji mingine yote ya California? Maelfu kwa maelfu ya watu wanaoishi katika miji iliyo karibu nasi wanahitaji msaada kwa njia mbalimbali. Hebu wahudumu wa injili wakumbuke kwamba Bwana Yesu Kristo aliwaambia wanafunzi Wake, “Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliowekwa juu ya mlima hauwezi kusitirika.” “Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imepoteza ladha yake, itatiwa nini hata ikolee?”— Manuscript 81, 1902 ( The Kress Collection, 139 ). MTC 189.3

## MAANDALIZI NI MUHIMU

**Maandalizi Ni Muhimu Kabla ya Kazi ya Uinjilisti Kuanza.—** Mzee [William Ward Simpson] alikuwa ameweka hema kubwa la mikutano ya kambi Oakland. Wakati wa maandalizi alikuwa tayari kuongoza kwa vitendo, na alifanyakazi kwa bidii sana ili kufanya maeneo ya kambi yawe na mwonekano mzuri kwa kadri iwezekanavyo.— Letter 352, 1906 ( Evangelism, 76 ). MTC 189.4

## PROGRAMU YA UIN JILILISTI YENYE MAMBO MENGI, Yaliyo TOFAUTI TOFAUTI INAPONGEZWA

**Njia Tofauti za Kufikia Zinatumiwa.—** Katika miaka michache iliyopita, "mzinga wa nyuki" wa San Francisco umekuwa wenye shughuli nyingi. Njia nyingi za juhudi za Kikristo zimesonga mbele. ... Haya yalijumuisha kuwatembelea wagonjwa na watu fukara kabisa, kuwatafutia yatima nyumba, na kufanya kazi kusaidia wale wasio na ajira; kuuguza wagonjwa, na kufundisha Ukweli nyumba kwa nyumba; kusambaza machapisho, na ... madarasa ya maisha yenye afya na utunzaji wa wagonjwa. Shule ya watoto imeendeshwa katika sehemu ya chini ya ardhi ya nyumba ya mikutano ya Mtaa wa Laguna (basement). Hosteli ya wanaume wanaofanya kazi na umishenari wa tiba ulidumishwa. Kwenye mtaa wa Market Street, karibu na Ukumbi wa mkutano wa jiji, kulikuwa na vyumba vya tiba vilivyoendeshwa kama tawi la Sanitarium ya St. Helena. Katika eneo hilo hilo kulikuwa na duka la chakula cha afya. Karibu na katikati ya jiji, si mbali na jengo la Call, palikuwa na... ... mkahawa wa chakula cha mboga-mboga (vegeterian), ambao ulifunguliwa siku sita za juma, na kufungwa kabisa siku ya Sabato. Kando na ufukwe wa bahari, kazi ya utume wa meli Ulifanyika (Meli iliwekwa watu walikuja kwa mashauri, tiba, injili nk). Nyakati mbalimbali wahudumu wetu walifanya mikutano katika

kumbi kubwa jijini. Hivyo ujumbe wa onyo ulitolewa na wengi.— { R&H, Julai 5, 1906 ( Welfare Ministry, 112 ). MTC 190.1

**Ongezeni Ufanisi Kupitia Upanuzi wa Juhudi Zenu.—** Huko San Francisco mgahawa wa afya na Usafi umefunguliwa (Hygenic Restaurant), pia duka la chakula na vyumba vya tiba. Hawa wanafanya kazi nzuri, lakini ushawishi wao unapaswa kupanuliwa sana. Migahawa mingine inayofanana na ile ya Market Street inapaswa kufunguliwa huko San Francisco na Oakland.— { 7T.110 . (1902) MTC 190.2

**MGAHAWA WA VYAKULA VYA MIMEA (Vegeterian Restaurant) Migahawa ya Kufundisha Kanuni za Afya.—** Ikiwa ... migahawa zaidi inaweza kuendeshwa huko San Francisco, ingekuwa baraka kiasi gani. Kwa vitendo halisi vya jinsi ya kuandaa vyakula vyenye afya, visivyokobolewa au kusindikwa, vyenye ladha nzuri bila kutumia nyama ya aina yoyote, wengi wangejifunza masomo yenye thamani. Watu hawa wangezifahamu kanuni za afya.— Ms.1, 1901 ( Manuscripts Released 17:42, 43 ). MTC 190.3

**Sabato Inapaswa Kuendelea Kutunzwa Katika Migahawa.—** Swali limeulizwa: "Je, migahawa yetu inapaswa kufunguliwa siku ya Sabato?" Jibu langu ni: Hapana, hapana! Utunzaji wa Sabato ni ushuhuda wetu kwa Mungu, alama, au ishara, kati Yake na sisi kwamba sisi ni watu Wake. Kamwe alama hii isifutiliwe mbali. ... MTC 191.1

Tunapaswa kutii "Bwana asema hivi," ingawa kwa utii wetu tunaleta usumbufu mkubwa kwa wale ambao hawaiheshimu Sabato. Kwa upande mmoja tuna mahitaji ambayo mwanadamu anadhani kwamba anayahitaji ; na kwa upande mwingine, tuna amri za Mungu. Je, kati ya hivi viwili ni jambo lipi lenye uzito mkubwa zaidi kwetu?— { 7T:121, 122 . (1902) MTC 191.2

**Watendakazi wa Nyumba kwa Nyumba Wanapaswa kufuatilia Mikutano ya hadhara.—** Imepangwa kwamba Mzee WW Simpson aanze mfululizo wa mikutano mjini Oakland ndani ya majuma machache sana. Pamoja naye kunapaswa kuwa na nguvu kali ya wafanyakazi wa nyumba kwa nyumba. Usomaji wa Biblia unapaswa kufanywa katika nyumba za watu, na machapisho yetu yanapaswa kusambazwa.— {R& H, Oktoba 4, 1906 . MTC 191.3

## MAFUNZO YA WAFANYAKAZI

**Wafanyakazi Waliofundishwa na Kuzoezwa Wanapaswa Kufanya Uenezaji wa Uinjilisti binafsi.— Mchungaji** na Bi. [Stephen na Hetty] Haskell walikuwa wakiongoza mafunzo ya Biblia [madarasa] adhuhuri, na alasiri wafanyakazi waliokuwa katika mafunzo na mazoezi ya uinjilisti, walikuwa wakitoka na kuzuru nyumba kwa nyumba. Ziara hizi za kimishenari, na uuzaji wa vitabu vingi na majarida, vilifungua njia ya kuwezesha usomaji wa Biblia [yaani, mafunzo ya Biblia]. ... MTC 191.4

Kwa sababu ya umuhimu wa kazi hii, nimemhimiza kwamba Mchungaji Haskell na mke wake, kama wahudumu wa Mungu, watoe mafundisho ya Biblia kwa wale ambao watajitoa wenyewe kwa ajili ya utumishi. Mungu atatumia watu wanyenyekevu. Atamfanya kila mtu aliyejitoa wakfu kuwa Mkristo mwenye kubeba nuru. Sio watu wenye ufasaha zaidi wa usemi, sio wale walio na ujuzi bora zaidi wa ile iitwayo theolojia, ndiyo ambao sikuzote hufaulu zaidi, bali wale ambao watafanya kazi kwa bidii na unyenyekevu kwa ajili ya Bwana na Mwalimu.— { R&H, Novemba 29, 1906 (sehemu) . katika Ev.470 ). MTC 192.1

## MBINU BUNIFU ZA UINJILISHAJI

**Mbinu za Ubunifu za Uinjilisti, Zinazotumiwa.—** Namna ya Kazi ya Mchungaji [William Ward] Simpson inanikumbusha juu ya jitihada ambazo zilifanywa mwaka wa 1843 na 1844. Huyu hayafanyi maneno yake mwenyewe yaonekane, bali husoma mengi kutoka kwenye Biblia, akifafanua Andiko moja baada ya nyingine. Anakazia zaidi unabii wa Danieli na Ufunuo, na anatumia vielelezo vingi na takwimu zinazofaa ili kukazia Ukweli moyoni. Ili kuwakilisha wanyama waliowasilishwa kwenye vitabu vya Danieli na Ufunuo, ametayarisha sanamu zenye uhai za makaratasi mengi (papiermâché). MTC 192.2

Mzee Simpson anajitahidi kuepuka kuingia kwenye mabishano na wapinzani. Anawasilisha Biblia kwa uwazi sana hivi kwamba ni wazi kwamba yeyote anayetofautiana lazima afanye hivyo kinyume na Neno la Mungu.— { R& H Februari 7, 1907 . MTC 192.3

**Wasemaji Mbalimbali ni Bora Kuliko Mzungumzaji Mmoja.—** Katika mikutano yetu ya hema ni lazima tuwe na wahubiri/wazungumzaji wanaoweza kuwavutia watu. Uwezo wa mtu mmoja, haijalishi mtu huyu anaweza kuwa na akili nyingi kiasi gani, hautoshi kukidhi hitaji. Vipawa mbalimbali vinapaswa kuletwa katika mikutano hii.— {Manuscript 104, 1902 ( Ev, 70 ). MTC 192.4

**Mikutano Mingi ya Watu Wote Inayofanywa Wakati Mmoja.—** Mikutano ya kambi lazima iongezwe mahali pengine. Maeneo baada ya maeneo yanapaswa kufikiwa. Masilahi yaweza kugawanywa, mikutano ikifanywa katika sehemu zaidi ya moja kwa wakati mmoja, ikiwa watu wetu wenye uwezo hawatarandaranda juu ya majiji wakati ambapo wangeweza kufikia watu wengi katika mikutano mikubwa ya hema.— {Ms 104, NW. 1902 ( Manuscripts Released17:52 ). MTC193.1

## UKWELI WA BIBLIA UWASILISHWE

**Kweli Iwasilishwe Kwa Uwazi na kwa Usahili.—** Ndugu S [William Ward Simpson] ni mwinjilisti mwenye akili. Anazungumza kwa usahili wa mtoto. Kamwe yeye haleti msukosuko wowote katika hotuba zake. Yeye huhubiri moja kwa moja kutoka kwa Neno la Mungu, akiruhusu Neno kunena kwa matabaka yote. Hoja zake zenye nguvu ni maneno ya Agano la Kale na Agano Jipya. Hatafuti maneno ambayo yangewavutia tu watu kwa usomi wake, bali anajitahidi kuruhusu Neno la Mungu lizungumze nao moja kwa moja kwa matamko yaliyo wazi na ya kipekee. Ikiwa yeyote atakataa kuukubali ujumbe huo, ni lazima akatae Neno.— {Lt 326, 1906 ( Ev. 204 ). MTC 193.2

## UFUATILIAJI UNAHITAJIKA

**Kazi ya Nyumba kwa nyumba Kufuatilia Mikutano ya hadhara.—** Kuna kazi nyingi za nyumba kwa nyumba zinazopaswa kufanywa na wafanyakazi waaminifu. Juhudi zetu hazitakoma kwa sababu mikutano ya hadhara imekatishwa kwa muda. Maadamu kuna watu wenye shauku ya Neno, ni lazima tuwape nafasi ya kujifunza Ukweli. Na waongofu hawa wapya watahitaji kufundishwa na waalimu waaminifu wa Neno la Mungu, ili wapate kuongezeka katika ujuzi na upendo wa kweli, na kukua hata kufikia kimo kamili cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu. Ni lazima sasa wazungukwe na mivuto ifaayo zaidi kwa ukuaji wa kiroho.— { R&H Februari 14, 1907 (sehemu katika Ev, 337 ). MTC 193.3

## WAKOSOAJI NA WAPINZANI WAPO

**Upinzani Utatokea, Hata Kutoka kwa Washiriki wa Kanisa.—** siku mbili kabla sijaondoka nyumbani kwangu, niliagizwa, wakati wa maono ya usiku, kuliambia kusanyiko ambalo ningepaswa kukutana nalo Oakland siku ya Sabato, kwamba maneno maovu yaliyokuwa yakitoka midomoni mwao, kuhusu makosa yanayodhaniwa ya watumishi wa Mungu wanaofanya yote wawezayo ili kueneza Ukweli na kuendeleza kazi Yake yote wameandikwa katika vitabu vya kumbukumbu vya mbinguni. Wale wanaosema maneno haya wasipotubu, hatimaye watajipata wenyewe wakiwa nje ya mji wa Mungu. Mungu hataruhusu mtu mwenye malumbano aingie katika jiji la mbinguni.— {Ms 95, 1906 ( Sermons and Talk 1:375, 376 ). MTC 194.1